

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Thelathini na Tatu – Tarehe 30 Mei, 2022

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa tukae.

Katibu.

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU WA BUNGE:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA
AFRIKA MASHARIKI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE K.n.y. MWENYEKITI
WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA
MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

SPIKA: Ahsante sana.

Katibu.

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Maswali Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Kwela sasa aulize swali lake.

Na. 283

**Ujenzi wa Barabara inayounganisha Mtowisa na
Sumbawanga**

MHE. DEUS C. SANGU aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami inayounganisha Mji Mdogo wa Mtowisa na Sumbawanga Mjini kupitia Mlima Ng'ongo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA
SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Jimbo la Kwela kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali barabara hii ilisanifiwa kujengwa kwa kiwango cha changarawe kabla ya ahadi ya Mheshimiwa Rais kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami ambapo katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga shilingi milioni 875 kwa ajili ya kujenga urefu wa kilometa 25 kwa kiwango cha changarawe.

SPIKA: Mheshimiwa Deus Sangu, swali la nyongeza.

MHE. DEUS C. SANGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii ya maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nishukuru na kuipongeza Serikali kutenga hiyo fedha ambayo itakuwa na matumaini makubwa kwa wananchi wa Mtowiso wanaosubiri barabara hiyo ya Ng'ongo.

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza la nyongeza; kwa kuwa Serikali mmetumia shilingi milioni 900 kujenga barabara ya Msia - Mawezuzi, kwenda Sumbawanga Mjini na bado haijakamilika.

Je, ni lini mtaleta shilingi bilioni 1.5 zilizobaki ili kukamilisha barabara hii ipitike?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili la nyongeza; kutokana na mvua nyingi mwaka huu barabara za Kijiji cha Kamsamba ambayo inaunganisha Kijiji cha Kavifuti na Miangalua ilibebwa na maji na mpaka sasa tumeandika andiko liko Wizarani. Nataka kujua je, ni lini fedha hizo za dharura zitakuja ili kutengeneza Daraja hilo la Kamsamba?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Deus Clement Sangu, Mbunge wa Jimbo la Kwela, kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ilikuwa imetoa fedha milioni 900 na mpaka sasa tunahitaji kuongezea fedha ambapo ziko katika mchakato na mchakato ukikamilika fedha ile itapelekwa ili barabara hiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameianisha hapa iweze kumalizia hicho kipande kilichobakia.

Mheshimiwa Spika, lakini suala la pili, wameomba fedha kwa ajili ya barabara ambayo imeharibika kutokana na mvua na fedha hizo ni za dharura, na ni kweli hilo andiko lipo Ofisi ya Rais, TAMISEMI (*TARURA*) na sisi tuko katika hatua za mwisho kuhakikisha kwamba hiyo fedha tunaipata ili tulete na turekebishe barabara hiyo, kwa hiyo, hayo ndiyo majibu.

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David Mbunge wa Same Magharibi, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Zainab Athman Katimba.

Na. 284

Bajeti ya Barabara Wilaya ya Same

MHE. ZAINAB A. KATIMBA K.n.y. MHE. DKT. DAVID M. DAVID aliuliza:-

Je kwa nini Serikali haitengi fedha za *TARURA* kwa kuzingatia jiografia, ukubwa wa eneo na mazingira ya Wilaya au Jimbo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA ZA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu: -

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Jimbo la Same Magharibi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, *TARURA* inaendelea na zoezi la uandaaji wa *formula* itakayotumika kwenye ugawaji wa rasilimali fedha zinazohitajika kwenye ujenzi na matengenezo na miundombinu ya barabara kulingana na mahitaji ya eneo husika. *Formula* itazingatia ukubwa wa mtandao wa barabara (*road network*), thamani ya miundombinu ya barabara iliyopo (*asset value*), hali ya barabara (*road condition*), wingi wa magari (*traffic volume*), idadi ya wakazi (*population*), mazingira (*geographical terrain*), kiwango cha mvua (*annual rainfall*) na kilimo (*agriculture potential*).

SPIKA: Mheshimiwa George Mwenisongole swali la nyongeza.

MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Napenda kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa mfano jimbo lake lile la Tunduma, linaingia mara sita kwa jimbo langu, lakini wote tunapata fedha sawa za mgao wa barabara, sasa haoni kama hiyo siyo sawa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Mwenisongole, Mbunge wa Jimbo la Mbozi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli ukichukulia Jimbo la Mbozi, ukifananisha na Jimbo la Tunduma, Jimbo la Mbozi ni kubwa zaidi kuliko Jimbo la Tunduma na utaratibu ambao ulikuwa unatumika mwaka uliopita ni utaratibu ambao tulikubaliana wote Wabunge humu ndani na ndiyo maana sasa hivi

tunarekebisha hiyo *formula* ili majimbo yote yapate kulingana na ukubwa wa eneo na mahitaji ya eneo husika. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kutoa pesa nyingi kwa ajili ya miradi ya barabara hizi zinazosimamiwa na *TARURA*, bado miradi mingi kwenye maeneo imesimama au inasuasua ikiwemo Jimbo la Ukerewe kwa sababu wakandarasi ama kutokuwa na uwezo au kuwa na mrundikano wa kazi nyingi.

Nini kauli ya Serikali juu ya hali hii?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joseph Mkundi, Mbunge wa Jimbo la Ukerewe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kauli ya Serikali katika maeneo yote ambayo wakandarasi hawafanyi vizuri ni kuhakikisha kwamba wanamaliza ndani ya muda kwa sababu tumetoa muda kamili wa kufanya ile kazi.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, kama kuna maeneo ambayo wakandarasi wamekuwa hawatekelezi kabisa wajibu wake tunaomba maeneo hayo mtuletee sisi ofisi ya Rais - TAMISEMI kupitia *TARURA*, ili tuweze kuchukua hatua zikiwemo kuvunja mikataba kwa sababu wanachelewesha hizo kazi. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anaongea na Mameneja wa *TARURA* nchini, alisema kuna

mikoa kama Njomba na Mbeya ambayo hali ya barabara ni mbaya lakini ni mikoa ya uzalishaji, *TARURA* lazima muwape kipaumbele kuwapa fedha; kwa mfano Makete, hali ya barabara ni mbaya.

Ni lini mtaongeza fedha kwa ajili ya mikoa hii ya uzalishaji katika Taifa letu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Festo Sanga, Mbunge wa Makete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuonesha kwamba Serikali inazingatia maeneo yenye uzalishaji mkubwa ndiyo maana utaona katika hizo nyanda ambazo Mheshimiwa Mbunge ameziainisha kuna miradi maalum ikiwemo miradi ya *RISE* ambayo haiko maeneo mengine, lakini iko katika maeneo ambayo yanazalisha. Tumepeleka huko ili kuongeza fedha nyingi kwa ajili ya uzalishaji katika maeneo hayo. Kwa hiyo, hilo ndiyo jibu sahihi, sio tu fedha za *TARURA*, ni pamoja na miradi husika. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum sasa ulize swali la ke.

Na. 285

**Mafunzo kwa Maafisa Masuuli na Wahasibu
katika Halmashauri**

MHE. GRACE V. TENDEGA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Maafisa Masuuli na Wahasibu katika Halmashauri wanapata mafunzo juu ya uandaaji wa taarifa za fedha za mwisho za halmashauri?

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetoa mafunzo kwa jumla ya watumishi 210 juu ya uandaaji wa taarifa za fedha za mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2022. Mafunzo hayo yametolewa kwa watumishi waliopo ngazi ya mikoa na halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha Mwongozo wa Uhasibu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa wa mwaka 2020 (*Local Authority Accounting Manual*) na Waraka wa Ufungaji Hesabu kila mwaka. Maboresho hayo yanakusudia kuzikumbusha taasisi za umma juu ya mambo ya msingi ya kuzingatia na kuwaongoza Maafisa Masuuli na Wahasibu katika kutekeleza majukumu yao ikiwa ni pamoja na uandaaji wa hesabu za mwisho.

SPIKA: Mheshimiwa Grace Tendega swali la nyongeza.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Spika, nauliza maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kutokana na uelewa wangu halmashauri zote zilizo nchini zinatofautiana mapato na Serikali imekuwa ikitangaza tu mafunzo ili halmashauri zijihudumie; je, hamuoni sasa kuna umuhimu wa Serikali kupeleka fedha kwa uwiano sawia?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kumekuwa na mfululizo wa hati chafu ambazo ni zaidi ya miaka kumi mfululizo; je, Serikali haioni kwamba inaendelea kupoteza

fedha za wananchi kwa kutokuwa na watu wenye weledi au ufanisi mkubwa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja ya lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba tunaongeza fedha kwa ajili ya mafunzo na tutazigawa kulingana na uwiano katika halmashauri moja na nyingine, kwa hiyo, hilo ndiyo lengo la Serikali, lengo letu ni kuhakikisha kwamba tunazuia wizi kwa kuwapa mafunzo ya kuweza kuzuia vitendo hivyo vya kihalifu katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, lakini suala la pili kuhusu hati chafu katika maeneo mengi nchini, moja ya kazi kubwa ambayo tumeifanya sasa hivi ni kuhakikisha moja tunawaondoa watu wote wanaosimamia fedha katika maeneo hayo wakiwemo wahasibu, ma-*DT* pamoja na wakurugenzi.

Kwa hiyo, hizo ni hatua ambazo tunachukua, lakini sasa hivi tutakuwa tunaleta watu ambao ni waadilifu katika maeneo yetu na hatutakuwa tunahamisha kama ambavyo ilikuwa awali mtu anafanya tukio baya upande mmoja tunahamisha katika halmashauri nyingine. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Japhet Hasunga swali la nyongeza.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana; kwa kuwa katika halmashauri kwanza Serikali imetoa mafunzo kwa maafisa 210 ambao ni wachache sana ukilinganisha na halmashauri zilizopo hapa nchini mikoa iliyopo; na kwa kuwa uandaaji wa hesabu unahitaji ujuzi na

maarifa maalum ambayo yanatakiwa yatolewe na wafanyakazi wengi wamekuwa hawana maarifa hayo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba Wahasibu pamoja na Wakaguzi wa Ndani wanapatiwa mafunzo wanayostahili katika utayarishaji wa hesabu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mbunge wa Jimbo la Vwawa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana tumejibu hawa tumetoa mafunzo kwa maafisa 210 sasa hivi tumeongeza fedha katika bajeti yetu, kuhakikisha tunawafikia watu wote wa vitengo, wahasibu pamoja na wakaguzi wa ndani ili kuhakikisha kwamba sasa wanafanya kazi ambayo imekusudiwa. Kwa hiyo, fedha zimeongezeka na mwakani tutafanya hivyo kwa watu wote wa idara hiyo.

SPIKA: Mheshimiwa Simon Songe, swali la nyongeza.

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sheria za uandaaji wa hesabu zimekuwa zimekubadilika mara kwa mara kulingana na mahitaji ya kimataifa; je, sasa Serikali haioni ni wakati sahihi sasa wa kutenga fungu rasmi kwa ajili ya hawa wahasibu ili wakaweze kuhudhuria *classes* za *NBAA*?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Simon Songe, Mbunge wa Jimbo la Busega kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali tutaendelea kutenga fedha kadri inavyopatikana lakini kwa sasa tutaendelea na mafunzo ili kuhakikisha kwamba haya yanayotokea sasa hayaendelei. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, sasa aulize swali lake.

Na. 286

Kuwalipa wananchi wanaopanda misitu kupunguza hewa ukaa-Kilolo

MHE.JUSTIN L. NYAMOGA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuomba fedha katika mifuko ya kupunguza hewa ukaa duniani na kuwalipa wananchi wanaopanda na kutunza misitu katika Wilaya ya Kilolo?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira Mheshimiwa Seleman Jafo majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Justine Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, Mbunge wa Kilolo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hewa ukaa ni moja ya gesijoto ambazo mrundikano wake angani husababisha mabadiliko ya tabianchi. Moja ya njia zinazotumika kupunguza hewa ukaa chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko

ya Tabianchi ni misitu ambayo hunyonya hewa ukaa wakati mimea inapotengeneza chakula.

Mheshimiwa Spika, Mkataba huo hauna mfuko mahsusi wa kulipa miradi ya uhifadhi ya misitu inayotekelezwa katika nchi wanachama zinazoendelea kwa ajili ya kupunguza hewa ukaa. Badala yake mkataba huo umeweka utaratibu wa kibiashara ambapo makampuni kutoka nchi zilizoendelea ambazo zinawajibika chini ya mkataba huo kupunguza gesijoto hulipa miradi ya kupunguza hewa ukaa kupitia hifadhi ya misitu katika nchi zinazoendelea. Mfano wa kampuni kutoka nchi zilizoendelea ni *Carbon Tanzania* kutoka Uingereza ambayo hugharamia miradi ya MKUHUMI katika mikoa ya Manyara na Katavi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ongezeko kubwa la wadau wanaotaka kufanya biashara hii, Ofisi ya Makamu wa Rais inaandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Biashara ya Hewa Ukaa utakaotumiwa na wawekezaji, taasisi, watu binafsi na kadhalika wenye nia kufanya biashara hii hapa nchini.

SPIKA: Mheshimiwa Justin Nyamoga, swali la nyongeza.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru; katika Kata ya Kimara na Kata ya Idete yupo mwekezaji ambaye ni Kampuni inaitwa *Odzungwa Corridor* na yeye anafanyakazi ya kupanda miti kwa ajili kuja kuvuna hewa ya ukaa miaka ijayo.

Sasa je, Serikali haioni umuhimu wa kuzungumza naye ili aweze pia kushirikisha misitu iliyopo tayari ili huo uvunaji uweze kuanza na malipo yaweze kufanywa kwa sababu ipo miti ambayo iko tayari?

Lakini swali la pili; moja kati ya lengo la kuwepo kwa misitu kimsingi ni hifadhi ya mazingira na hivi karibuni bei za mazao ya misitu hususan mbao imeshuka sana na kama inakatisha tamaa wakulima kuendelea kulima miti na baadaye tutapata madhara makubwa.

Ni nini kauli ya Serikali kuhusu tatizo hili ambalo linaweza likawa na matatizo makubwa baadaye? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, majibu.

WAZIRI WA NCHI. OFISI YA MAKAMU WA RAIS MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la ndugu yangu Justin Nyamoga Mbunge wa Kilolo kama ifuatavyo:-

Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa sababu kwa mara kadhaa alikuwa akizungumzia hoja ya upandaji wa miti wa kibiashara hususan katika wilaya yake ya Kilolo na Mkoa mzima wa Iringa pamoja na Mkoa wa Njombe wanavyojihusisha na upandaji wa miti.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ajenda ya huyu mkulima ambayo analima hii miti ni kama tunavyosema kwamba tumeandaa mwongozo sasa, mwongozo huu uta-*address* suala zima la uhifadhi wa mazingira na watu mmoja mmoja mara baada ya mwongozo huu watapewa maelekezo jinsi gani ya kushiriki vyema kwa ajili ya kupata utajiri mkubwa kupitia suala la misitu. Kwa hiyo, afanye subira tu nadhani kwa malengo yake yanaendana pamoja na mkakati wa Serikali tunaoendelea nao.

Mheshimiwa Spika, lakini suala zima misitu, thamani ya miti inashuka, basi niseme kwamba katika hilo kwetu sisi upande wa Mazingira tuseme kwamba hiyo ni fursa sasa kwa wale ambao wanaopanda miti ambao kesho na keshokutwa biashara hii hewa ya ukaa itapokuwa kubwa tutaenda kufanya mambo mawili; kwanza kutunza mazingira, lakini jambo la pili vilevile kuhakikisha kwamba tunakabiliana na mabadiliko ya tabianchi lakini kikubwa zaidi kuhakikisha tunapeleka utajiri wa mtu mmoja mmoja kupitia ajira ya misitu, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Asya swali la nyongeza.

MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi; kwa kuwa utunzaji wa misitu iwe ya mikoko ama ya kawaida husaidia sana katika utunzaji wa mazingira.

Swali langu kwa Serikali; je, Serikali ina mpango gani wa kuvitambua vikundi vyote vinavyojitolea kwa maksudi katika utunzaji wa mikoko hasa kwa upande wa Zanzibar?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la dada yangu Asya, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Zanzibar kama ifuatavyo:-

Kwanza nipongeze vikundi vyote ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bara na Visiwani wanajihusisha katika ajenda ya mazingira jambo hilo ni jambo jema sana na sisi kama Serikali jukumu letu kubwa ni kuwatambua. Lakini si kuwatambua peke yake, juzi juzi tulikuwa na mkutano kule Belgium katika miradi maalum inayosemwa miradi ya hewa ukaa na miongoni mwa ajenda kubwa jinsi gani vikundi hivi vidogo vidogo vinavyochipua katika ajenda ya mazingira baadaye vifanyiwe utaratibu maalum wa uwezesaji kwa ajili ya ajenda ya kulinda mazingira, lakini ajenda ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo jambo hilo ni jukumu letu Ofisi ya Makamu wa Rais tutaendelea kulifanya na kama mnavyoona bajeti yetu iliyopita imelenga vilevile katika suala zima la *capacity building* katika makundi na vikundi mbalimbali hilo ni jukumu letu tutaenda kulifanya kwa upana mkubwa zaidi ikiwemo Zanzibar. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara swali la nyongeza.

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri; je, Serikali ina mpango gani wa kuwatumia vijana waliohitimu masomo ya

environmental science katika kusaidia kueneza elimu hii ya kupunguza hii hewa ya ukaa?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, majibu.

WAZIRI WA NCHI. OFISI YA MAKAMU WA RAIS MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la mama yangu Daktari Thea Ntara kutoka Mkoa ule wa Ruvuma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli sasa hivi tuna vijana wengi sana wamehitimu *environmental science* katika vyuo mbalimbali ikiwepo Dar es Salaam, SUA pamoja na *University of Dodoma* na vyuo vingine.

Mheshimiwa Spika, na ndiyo maana katika ajenga hiyo kikubwa zaidi tunachokifanya ni kwamba si rahisi Serikali ikaajiri watu wote, lakini tumeweka suala zima la kuleta hamasa katika makundi mbalimbali hasa kutumia vijana hawa na hasa wakati fulani nilipokuwa katika mkutano pale Dar es Salaam, mkutano unaohusiana na masuala ya mabadiliko ya tabia nchi tulitoa maelekezo katika *NGOs* mbalimbali sasa zifungue milango kwa vijana waliosoma *environment science*. Hata kuwapa *internship* au mikataba ya muda mfupi kwa lengo kubwa vijana hawa waweze kutumia kiupana zaidi kwa ajili ya Taifa letu hili.

Mheshimiwa Spika, imani yangu maelekezo yale tuliyoyatoa katika taasisi mbalimbali wenzetu wataenda kuyazingatia kwa lengo kubwa vijana hawa waweze kutumika kwa mustakabali wa nchi yetu katika utunzaji wa mazingira.

SPIKA: Haya ahsante sana, Mheshimiwa Ramadhan Ramadhan swali la nyongeza.

MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza; kwenye majibu yake Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba

wapo kuandaa mwongozo utakaoruhusu wawekezaji kuja kuwekeza kwenye kupunguza makali ya hewa ya ukaa; ni lini mwongozo huo utakamilika?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, majibu kwa kifupi.

WAZIRI WA NCHI. OFISI YA MAKAMU WA RAIS MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, ni kwamba kwanza nimshukuru Mheshimiwa Ramadhan na nilijua kama ni miongoni wa vijana machachari na hata mwaka huu wanawezekana wakaenda kutuwakilisha kule Misri katika ajenda ya mabadiliko ya tabia nchi.

Mheshimiwa Spika, katika upande huo Serikali ni kama nilivyosema ni kwamba mwongozo huu uko katika hatua za mwisho, takriban mwezi mmoja uliopita tulikuwa katika kile kituo cha *Carbon Tanzania* ambacho sisi tumeki-center pale *University of Sokoine Morogoro*, tulikuwa na kikao hicho imani yetu ni kwamba mwanzoni mwa mwaka wa fedha unaokuja maana yake kuanzia Julai kwenda hapa mbele si muda mrefu mpango huo utaweza kukamili ili mradi kwamba watu waweze kushiriki katika ajenda hii kubwa ya kibiashara.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri itakapotokea umeteua watu halafu umemuacha Mheshimiwa Ramadhan Ramadhan umesemea humu Bungeni kwa hiyo, naamini jina lake lipo huko unakoteua majina. (*Makofi*)

Mheshimiwa Hamad swali la nyongeza.

MHE. BAKAR HAMAD BAKAR: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana mimi nilitaja kujua tu kwamba je, Wizara hii ya Muungano na Mazingira ni kwa kiasi gani inashirikiana na Wizara ya Makamu wa Kwanza wa Rais ambayo pia nayo inashughulikia masuala ya mazingira katika kukabiliana na suala hili la changamoto ya gesi ukaa au hewa ukaa?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais ina *deal* na masuala ya Muungano Bara na Visiwani, lakini masuala ya mazingira upande wa Zanzibar ni chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Hata hivyo tunafahamu kwamba ajenda ya mazingira ni ajenda mtambuka haina mipaka, ndiyo maana muda wote tumeweza kushirikiana vya kutisha kabisa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na ndiyo maana hata ukiangalia miradi mingine tunayoandika katika bajeti yetu Madam Maryam pale Mbunge wa Pandani anafahamu kwamba katika jambo tulijadili katika kikao chetu katika Kamati yetu ya Bunge, miongoni mwa mambo jinsi gani miradi mbalimbali inaenda mpaka kule Zanzibar na hata hivyo ndiyo maana leo hii tuna miradi Kaskazini A, na hata mradi wa Sepwese pale tunaenda kujenga ukuta pale hii yote ni suala zima la mpango wa pamoja jinsi gani tunashughulika na ajenda ya mazingira katika maeneo yetu.

SPIKA: Haya ahsante sana Mheshimiwa Soud swali la nyongeza.

MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mie kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa misitu mingi ipo katika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa; je, kuna utaratibu gani wa Serikali kuzihamasisha taasisi za Serikali kuweza kushiriki katika biashara hii ya hewa ukaa?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu kwa kifupi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la kaka yangu Mheshimiwa Soud mimi namuita *encyclopedia* ya mambo ya mazingira kwa sababu amebobea sana katika mambo ya mazingira katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni kwamba kama tulivyosema ni kwamba katika kushirikisha taasisi hizi hata sasa hivi ukiangalia kwa mfano *TFS* wana misitu mingi sana, lakini bado hawajanufaika katika hewa ya ukaa, ni halmashauri ya Katavi peke yake na kule kama tulivyosema Simanjiro ambao wao kwa mwaka ile *own source collection* katika hewa ya ukaa ni kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ndiyo maana tumeweka mwongozo kwa lengo kubwa ni kwamba taasisi kwa mfano *TFS*, vijiji vyetu, halmashauri zetu na watu binafsi waweze kushiriki vizuri katika hewa ya ukaa. Kwa hiyo ndiyo jambo ambalo tuliona kulikuwa na *gap* hapo tunaenda kuya-*address gap* hii kwa lengo kubwa ni kwamba kujenga uchumi wa nchi yetu katika suala zima la hewa ya ukaa.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya habari Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo Mbunge wa Muleba Kusini sasa aulize swali lake.

Na. 287

Hitaji la Minara ya Mawasiliano katika Wilaya ya Muleba

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga minara ya mawasiliano katika Kata za Karambi, Mubunda, Ngenge na Rutoro katika Wilaya ya Muleba?

SPIKA: Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi kwa niaba ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) K.n.y. WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo Mbunge wa Muleba Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi Disemba, 2021 Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ilifanya tathmini ya upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya simu katika Kata za Karambi, Mubunda, Ngenge na Rutoro.

Mheshimiwa Spika, Kufuatia tathmini hiyo, kata tajwa zilibainika kuwa na changamoto ya upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya simu na hivyo zimejumuishwa katika zabuni inayotarajiwa kutangazwa kabla ya mwaka wa fedha 2021/2022 kukamilika, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, swali la nyongeza

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri yenye kutia matumaini kwenye hizi kata ambazo kwa kweli zina changamoto kubwa ya mawasiliano.

Je, niombe kupata *commitment* ya Serikali ni lini sasa kama zimetwa kwenye mpango, ujenzi wa minara hii utafanyika kwa ajili ya hizo kata tajwa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi kwa niaba ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) K.n.y. WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya

Habari napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo Mbunge wa Muleba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi minara hii itaanza kujengwa kwa mujibu wa sheria kwa kuwa tutatangaza kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha huu, kwa hiyo, tunaamini mchakato umeshaanza na mara mzabuni atakapoanza basi minara hii itaanza kujengwa kufuata na taratibu za manunuzi ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Vunjo sasa aulize swali lake.

Na. 288

Ujenzi wa Soko la Lokolova

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa soko la Kimataifa katika eneo la Lokolova mpakani mwa Tanzania na Kenya?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exaud Kigahe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA, alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Vunjo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Moshi imetenga eneo lenye ukubwa wa ekari 140

katika eneo la Lokolova kwa ajili ya ujenzi wa soko la mpakani. Hatua inayofuata ni kupata hati miliki ya eneo hilo na hatimaye kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya soko hilo, nakushukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, swali la nyongeza.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Je, Mheshimiwa Waziri atakubali kuongozana nami kutembelea eneo hili ili aone umuhimu wake na fursa zilizopo kwa kuongeza ajira na biashara kwenye ukanda huu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki?

Mheshimiwa Spika, la pili; kwa vile Serikali imeanza sasa kuboresha mazingira ya machinga huku mjini kwa kuwajengea maeneo mazuri na kuwawekea mapaa kwenye biashara zao.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwezesha wanawake, akinamama, mabinti zetu kule kwenye vijiji ambao wanaenda kwenye magulio kama yale ya Mwika, Kisambo, Marangu, Lyamombi, Kinyange wakinyeshewa mvua mazao yao yakiharibiwa kwakati mvua zinaponyesha ni pamoja na kupigwa na jua kali.

Je, Serikali haioni haina mkakati wa kuwajengea mapaa angalau kwenye maeneo machache kwenye masoko haya? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara majibu.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Charles Kimei Mbunge kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Dkt. Kimei kwa ufuatiliaji kwa ajili ya maendeleo ya Jimbo la Vunjo amekuwa akifuatilia sana kuhusiana na ujenzi wa masoko.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu kuongozana nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya Bunge hili tutapanga na tutaongozana ili tuweze kutembelea maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuhamasisha maendeleo katika Jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili ni kweli Serikali inapambana kuhakikisha tunaweka miundombinu wezeshi ikiwemo masoko, maeneo ya kuuzia bidhaa mbalimbali hasa kwa wanawake, vijana na wamachinga na hii Serikali imeshaanza kupitia TAMISEMI kujenga mabanda na kuzeka maeneo mbalimbali ambayo yanatumika kama masoko ili kuhifadhi bidhaa wakati wa mvua na jua ili wakinamama wafanyabiashara waweze kufanyakazi. Naomba halmashauri waweze kufanya hivyo ili kuhakikisha bidhaa hizo zinatunzwa na kuuzwa katika mazingira mazuri, nakushukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 289

Mazingira Wezeshi ya Kupata Mbegu Bora za Malisho pamoja na Mitamba

MHE. SHALLY J. RAYMOND aliuliza:-

Je, kuna mipango gani ya kuweka mazingira wezeshi ya kupata mbegu bora za malisho kama Luseni pamoja na kuwezesha uzalishaji wa mitamba?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shally Josepha Raymond Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuimarisha mashamba yake ya kuzalisha mbegu za malisho kwa kuyapatia vitendea kazi na kuongeza ukubwa wa maeneo ya kuzalisha mbegu za malisho na malisho.

Aidha, nitumie fursa hii kuendelea kuihamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa mbegu za malisho na malisho kibiashara ili kukidhi mahitaji ya ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha uzalishaji wa mitamba, mpango wa Serikali ni kuendelea kuyaimarisha mashamba yake ya kuzalisha mitamba ya kituo cha kuzalisha mbegu za mifugo kwa ajili ya uhimilishaji cha *NA/C*- Arusha ili kuzalisha na kusambaza mitamba na mbegu bora za ng'ombe kwa gharama nafuu.

SPIKA: Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Spika, ahsante sana nashukuru kwa majibu haya mazuri; lakini kwa kuwa Serikali imeelemewa sana na jambo hili, ina mpango gani sasa au ina vivutio gani kwa sekta binafsi kuzalisha mbegu hizo za malisho pamoja na kuzalisha madume bora ya mbegu? (*Makofi*)

Swali la pili kwa kuwa kuna uhitaji mkubwa sana wa mitamba bora, mbuzi mapacha, pamoja na vifaranga vya kuku vilivyoboreshwa kwa wanawake wa Mkoa wa Kilimanjaro ambao wanasubiri kwa muda mrefu hata wakati wa kampeni walimuomba Waziri Mkuu alipokuja kufungua kampeni ya Mkoa wa Kilimanjaro. Serikali iko tayari sasa kutoa vitu hivyo kwa ruzuku kwa wanawake hao?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge Shally Josepha Raymond Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza ni juu ya vivutio tulivyoviweka; Serikali imejipanga mara baada ya kupokea maoni ya wadau juu ya kuweza kuweka vivutio kwenye upande wa uzalishaji wa mbegu za malisho, lakini na upande wa uzalishaji wa ng'ombe bora kwa maana ya madume ya mbegu kwa kuondoa baadhi ya tozo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ng'ombe bora Serikali imeondoa tozo ya *import* ya ng'ombe wanaotoka nje ya nchi tulikuwa tukilipisha shilingi 10,000 kwa ajili ya ng'ombe kumkagua na sasa Wizara imependekeza kuondolewa kwa tozo hii na bado tupo katika mazungumzo ndani ya Serikali ya tozo kwa upande wa mbegu za kutoka nje za malisho ili kusudi na zenyewe ikiwezekana ziweze kuondolewa ile tozo na wawekezaji waweze kuweza kufanya kazi hii kwa ufasaha.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni juu ya jambo linalohusu Mkoa wa Kilimanjaro na akinamama kupata ng'ombe wa ruzuku. Katika mwaka huu wa fedha 2022/2023 Serikali imejipanga kuyaimarisha mashamba ya uzalishaji wa ng'ombe bora na ili tuweze kuwasambaza kwa wafugaji kote nchini. Nina imani kuwa akinamama wa Mkoa wa Kilimanjaro watakuwa ni miongoni mwa wanufaika, ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Neema Mgaya swali la nyongeza.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi; Serikali ina mpango gani wa kuimarisha Shamba la Mifugo la Kitulo wilaya ya Makete na shamba la mifugo la *Sao Hill* Iringa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Neema Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Njombe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 tumedhamiria kuhakikisha kwamba tunaimarisha mashamba yetu matano likiwemo hili la Kitulo na lile la Mabuki na *Sao Hill* ambayo tutayaongezea zana za kazi kama vile matrekta na zana zile za kuweza kuvunia majani kwa maana ya malisho, lakini pia vilevile kwa kuyaongezea ng'ombe wazazi bora ili tuweze kuzalisha zaidi ya ng'ombe 3,500 na kuwasambaza nchini kote, kwa hivyo, mpango huu tunao na tunaelekea katika kuutekeleza, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Nishati Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mbunge wa Msalala sasa aulize swali lake.

Na. 290

Kuanzisha Mkoa wa *TANESCO* – Kahama

MHE. IDDI K. IDDI aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanzisha Mkoa wa *TANESCO* katika Wilaya ya Kahama na kujenga Ofisi ya *TANESCO* Halmashauri?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Stephen Lujwahuka, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mbunge wa Msalala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* imekuwa ikifungua Ofisi za Mikoa na Wilaya katika maeneo mbalimbali nchini kwa kuzingatia mahitaji na vigezo muhimu ikiwa ni pamoja na Wilaya, ongezeko la wateja, ukubwa wa mtandao na miundombinu ya umeme katika maeneo husika. Katika Halmashauri ya Mji wa Kahama ipo Ofisi ya *TANESCO* ya Wilaya ya Kahama inayotoa huduma kwa wananchi wa Mji wa Kahama pamoja na Halmashauri za Msalala na Ushetu.

Mheshimiwa Spika, katika hatua ya kusogeza huduma zaidi kwa wananchi, *TANESCO* imefungua Ofisi ndogo yaani *Sub Offices* katika maeneo ya Nyamilangano, Ilogi na Isaka. *TANESCO* inaendelea kuongeza Ofisi ndogo nyingine katika maeneo ya Segese, Bulungwa, Bulige na Chambo pamoja na kuongeza watumishi, magari na majengo. *TANESCO* inaendelea na tathmini ya mahitaji na vigezo kwa ajili ya kufungua Ofisi ngazi ya Mkoa katika Mji wa Kahama.

SPIKA: Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, swali la nyongeza.

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Spika, kwanza niseme tu kwamba sijaridhika na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu hata maeneo ambayo ameyataja hapa kwamba yamejengewa ofisi kwa mfano mimi kwenye Jimbo langu hakuna kata inayoitwa Bulungwa wala Chambo.

Sasa Mheshimiwa Waziri niseme kwamba ni lini sasa mtaanzisha ofisi hizo ambazo wewe umezitaja hapa ikiwemo Kata ya Isaka, Kata ya Segese, Kata ya Bulige na Kata ya Jana? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili la nyongeza wakati mnaendelea kufanya upembuzi yakinifu au tathmini, Mheshimiwa Waziri alifanya ziara kwenye Halmashauri ya Msalala na tukampatia kiwanja na tofali 1000 na akaahidi kujenga ofisi kwenye Halmashauri ya Msalala.

Sasa ni lini Serikali mtaanza ujenzi wa ofisi ya Wilaya kwenye Halmashauri ya Msalala? Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mbunge wa Msalala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nikianza na swali la pili la ni lini Serikali itaanza kujenga ofisi; kama tulivyoeleza kwenye jibu la msingi *TANESCO* inaendelea na tathmini mahitaji ya vigezo kwa ajili ya kufungua ofisi hiyo, kwa hiyo tathmini itakapokamilika mara moja mahitaji yakabainika ni kwa kiasi gani basi itaamuliwa ijengwe hiyo ofisi kwa mazingira yatakayo kuwepo.

Mheshimiwa Spika, lakini kweli swali la kwanza kwamba ofisi hazijafunguliwa; kwa sababu ya uhaba wa watumishi tuliokuwa nao na kwa sababu ya ufinyu wa bajeti ya kujenga majengo yetu katika maeneo yote wenzetu wa *TANESCO* walianzisha utaratibu wa kufanya *visiting offices* ambazo ni katika haya maeneo ya hizo ofisi ndogo tukiazima maeneo ya ofisi za kata.

Kwa hiyo, maeneo haya hautaenda na kukuta jengo limejengwa lakini tunapata vyumba kwenye ofisi za watendaji wa Kata na tunaanza kuhudumia watu kutokea kwenye maeneo hayo, wakati Serikali ikiwa inajihimu kuongeza bajeti kwa ajili ya kuweza kujenga majengo hayo kwenye maeneo yote yanayohitajika. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Moja ya sababu za kujenga ofisi na kupeleka vifaa ni pamoja na kuhakikisha huduma ya *TANESCO* inakuwepo kwa wananchi; sasa pale Halmashauri ya mji wa Bunda tuna ofisi

lakini bado hamjaweza kutoa huduma stahiki ya umeme, watu wameomba maombi ya umeme, wana *control number*, lakini mpaka leo hawajaunganishiwa umeme.

Ni lini mtahakikisha huduma bora inaenda kwa wananchi na sio tu ofisi peke yake?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika bajeti tutakayoisoma hapa siku chache zijazo itaoneshwa ni kwa kiasi gani Serikali ya Awamu Sita imejipanga kuwahudumia wananchi kwa kuongeza fedha kiasi zaidi ya bilioni 500 kwa ajili ya kupeleka huduma kwa wananchi. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya siku mbili ataona neema iliyoshushwa na Mheshimiwa Rais kupitia Wizara ya Nishati. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya Wizara ya Nishati kuweka yale mabanda pale ya maonesho, mimi nilipata picha kwamba Wabunge mtakuwa mmetumia fursa ile kwenda kupata majibu kwenye maeneo yenu. *(Makofi)*

Lakini sasa mnavyokuwa bado mna maswali mengi humu ndani nashindwa kuwaelewa kwamba wale Mameneja wa Mikoa, wa Wilaya wote walishindwa kutoa majibu wakati huo.

Kwa hiyo Waheshimiwa pia tuwe tunatumia fursa tunazoletewa hapa Bungeni ili wananchi wetu waweze kupata uwakilishi mzuri. *(Makofi)*

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, Mbunge wa Muhambwe swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Aloyce Kamamba.

Na. 291

Hitaji la Vitambulisho vya *NIDA* – Mkoa wa Kigoma

MHE. ALOYCE J. KAMAMBA K.n.y. MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa Vitambulisho vya *NIDA* kwa wananchi wa Mkoa wa Kigoma hususan Jimbo la Muhambwe?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, Mbunge wa Muhambwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imesajili jumla ya wananchi 975,844 katika Mkoa wa Kigoma wakiwemo wananchi wa Jimbo la Muhambwe na jumla ya vitambulisho 123,962 vimezalishwa kwa ajili ya wananchi wa mkoa huo.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Muhambwe ambalo liko katika Wilaya ya Kibondo, wananchi 139,588 walitambuliwa na vitambulisho 5,126 vilitolewa na kugaiwa kwa wananchi. Serikali inatarajia kukamilisha utoaji wa vitambulisho kwa wananchi wote wenye sifa katika mwaka wa fedha 2022/2023. Nashukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Aloyce Kamamba swali la nyongeza.

MHE. ALOYCE J. KAMAMBA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, bado kwa takwimu Mkoa wa Kigoma una zaidi ya wananchi 2,000,000 lakini waliotambuliwa ni 975,844 na waliopata vitambulisho ni 123,962 sawa na asilimia 12 tu. Jibu lake anasema kwamba mwaka huu watapewa vitambulisho; sasa swali nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba wananchi wote wanaostahili ambao wako katika Mkoa wa Kigoma wanapata vitambulisho vya *NIDA*?

Mheshimiwa Spika, la pili; wananchi wa Wilaya ya Kakonko muda mwingine wanaombwa vitambulisho ambavyo ni vya *NIDA* ambavyo hakika Serikali inajua kwamba haijavitoea kwa wananchi hao, mpango ukoje kuhakikisha kwamba wananchi wa Wilaya ya Kokonko sasa wanapata vitambulisho vya *NIDA*? Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kamamba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwa takwimu hizo idadi ya waliopata vitambulisho ni ndogo sana, lakini kama ilivyoelezwa wakati nawasilisha bajeti hapa kulikuwa na changamoto ya kimkatiba kati ya Serikali na mzabuni, na hivyo karatasi za kutolea vitambulisho hivi hazikuwepo, lakini tatizo hilo limeondolewa, tumeshahuisha mkatiba na ndio maana tunauhakika kwamba kwa mwaka ujao wa fedha tutatatua tatizo hilo kwa wale wote waliotambuliwa na kusajiliwa na wale wapya tutakaokuwa tunaweza kutawambua na kuwasajili, nashukuru kwa swali la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kuhusu kugawa vitambulisho kama nilivyosema kwenye jibu la msingi linahusiana moja kwa moja kwa mwaka ujao tunauhakika wananchi wale ambao wameshatambuliwa watapewa vitambulisho na wale wapya watakaokuwa wanaendelea kutambuliwa watapewa vitambulisho, nashukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Asia Halamga swali la nyongeza.

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi; kwa kuwa kuwa na kitambulisho cha Taifa ni haki ya kila Mtanzania, je, ni nini kauli ya Serikali kwa wafungwa na maabusu wa muda mrefu juu ya kupatiwa huduma hii?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asia Halamga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ni haki la kila raia kupata kitambulisho, lakini kwa hawa ambao wamefungwa sidhani kama kuna dharura ya kiasi hicho, kwa sababu hawa wapo jela vitambulisho vinatakiwa kwa ajili ya kupata huduma mbalimbali ikiwemo elimu, mikopo, safari, *passport* na kadhalika, sasa huyu mfungwa tuhangaikie kumpa kitambulisho anakwenda kukitumia wapi. Lakini tuahidi atakapokuwa amemaliza kifungo chake akirudi uraiani atatambuliwa na kupewa kitambulisho kama inavyopaswa, nashukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Anastazia Wambura, swali la nyongeza.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi; moja ya changamoto ambayo inayopelekea kuchelewa kuwapa vitambulisho vya *NIDA* wananchi wa Mkoa wa Mtwara ni pamoja na uhaba wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

watumishi; je, Serikali imejipanga vipi kuondoa changamoto hii? Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI: Mheshimiwa Spika samahani walipiga makofi kile alichouliza sikukipata vizuri hiyo changamoto alisema ni kitu gani ili niweze kumjibu kwa ufasaha.

SPIKA: Mheshimiwa Anastazia Wambura.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Spika, nakushukru kwa kunipa nafasi, ya kurudia.

Ni kwamba moja ya changamoto ambayo inayopelekea kuchelewa kutoa vitambulisho vya *NIDA* katika Mkoa wa Mtwara ni uhaba wa watumishi.

Je, Serikali imejipanga vipi kuondokana na changamoto hiyo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anastazia Wambura kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye majibu ya maswali yaliyopita, kwa kweli changamoto sio idadi ya watumishi changamoto ilikuwa ni kukosa vitendea kazi vilivyokuwa vimesababishwa na kukwama kwa mkataba, sasa baada ya suala la mkataba tumeshalitua bila shaka ataona kasi ya utoaji wa vitambulisho kule Mtwara inatatuliwa, lakini pale itakapoonekana kwamba shida ni watumishi Serikali itaendelea kuajiri watumishi wanaohitajika ili kutekeleza majukumu yako ya utoaji wa vitambulisho itasavyo.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, Mbunge wa Kalenga swali hili Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka lilikuwa ni swali ambalo aliluzwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na lilielekezwa litajibiwa na Serikali na sekta inayohusika Mheshimiwa Jackson Kiswaga sasa uliza swali lako.

Na. 292

Ujenzi wa Vituo vya Polisi katika Mahakama za Kata Nchini

MHE. JACKSON G. KISWAGA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga vituo vya polisi katika Mahakama za Kata nchini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimwa Jackson Gedion Kiswaga Mbunge wa Kalenga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuwa na vituo vya polisi kila kata na ndio maana imeanzisha utaratibu wa Polisi Kata inayoongozwa na Mkaguzi wa Polisi. Ujenzi wa vituo hivyo utaendelea kufanyika kwa awamu kutegemea upatikanaji wa fedha. Vituo hivyo hutumiwa na mahakama zilizoko kwenye kata husika pindi vinapohitajika, nashukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Jackson Kiswaga swali la nyongeza.

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali sasa nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza; swali la kwanza, kwa kuwa katika Mahakama ya Tarafa iliyopo pale Kiponzelo ilishatokea

miaka ya nyuma hapo kwamba wakati mtuhumiwa anasafirishwa kwenda Ifunda alitoroka na kuonesha kwamba kulikuwa hakuna usalama.

Je ni lini sasa Serikali itaanza angalau kujenga vituo hivi vya polisi kwenye maeneo ya Tarafa hasa pale Kiponzelo?

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili Ifunda tuna Kituo cha Polisi kikubwa bahati mbaya hatuna gari wala nyumba za polisi; je, ni nili Serikali sasa itaturekebisha angalau kupata gari hapo Ifunda? Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kiswaga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu mfungwa aliyetoroka kwasababu ya umbali kama nilivyosema katika nyakati tofauti ninapojibu maswali haya kadri tutakapopata fedha tutajenga vituo vya polisi viwe karibu kabisa na maeneo ambayo yanahitajika ikiwemo karibu na Mahakama zilizopo ngazi ya Tarafa na ninajua pia mpango wa Serikali upande wa Wizara ya Katiba na Sheria ni kuweka Mahakama hizi katika kila Kata. Kwa hiyo niendeleo kusisitiza wadau mbalimbali wakiwemo Serikali za Mitaa wadau kama yeye Mheshimiwa Kiswaga mwenyewe ana mpango wa kusaidia kujenga kituo cha polisi, vituo hivi vitakapojengwa tutapeleka askari.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu swali la pili kwamba kuna kituo lakini hakina gari wala nyumba nimeeleza mara kadhaa hapa kulingana na bajeti yetu ya mwaka huu na mkataba tulionao na kampuni ya Ashok Leyand tunayo magari ambayo tutapokea 78 mwezi huu, lakini vilevile hayo magari 78 yameshapokelewa ni taratibu za kuyatoa bandarini lakini mpaka mwezi Septemba tutakuwa tumekamilisha magari 396. Maeneo yenye changamoto

kama haya ya Kalenga yatazingatiwa, nashukuru sana.
(*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge mliosimama niwakumbushe pamoja na kwamba muuliza swali ameingiza hapo habari ya magari, lakini swali la msingi linahusu ujenzi wa vituo vya polisi. Mheshimiwa Hussein Amar swali la nyongeza. (*Makofi*)

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwanza niipongeze Serikali kwa kusikia kilio change cha ujenzi wa Mahakama ya Wilaya katika Wilaya ya Nyang'hwale swali. Ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Gereza la Wilaya ya Nyang'hwale?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hussein Amar kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa gereza la Nyang'hwale kama lilivyooombwa na Mheshimiwa Amar utanza baada ya kuwa tumepata fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi huo, kwa kweli kwa mwaka ujao hatuna bajeti hiyo, lakini tutaingiza kwenye kipaumbele kutokana na mahitaji ya Wilaya ya Nyang'hwale, nashukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga swali la nyongeza.

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA: Mheshimiwa Spika, pamoja na furaha tuliyonayo wananchi kuhusu mambo yaliyotokea Jumamosi huko Mwanza naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. (*Makofi*)

Wakati wenzetu wanang'ang'ania vituo vya Kata vya Tarafa Wilaya ya Kilombero ina Kata 35 na haina Kituo cha

Polisi cha Wilaya; je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Kilombero?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asenga, Mbunge wa Kilombero kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumeshazungumza na Mbunge hiyo changamoto yake ya kituo, lakini tumesema katika maeneo yatakayopewa kipaumbele katika miaka ijayo tukianza na mwaka wa fedha 2022/2023 ni maeneo ya Wilaya ambayo hayana kabisa Vituo vya Polisi. Kwa hiyo matarajio yangu ndani ya mwaka mmoja miwili ijayo tutakuwa tumeanza ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Kilombero kama ilivyoombwa na Mheshimiwa Mbunge.

SPIKA: Mheshimiwa Daniel Baran Sillo swali la nyongeza.

MHE. DANIEL B. SILLO: Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mji wa Bashnet ambao ni Makao Makuu ya Tarafa hauna kituo cha polisi na badala yake polisi hutoka Mji wa Babati ambao ni kilometa 60 na kurudi jioni.

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi katika Mji wa Bashnet ambao ni Makao Makuu ya Tarafa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Daniel Baran Sillo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunatambua baadhi ya maeneo kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge ana uhaba wa vituo umbali wa kilometa 60 ni umbali mkubwa na haukubaliki. Naomba nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaweka kipaumbele kwenye eneo lake ili kuweza kuanza ujenzi wa Kituo hicho cha Polisi, nashukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Phillipo Mulugo swali la nyongeza.

MHE. PHILLIPO A. MULUGO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza kwa Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Waziri mwaka 2017 mimi kama Mbunge na mwananchi wa Kata ya Mpona tulichanga fedha tukaanza kujenga Kituo cha Polisi kata ya mpona na angalau kwa asilimia 80 kimekamilika bado asilimia 20; je, Serikali haioni haja ya kuniongezea fedha kwa ajili ya kufanya *finishing* ya kituo hicho? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza tunawapongeza wananchi waliojitokeza na Mbunge wao kujenga kwa asilimia 80 kituo hicho na kuahidi kulipa kipaumbele. Nitamwelekeza *JGP* katika fungu lake la tuzo na tozo aweze kuweka kipaumbele katika eneo hili ili kuweza kukikamilisha kituo hicho. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge tunaenda Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa,

Mbunge Handeni Mjini na yeye swali lake linajibiwa leo ni swali ambalo lililotolewa Mwongozo hapa kwamba lijibiwe upya. Mheshimiwa Reuben Kwagilwa.

Na. 293

Ujenzi wa Barabara ya Handeni – Kibirashi – Kondoa hadi Singida

MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Handeni Kibirashi, Kondoa hadi Singida kwa kiwango cha lami?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa, Mbunge wa Handeni Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza utekelezaji wa ujenzi wa barabara ya Handeni – Kiberashi – Kibaya – Chemba – Farkwa – Kwa Mtoro hadi Kittimo Singida kwa awamu ambapo mkataba wa mkandarasi wa kujenga sehemu ya Handeni – Mafuleta kilometa 20 ulisainiwa tarehe 11 Aprili, 2022. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Reuben Kwagilwa swali la nyongeza.

MHE. REUBEN N. KWAGILWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kwenye swali hili.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; ni lini sasa Serikali itamkabidhi mkandarasi huyu *site* ili ujenzi uweze kuanza mara moja? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili la nyongeza; barabara ya Handeni – Mziha – Turiani ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa miaka karibia 30.

Je, Serikali haioni kwamba inakikosea Chama cha Mapinduzi kwa kutotekeleza ahadi yake ambayo ipo kwenye Ilani kwa miaka 30 iliyopita? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Reuben Kwagilwa, Mbunge wa Handeni Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii kama nilivyosema kwenye jibu la msingi mkandarasi ameshasaini tangu tarehe 11 Aprili na anaitwa *Hernan Highway Engineering Group Company Limited* na sasa hivi anachofanya ni maandalizi kwa ajili ya kuanza ujenzi. Kwa hiyo, taratibu zitakapokamilika ili akamilishe *site* tutamkabidhi na tutapenda kwa kweli Mheshimiwa Mbunge aweze kuwepo wakati sasa anaanza kazi rasmi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu barabara ya Magole – Mziha – Handeni; Serikali imeeshaanza kwa kipande cha Magole – Turiani na katika mwaka huu wa fedha, fedha imetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi lakini pia kuhakikisha kwamba hii barabara tunaijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa David Kihenzile, swali la nyongeza.

MHE. DAVID M. KIHENZILE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa swali la nyongeza.

Katika bajeti iliyopitishwa hapa siku ya Jumanne tumeona barabara za Mafinga – Mgololo na Nyororo – Mtwango zimo katika bajeti hiyo, lakini pia tumeona barabara mbalimbali, lakini kiwango kilichotengwa kwa mfano barabara ya Mafinga - Mgololo yenye kilometa 78 imetengwa bilioni nne na ile nyingine ya Nyororo – Mtwango imetengwa milioni 400; wananchi wangependa kupata ufafanuzi juu ya kiwango hiki kilichotengwa dhidi ya urefu wa kilometa ni upi ufafanuzi wa Serikali? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Kihenzile swali lako ni la nyongeza umetaja barabara mbili hapo unataka ujibiwe ipi kati ya hizo?

MHE. DAVID M. KIHENZILE: Mheshimiwa Spika, kwa sababu nilitaka anipe jibu la jumla maana kote ukiangalia kiwango kilichotengwa kilometa 78 zimetengwa shilingi bilioni nne, kilometa 40 zimetengwa milioni 400 nataka tu anipe ufafanuzi wa Serikali pengine tutawasaidia na Wabunge wengine ambao pia imetengwa kiasi kidogo ukilinganisha...

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri swali hilo lina takwimu maalum kabisa kwa ajili ya hizo barabara. Sasa unao uhuru wa kujibu hilo swali sasa kama majibu unayo, kama huzikumbuki hizo takwimu sasa hilo swali uje umjibu baadaye. Unao uchaguzi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nitaomba swali hili lije kama swali maalum ili tuweze kulijibu kikamilifu. Ahsante.

SPIKA: Haya ahsante sana Mheshimiwa Maimuna Pathan, swali la nyongeza.

MHE. MAIMUNA A. PATHAN: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya kutoka Masasi – Nachingwea kuelekea Liwale kwa kiwango cha lami? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi...

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi...

SPIKA: Ngoja, ngoja, ngoja Mheshimiwa.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maimuna Pathan, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Lindi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Masasi – Nachingwea kwenda Liwale Serikali imetenga bajeti kwenye bajeti ambayo imepitishwa kuanza na eneo la Masasi kwenda Nachingwea. Kwa hiyo, barabara hiyo tuna hakika itaanza utekelezaji kwa kiwango cha lami kwa mwaka fedha tunaoenda kuanza sasa. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Maimuna Mtanda, swali la nyongeza.

MHE. MAIMUNA S. MTANDA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi kupata nafasi.

Nilitaka kujua ni lini Serikali itatafuta fedha kwaajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Amkeni – Kitangali kwenda Mtama? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maimuna Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina azma ya kujenga barabara zote kwa kiwango cha lami lakini kinachotegemea ni upatikanaji wa fedha na bajeti itakavyoruhusu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kadri fedha itakavyopatikana barabara hii pia itaingizwa kwenye mpango ya kujenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Dennis Londo, swali la nyongeza.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya kutoka Kilosa – Ulaya kwenda Mikumi ambayo inapitia Masanze - Zombo na Ulaya ni barabara muhimu sana kwa kuchukua watalii kutoka *SGR Station* pale Kilosa kuja Mikumi mbugani na barabara hii ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2010, 2015 na 2020.

Sasa kwa kuwa mimi siwezi kuruka sarakasi, nifanye nini ili Serikali ijue kwamba barabara hii ni muhimu kutengenezwa? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dennis Londo, Mbunge wa Mikumi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba barabara hii ilishaanza kujengwa ila bado haijakamilika nani azma ya Serikali

kuikamilisha barabara hii na ni barabara ambayo inaunganishwa na barabara ya Mikumi – Kidatu hadi kwenda Songea.

Kwa hiyo, katika mipango ambayo Serikali inaendelea nayo kama alivyowasilisha Mheshimiwa Waziri wakati wa bajeti barabara ambazo zinafikiriwa pengine kujengwa kwa mpango wa *EPC* ili kuikamilisha barabara yote. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu Wabunge na majibu kutoka Serikalini na sasa nilete matangazo niliyonayo hapa, naona kuna Wabunge wanatembea, wakae.

Waheshimiwa Wabunge, jambo la kwanza kabisa ambalo nitalizungumza kwenu ni barua mahsusi ambayo Bunge tumeandikiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nimepokea barua kwa niaba yenu nyote ikiwa ni salamu za shukrani kutoka kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uzito wa barua yenyewe naomba niwasomee.

Mheshimiwa Rais anasema hivi; Nimepokea kwa furaha taarifa kwamba Bunge sasa kwa sababu alikuwa ananiandikia mimi kwa niaba yenu anasema Bunge lako tukufu siku ya tarehe 26 Mei, 2022 lilijadili na kutoa Azimio la kunipongeza kwa kutunukiwa tuzo ya *Babacar Ndiaye Trophy 2022* ambayo upatiwa Rais wa Nchi za Afrika zinazofanya vizuri katika miradi ya miundombinu ya barabara. (*Makofi*)

Nakuomba wewe binafsi pamoja na Wabunge wote Wabunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mpokee shukrani zangu za dhati tuzo hii imekabidhiwa kwangu lakini ni tuzo ya Watanzania wote. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Na kwa kipekee kabisa ni tuzo ya Waheshimiwa Wabunge kwa kutambua mchango wenu katika kusimamia miradi. *(Makofi)*

Ngoja nirudie hapo; Na kwa kipekee kabisa ni tuzo ya Waheshimiwa Wabunge kwa kutambua mchango wenu katika kusimamia miradi, matumizi sahihi ya fedha za miradi na kupitisha na kusimamia bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Hivyo ninaomba Watanzania wote wafurahie tuzo huku tukiendelea kusimamia, kuilinda na kuitunza miundombinu yetu kwa maslahi yetu ya sasa na baadaye. *(Makofi)*

Mungu Ibariki Afrika, Mungu Ibariki Tanzania na Kazi lendelee. *(Makofi)*

Imesainiwa hapa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Na sisi kwa sababu jibu la shukrani huwa ni karibu, kwa hiyo, karibu sana Mheshimiwa Rais tunashukuru sana kwa haya ambayo umeyasema na sisi tunakutakia kila la kheri katika utendaji kazi wako na tunaamini hizi tuzo zitaendelea kuja nyingi nyingi katika sekta nyingine pia ambazo unafanya kazi kubwa sana na sisi kama Wabunge na wawakilishi wa wananchi tunatambua kazi hizo nyingi na tunaendelea kukupongeza na tunaendelea kufanya hivyo kila mara. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunayo matangazo mengine hapa na mojawapo ya hayo matangazo ni matangazo kuhusu wageni. Tutaanza na wageni walioko Jukwaa la Spika na kipindi hiki cha mpito wa mabadiliko ya matangazo ya wageni, kwa hiyo, kwa sababu wageni ni wageni wakati mwingine hawajapata fursa ya kufahamu kwamba tunafanya mabadiliko kidogo ya matangazo, kwa hiyo, pengine mtu asipotajwa asijisikie vibaya sana akiwa humu ndani tunajaribu kutunza muda kwa ajili ya Wabunge wapate nafasi ya kusema mambo ambayo wananchi wao

wamewatuma huko ili waje waje wayawasilishe kwa Serikali. Kwa hiyo, matangazo yetu ya wageni yanakuwa kwa kifupi na tunaomba mtuvumilie katika kipindi hiki cha mpito.

Wapo wageni wangu mmoja ni Mheshimiwa Hossein Bahineh ambaye ni Kaimu Balozi wa Jamhuri ya Kiislam ya Iran, karibu sana Mheshimiwa Balozi. *(Makofi)*

Lakini pia yupo Ndugu Kenani Kihongosi ambaye ni Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (CCM), ahsanteni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni 234 wa Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima ambaye ni Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na hawa ni viongozi na watendaji wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo wakiongozwa na Dkt. Zainab Chaula ambaye ni Katibu Mkuu, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Amon Mpanju ambaye ni Naibu Katibu Mkuu, karibu sana. *(Makofi)*

Sasa hawa watendaji wengine wote na viongozi kutoka Wizara hii wote wasimame kwa pamoja, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima amekuja pia na mume wake Wakili Msomi Gwajima, karibu sana na ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Jukwaa la Spika pia wapo wageni wengine, wengine nawaona kwa mbali wengine siwafahamu, lakini wote tusimame kwa pamoja wageni wote walioko Jukwaa la Spika ambao hamjatambulishwa msimame wote kwa pamoja, karibuni sana, sana. *(Makofi)*

Yupo pia mzazi wa Mheshimiwa Deo Ndejemi ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Ndugu Bona Tisha Ndejemi, karibu sana *(Makofi)*

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao wamealikwa pia kuja kuangalia shughuli za Bunge lakini pia kushuhudia Wabunge wao namna wanavyowakilisha na sasa wageni wote wa Waheshimiwa Wabunge wasimame kwa pamoja, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo tunao wanafunzi 41 na walimu sita kutoka Shule ya Msingi Eckernforde Tanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia vijana 50 kutoka taasisi ya *Mutual Generation of Tanzania* ya Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo hapa la matokeo ya mchezo uliochezwa siku ya Jumamosi tarehe 28 Mei, 2022 kati ya *Bunge Queens* na Waandishi wa Habari Wanawake kwenye uwanja wa Jamhuri wa Dodoma, matokeo ya mchezo huo *Bunge Queens* walipata magoli 31 na Waandishi wa Habari walipata magoli kumi na nyota wa mchezo alikuwa Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, ahsante sana, yaani pamoja na kujitangaza *goal shooter* wa kimataifa sijafua dafu. *(Makofi/Kicheko)*

Haya ahsanteni sana tunawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge na watumishi mliojitokeza kwa ajili ya kutuwakilisha kwenye mchezo huu ambao mnaendelea kuonesha heshima ya Bunge kushikilia rekodi ya kutokufungwa.

MBUNGE FULANI: Mwanza.

SPIKA: Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge kwa sababu huwa matangazo yetu ni machache hao wanaosema Mwanza hizo habari hatutazisema. *(Makofi/ Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge anawakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba leo siku ya tarehe 30 Mei, 2022 saa saba mchana

mara baada ya kusitisha hapa shughuli za Bunge, Waheshimiwa Wabunge wote tutaelekea ukumbi wa Msekwa kwa ajili ya semina inayohusu Maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi kwa mwaka 2022.

Waheshimiwa Wabunge, Ofisi ya Taifa ya Takwimu iko tayari kabisa kutoa mafunzo haya na ni muhimu sana sisi kama wawakilishi wa wananchi sababu ndiyo tutakaokuwa tunaenda huko kuwasisitiza na kuwahamasisha wananchi kushiriki kwenye sensa. Ni muhimu sana kuhudhuria mafunzo haya kwa sababu sisi wote tunafahamu kama wawakilishi wa wananchi tusipojua kwenye maeneo yetu kuna watu wangapi kila siku hapa tutakuwa tunalalamika kwamba kwenye maeneo yetu kuna bajeti ndogo kwa sababu watu wako wasipohesabiwa wote itaonekana ni wachache, kwa hiyo fedha zitapelekwa kule ambako kwa kiasi kile ambacho unao hao watu.

Kwa hiyo, ni muhimu sisi kama wawakilishi wananchi kushiriki kwenye semina hii ili tukapate kutumia huo ujuzi tutakaopewa kuwashawishi wananchi, kuwahamasisha lakini kuwafunza pia umuhimu wa sensa.

Waheshimiwa Wabunge tangazo lingine naambiwa kuna maonesho ya viatu vya ngozi vinavyotengenezwa na malighafi za hapa nchini katika viwanja vya Bunge kuanzia leo mpaka tarehe 3 Juni. Wabunge wote mnakaribishwa na Mheshimiwa anayefanya maonesho haya ni Mheshimiwa Sekiboko ndiyo anayeongoza hayo maonesho. Kwa hiyo, tushiriki kwa pamoja. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hili lingine si tangazo, nadhani ni maelekezo kwa Katibu kufanya marekebisho kidogo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi alipokuwa anajibu swali amemtambua Mheshimiwa Maimuna Mtanda kama Mbunge wa Viti Maalum, huyu ni Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini. Kwa hiyo, Kumbukumbu za Bunge ziadikwe sawasawa ni Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. *(Makofi)*

MHE. AGNES M. MARWA: Mheshimiwa Spika, Mwongozo.

SPIKA: Mbunge gani anasema Mwongozo?

MHE. AGNES M. MARWA: Agnes Marwa.

SPIKA: Yuko wapi? Simuoni akisimama. Kasimama wapi? Ahaa Mheshimiwa, jamani muwe mnakaa kwenye viti vyenu inatusaidia sana. Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. AGNES M. MARWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, kuna jambo limejitokeza hivi karibuni, nimeomba Mwongozo kwako kwa sababu linapotokea kwa upande mwingine huwa unatoa tangazo lakini likitokea kwa upande mwingine hujafanya tangazo hilo. Yaani mechi ya Simba na Yanga. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa, hata najishauri kama nisimame au nikae kuelezea huo Mwongozo. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ngoja nisimame. Waheshimiwa Wabunge ngoja, ngoja, tuelewane vizuri, tuelewane vizuri. Matangazo ya namna hiyo hutolewa kama hao watu wako hapa ndiyo naweza kutoa tangazo la namna hiyo. Lakini tukisema kwamba kila mechi inayotokea huko nje tutatangaza hapa ndani, hayo yatakuwa ni matumizi mabaya ya muda wa Waheshimiwa Wabunge, lakini pia na wananchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Sasa Waheshimiwa Wabunge, matangazo yanayotolewa hapa kwa kushinda mechi fulani, aaah nataka hili lieleweke vizuri isije ikaonekana kuna watu wanapendelewa hivi, mimi mwenyewe nimevaa njano hapa leo mbele. *(Makofi/Kicheko)*

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Kwa hiyo, isije ikaonekana kuna watu wanapendelewa, tuweke picha nzuri kwa wananchi. Hakuna timu yoyote inayopendelewa na Bunge kama taasisi. Kwa hivyo, matangazo aidha yanatolewa ya kupongeza timu ikiwa humu ndani kama haiko humu ndani ikishinda kombe maalum. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hiyo tuiweke sawasawa, tusije tukawaweka wananchi mazingira ambayo wanaona mtu anayeongoza hapa kama yeye ni Yanga kama yeye ni Simba basi mazingira yanakuwa namna fulani, hapana. Hata Yanga watakapochukua kombe wasiwe na wasiwasi watatangazwa tu hapa mbele na Simba pia wakichukua kombe vivyo hivyo na Yanga humu ndani kwa sababu mko wengi waleteni hao Yanga hapa ndani tuwapongeze, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwenye jambo hilo kimsingi hakuna Mwongozo wowote.

Katibu.

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimuite sasa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE
NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba hotuba yangu kama ilivyoandikwa na kuwasilishwa kwenye kitabu changu iingie kwenye *Hansard* za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ndani ya Bunge lako tukufu ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ninaomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum - Fungu 53 kwa mwaka 2021/2022 na vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2022/2023. Aidha, naomba Bunge lako tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida pamoja na Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu kwa kunijalia kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha hotuba yangu. Namshukuru sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri katika kuimarisha utoaji wa huduma za ustawi na maendeleo ya jamii. Kipekee ninamshukuru kwa kuunda Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na kuiteua kuiongoza. *(Makoff)*

Natambua matarajio ya Mheshimiwa Rais ni kuona hali ya usawa wa jinsia inafanyika kwa kasi na ufanisi. Ninamuahidi nitaendelea kutimiza majukumu yangu kwa bidii ili kuhakikisha matarajio yake yanafikiwa.

Aidha, nampongeza kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa ufanisi mkubwa ambapo sote tumeendelea kushuhudia mafanikio mengi chini ya uongozi wake.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake katika kuboresha huduma za maendeleo na ustawi wa jamii, kuhimiza usawa wa jinsia, uwezesaji wa wanawake kiuchumi na kuzingatia haki za mtoto katika jamii. Wizara yangu itaendelea kutekeleza kikamilifu maelekezo na mikakati anayotupatia.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mbunge), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi na maelekezo yake mahiri kwa Wizara yangu ambapo amewezesha kuleta tija na ufanisi na kuimarisha huduma za maendeleo na ustawi ya jamii. Aidha, nampongeza kwa hotuba yake aliyotoa hapa Bungeni tarehe 6 Aprili, 2022 ambayo imetoa mwelekeo wa majukumu yatakatotekelezwa na Serikali katika kwa mwaka mpya wa fedha.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuaminiwa na Waheshimiwa Wabunge na kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mbunge) kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Ni imani yangu kuwa mtatekeleza majukumu yenu kwa weledi na ufanisi mkubwa. Vilevile nawapongeza sana Wenyeviti wa Bunge kwa kuendelea kusimamia vyema mijadala hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, vilevile nitumie fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naamini Bunge lako tukufu litaendelea kushirikiana nao ili waweze kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwashukuru Mawaziri wenzangu kwa ushirikiano wanaonipatia, Wizara itaendelea kushirikiana nao kuhakikisha tunatimiza ndoto na dhamira ya Rais wetu katika kusukuma maendeleo ya ustawi wa jamii. Kipekee ninapenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo (Mbunge) pamoja na Makamu wake, Mheshimiwa Aloyce John Kamamba (Mbunge) kwa ushauri na maelekezo ambayo wamekuwa wakitupatia wakati wote wa maandalizi ya bajeti hii. Aidha, ninawashukuru Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri la

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Muungano wa Tanzania kwa ushirikiano mzuri mnaotupatia. Tutaendelea kuzingatia ushauri wenu na kuwapa ushirikiano daima.

Mheshimiwa Spika, natoa pole kwako, Bunge lako tukufu na wananchi wote kwa vifo vya wapendwa wetu Mheshimiwa Elias John Kwandikwa aliyekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Mbunge wa Jimbo la Ushetu; Mheshimiwa William Tate Olenasha aliyekuwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Ofisi ya Waziri Mkuu na Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro; Mheshimiwa Khatibu Said Haji aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Konde Zanzibar na Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa - CCM. Nawapa pole Watanzania wenzetu waliopoteza maisha kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ukatili. Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahala pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo haya ya awali, sasa naomba kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2021/2022, Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi pamoja na maombi ya fedha kwa ajili ya kutekeleza vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022 Wizara ilipanga kutekeleza vipengele 15 kama inavyooneshwa kwenye ukurasa wa saba wa Hotuba yangu niliyoiwasilisha. Aidha, kwenye makadirio ya mapato Fungu 53 Wizara ilipanga kukusanya bilioni sita ambapo hadi Aprili tumekusanya bilioni 3.57 sawa na asilimia 59. Haina shaka kwamba tunaendelea kusimamia kwa kasi ili tukusanye sehemu iliyobakia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sura ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2021/2022 ni kwamba Wizara iliidhinishiwa na Bunge lako tukufu shilingi bilioni 45.97 ambapo hadi Aprili, 2022 imepokea shilingi bilioni 31.3 sawa na asilimia 68 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo, iko kwenye ukurasa wa 11 wa hotuba yangu.

Naipongeza Serikali yetu kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kwa kutoa kiasi hicho cha fedha kwa mtiririko mzuri kiasi kwamba tumeweza kutekeleza shughuli tulizojipangia kama ilivyotarajiwa na tunaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kuchambua utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2021/2022 kwa baadhi ya maeneo kama ilivyo kwenye ukurasa wa 12 hadi wa 80. Nikiri mambo ni mengi kwenye Wizara hii ni pana sana, lakini nitakwenda kwenye baadhi ya mambo muhimu.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la maendeleo ya jamii; Wizara imeimarisha uratibu na usimamizi wa shughuli za wafanyabiashara ndogo ndogo maarufu kama machinga kufuatia maelekezo ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyotoa tarehe 25 Januari, 2022 kwamba Serikali sasa imewatambua rasmi machinga wote nchini kama kundi maalum.

Mheshimiwa Spika, hivyo, uongozi wa Wizara mara moja tuliwapokea viongozi wa kundi hili wanaojulikana kama Taasisi ya SHIUMA na kuanzia Februari hadi Aprili tuliweza kujadiliana nao na kubaini changamoto za shirikisho hilo kwamba ni pamoja na uongozi, usimamizi, changamoto za kiuchumi, mifumo ya TEHAMA, kutokuwa na usajili, kutokuwa na mahali pa kufanyia kazi pa uhakika pamoja na kutokuwa na anuani. Hivyo, tumeshirikiana nao, tukaweza kupata usajili wenye cheti namba 21825 kwa pamoja kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Wizara imewajengea uwezo viongozi zaidi ya 800 wa SHIUMA ngazi zote kwa lengo la kuimarisha uongozi bora, kutambua fursa za kifedha, mbinu za ujasiriamali na umuhimu wa utii wa sheria bila shuruti.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha shirikisho hii la machinga ili liweze kuwa bora zaidi kiutendaji na kupitia Taasisi ya Maendeleo ya Jamii ya Tengeru ikishirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) wanaandaa mfumo wa eletroniki wa utambuzi wa machinga

unaoitwa *Wajasiriamali Connect* na huu utawawezesha sasa waweze kupata fursa mbalimbali ikiwemo mikopo nafuu kutoka taasisi za fedha.

Mheshimiwa Spika, kwenye mafunzo ya viongozi wa SHIUMA yaliyofanyika Mei hapa Dodoma kwa kaulimbiu ya Machinga ni Fursa Sahihi ya Kukuza Uchumi wa Nchi Yetu. Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuwa anashiriki kikao hiki kwa njia ya mtandao ambapo alipiga simu na kuahidi kutoa shilingi milioni kumi kwa kila Ofisi ya Machinga Mkoa kuanzia mwaka 2022/2023. Lengo ni waweze kukabiliana na changamoto wanazopata katika uendeshaji wa ofisi zao. Mwelekeo tulionao sasa ni kuandaa sheria moja ya machinga pamoja na mkakati wao hatua ambazo tumeshaanza kuchukua.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wataalam wa maendeleo ya jamii nchini kote hawa wameendelea kuwa chachu ya kutekeleza kampeni mbalimbali za kitaifa na kuamsha ari ya jamii ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ya sekta mbalimbali katika Halmashauri zetu. Lakini pia wamekuwa wakifanya kampeni ya kuboresha makazi kwa wananchi wenye makazi duni kwa kutumia mifumo ya asili ya kusaidiana. Kampeni ya ujenzi wa nyumba kwa gharama nafuu imekuwa ikifanyika kwa takribani kati ya shilingi milioni saba hadi milioni kumi nyumba inasimama na nyumba hizi zimeongezeka kutoka 751 mwaka 2021 hadi nyumba 5,002 kufikia Aprili, 2022. Tunawashukuru sana Shirika la wadau Kivulini kwa kutusaidia kwenye kampeni hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maendeleo ya mafunzo ya taaluma ya maendeleo ya jamii, tunavyo vyuo nane imeelezwa kwenye ukurasa wa 19. Naipongeza Serikali kutupatia shilingi bilioni 3.6 kwa ajili ya ukarabati wa majengo na miundombinu katika vyuo hivyo. Changamoto kubwa ni uhaba wa Maafisa Maendeleo ya Jamii ambapo kufikia Aprili, 2022 waliopo ni 3,014 kati ya Maafisa 5,296 wanaohitajika, hivyo upungufu ni asilimia 43. Hivyo kadri tunavyokuwa na upungufu huu maana kule kuchochea ari ya wananchi

kujiletea maendeleo na kwenyewe kunakuwa kunakwenda polepole, hii iko ukurasa wa 23.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kuajiri kadri bajeti ya Wizara itakavyoruhusu, lakini tumejipanga kutumia mbinu shirikishi mfano kushawishi wadau wa maendeleo nao watenge nafasi za ajira, kuandaa mwongozo wa ajira za muda na vilevile kwa sababu tunaandaa sheria ya taaluma hii ya maendeleo ya jamii, tunapanga pengine tuweze kuwa na *interns* kabla hawajamaliza shule kama madaktari wanavyofanya au ma-*nurse* wanavyofanya na wengine lakini tuweze kutoa fursa kwa wastaafu ambao wamestaafu lakini hawachoka wenye moyo wa uzalendo waendeleo kusaidia jamii kwenye mazingira waliyopo pale.

Mheshimiwa Spika, kuhusu haki na maendeleo ya mtoto iko ukurasa wa 27 hadi 42; hadithi ni ndefu ni nzuri, lakini niseme Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa mkakati wa Taifa wa kutokomeza ukeketaji wa mwaka 2021 hadi 2025. Naomba niseme mikoa yenye takwimu za juu za ukeketaji ni pamoja na Manyara asilimia 58; Dodoma asilimia 47; Arusha asilimia 41; Mara asilimia 32; na Singida asilimia 31.

Mheshimiwa Spika, afua za kutokomeza ukeketaji kwenye mikoa hii zimekuwa zikifanyika ambapo takribani ngariba 1,800 waliachana na vitendo hivyo kuanzia mwaka 2015/2016 hadi Aprili, 2022. Niseme ukeketaji una madhara makubwa ya kiafya, kisaikolojia, vifo na hadi kuvunja ndoa kabisa na watoto kukosa malezi. Hivyo, ndugu wanajamii ukeketaji siyo dili bali ni ukatili, hivyo tubadilishe fikra.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliwa na aina mpya ya ukatili dhidi ya watoto mitandaoni Serikali imeunda kikosi kazi cha Taifa cha ulinzi na usalama wa watoto mtandaoni. Lakini tumeanza hatua za kuifanyia marekebisho Sheria ya Mtoto ili iakisi mazingira ya sasa ikiwemo uhibitaji wa ukatili mtandaoni.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kidogo kuhusu programu jumuishi ya Taifa ya malezi na makuzi na

maendeleo ya awali ya mtoto ambayo tumeizindua inaanza mwaka 2021/2022 inakwenda mpaka mwaka 2025/2026 na hii inalenga kutatua changamoto za ukuaji na maendeleo ya watoto wenye umri wa miaka sifuri hadi nane na kuhakikisha watoto wote wapo kwenye mwelekeo sahihi wa kufikia ukuaji timilifu, hii ipo ukurasa wa 33 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na wadau wetu wa Shirika la Kimataifa la *BRAC* Maendeleo tumejenga vituo kumi vya mfano vya kijamii vya *program* hii Jijini Dar es Salaam, lakini pia na hapa Dodoma vipo 20; ambapo 15 vimeanza kufanya kazi na tayari watoto 883 wameanza kupata huduma kwenye vituo hivi.

Kwa upande mwingine Wizara imeendelea kushirikiana na wadau kutekeleza ajenda ya kitaifa ya kuwekeza katika afya na maendeleo ya vijana balehe nchini na hii programu inaanza 2021 inakwenda mpaka 2024/2025. Programu hizi mbili ni mapinduzi makubwa sana kwenye maendeleo ya watoto ambao ni Taifa letu la kesho.

Mheshimiwa Spika, malezi bora katika ngazi ya familia imekuwa mtihani na mtihani kweli kweli na umekuwa ukiathiri watoto wa Taifa hili. Hivyo ili kuimarisha msingi wa malezi bora ngazi ya familia, Wizara na washirika wetu tumeandaa na kusambaza kitini cha elimu ya malezi katika familia na tumetoa elimu ya malezi chanya katika mikoa nane, tumeweza kufikia wazazi na walezi 800,000. Mwongozo huu tumeuzindua tarehe 15 Mei, mwaka huu siku ya Kimataifa ya Familia.

Mheshimiwa Spika, aidha, Mabaraza ya Watoto ni jukwaa linalotumika kuelimisha maswala yanayohusu maisha yao ya sasa na maisha yao ya baadae na hii ni nje ya mfumo rasmi wa elimu. Hadi Aprili, 2022 tuna Mabaraza 2,669 ambayo tumeyaanzisha ikiwa ni pamoja na Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hii iko ukurasa wa 40 hadi 42 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Wizara kwa kushirikiana na Wizara za kisekta ikiwepo Wizara ya Elimu na Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumesharatibu uandaaji wa Mwongozo wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule ambapo kuanzia Julai tunaanza kusambaza mwongozo huu kwa kasi na nguvu sana.

Mheshimiwa Spika, niseme kidogo kuhusu huduma za ustawi wa jamii, iko ukurasa wa 43 hadi 58; tumeendelea kutoa huduma kwa watoto waliokinzana na sheria ambapo kufikia Aprili, 2022 watoto 2,109 wamepata huduma. Pia tumeendelea kusimamia marekebisha ya tabia kwa watoto wenye makosa ya jinai kupitia shule yetu ya maadilisho Irambo, Mbeya.

Mheshimiwa Spika, hivyo niwaombe wazazi wa Tanzania tuache kuwakatili watoto, tukishaona anautukutu tujue daktari wake ni Afisa Ustawi wa Jamii, tunao na tunatoa huduma za *mobile* kwenye eneo hili, simu zetu tumetangaza zipo kwenye *website* ya Wizara na mitandao yote ya kijamii na ya Wizara yetu na simu yangu iko pale. Usimpige ukamuumiza, utakutana na Sheria ya Mtoto, wewe mlete kwenye madaktari wa kurekebisha ustawi wa afya ya akili yao, hutaweza kupata matatizo. Vinginevyo ujiandae mzazi kupambana na Sheria ya Mtoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara pia imendelea kuratibu huduma kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi ambapo jumla ya watoto 218,369 walitambuliwa na kupewa huduma mbalimbali, watoto hawa wanaishi mitaani na kufanya kazi kwa sababu ndoa zinavunjika, kuna malezi hafifu kwa familia, lakini kuna msongorika kati ya watoto wenyewe pamoja na umaskini wa kaya. Tunazo programu nyingi za kusaidia umaskini wa kaya uondoke kama *TASAF* tuna mikopo mbalimbali katika maeneo mbalimbali, lakini bado tumeendelea kuona watoto hawa mtaani hivyo hii ni changamoto.

Katika suala la migogoro ya ndoa kufikia mwezi Aprili jumla ya mashauri 39,571 yalipokelewa ambapo mashauri

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

4,576 yamekwenda mahakamni 19.2 yalisuluhishwa na mengine 15,718 yanaendelea. Wito kwa wanajamii tuepuke migogoro ya ndoa kama tukishindwana na inabidi tutengane lazima tufuate taratibu za kumlinda mtoto na haki zake. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mwezi Machi, 2020 Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na wadau mbalimbali tuliona tuandae hafla ya chakula pamoja na watoto waishio na kufanya kazi mtaani kwa lengo la kuwaonyesha upendo wa Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan kwao lakini kupata maoni yao tuwezeje kupata ufumbuzi wa kudumu kwenye shida hii, lakini kubaini vibaji vyao kupitia nyimbo, michezo walioweza kutuonyesha pale. Tumbaini kuna vipaji vingi sana ndani ya watoto hawa. Lakini pia tukaona tuunde kikosi kazi cha kuweza kushirikiana nao wao wenyewe kutafuta ufumbuzi tumekiunda kinaongozwa na bwana David Mlongo, Mkurugenzi wa Shirika la *SOS Tanzania* ili waweze kuja na ufumbuzi utakaotumika kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, natoa wito tena kila mzazi kuhakikisha anatimiza wajibu wake sambamba na mapenzi yake ya kumleta mtoto duniani.

Mheshimiwa Spika, huduma za malezi ya kambo ya kuasili zimeendelea kutolewa, tuna watoto wengi tumeelezea kwenye ukurasa wa 49 lakini niwapongeze wale walioweza kuwachukua na kuwasili na nitoe wito kwa wengine wenye mapenzi mema waweze kuleta maombi yao wawaasili.

Kuhusu usajili wa makao ya watoto tumefikia vituo 301 vinavyohudumia Watoto jumla 11,341 lakini tuna makao yetu ya Serikali hapa Dodoma Kikombo ambayo ni ya mfano ukanda mzima wa Afrika Mashariki na mengine yapo Kurasini. Haya ya Kikombo yanabeba watoto 250 na Kurasini watoto 100.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza *Abbott Fund Tanzania* kwa msaada wa kutujengea na kutuwezeshea kituo

hiki kianze kufanya kazi. Lakini pia tunasimamia vituo 2,512 vya kulelea watoto mchana ambavyo vinahudumia watoto 173,032. Kwa hiyo ni *operation* kubwa sana inafanywa na Wizara hii kwenye dhamana ya watoto.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia haijawaacha kundi maalumu la wazee tunaratibu uwendeshaji wa makazi 14 ya wazee wasiojiweza ya Serikali ambapo kufikia Aprili, 2022 tunao wazee 271 lakini wenzetu pia wa sekta binafsi na wale wenye makao ya hiyari jumla wako 20 na yanawaze 451 changamoto kubwa eneo hili ni uchakavu wa mindombinu hivyo tunaendelea kutafuta fedha tuweze kuboresha vituo hivi tukianza na cha Misufini, Tanga kile pale ili kiweze kuwa bora na kuwa cha mfano katika vituo vingine vitakavyojengwa.

Mheshimiwa Spika, lakini tumeona tunamakazi mengi sana ya wazee katika mikoa mbalimbali kwenye mikoa mingine yako mawili/mawili watumishi wachache wazee wachache huduma zinakuwa siyo bora, tumeamua tuje na mpango wa makazi ya wazee kikanda ili yapungue ili zile huduma ziweze kuwa bora sambamba na rasilimali tulizonazo hili nalo tunatekeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini tumekwenda mbele tutaanzisha miradi ya maendeleo/miradi ya kiuchumi katika kaa mbili hizi za wazee wapo wazee hata kama wangukuwa nyumbani kwao wangukuwa na miradi ya kufuga ng'ombe kuku, sungura na vitu kama hivyo tupanue ili tuweze kupunguza ile dhana ya kusema mzee akizeeka amekuwa *written off* hapana, aweze kuendelea kuwa na faida katika jamii na yeye mwenyewe kupata afya njema na mazoezi na lishe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara pia imeratibu uundwaji wa Baraza la Taifa la Ushauri la Wazee lenye Wajumbe 31 na tulishalizindua hapa Dodoma mwezi Machi, 2022 na pia hawa wazee sasa wamepata fursa ya kuipita sera yao na mwongozo wao wa uratibu wa mabaraza haya tumepata maoni yao hivyo tunakwenda sambamba na wazee

kuhakikisha hatuwaachi nyuma, kilio chao cha muda mrefu sasa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassani amekizika rasm maana yake baraza lilikuwa halizinduliwi halizinduliwi, lakini hatimaye yamekuwa. Tunawashukuru Shirika la *Help Age International* kwa kutusaidia katika uratibu wa shughuli hizi za wazee. Pamoja na kazi nzuri ya Maafisa Ustawi wa Jamii inayofanywa nchini kote tuna changamoto mkubwa ya upungufu wa kada hii. Maafisa wanaopungua ni 22,395 sawa na asilimia 97; hii ni sawa na kusema kwamba kata zote *almost* hazina hawa wanataaluma, lakini matatizo hayo ya ukatili, nyanyasaji na huduma za kijamii zinahitajika kule chini. Habari zaidi ziko katika Jedwali Namba 4 ukurasa 58. Tunaendelea kushawishi kibali cha ajira cha upendeleo huku tukikabiliana na njia mbadala kama nilivyosema kwa upande wa maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maendeleo ya jinsia na uwezeshaji wanawake; hiki ni kipaumbele cha kitaifa na maono ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, hivyo basi, Wizara ilizindua Kamati ya Ushauri ya Kitaifa ya Utekelezaji wa Ahadi za Nchi kuhusu Kizazi chenye Usawa (*GEF*) Desemba, 2021 Jijini Dodoma ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Andiko hili limeshakamilika na ifikapo Juni litakabidhiwa chini ya uongozi mahiri Anjellah Kairuki ambaye ni Mwenyekiti Mteule anayeongoza kikosi kazi hiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hili tumeenda kukamilisha Mwongozo wa Uundaji Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi, yataundwa kuanzia kitongoji, kata, mtaa, halmashauri, mikoa mpaka Taifa, kwa hiyo kuelekea mwezi Julai tutakuwa tunaongea habari nyingine za wanawake na maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia ilishiriki kwenye Mkutano wa 66 wa Kamisheni ya Wanawake Duniani uliofanyika New York, Marekani lakini baada ya kufanya vizuri kule Marekani tukaalikwa tena kwenda Ujerumani kushiriki Mkutano wa G7 uliofanyika Berlin, Aprili, 2022 uliolenga kujadili

masuala mbalimbali kuhusu uzingatiaji wa usawa wa kijinsia na uthaminishaji mchango wa wanawake wanaofanya kazi zisizo na ujira katika uchumi wa familia na Taifa. Maana mama anafanya kazi za ofisini anaupiga mwingi, akirudi nyumbani anafanya kazi za nyumbani anaupiga mwingi, hivyo basi dunia imeona iwaangazie wanawake wanamna hii ili waweze kutendewa haki katika safari yao ya maendeleo na usawa wa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, mataifa yamepongeza uwamuzi wa Serikali wa kuhakikisha kwamba uwezeshaji wanawake kiuchumi nchini Tanzania ni kipaumbele cha Taifa na wameahidi kuja kushirikiana na sisi tunawashukuru *UN Woman* na Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) kwa uwezeshaji huo.

Mheshimiwa Spika, wanawake wameendelea kujengewa uwezo na stadi za kufanya biashara ambapo kufikia Aprili, 2022 wanawake 1,167 walifikwa na mafunzo yataendelea mikoa yote. Mikopo na mitaji imeendelea kutolewa na Benki ya Biashara ya Tanzania (*Tanzania Commercial Bank*) ambako tayari tumeweza kurekodi mikopo ya shilingi bilioni 16.1 kwa wanawake 3,421 wa Tanzania Bara hadi kufikia mwezi Aprili, 2022. Hii yote ni kazi njema ya Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenda kwenye *gender equality forum*.

Kuhusu unyanyasaji wa kijinsia vyuoni, hatuko nyuma Wizara tumeandaa Mwongozo wa Uanzishaji, Uendeshaji na Ufuatiliaji wa Dawati la Jinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati uliozinduliwa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mbunge), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hapo Novemba, 2021.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uratibu *NGO*stunaendelea vizuri, tumesajili *NGOs* 1,217 kwenye kipindi hiki cha taarifa kati ya 500 tulizopanga kusajili na hii imechangiwa na kuwa na mfumo sasa wa TEHAMA wa usajili na elimu inayotolewa kwenye jamii. Kifupi niseme sasa rekodi ipo inasema tunayo mashirika 7,533 yaliyo hai, kati ya mashirika 12,442 yaliyopo kwenye kanzidata hiyo. Wito kwa *NGOs* na wamiliki mfuate

sheria, kanuni na taratibu daima ili tuwe na takwimu zenu hai, lakini limeundwa Baraza la *NGO's* ambalo kwa kushirikiana na Serikali limewezesha mkutano wa kwanza wa kihistoria wa mwaka 2021 ambapo Mgeni Rasm alikuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na hii ilikuwa Septemba, 2021 Jijini Dodoma ambako wadau walihudhuria maelfu, jumla ya 1,444 walishiriki kwenye mkutano huu. Mheshimiwa Rais alielekeza kuandaa mkakati wa Taifa wa uendeleu wa *NGOs* ambako waweze kupunguza wategemezi na kuwa wahimilivu. Andiko limekamilika na maoni ziko kwenye hatua za mwisho liweze kuwasilishwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango kazi wa Taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake unaisha Juni, 2022; tumeeleza hapo kwenye hotuba yangu na tumeshaanza tathimini ili tuweze kuwa na uwendeleu wa mpango huu.

Mheshimiwa Spika, Wizara imetekeleza miradi mbali ya maendeleo ikiwemo ujenzi na ukarabati wa majengo na miundombinu katika vituo vya ustawi, taasisi na vyuo vilivyo chini yake ipo ukurasa wa 91 hadi 93 na kama pale kwenye picha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2022/2023; tumepanga kutekeleza vipaumbele nane tumeripoti kwenye ukurasa wa 94 na 95 na tumekaridia kutumia shilingi bilioni 43.4 na baadhi ya maeneo makuu yaliyotengewa fedha kwa mwaka huu unaokuja tumeainisha kwenye ukurasa 95 na 97 na hapa naomba niyatambue machache.

Mheshimiwa Spika, katika kupambana na ukatili na masuala ya usawa wa kijinsia, shilingi bilioni 2.65 tumetenga kuwezesha afua za kutokomeza ukatili kwa wanawake na watoto ikiwemo kampeni mbalimbali; mafunzo wezeshi kwa watoa huduma za madawati ya jinsia vyuoni na taasisi, kusambaza Mwongozo na Uwezeshaji wa Majukwaa ya Wanawake Kiuchumi, kuwezesha utekelezaji wa Ahadi zetu pendwa za nchi kuhusu Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa yaani

GEF au *Gender Equality Forum* na kuwezesha ushiriki wa wanawake katika Maonesho ya Kitaifa na Kimataifa ili waweze kukaa vizuri na kuendelea kuupiga mwingi.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili tumetenga kwenye eneo la watoto shilingi bilioni 2.36 kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa huduma kwa watoto wanaoishi mazingira hatarishi na marekebisho ya tabia kwa watoto waliokinzana na sheria, kukarabati mahabusu za watoto katika mikoa ya Mbeya na Arusha, kujenga mahabusu mpya ya watoto katika mkoa wa Mwanza na kutekeleza mpango huu wa malezi, makuzi ya watoto nilioutaja na kuanzisha vituo vya kijamii vya malezi na makuzi na maendeleo ya mtoto ili mama akiwa anakwenda kazini na baba hayupo mtoto asiwe kwenye *risk*, anakaa kwenye hivi vituo mpaka wazazi wake warudi maana tumepata ukatili mwingi sana kwenye eneo hili kwa watoto kuachwa peke yao wazazi wameenda kwenye mihangaiko.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la wazee tumetengwa shilingi bilioni 1.45 kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa huduma za ustawi jamii kwa wazee wasiojiweza katika makazi 14 na ukarabati wa majengo na miundombinu katika Makazi ya Wazee ya Ipuli na Njoro. Aidha, kwenye eneo la taasisi na vyuo, kiasi cha shilingi bilioni 5.6 kimetengwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo na miundombinu katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kampasi ya Kisangara na vyuo nane vya maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni kubwa na pana na ni mtambuka ni ya kisekta kuna mambo mengine ya maendeleo ya jamii yanatekelezwa kwenye wizara zingine mbalimbali. Kwenye Wizara ya Elimu yapo, kwenye *TASAF* yapo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI yapo kila sehemu kuna vitu vinatekelezwa vinavyogusa jamii. Kwa hiyo, mimi nimetoa *summary* ya yale ambayo yalikuwa hayajasemwa.

Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako naomba nitoe shukrani ambazo pia nimezitaja kwenye ukurasa wa 98 hadi 102. Shukrani kwa nchi rafiki zikiwemo Marekani, Ujerumani,

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Ubelgiji, Ufaransa, Uingereza na nchi nyingine zote ambazo zimeendelea kuisaidia wizara. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nayashukuru Mashirika ya Kimataifa *UNICEF, UN-Women, UNFPA, WHO, IOM* na *UNESCO*; Umoja wa Nchi za Ulaya (*EU*); Benki ya Maendeleo ya Afrika; *USAID*; *Abbott Fund* na *Global Fund*, shukrani kwa taasisi za kifedha zikiwemo *NMB, CRDB, Stanbic Bank* na Benki ya Biashara Tanzania (*TCB*).

Mheshimiwa Spika, nazishukuru *NGOs* za ndani ya nchi na mashirika ya dini yakiwemo *WILDAF, TCRF, TAMWA, TAWLA, TGNP, TAYOA, LSF, Plan International - Tanzania, Kivulini, Brac Maendeleo, FSDT, The Aga Khan Foundation, CBM International, Segal Foundation, HelpAge International, Save the Children, World Vision, PACT Tanzania, Trademark East Africa, Equality for Growth, Landesa, TAWIA, CAMFED, SOS Children's Village Tanzania, CISEMA; Railway Children Africa, REPPSI, Amani Girls Home, Pelum Tanzania, LHRC, ECPAT, INTERPOL, Haki Elimu, TWCC, Compassion International, Care International, TECDEN, Pact Tanzania, BAKWATA* na *CCT*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, shukrani kwa Taasisi za Serikali zikiwemo *SIDO, BRELA, NIMR, TBS*, Shirika la Posta Tanzania, *NSSF, TFS, TASAC, TPA, NHIF, UCSAF, TASAF*, Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza na *TAKUKURU*, Vyama vya Kitaaluma ikiwemo *CODEPATA, TASWO* na *Tanzania Bankers Association* na wanaharakati wote wa Wizara yetu.

Mheshimiwa Spika, shukrani kwa Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis (Mbunge), Naibu Waziri kwenye Wizara yangu kwa ushirikiano mkubwa sana anaonipatia hapa Bungeni kujibu maswali na kufuatilia mambo mengi sana hapa kwa niaba yangu. Lakini kipekee nimshukuru Dkt. Zainab Chaula, Katibu Mkuu ambaye amekuwa ni mama jembe kabisa anayenifanya nilale usingizi bila kumsahau Wakili Msomi Amon Mpanju, Naibu Katibu Mkuu kwa mchango na ushirikiano wao mkubwa sana. (Makofi)

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Aidha, nawashukuru wataalamu wangu wote wa Wizara yangu kwa ushirikiano wao daima kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI, nawashukuru viongozi wa Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali ya Mitaa kwa ushirikiano wao mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nazishukuru taasisi chini ya Wizara yangu na vyo vyote. Naishukuru Kamati ya Ushauri ya Kitaifa ya Utekelezaji Ahadi za Nchi kuhusu Kizazi Chenye Usawa chini ya Mwenyekiti Anjellah Kairuki ambaye ni amebebeshwa zigo hili la Taifa la kufanya wanawake waweze kujikomboa kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kumshukuru sana mume wangu mpendwa Mheshimiwa *Advocate* Metusela Gwajima, Wakili Msomi kwa kuthamini usawa wa jinsia kwenye maendeleo ya familia na kunipa nafasi ya kutekeleza majukumu yangu kitaifa katika mapito yote ya nyakati nyepesi na nyakati ngumu. Nawashukuru sana watoto wetu wapendwa na wote ambao wamekuwa sehemu ya familia yetu nawapenda sana na Mungu awabariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijielekeze kwenye kuomba fedha; naomba kuomba fedha kwa utekelezaji wa mwaka 2022/2023 kama ifuatavyo; Wizara imekadiria kukusanya shilingi bilioni 8.5 kutoka vyanzo vyake vya ndani vyote. Aidha, inakadiria kutumia shilingi 32,310,981,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 18,169,057,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi 14,141,924,000 ni kwa Mishahara ya Watumishi.

Mheshimiwa Spika, Wizara inakadiria kutumia shilingi 11,092,080,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo kati ya fedha hizo shilingi 6,900,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 4,192,080,000 ni fedha za nje. Hivyo kwa mwaka 2022/2023 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum - Fungu 53 kwa heshimiwa tunaomba jumla ya shilingi 43,403,061,000 ili kutekeleza majukumu yake kwa maendeleo na ustawi wa jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara yangu www.jamii.go.tz.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima naomba kutoa hoja. (Makofi)

HOTUBA YA WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM, MHE. DKT. DOROTHY GWAJIMA (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2022/23 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

A. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ndani ya Bunge lako Tukufu, ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ninaomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (Fungu 53) kwa mwaka 2021/22 na Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2022/23. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida pamoja na Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa mwaka 2022/23.

2. Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Pia, nitumie fursa hii kumshukuru sana **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri katika kuimarisha utoaji wa huduma za ustawi na maendeleo ya jamii kwa Watanzania. Kipekee ninamshukuru kwa kuunda Wizara mpya ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na kunitiua kuiongoza Wizara hii.

Natambua kuwa matarajio ya Mheshimiwa Rais ni kuona hali ya usawa wa kijinsia hapa nchini inaimarika na utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii unafanyika kwa kasi kubwa na ufanisi. Ninamuahidi kwamba nitaendelea kutimiza majukumu yangu kwa weledi mkubwa ili kuhakikisha kwamba matarajio yake yanafikiwa kikamilifu. Aidha, nampongeza kwa kuendelea kuongoza nchi yetu kwa mafanikio makubwa tangu aingie madarakani akiwa ni Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sote tumeshuhudia mafanikio makubwa yaliyopatikana katika nyanja mbalimbali chini ya uongozi wake.

3. Mheshimiwa Spika, pia, napenda kumshukuru **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye amekuwa mstari wa mbele katika jitihada za kuboresha huduma za maendeleo na ustawi wa jamii, kuhimiza usawa wa jinsia, uwezeshaji wa wanawake kiuchumi na kuzingatia haki za mtoto katika jamii. Wizara yangu itaendelea kutekeleza kikamilifu maelekezo na mikakati inayotolewa na Ofisi yake.

4. Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumshukuru **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri uliowezesha kuleta tija na ufanisi katika utendaji na kuimarisha huduma zinazotolewa katika Sekta ya Maendeleo na Ustawi ya Jamii. Aidha, ninampongeza kwa hotuba yake aliyoiwasilisha kwenye Bunge lako Tukufu tarehe 6 Aprili, 2022 ambayo imetoa mwelekeo wa majukumu yatakayotekelezwa na Serikali katika mwaka 2022/23.

5. Mheshimiwa Spika, ninapenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuaminiwa na Waheshimiwa Wabunge na kuweza kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninampongeza **Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb)** kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Ni imani yangu kuwa

mtatekeleza majukumu yenu kwa weledi na ufanisi mkubwa katika kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, nawapongeza sana Wenyeviti wa Bunge kwa kuendelea kusimamia vyema mijadala mbalimbali ndani ya Bunge hili Tukufu.

6. Mheshimiwa Spika, vilevile, nitumie fursa hii kuwapongeza **Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai** kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na **Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha** kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naamini kuwa Bunge lako Tukufu litaendelea kushirikiana nao ili waweze kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

7. Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwashukuru Mawaziri wenzangu kwa ushirikiano wanaonipatia ambao unaiwezesha Wizara yangu kuendelea kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Wizara itaendelea kushirikiana nao na kuhakikisha tunatimiza dhamira ya **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuhakikisha kuwa Sekta ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii inaratibiwa vyema kwa matokeo chanya.

8. Mheshimiwa Spika, kipekee ninapenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti **Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo (Mb)** na Makamu wake, **Mheshimiwa Aloyce John Kamamba (Mb)** kwa ushauri na maelekezo waliyoyatoa wakati wa maandalizi ya Bajeti hii. Aidha, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mzuri wanaotupatia ikiwemo kutoa ushauri na maoni mbalimbali yenye lengo la kuboresha huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Ninawaahidi kwamba, Wizara ninayoiongoza itazingatia ushauri wao na kuendelea kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya kuwatumikia wananchi kwa moyo wote ndani na nje ya Bunge.

9. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pole kwako, Bunge lako Tukufu na wananchi wote kwa vifo vya wapendwa wetu **Mheshimiwa Elias John Kwandikwa**, aliyekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Mbunge wa Jimbo la Ushetu; **Mheshimiwa William Tate Olenasha**, aliyekuwa Naibu Waziri wa Uwekezaji (Ofisi ya Waziri Mkuu) na Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro; **Mheshimiwa Khatibu Said Haji**, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Konde Zanzibar); na **Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama**, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa (CCM). Aidha, nawapa pole Watanzania wenzetu waliopoteza maisha kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ukatili. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahala pema peponi. Amen.

10. Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo ya awali, ninapenda sasa kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2021/22, Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi pamoja na Maombi ya Fedha kwa ajili ya kutekeleza Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2022/23.

B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2021/22

11. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sera, Mpango Mkakati pamoja na Makubaliano ya Kitaifa na Kimataifa yenye lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii nchini. Sera hizo ni pamoja na Sera ya Maendeleo ya Jamii (1996); Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000); Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2001); Sera ya Taifa ya Wazee (2003); na Sera ya Maendeleo ya Mtoto (2008). Vilevile, katika kuandaa mpango na bajeti, Wizara imezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26), Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020, Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (2017/18 – 2021/22), Malengo ya

Maendeleo Endelevu (SDGs 2030) na Agenda ya Afrika Tuitakayo (2063). Aidha, Wizara inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Ahadi za Nchi katika Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa (*Generation Equality Forum* – GEF, 2021 – 2026).

12. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/22, Wizara ilipanga kutekeleza afua mbalimbali zenye lengo la kuboresha utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii katika maeneo yafuatayo: -

(i) Kukuza ari ya jamii, uzalendo na kujenga moyo wa kujitolea katika kujiletea maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa kutumia nguvukazi na rasilimali zinazowazunguka;

(ii) Kutekeleza dhana ya uanagenzi, ubunifu na ushirikishwaji jamii kwenye Taasisi na Vyuo ili kuzalisha wanafunzi wanaoajirika na kujiajiri na kuwa chachu ya maendeleo;

(iii) Kuratibu uwezeshaji wa wanawake kiuchumi na uingizaji wa masuala ya jinsia katika Sheria, Sera, Mipango, Mikakati, Programu na Bajeti;

(iv) Kuendelea kuimarisha huduma za ustawi wa jamii na haki kwa familia na watoto ikiwemo malezi ya kambo na kuasili, watu/walezi wa kuaminika, malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya watoto, ulinzi na usalama kwa watoto dhidi ya vitendo vya ukatili pamoja na huduma za utengemao katika familia kwa watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani;

(v) Kuimarisha huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa na familia, Msaada wa Kisaikolojia na Kijamii kwa familia, jamii na makundi mbalimbali wakiwemo wazee, watoto walio katika mazingira hatarishi pamoja na manusura wa ukatili na majanga mbalimbali;

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

- (vi) Kuimarisha ufuatiliaji na uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili yaweze kutoa mchango chanya katika ujenzi wa Taifa;
- (vii) Kuendelea kuratibu kampeni mbalimbali za kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto;
- (viii) Kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ili kutoa mafunzo yanayokidhi mahitaji ya soko;
- (ix) Kusimamia, kufuatilia na kuimarisha uanzishaji na uendelezaji wa Vituo vya Kulelea Watoto Wadogo na Vituo vya Kijamii vya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto katika ngazi ya jamii ili kuboresha malezi na makuzi ya kila mtoto;
- (x) Kuendelea kuimarisha utoaji wa huduma za msingi katika Vituo vya Ustawi wa Jamii ikiwemo Makazi ya Wazee na Watu wenye Ulemavu, Mahabusu za Watoto, Makao ya Watoto na Shule ya Maadilisho;
- (xi) Kuimarisha mifumo ya kusimamia, kufuatilia na kutathmini viwango vya huduma za ustawi wa jamii zinazotolewa nchini;
- (xii) Kuanzisha na kuimarisha utendaji wa Mabaraza ya Watoto na Dawati la Ulinzi la Watoto Shuleni;
- (xiii) Kuendelea kuratibu uundwaji wa Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto pamoja na kuzijengea uwezo;
- (xiv) Kuratibu uanzishwaji wa vikundi vya malezi katika ngazi ya jamii; na
- (xv) Kuhamasisha ushiriki wa wanawake katika ngazi za uongozi na nafasi mbalimbali za maamuzi.

MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA (FUNGU 53)

13. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/22, Wizara ilipanga kukusanya kiasi cha **Shilingi 6,000,000,000** kutokana na ada za wanafunzi katika Vyuo nane (8) vya Maendeleo ya Jamii, uuzaji wa Mitaala ya Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, usajili na ada za mwaka za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs), uuzaji wa Mitaala ya Vyuo vya Ustawi wa Jamii, ada za mwaka, uuzaji wa Mitaala ya Vituo vya kulelea Watoto Wadogo Mchana na vyanzo vingine vya mapato. Hadi kufikia mwezi Aprili 2022, Wizara imefanikiwa kukusanya kiasi cha **Shilingi 3,566,324,302** sawa na asilimia 59 ya makadirio ya mapato. Ni matarajio yangu kuwa hadi kufikia mwezi Juni 2022, Wizara itafikia lengo la asilimia 100 ya makusanyo kama ilivyopangwa.

14. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/22, Wizara iliidhinishiwa na Bunge lako tukufu jumla ya matumizi ya **Shilingi 45,966,248,430.83**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 31,066,248,430.83** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 18,080,576,430.83** ni fedha za Matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi 12,985,672,000** ni kwa ajili ya Mishahara. Aidha, kiasi cha **Shilingi 14,900,000,000** kilikuwa ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi 4,900,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 10,000,000,000** ni fedha za nje.

15. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili 2022, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 31,315,282,868.47** sawa na asilimia 68 ya bajeti kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha zilizopokelewa, Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi 25,143,892,668.47** sawa na asilimia 81 ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 14,294,778,313.27** ni Matumizi Mengineyo na **Shilingi 10,849,114,355.20** ni kwa ajili ya Mishahara.

Aidha, **Shilingi 6,171,390,200** ni Fedha za Maendeleo ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 4,900,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 1,271,390,200** ni fedha za nje.

Naipongeza sana Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuipatia Wizara kiasi hicho cha fedha kwa mtiririko mzuri unaowezesha utekelezaji wa majukumu.

C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA (FUNGU 53)

16. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/22, utekelezaji wa majukumu ya Wizara ulilenga kuimarisha ushiriki wa jamii katika shughuli za maendeleo, kuimarisha upatikanaji wa haki na maendeleo ya mtoto, kuboresha huduma za ustawi wa jamii, kuchochea maendeleo ya jinsia na uwezesaji wa wanawake, kuratibu utekelezaji wenye ufanisi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA). Uratibu wa utekelezaji wa majukumu haya ulifanywa na Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zake pamoja na wadau mbalimbali.

ENEO LA 1: MAENDELEO YA JAMII

17. Mheshimiwa Spika, Wizara ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Jamii ya Mwaka 1996, ambayo inasisitiza dhana ya ushiriki wa jamii katika kujiletea maendeleo kwa kutumia rasilimali zilizopo katika maeneo yao. Aidha, inasisitiza kuendeleza na kukidhi mahitaji ya makundi maalum wakiwemo wafanyabiashara ndogondogo (Machinga) ambao wengi wao ni vijana. Katika utekelezaji wa jukumu hilo, yafuatayo yamefanyika: -

18. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi mwezi Aprili 2022, Wizara imeimarisha uratibu na usimamizi wa shughuli za wafanyabiashara ndogondogo wajulikanao kama Machinga, kufuatia maelekezo ya **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyotoa tarehe 25 Januari 2022 kwamba Serikali anayoiongoza inawatambua Machinga wote nchini kama kundi maalum ambalo litakuwa chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Hivyo,

uongozi wa Wizara uliwapokea rasmi na kukutana na viongozi wa Shirikisho la Umoja wa Machinga Tanzania (SHIUMA) ngazi ya Taifa. Aidha, katika vipindi tofauti kuanzia mwezi Februari hadi Aprili 2022, Wizara imejadiliana nao na kubaini kuwa Shirikisho hilo lilikuwa linakabiliwa na changamoto za kiuongozi na kiusimamizi, kiuchumi, kimumo (TEHAMA), kutokuwa na usajili, kutokuwa na mahali pauhakika pa kufanyia kazi na kutokuwa na anwani.

19. Mheshimiwa Spika, katika kutatua changamoto hizo, Wizara imewezesha usajili wa SHIUMA kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na kupatiwa cheti chenye usajili **Namba 21825**. Pia, imewajengea uwezo viongozi 10 wa SHIUMA ngazi ya Taifa pamoja na washiriki 198 kutoka Mkoa 26 ya Tanzania Bara. Lengo la mafunzo hayo lilikuwa ni kuwajengea uwezo kuhusu uongozi bora, fursa za kifedha, ujasiriamali na utii wa sheria bila shuruti. Aidha, imewapatia sehemu ya kufanyia kazi ndani ya jengo lake. Vilevile, inaendelea kuimarisha mahusiano ya kiutendaji baina ya viongozi na wanachama wa shirikisho kuanzia ngazi ya Taifa hadi kwenye masoko. Wizara kupitia Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) imeanza kutengeneza Mfumo wa Kieletroniki wa utambuzi wa wafanyabiashara ndogondogo (Machinga) ujulikanao kama "*Wajasiriamali Connect*". Mfumo huo utawawezesha wafanyabiashara hao kupata fursa mbalimbali ikiwemo upatikanaji wa mikopo nafuu kutoka katika taasisi za fedha.

20. Mheshimiwa Spika, Wizara imeratibu mafunzo kwa viongozi 803 wa SHIUMA kuanzia tarehe 16 – 19 Mei, 2022 Jijini Dodoma. Kaulimbiu ilikuwa "Machinga ni Fursa Sahihi ya Kukuza Uchumi wa Nchi Yetu". Katika mafunzo hayo, **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alishiriki kwa njia ya simu ambapo aliweza kuahidi kutoa **Shilingi Milioni 10** kwa kila Mkoa kuanzia mwaka 2022/23 ili kukabiliana na changamoto

wanazopata Machinga katika uendeshaji wa shughuli zao. Mwelekeo zaidi kuhusu Machinga ni kuandaa Sheria moja ya Machinga pamoja na Mkakati wa Maendeleo ya Machinga hatua ambazo zimeanza kuchukuliwa.

21. Mheshimiwa Spika, Wizara inapenda kutambua mchango wa Wadau mbalimbali, Taasisi na Wizara za Kisekta ikiwemo: Ofisi ya Makamu wa Rais; Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu; Ofisi ya Rais – TAMISEMI; Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Wizara ya Fedha na Mipango; Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara; Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Wizara hizi kwa pamoja zimeweza kutekeleza majukumu yake katika kutatua changamoto za Machinga kama ifuatavyo: kuratibu zoezi la utambuzi wa Machinga kwa kuwapa vitambulisho na kuondoa kodi zilizokuwa zinakwamisha ukuaji wa biashara za Machinga; kutenga na kujenga miundombinu ya masoko katika Mikoa mbalimbali ili kurahisisha utendaji wa shughuli za Machinga; kuwapa elimu juu ya utambuzi wa bidhaa bandia; athari zinazotokana na bidhaa bandia kwa Machinga na katika uchumi wa nchi; na kuwapa elimu juu ya kuheshimu sheria za Nchi wakati wa utekelezaji wa majukumu yao.

22. Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za dhiti kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri nchini na Wadau wengine kwa namna wanavyoshughulikia suala la ujenzi wa miundombinu na upangaji wa wafanyabiashara ndogondogo nchini. Aidha, shukrani zangu za dhiti ziwafikie viongozi wa SHIUMA ngazi ya Taifa kwa kuendelea kushirikiana na Wizara yangu katika kuhakikisha kuwa changamoto za Machinga Nchini zinapatiwa ufumbuzi.

23. Mheshimiwa Spika, Wataalam wa Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na viongozi ngazi mbalimbali

wamekuwa chachu ya kutekeleza kampeni mbalimbali za Kitaifa na wanaendelea kuamsha ari ya jamii kuboresha makazi yao. Kampeni hii inatumia mfumo wa asili wa kusaidiana katika maeneo yenye makazi duni ikiwemo Mikoa ya Lindi, Kagera, Tanga, Tabora, Pwani, Arusha, Kigoma, Singida, Mtwara na Katavi. Ujenzi wa nyumba hizo unatumia gharama nafuu kati ya **Shilingi 7,000,000** hadi **Shilingi 10,000,000** ambapo jamii au kikundi humsaidia mmoja wao anayejenga nyumba kufyatua tofali za kuchoma, kukusanya mawe, mchanga na kuchota maji ya kujengea ili kupunguza gharama za ujenzi. Fedha taslimu hutumika kununua vifaa vya dukani kama bati na saruji. Aidha, jamii hutumia vikundi vya kuweka na kukopa (VICOBA) au mtindo wa kupeana fedha kwa ajili ya kununua vifaa vya dukani.

Vilevile, ili kurahisisha ujenzi wa nyumba bora, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii Ufundi vya Mabughai na Misungwi vimekuwa na utaratibu wa kuandaa ramani za makazi na kuzitoa kwa gharama nafuu. Katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi mwezi Aprili 2022, kampeni ya makazi bora imetekelezwa katika Mikoa 10. Nyumba zilizojengwa zimeongezeka kutoka nyumba 751 mwaka 2020/21 hadi nyumba 5,002 kufikia mwezi Aprili, 2022. Nyumba hizo zimejengwa katika Mikoa ya Arusha (683), Morogoro (2,397), Songwe (225), Shinyanga (698), Rukwa (22), Mwanza (273), Tanga (350), Ruvuma (2), Pwani (186) na Geita (166). Kampeni inalenga kufikia Mikoa 26 ifikapo mwaka 2025. **Nitumie fursa hii kuishukuru Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa miongozo ya Kiseru, OR-TAMISEMI kwa kusimamia utekelezaji wa kampeni na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hususan Shirika la Kivulini kwa kushiriki kuhamasisha jamii kuboresha makazi yao.**

24. Mheshimiwa Spika, katika kuamsha ari ya jamii kushiriki kikamilifu kwenye miradi ya kijamii kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi mwezi Aprili 2022, Maafisa Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na viongozi ngazi

mbalimbali kuanzia Taifa, Mkoa, Halmashauri hadi Kata wameendelea kuhamasisha jamii kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye Mikoa 26 ya Tanzania Bara, ambapo jamii imeshiriki kikamilifu kwenye miradi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 963 katika Mikoa ya Singida, Morogoro, Arusha, Kilimanjaro, Rukwa, Katavi, Dodoma, Dar es Salaam, Geita, Kagera, Kigoma, Lindi, Mara, Mbeya, Mtwara, Pwani, Njombe, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu, Tabora, Tanga, Iringa na Lindi.

Aidha, jamii imeshiriki katika ujenzi wa vituo 294 vya kutolea huduma za afya katika Mikoa ya Iringa, Singida, Morogoro, Arusha, Katavi, Dar es Salaam, Geita, Kagera, Kigoma, Lindi, Mara, Mbeya, Mtwara, Njombe, Pwani, Ruvuma, Rukwa, Tanga, Tabora, Simiyu na Kilimanjaro. Juhudi za ujenzi wa madarasa hayo kupitia utaratibu huu zinachangia hesabu ya madarasa kama ilivyowasilishwa na Waziri wa Nchi, OR-TAMISEMI, **Mhe. Innocent Lugha Bashungwa** wakati akiwasilisha Bungeni Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2022/23 hivyo kuleta msukumo wa maendeleo ya jamii kwenye Sekta ya Elimu.

25. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuboresha utoaji wa mafunzo ya Taaluma ya Maendeleo ya Jamii katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vya Buhare, Mlale, Misungwi, Rungemba, Mabughai, Ruaha, Uyole na Monduli kwa kusimamia ubora wa mafunzo na kuboresha miundombinu. Udahili wa wanafunzi umeongezeka kutoka wanafunzi 4,753 (Me 1,871 na Ke 2,882) mwaka 2020/21 hadi wanafunzi 5,135 (Me 2,112 na Ke 3,023) kufikia mwaka 2021/22 ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 382 sawa na asilimia 8. Aidha, mwaka 2020/21, wanafunzi 2,759 walihitimu katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ikilinganishwa na wanafunzi 3,953 waliohitimu mwaka 2019/20 sawa na upungufu wa asilimia 30 ya wahitimu. Hii ni kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kuahirisha masomo na kushindwa kulipa ada.

26. Mheshimiwa Spika, katika kutatua changamoto hizo, Wizara imefanya jitihada mbalimbali ikiwemo kuwaunganisha wanafunzi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanayosaidia wanafunzi wanaoishi katika mazingira magumu yakiwemo; *Compassion*, CAMFED, Tumaini Fund, *Black School Learning*, SEMA Singida, *King Lion* na Ngorongoro *Community-Based Organization*.

Aidha, wanafunzi wengine wamekuwa wakiunganishwa na Mikoa na Halmashauri ili kuwawezesha kuendelea na masomo kupitia mafungu ya kuwasaidia wanafunzi wasio na uwezo. Hadi Aprili 2022, jumla ya wanafunzi 29 wasio na uwezo wa kulipa ada wameunganishwa na Mashirika mbalimbali ambapo wamewezesha kuendelea na masomo yao.

27. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuboresha utoaji wa mafunzo ya Taaluma ya Maendeleo ya Jamii katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru (TICD) na Vyuho nane (8) vya Maendeleo ya Jamii (CDTIs) kwa kutekeleza dhana ya Uanagenzi ili kuzalisha wahitimu wenye weledi na umahiri unaoendana na soko la ajira. Uanagenzi (*apprenticeship*) ni programu ya kukuza ujuzi ambapo vyuo huwaunganisha wanafunzi/wahitimu wake na Kampuni, Mashirika na Taasisi mbalimbali ili waweze kupata ujuzi/kujengewa uwezo katika eneo fulani kulingana na mahitaji yao. Programu hii ilianzishwa rasmi mwaka 2019/20. Aidha, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi Ibara ya 22 (a) ukurasa wa 22 imehimiza kuongeza ujuzi wa mafunzo kwa vitendo kwa vijana ili kuwasaidia vijana kujajiri, kuajiriwa na kuajiri wengine.

28. Mheshimiwa Spika, jumla ya wanafunzi na wahitimu wa Vyuho 721 walijiunga na programu ya uanagenzi mwaka 2021/22 ambapo kati ya hao, vijana 114 sawa na asilimia 16 wamehitimu programu ya uanagenzi katika mwaka huu wa fedha na kupata ujuzi katika maeneo ya ujasiriamali, ujenzi wa barabara, usimamizi wa miradi, uandishi wa maandiko ya miradi, uelimishaji rika na ujenzi wa majengo. Aidha, kati ya hao, vijana 40 wamepata ajira (27 wamejajiri na 13 wameajiriwa katika

Kampuni na Mashirika mbalimbali) na wengine 607 bado wanaendelea na programu ya uanagenzi. Katika mwaka 2022/23, vyuo vinatarajia kupeleka wanafunzi 931 kujifunza mafunzo mbalimbali kwenye Kampuni, Mashirika na Taasisi 334. Kwa maelezo hayo, ni dhahiri kuwa Wizara imejielekeza kwenye mapinduzi ya mafunzo ili wahitimu waweze kujijiri na kuajiri.

29. Mheshimiwa Spika, Wizara inatekeleza programu ya ushirikishaji jamii zinazozunguka Taasisi na Vyuo nane vya Maendeleo ya Jamii kutatua changamoto zinazowakabili kwa kutumia rasilimali zinazowazunguka kama ifuatavyo: elimu ya lische imetolewa kwa wananchi 825 wanaozunguka Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vya Rungemba na Ruaha; na hamasa ya kilimo cha parachichi imetolewa na Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba katika Vijiji vya Kitelewasi, Itimbo na Rungemba ambapo jumla ya miche 6,120 imepandwa katika Vijiji hivyo. Pia, elimu ya ujasiriamali imetolewa kwa wananchi 376 wanaozunguka Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vya Mlale na Monduli. Aidha, mafunzo ya ufundi ujenzi yametolewa na Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ufundi Misungwi kwa mafundi 40.

Napenda kutoa wito kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii waliopo katika ngazi ya Mkoa, Halmashauri na Kata kushirikiana na wadau wengine wote na kuendelea kwa kasi zaidi kuelimisha na kushirikisha jamii kuimarika katika dhana nzima ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo.

30. Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za dhiti kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuipatia Wizara fedha za maendeleo kiasi cha **Shilingi Bilioni 3.6** kwa ajili ya ukarabati wa majengo na miundombinu katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Hatua hii itaboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Vyuo hivyo.

31. Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi zote za ushirikishaji jamii zinazofanywa na Maafisa Maendeleo

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

ya Jamii nchini, bado tunakabiliwa na changamoto ya uhaba wa Maafisa hao. Jumla ya Maafisa Maendeleo ya Jamii 5,296 wanahitajika nchini. Hadi mwezi Aprili 2022, Maafisa waliopo katika ngazi ya Mkoa, Halmashauri na Kata ni 3,014 ambapo upungufu ni Maafisa 2,282 sawa na asilimia 43 kama inavyoonesha katika **Jedwali Na. 1**. Mahitaji makubwa zaidi ya wataalam hawa yapo ngazi ya Kata ambapo kuna changamoto nyingi za jamii zinazopaswa kushughulikiwa.

Jedwali Na. 1: Idadi ya Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Ngazi Mbalimbali

NA.	NGAZI	MAAFISA WANAOHITAJIKA	MAAFISA WALIPO		JUNGUFU / ZIADA	
			IDADI	%	IDADI	%
1.	Mkoa	52	51	98	-1	-2
2.	Halmashauri	1,288	1,329	103	41	3
3.	Kata	3,956	1,634	41	-2,322	-59
	JUMLA	5,296	3,014	57	-2,282	-43

Chanzo: OR-TAMISEMI

32. Mheshimiwa Spika, ili kukabiliwa na changamoto ya upungufu wa Maafisa Maendeleo ya Jamii, Wizara itaendelea kuwasiliana na OR- TAMISEMI pamoja na OR-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili kutatua changamoto ya upungufu wa Maafisa hao katika ngazi ya Kata kwa kuwaajiri kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kadiri bajeti ya Serikali itakavyoruhusu kila mwaka.

Nitoe rai kwa Wadau wa Maendeleo yakiwemo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutoa ajira za muda kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii hususan katika ngazi ya Kata ambapo kuna upungufu mkubwa ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa afua za kutatua changamoto zinazoikabili jamii yetu. Pia, Wizara inatoa wito kwa wote wenye taaluma ya maendeleo ya jamii ambao wapo katika jamii baada ya kustaafu wajitokeze ili kuendelea kutoa mchango wao kwenye jamii kama ambavyo taaluma zingine zimekuwa zikifanya. Lengo

ni kila mzalendo mwenye nafasi na nia ya kuchangia maendeleo ya jamii apewe nafasi.

33. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Vyuo nane vya Maendeleo ya Jamii vya Buhare, Monduli, Rungemba, Ruaha, Uyole, Mlale, Misungwi na Mabughai imeendelea kutekeleza programu mbalimbali zinazolenga kukuza ubunifu na maarifa. Ubunifu na Maarifa ni programu ambayo wanafunzi na jamii inayozunguka vyuo wanapewa fursa ya kutoa mawazo yao ya kibunifu ambayo yanalenga kutatua changamoto fulani katika jamii ambapo mawazo hayo hulelewa ili yafikie hatua ya kuwa huduma au bidhaa iliyokusudiwa. Programu zinazotekelezwa katika Taasisi na Vyuo hivyo ni pamoja na: kutoa uelewa kwa wananchi kuhusu uwepo wa nafasi za kupokea na kulea mawazo ya kibunifu kwenye vituo na umuhimu wa ubunifu katika kuongeza kipato chao; kuwajengea uwezo wanafunzi na wananchi katika eneo la ubunifu kwa kuwaunganisha na wabunifu wakubwa pamoja na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali; na kuwaunganisha wabunifu na masoko kwa ajili ya kutangaza na kuuza bidhaa/huduma zinazotokana na ubunifu wao.

34. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya mawazo ya kibunifu saba (7) yameibuliwa na hivyo kuwa na jumla ya mawazo ya kibunifu 61 tangu kuanzishwa kwa dhana ya ubunifu na maarifa mwaka 2019/20. Kati ya hayo, mawazo ya kibunifu 23 (sawa na asilimia 38) yamekamilika na yapo kwenye hatua za mwisho kuwa bidhaa au huduma. Huduma/bidhaa hizo ni pamoja na: kifaa cha kugundua madini ardhini katika Chuo cha Maendeleo Jamii Ufundi Misungwi ambapo mbunifu ametengeneza sampuli kifani na Chuo kimeshirikisha Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) ili kukamilisha wazo hilo kuwa bidhaa; mashine ya kuchakata viazi katika Chuo cha Maendeleo Jamii Ufundi Misungwi ambapo Chuo kimeshirikisha SIDO

kukamilisha wazo hilo; na mashine ya kusukuma maji inayotumia nishati ya maji katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Mlale ambapo mbunifu huyo amefanikiwa kutengeneza mashine tatu na kuziua kwa kiasi cha **Shilingi Milioni 2.2** kila moja. Aidha, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru imeanzisha huduma ya **web application** kwa ajili ya kusaidia uzaji, utunzaji wa hesabu na kutangaza masoko ya bidhaa za wajasiriamali.

35. Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani kwa COSTECH kwa kutoa mafunzo ya namna ya kuanzisha, kusimamia na kuviendesha vituo vya kidijitali vya ubunifu na maarifa katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Aidha, Wizara inaendelea kushirikiana na Maafisa Maendeleo ya Jamii kuhamasisha jamii kwenda kwenye vituo vya kidijitali vya ubunifu na maarifa kwa kuonesha vipaji vya kibunifu walivyonyo vya kufanya uhamasishaji kwa Taasisi za elimu ya juu, kati na Sekondari ili kuongeza mwingi wa jamii kujiunga katika vituo hivyo. Wizara inaendelea kutafuta wadau kwa ajili ya kufadhili wabunifu kufikia malengo yao.

ENEO LA 2: HAKI NA MAENDELEO YA MTOTO

36. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba vitendo vya ukeketaji kwa watoto wa kike na wanawake vinatokomezwa, Wizara imeshirikiana na wadau kuandaa Mkakati wa Taifa wa Kutokomeza Ukeketaji utakaotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2020/21 – 2024/25. Mkakati unalenga kupunguza ukeketaji nchini kutoka asilimia 10 mwaka 2015/16 hadi asilimia 5 mwaka 2021/22 na hatimaye kutokomeza ukeketaji ifikapo mwaka 2024/25. Mkakati huo utafikia malengo yake iwapo: (i) Wasichana na wanawake watakataa vitendo vya ukeketaji; (ii) Msaada na huduma zitapatikana kwa waathirika wa ukeketaji kwa wakati; (iii) Familia zitakataa kuwatoa watoto wao wa kike kwa ajili ya kukeketwa; (iv) Jamii zitapinga na

kukataa ukeketaji ikiwemo jamii ya wanaume wa rika zote; (v) Ngariba wengi watakataa na kuacha vitendo vya ukeketaji; na (vi) Uratibu wa wadau katika kushughulikia masuala ya ukeketaji utaimarishwa. Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kutokomeza Ukeketaji utachangia katika utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008; Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000; Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 na Sheria mbalimbali zikiwemo Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 na marekebisho yake ya mwaka 2019; na Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2018.

37. Mheshimiwa Spika, ukeketaji una madhara makubwa katika maendeleo na ustawi wa jamii. Madhara hayo ni pamoja: maumivu makali kwa mtoto (ukatili wa kimwili); kutokwa damu nyingi kwa mtoto jambo linaloweza kusababisha kupoteza maisha; na kovu la kudumu linalosababisha maumivu wakati wa kujamiiana na hatimaye kupoteza hisia na kusababisha migogoro katika ndoa. Aidha, ukeketaji unaweza kusababisha kupata magonjwa kama Fistula (kutokwa na haja ndogo mara baada ya kujifungua) na maambukizi katika njia ya mkojo (UTI).

38. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa ukeketaji inaratibu utendaji wa Muungano (coalition) wa Taifa wa utekelezaji wa afua za Kutokomeza Ukeketaji Nchini. Muungano huo unajumuisha watendaji wa Wizara za Kisekta, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Wadau wengine wa masuala ya ukeketaji. Vilevile, Wizara inaratibu utekelezaji wa Maazimio na Mpango Kazi wa Kushughulikia Ukeketaji Mipakani mwa nchi za Afrika Mashariki. Mpango huo unalenga kuzuia vitendo vya ukeketaji wa kuvuka mipaka ambapo familia zinawavusha watoto kwenda nchi jirani kwa kuhofia vyombo vya dola kuwachukulia hatua. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2022 jumla ya Kamati tano (5) za Ulinzi na Usalama katika Wilaya za Tarime

(Sirari), Longido (Namanga), Mkinga (Hororo), Rombo (Holili) na Serengeti zimejengewa uwezo ili kukabiliana na vitendo vya ukeketaji wa kuvuka mipaka. Serikali kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutekeleza afua za kutokomeza ukeketaji katika mikoa yenye takwimu za juu ambayo ni Manyara kwa asilimia 58; Dodoma asilimia 47; Arusha asilimia 41; Mara asilimia 32; na Singida asilimia 31. Afua hizo zimewezesha takribani ngariba 1,800 katika mikoa hiyo kusalimisha zana za ukeketaji na kuachana na vitendo hivyo kwa kipindi cha mwaka 2015/16 hadi kufikia Aprili, 2022.

39. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na aina mpya ya Ukatili dhidi ya Watoto Mitandaoni unaosababishwa na kukua kwa maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Serikali imeunda kikosi kazi cha Taifa cha Ulinzi na Usalama wa Mtoto mtandaoni chenye lengo la kuhakikisha kuwa watoto wanalindwa dhidi ya ukatili wa mtandaoni na kuwasaidia kutumia vifaa vya kieletroniki kwa usahihi na usalama. Pia, Kikosi Kazi kina jukumu la kuratibu wadau katika Serikali na Sekta Binafsi kuhuisha masuala ya ukatili dhidi ya watoto mtandaoni na utekelezaji wa Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015 na Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009. Aidha, Serikali imeandaa machapisho/majarida ya kufundishia watoto, wazazi na walimu kuhusu ukatili wa watoto mtandaoni.

40. Mheshimiwa Spika, katika kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 na Kanuni zake, Wizara imebaini kuwa kuna uhitaji wa kuifanyia marekebisho Sheria hiyo ili iweze kuakisi mazingira ya sasa ikiwa ni pamoja na ukatili wa watoto mtandaoni (*online child abuse*). Ili kutekeleza hilo, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Mwandishi Mkuu wa Sheria) imeshaandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria na kuyawasilisha kwa wadau ili kutoa maoni ambapo tayari Wizara imeanza kupokea maoni. Mchakato wa marekebisho ya Sheria hiyo unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Desemba, 2022.

Pia, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inayosimamia Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015 inafanya mapitio ya Sera ya hali ya usalama katika mitandao ili kubaini maeneo ya kuboresha. Aidha, ifikapo mwezi Oktoba, 2022 zoezi la tathmini litakuwa limekamilika na litatoa mwelekeo wa kuandaa Sera na Sheria mpya ya Makosa ya Mtandao.

41. Mheshimiwa Spika, mwezi Machi 2022, Wizara ilizindua Taarifa ya Utafiti kuhusu Hali ya Ukatili wa Watoto Mtandaoni nchini (*Disrupting Harm Report in Tanzania*). Utafiti huo ulifanywa mwaka 2021 kwa ushirikiano wa Mashirika yafuatayo: Shirika la kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF – Tanzania), Shirika la ECPAT International na INTERPOL kwa uratibu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya usimamizi wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Aidha, nchi nyingine 12 za Afrika zilifanya utafiti kama huu kutoka Barani Afrika (Nchi 6 kutoka Mashariki na Kusini mwa Afrika na 6 Kusini Mashariki mwa Bara la Asia). Taarifa hiyo inaeleza tathmini ya kina ya hali ya ukatili nchini, athari za ukatili wa kingono, mitazamo ya watoto juu ya ukatili wa kingono mtandaoni na mwitikio wa kitaifa wa namna ya kupambana na aina hii ya ukatili. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa: -

(i) Asilimia 4 ya watumiaji wa mtandao wenye umri wa miaka 12 – 17 nchini Tanzania ni manusura wa ukatili wa mtandaoni;

(ii) Watoto wengi hufanyiwa vitendo vya ukatili kupitia mitandao ya kijamii kama vile *WhatsApp*, *Instagram*, *Facebook*, *Tik Tok*;

(iii) Wanaofanya vitendo vya ukatili ni watu wanaofahamika na watoto wakiwemo ndugu wa karibu na marafiki; na

(iv) Watoto wanaofanyiwa ukatili hawajui namna na sehemu ya kutoa taarifa ili wapate msaada.

42. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha Malezi na Makuzi Jumuishi ya Watoto wa umri wa miaka 0 - 8 ambao ndio umri muhimu sana katika ukuaji wa ubongo wa binadamu, Wizara imezindua Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT- MMMAM) itakayotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2021/22 – 2025/26). Programu hii inalenga kutatua changamoto za ukuaji na maendeleo ya watoto wenye umri wa miaka 0-8 na kuhakikisha watoto wote Tanzania wapo kwenye mwelekeo sahihi wa kufikia ukuaji timilifu. Pia, Programu ya MMMAM inalenga kuharakisha upatikanaji wa matokeo chanya kwenye malezi na makuzi ya watoto kwa kuhimiza ushiriki wa Sekta mbalimbali katika kutoa huduma za malezi jumuishi kwa watoto kwenye maeneo makuu matano (5) ambayo ni: ***Afya bora kwa Mtoto na Mama/Mlezi; Lishe ya kutosha kuanzia Ujauzito; Malezi yenye Mwitikio; Fursa za Ujifunzaji wa Awali; na Ulinzi na Usalama.*** Aidha, ili kuhakikisha programu hiyo inaleta matokeo chanya kwa watoto wadogo, itatekeleza mambo makuu manne ambayo ni: kuboresha mazingira wezeshi ili kuwezesha uratibu wenye ufanisi na utoaji wa huduma za malezi jumuishi; kuimarisha mifumo ya utoaji wa huduma jumuishi za MMMAM na uthibiti ubora; kuongeza upatikanaji wa huduma bora na zilizoratibiwa za malezi jumuishi kwa watoto wenye umri wa miaka 0-8 na walezi wao; na kuwawezesha wazazi, walezi, familia na jamii kutoa huduma za malezi jumuishi.

43. Mheshimiwa Spika, katika hatua za awali za utekelezaji wa Programu ya MMMAM, mwezi Desemba 2021, mafunzo ya uelewa kuhusu Programu hiyo yalitolewa kwa Watendaji wa Sekretarieti za Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara ambapo kila Mkoa uliwakilishwa na watendaji watano (5) wakiwemo Maafisa Maendeleo ya Jamii, Maafisa Ustawi wa Jamii, Waganga Wakuu, Maafisa Elimu na Maafisa Lishe wa Mikoa. Pia, mafunzo hayo yalitolewa kwa wanahabari vinara wa Programu hiyo ili kuwajengea uwezo wa kutoa taarifa za utekelezaji wake. Aidha, Wizara kwa

kushirikiana na wadau ilijenga hamasa kwa Waheshimiwa Wabunge ambao wameanzisha Kikundi cha Wabunge Vinara (*champions*) wapatao 30 kuwa Mabalazi katika kusukuma Ajenda ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto ndani na nje ya Bunge. Kikundi hicho kinaongozwa na **Mhe. Dkt. Pius Chaya** (Mwenyekiti), **Mhe. Esther Matiko** (Makamu Mwenyekiti) na **Mhe. Justine Nyamoga** (Katibu). Aidha, kikundi hicho kimeandaa Katiba na Mpango Mkakati wa Miaka Mitatu (3) utakaowaongoza katika kutekeleza majukumu yao. **Nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge hawa kwa kujitolea kusukuma Ajenda hii muhimu katika Nchi yetu inayolenga kuimarisha malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya Mtoto.**

44. Mheshimiwa Spika, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la BRAC Maendeleo imeratibu ujenzi wa Vituo 30 vya mfano vya Kijamii vya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (*Community-Based Early Childhood Development Centers*) katika Mikoa ya Dar es Salaam (10) na Dodoma (20). Vituo hivyo vina lengo la kutoa huduma jumuishi za Malezi na Makuzi kwa Watoto walio na umri kuanzia miaka miwili (2) hadi chini ya miaka mitano (5) kwa kuwapatia huduma jumuishi za afya, lishe, ulinzi, ujifunzaji na uchangamshi wa awali kabla ya kujiunga na darasa la awali. Katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya Vituo vya mfano 15 kati ya 30 vimeanza kufanya kazi na jumla ya watoto 883 (Wavulana 426 na Wasichana 457) wamesajiliwa na kupatiwa huduma katika Vituo hivyo kama inavyoonesha katika **Kiambatisho Na. 1**. Aidha, vituo hivyo vitatumika kama mfano katika ujenzi wa vituo vingine vitakavyojengwa katika Vijiji/Mitaa yote ya Tanzania Bara.

45. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha Programu hii ina mfumo madhubuti wa kukusanya na kutunza taarifa za utekelezaji, Wizara kwa kushirikiana na UNICEF

na Wataalam wa Mifumo kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam imetengeneza Dashbodi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (*ECD Dashboard*) ambayo itawezesha ukusanyaji na utunzaji wa taarifa mbalimbali zinazohusu masuala ya Lishe, Afya, Fursa za Ujifunzaji wa Awali, Malezi yenye Mwitikio, Ulinzi na Usalama kwa Watoto wenye umri kati ya miaka 0-8. Aidha, Dashbodi hii imeunganishwa na mifumo mbalimbali inayotoa taarifa zinazohusu watoto wadogo.

46. Mheshimiwa Spika, katika kushughulikia changamoto zinazowakabili vijana balehe wenye umri wa kati ya miaka 10 - 19, Wizara imeandaa na inatekeleza Ajenda ya Kitaifa ya Kuwekeza katika Afya na Maendeleo kwa Vijana Balehe nchini (2021/22-2024/25). Ajenda imeandaliwa kwa ajili ya kutatua changamoto za upatikanaji wa huduma rafiki za afya na kuondoa vikwazo vya maendeleo kwa vijana balehe nchini ambapo makadirio ya idadi ya vijana balehe kwa mwaka 2020 ni milioni 13 sawa na asilimia 23 ya watu wote nchini. Ajenda hii imejikita katika nguzo kuu sita (6) ambazo ni: Kuzuia Maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI; Kutokomeza Mimba za Utotoni; Kuzuia Ukatili wa Kimwili, Kisaikolojia na Kingono; Kuboresha Lishe, Kuhakikisha Watoto wa Kike na Kiume Wanabaki Shule; na Kuwajengea Vijana Balehe Ujuzi na Uwezo wa Kufikia Fursa za Kiuchumi.

Ajenda imejikita katika kutekeleza afua za kipaumbele zitakazoleta matokeo makubwa katika kipindi cha muda mfupi na muda wa kati. Pia, afua saidizi na afua nyinginezo zitakazoibuka zitatekelezwa katika muda wa kati na muda mrefu. Afua zinazohitajika katika kuboresha afya na maendeleo ya vijana balehe zinagusa maeneo mahsusi ya **Mahitaji, Usambazaji na Mazingira Wezeshi**. Kwenye eneo la **Mahitaji**, afua zinalenga kuboresha elimu, kupunguza kiwango cha umaskini, kupunguza athari zitokanazo na mila na desturi zenye viashiria vya kibaguzi katika jamii. Kwa upande wa **Usambazaji**, afua zinalenga kuongeza wigo

wa huduma bora na rafiki za afya kwa vijana balehe. Aidha, **Mazingira Wezeshi** yanalenga kutoa elimu na ujuzi kwa vijana ili kuondokana na vikwazo vinavyosababisha vijana balehe kushindwa kushiriki katika shughuli za kijamii, kiuchumi na kiutamaduni. Katika kuratibu na kutekeleza Ajenda hii, Wizara kwa hisani ya Shirika la UNICEF imeajiri Mtaalam Mshauri (*Individual Consultant*) kwa kipindi cha mwaka mmoja (Mei, 2022 - Aprili, 2023) ili kwa kushirikiana na Wataalam wa Wizara kuratibu na kusimamia utekelezaji wa ajenda hiyo. Vilevile, Mtaalam huyo atawajengea uwezo wataalam wetu katika uratibu na utekelezaji wa Ajenda hii baada ya kumaliza muda wake.

Uratibu na utekelezaji wa Ajenda utakuwa jumuishwa na **utahusisha wajumbe kutoka Wizara za Kiseka, Idara za Serikali, Vijana balehe na Sekta Binafsi** ikiongozwa na Wizara mtambuka na yenye dhamana ya watoto na vijana balehe Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Uratibu utakuwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kupitia kamati elekezi ya Taifa ambayo itawahusisha Makatibu Wakuu wa Taasisi za Serikali.

47. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha Elimu ya Malezi Chanya kwa Wazazi na Walezi, Wizara kupitia Kitini cha Elimu ya Malezi katika Familia imetoa elimu ya malezi chanya katika mikoa nane (8) ya Kigoma, Kilimanjaro, Songwe, Iringa, Mwanza, Tanga, Mtwara na Mbeya ambapo jumla ya wazazi/walezi 800,000 walifikiwa. Vilevile, Wizara imeandaa Ajenda ya Taifa ya Wajibu wa Wazazi na Walezi katika Matunzo ya Watoto na Familia. Kupitia Ajenda hiyo Wizara imeandaa jumbe mahsusi za kuelimisha wazazi wote wawili kushiriki kikamilifu katika malezi ya watoto. Ajenda imeandaliwa katika nguzo tatu ambazo ni: (i) Mjali Mtoto kwa kumpatia huduma zote za msingi; (ii) Mlinda Mtoto dhidi ya Ukatili; na (iii) Wasiliana na Mtoto mara kwa mara ili kuwa huru kueleza changamoto za makuzi yake na maendeleo kwa ujumla.

48. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha jumbe hizo zinafika kwa wazazi na walezi wengi na kwa ubora, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la PACT Tanzania na NIMR Mwanza imetambulisha na kufanya utafiti wa mbinu mpya ya utoaji elimu ya malezi kwa njia ya kidijitali kupitia simu zenye programu tumizi (*apps*) katika Mikoa ya majaribio ya Mwanza na Shinyanga. Programu tumizi itawezesha wazazi na walezi kupata ujuzi wa malezi bora na kubadilishana taarifa za malezi, makuzi na ulinzi wa watoto katika ngazi ya familia na jamii. Programu hiyo imezinduliwa mwezi Mei 2022 na itasambazwa katika mikoa yote nchini kuanzia mwezi Julai, 2022.

49. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha watoto wanapata haki ya kushiriki na kushirikishwa kwenye masuala yanayowahusu, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeanzisha Mabaraza ya Watoto kuanzia ngazi ya Mtaa/Kijiji, Mkoa na Taifa. Mabaraza ya Watoto ni jukwaa la watoto lililoanzishwa kwa lengo la kuwashirikisha watoto katika masuala yanayowahusu ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa na Kikanda ambayo nchi yetu ilisaini na kuridhia. Aidha, ni utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008, inayobainisha Haki ya Kushiriki kuwa ni moja ya haki za msingi za Watoto.

50. Mheshimiwa Spika, Mabaraza ya Watoto ni jukwaa linalotumika katika kuwaelimisha watoto masuala mbalimbali yanayohusu maisha yao ya sasa na baadaye nje ya mfumo rasmi wa elimu, ikiwa ni pamoja na uongozi, uadilifu, uzalendo kwa Taifa lao na masuala mengine mtambuka ikiwa pamoja na VVU na UKIMWI, mazingira, stadi za kazi na usawa wa Kijinsia. Mabaraza ya Watoto yameimarisha uwezo wa watoto katika kujitambua, kujiamini, kujieleza na kujilinda dhidi ya ukatili wa aina mbalimbali. Wizara imeanzisha Mabaraza ya Watoto katika ngazi ya Mtaa/Kijiji, Mkoa na Taifa. Hadi Aprili 2022, jumla ya Mabaraza ya Watoto 2,669 yameanzishwa nchini ikiwa pamoja na Baraza la

Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Baraza hilo linalojumuisha wajumbe wawili (2) kutoka katika kila mkoa kwenye Mikoa 26 ya Tanzania Bara na wajumbe 10 kutoka Tanzania Visiwani kwa kuzingatia uwiano wa jinsi zote.

51. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto za uundaji wa Mabaraza ya Watoto, Serikali imefanya mapitio ya Mwongozo wa uundaji na uimarishaji wa Mabaraza ya Watoto wa mwaka 2010 ili kuboresha maeneo yaliyokuwa na changamoto. Moja ya eneo lililoboreshwa ni muundo wa mabaraza hayo kupelekwa katika ngazi za shule badala ya kuwa ni jukumu la Kijiji/Mtaa ambapo ufanisi wake umekuwa mdogo. Hivyo, Baraza la Watoto katika ngazi ya chini litakuwa katika shule za msingi na sekondari zilizopo katika Kijiji/Mtaa husika sambamba na uanzishwaji wa Klabu za Watoto shuleni. Uratibu na usimamizi wa Mabaraza ya Watoto utafanywa na Maafisa Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na Afisa Elimu Wilaya na Kata kwa usaidizi wa Mkuu wa Shule au Mwalimu Mkuu. Kupitia Mabaraza hayo, watoto wamepata fursa ya kushiriki kwenye majukwaa mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa na kutoa maoni kwenye nyaraka mbalimbali kama vile maandalizi ya Ajenda ya Wajibu wa Wazazi na Walezi katika Malezi Bora ya Familia na Watoto ya mwaka 2021. Aidha, mwezi Februari, 2022 wajumbe wa Baraza la Watoto la Taifa walipata fursa ya kipekee ya kushiriki katika kutoa maoni ya maboresho ya Mtaala wa Elimu kwa Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ufundi Nchini unaoratibiwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta imedhamiria kuhakikisha watoto wa Taifa hili wanakuwa na ufahamu wa kutosha wa mambo yanayowahusu na hakuna anayekatisha ndoto zao kwa kutumia mwanya wa watoto kutofahamu haki zao.

52. Mheshimiwa Spika, Wizara imeratibu uandaaji wa Mwongozo wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto

ndani na nje ya shule. Dawati hilo linaundwa na Watoto Vinara wanaochaguliwa na Watoto wenzao chini ya usimamizi wa Maafisa Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na Mkuu wa Shule kwa lengo la kuwezesha watoto kutoa taarifa za vitendo vya ukatili na kuweza kubainisha viashiria vya ukatili ili wapate huduma stahiki kwa wakati. Mwongozo huo umefanyiwa majaribio kwa kuanzisha Madawati 185 katika Halmashauri tatu (3) za Mkoa wa Rukwa (Nkasi, Sumbawanga na Mlele). Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI pamoja na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tumekubaliana kuendelea kuanzisha Madawati ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto kwenye Shule za Msingi na Sekondari nchini kuanzia mwezi Julai, 2022. Utekelezaji wa Mwongozo huu unaenda sambamba na Mwongozo wa Malezi, Unasihi na Ulinzi wa Mtoto Shuleni na kwenye Vyuo vya Ualimu ulioandaliwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na kuanza kutumika Mwaka 2020.

ENEO LA 3: HUDUMA ZA USTAWI WA JAMII

53. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha huduma za ustawi wa jamii kwa watoto, Wizara imeendelea kutoa huduma kwa watoto waliokinzana na sheria katika Halmashauri zote hapa nchini. Kwa kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya watoto 2,109 (Me 1,715 na Ke 394) walipatiwa huduma mbalimbali ikiwemo marekebisho ya tabia, unasihi, chakula, malazi, mavazi, huduma za matibabu, msaada wa kisaikolojia na wa kisheria na wengine kuwekwa chini ya uangalizi wa Maafisa Ustawi wa Jamii. Hadi kufikia mwezi Aprili 2022, jumla ya watoto 127 (Me 115 na Ke 12) walifuzu programu za marekebisho ya tabia ikilinganishwa na watoto 82 (Me 77 na Ke 5) kwa mwaka 2020/21. Aidha, Wizara imetoa huduma kwa watoto 257 (Me 232 na Ke 25) katika Mahabusu za Watoto tano (5) za Mbeya, Kilimanjaro, Tanga, Arusha na Dar es Salaam ikilinganishwa na watoto 413 (Me 380 na Ke 33) mwaka 2020/21 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 2**.

Jedwali Na. 2: Mwenendo wa Watoto walio katika Mahabusu za Watoto.

MWAKA	WASICHANA	WAVULANA	JUMLA
2015/16	37	349	386
2016/17	18	237	255
2017/18	13	278	291
2018/19	34	320	354
2019/20	18	120	138
2020/21	33	380	413
Aprili, 2022	25	232	257

Chanzo: WMJJWM

Kupungua kwa idadi ya watoto katika Mahabusu za Watoto kunatokana na kuanzishwa kwa Programu za Kijamii za marekebisho ya tabia kwa watoto wanaokinzana na sheria ambayo inawachepusha watoto waliofanya makosa ya jinai kwa kutowashtaki Mahakamani na kuwaunganisha na huduma ya marekebisho ya tabia.

54. Mheshimiwa Spika, Wizara pia imeendelea kusimamia huduma ya marekebisho ya tabia kwa watoto waliobainika kufanya makosa ya jinai kupitia Shule ya Maadilisho Irambo Mbeya. Hadi kufikia mwezi Aprili 2022, watoto tisa (9) kutoka Shule hiyo wameunganishwa na familia zao katika Mikoa ya Njombe, Shinyanga, Iringa na Arusha baada ya kukamilisha hukumu za marekebisho ya tabia. Watoto hao ni miongoni mwa watoto 296 (Me 280 na Ke 16) waliopewa hukumu ya marekebisho ya tabia kupitia Mahakama mbalimbali za Watoto nchini baada ya kupatikana na hatia kwa makosa ya jinai ikilinganishwa na watoto 219 (Me 210 na Ke 9) waliopatiwa huduma hiyo mwaka 2020/21. Shule hii inatoa marekebisho ya tabia kwa watoto na kuwapatia ujuzi ili wanapokamilisha hukumu zao waweze kujitegemea na kuwa raia wema. Ninapenda kuwapongeza watumishi kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhakikisha kwamba watoto

waliokinzana na sheria wanarejea kuwa na maadili mema na kuwa raia wema.

55. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha upatikanaji wa haki kwa watoto wanaokinzana na sheria, Wizara imefanya ufuatiliaji katika Magereza yaliyopo Mikoa ya Rukwa, Katavi, Dar es Salaam, Morogoro na Dodoma. Ufuatiliaji huu umewezesha watoto 16 kuachiwa huru kutoka Gereza Kuu la Segerea na kuwekwa chini ya uangalizi wa Maafisa Ustawi wa Jamii, Jijini Dar es Salaam. Watoto hao kesi zao zimekamilika ambapo baadhi yao wamepewa adhabu kulingana na kesi zao na kutozwa faini na wengine walipewa adhabu ya huduma kwa jamii. Mtoto mmoja (1) kati yao amepata ufadhili kutoka Kanisa la *Assemblies of God* Dar es Salaam kwa ajili ya kusoma masomo ya uchungaji ambapo ameshajiunga Chuo cha Uchungaji Mtama - Lindi.

56. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kuratibu huduma kwa Watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi hapa nchini ambapo jumla ya watoto 218,369 (Me 85,699 na Ke 132,670) walitambuliwa na kupewa huduma mbalimbali zikiwemo msaada wa Bima za Afya, Ada, Lishe, vifaa vya shule, kuunganishwa na familia pamoja na msaada wa kisaikolojia na matibabu. Huduma hizo zimetolewa kwa kushirikiana na Halmashauri na wadau mbalimbali. Hata hivyo, bado nchi yetu inakabiliwa na uwepo wa watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani.

57. Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanyika mwezi Julai 2021 katika mikoa sita (6) ya Dodoma, Mwanza, Dar es Salaam, Mbeya, Arusha na Iringa ulibaini uwepo wa watoto 5,732 (Me 4,583 na Ke 1,149) wanaoishi na kufanya kazi mitaani. Sababu kuu za uwepo wa watoto hao ni pamoja na kuvunjika kwa ndoa, malezi hafifu kwa familia, msongo rika kati ya watoto wenyewe na umaskini wa kaya. Wengi wa watoto hao hukimbilia maeneo ya mijini na kufanya kazi mbalimbali zikiwemo

kuosha magari, kuombaomba, kuuza bidhaa ndogondogo na wengine kuajiriwa katika kazi hatarishi ambazo zinadumaza maendeleo yao na kuwakosesha haki za msingi ikiwemo shule, malezi na afya bora.

58. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na wadau mbalimbali iliandaa hafla ya kihistoria ya chakula cha hisani kwa ajili ya kula pamoja na watoto waishio na kufanya kazi mtaani katika Jiji la Dar es Salaam. Lengo la hafla hiyo iliyofanyika mwezi Machi 2022 lilikuwa ni kuwaonesha watoto hao kuwa Serikali ipo pamoja nao licha ya changamoto wanazokumbana nazo. Pia, hafla hiyo ililenga kuwasilikiza na kupokea maoni na mapendekezo yao kupitia umoja wao pamoja na kutambua vipawa na vipaji vyao kupitia burudani, michezo na nyimbo mbalimbali zenye ujumbe mahsus walizoimba wakati wa hafla na mwisho kupata mapendekezo ya pamoja ya namna bora ya kumaliza tatizo hilo.

Kupitia hafla hiyo, Wizara iliunda kikosi kazi chenye wajumbe kutoka Serikalini na Asasi za Kiraia kwa lengo la kutoa ushauri wa kitalaam wa namna ya kutatua tatizo la watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani. Kikosi kazi hicho kimeanza kazi na Wizara imekipatia Hadidu za Rejea ili kuja na ushauri wa namna bora zaidi ya kutokomeza tatizo la watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani hapa nchini. Kikosi kazi hicho kipo chini ya Mwenyekiti **Bw. David Mulongo**, Mkurugenzi wa Shirika la SOS Tanzania. Vilevile, namshukuru sana **Mhe. Amos Makalla**, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ambapo Mkoa huo utakuwa wa mfano katika kukabiliana na changamoto ya watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani.

59. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 kama ilivyofanyiwa urekebu mwaka 2019, Kifungu cha 9 (3) kimetoa wajibu kwa mzazi na mlezi kumlinda na kumtunza mtoto katika

maisha yake ya kila siku. Aidha, Kifungu cha 14 cha Sheria hiyo kimetoa adhabu kwa mtu yoyote atakayekiuka au kuvunja Sheria. Wizara imejipanga kuongeza kasi ya kuwafikia wazazi ambao hawakuwajibika ili hatua za kisheria zichukuliwe kwa wengi zaidi hivyo, natoa wito kwa kila mzazi kuhakikisha anatekeleza wajibu wake au kwa namna yoyote ile anahakikisha havunji sheria ya mtoto kwa kuweka mazingira mazuri ya mtoto husika. Aidha, natoa wito kwa Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto zilizopo ngazi zote kutekeleza majukumu yao kikamilifu na kuhakikisha wananchi wanazijua na kuzitumia. Lengo ni kila mtoto aishi maisha ya stahiki yake.

60. Mheshimiwa Spika, huduma za malezi ya kambo na kuasili zimeendelea kutolewa kwa watoto wasio na wazazi, walezi au ndugu. Huduma hii inalenga kuhakikisha kuwa watoto wanalelewa katika mazingira endelevu ya familia. Katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya watoto 46 (wavulana 27 na wasichana 19) walipata huduma ya malezi ya kambo na watoto 45 (wavulana 28 na wasichana 17) waliasiliwa. **Natoa rai kwa wananchi wenye mapenzi mema kuwasilisha maombi ya kulea watoto wenye uhitaji wa malezi ya familia.**

61. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu huduma ya uendeshaji wa makao ya watoto hapa nchini. Katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya Makao 118 yamesajiliwa yakiwa na jumla ya watoto 1,524 (Me 668 na Ke 856). Idadi hii imewezesha kuwa na jumla ya Makao ya Watoto 301 yaliyosajiliwa nchini yakihudumia jumla ya watoto 11,341 (Me 5,713 na Ke 5,628). Aidha, Wizara imeendelea kusimamia Makao ya Watoto yanayomilikiwa na Serikali ambayo ni Makao ya Taifa ya Watoto Kikombo (Dodoma) yenye uwezo wa kuwahudumia watoto 250 na Kurasini Dar es Salaam yenye uwezo wa kuhudumia watoto 100 walio katika mazingira hatari. Makao ya Taifa Kikombo ni ya mfano kwa ukanda wa Afrika

Mashariki. Ndani ya makao hayo kuna kituo cha kulelea watoto wadogo mchana ambacho kinahudumia watoto wanaozunguka eneo la makao. Pia makao yana maktaba, ukumbi wa mikutano, viwanja vya michezo mbalimbali, karakana, eneo la shamba lenye ukubwa wa hekari 15 na zahanati inayohudumia watoto na wananchi. ***Ninachukua fursa hii kuwapongeza Taasisi ya Abbott Fund Tanzania kwa msaada wao mkubwa wa kifedha katika kujenga makao haya ya Kikombo na ununuzi wa vifaa.***

62. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia huduma za malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana (Day Care Centers). Katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi Aprili 2022, Wizara imetoa leseni za uendeshaji kwa vituo 362 vikiwa na jumla ya watoto 9,638 (Wavulana 4,083 na Wasichana 5,555) wanaopata huduma ya malezi. Idadi hiyo imewezesha kuwa na jumla ya vituo 2,512 vilivyosajiliwa nchini ambavyo vinahudumia jumla ya watoto 173,032 (Wavulana 82,302 na Wasichana 90,730) kama inavyoonesha katika **Jedwali Na. 3.**

Jedwali Na. 3: Mwenendo wa Uandikishaji Watoto kwenye Vituo vya Kulelea Watoto Wadogo Mchana

MWAKA	WASICHANA	WAVULANA	JUMLA
2015/16	34,981	33,016	67,997
2016/17	39,790	33,791	73,581
2017/18	51,711	49,312	101,023
2018/19	76,094	72,999	149,093
2019/20	82,539	76,940	159,479
2020/21	85,175	78,219	163,394
Aprili, 2022	90,730	82,302	173,032

Chanzo: WMJJWM

Aidha, Wizara imeendelea kuboresha utoaji wa huduma katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana kwa kutoa mafunzo kazini kwa Wamiliki wa Vituo na Walezi wa Watoto 1,566 (Me 431 na Ke 1,135) katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Tabora, Shinyanga, Pwani,

Shinyanga na Iringa ili kuimarisha stadi za uchangamshi wa awali na makuzi ya watoto wadogo pamoja na kutoa ulinzi wa uhakika kwa watoto wakiwa vituoni.

63. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia vyuo 33 vinavyotoa Mafunzo ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto vilivyotambuliwa na kupewa vibali vya kuendesha mafunzo hayo. Kati ya vyuo hivyo, chuo kimoja ni cha Serikali kilichopo Kisangara mkoani Kilimanjaro kinachotoa taaluma ya malezi na makuzi ya awali ya mtoto katika ngazi ya stashahada na vyuo 32 ni vya Watu Binafsi.

64. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa na matunzo kwa watoto walio kwenye ndoa zenye migogoro na waliozaliwa nje ya ndoa kupitia Mabaraza ya Usuluhishi wa Ndoa nchini. Kwa kutambua hili, Serikali imeendelea kufanyia kazi mashauri ya migogoro ya ndoa kupitia Mabaraza ya Usuluhishi ambapo kwa kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya mashauri ya migogoro ya ndoa 39,571 yalipokelewa. Kati ya mashauri hayo, mashauri ya migogoro 4,576 yalifikishwa mahakamani, mashauri ya migogoro 19,262 yalisuluhishwa na kuwawezesha wanandoa kupata haki zao na mashauri 15,718 yanaendelea. ***Natoa wito kwa wanandoa kuzingatia kujifunza maadili ya ndoa kabla ya kupanga harusi kwani itaepusha migongano na migogoro ambayo mwisho wake inaumiza watoto wasio na hatia.***

65. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kuratibu uimarishaji wa utoaji wa Huduma za Ushauri na Msaada wa Kisaikolojia kwa familia na jamii. Huduma hii hutolewa kwa watu wenye misongo ya mawazo, manusura wa vitendo vya ukatili pamoja na migogoro ya ndoa na familia. Kwa kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya wahudumiwa 545,501 katika Makazi ya Wazee, Nyumba Salama, Mahabusu za Watoto, Makao ya

Watoto, Vituo vya Mkono kwa Mkono, waathirika wa majanga mbalimbali ikiwa ni pamoja na UVIKO- 19, Janga la moto katika Soko la Karume, manusura wa vita vya Ukraine waliorejea nchini na wazazi wao, wanandoa na wanajamii mmoja mmoja aliyehitaji huduma hii. Aidha, Taasisi ya Ustawi wa Jamii - Dar es Salaam imeanzisha Kituo cha Msaada wa Kisaikolojia na Kijamii kwa lengo la kutoa huduma kwa wanafunzi, wafanyakazi na jamii kwa ujumla. Huduma hizi za Msaada wa Kisaikolojia zinatolewa na Maafisa Ustawi wa Jamii katika Halmashauri na vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Wizara imeweka wazi simu za wataalam wake ngazi zote kuanzia Wizarani, Mikoani hadi Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kusogeza wataalam hao karibu na jamii kwa njia ya teknolojia ya mawasiliano ya simu. Wananchi wengi wameendelea kuwasiliana na wataalam hawa na kupata msaada wa huduma za unasihi hata wakiwa mbali. Hii ni sambamba na **Simu Namba 116** bila malipo ambapo mamilioni ya wananchi wanaoona au kuhisi mazingira ya ukatili hutoa taarifa na kupata msaada na huduma ya unasihi.

66. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kuratibu uendeshaji wa Makazi ya Wazee hapa nchini. Kupitia huduma hii Wizara inaratibu makazi 14 yanayoendeshwa na Serikali ambapo hadi kufikia mwezi Aprili 2022, wazee wasiojiweza 271 (Me 160 na Ke 111) wamehudumiwa katika makazi hayo kama inavyoonesha katika **Kiambatisho Na. 2**. Aidha, Wizara imeendelea kuratibu Makazi ya Wazee yanayoendeshwa na watu binafsi na wakala wa hiari 20 yanayohudumia wazee wasiojiweza 451 (Me 216 na Ke 235). Wazee wasiojiweza wamekuwa wakiongezeka na kupungua kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na baadhi ya wazee kuunganishwa na familia zao pamoja na vifo. Hata hivyo, pamoja na huduma zinazotolewa, baadhi ya Makazi ya Wazee ya Serikali yanakabiliwa na uchakavu wa majengo na miundombinu. Wizara inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuendelea kuboresha

majengo na miundombinu kwenye Makazi ya Wazee Misufini yaliyopo Wilaya ya Muheza mkoani Tanga. Makazi haya yakijengwa na kukarabatiwa yatakuwa ya mfano hapa nchini.

67. Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kuboresha huduma kwa wazee, Serikali ina mpango wa kuanzisha Makazi ya Wazee Kikanda. Lengo ni kuhakikisha tunaboresha zaidi huduma kwa Wazee na kuwezesha kuwa na Makazi ya Wazee kwa uwiano wa kikanda. Awali huduma zilikuwa zinatolewa kwenye Makazi ya Wazee yaliyopo katika Mikoa mbalimbali bila kuzingatia uwiano wa Kikanda. Aidha, baadhi ya Mikoa ina Makazi zaidi ya moja, uwepo wa Wazee wachache kwenye Makazi na kukosekana wahudumu wa kutosha. Wizara inaendelea kutoa elimu kwa jamii ili familia ziweze kuwalea wazee wao na wale wachache watakaokosa huduma katika familia kupata matunzo katika makazi hayo. Vilevile, Serikali ipo katika mchakato wa kuanzisha miradi katika Makazi ya Wazee ili yaweze kupunguza utegemezi kwa Serikali.

68. Mheshimiwa Spika, Wizara inaratibu uanzishaji na uendeshaji wa Mabaraza ya Wazee nchini. Kwa kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi mwezi Aprili 2022, Wizara imeratibu uundwaji wa Baraza la Taifa la Ushauri la Wazee lenye wajumbe 31 ambapo watano (5) ni viongozi wa kitaifa na 26 ni wajumbe/wawakilishi kutoka kila Mkoa. Uzinduzi wa Baraza hilo ulifanyika rasmi tarehe 11 Machi, 2022 Jijini Dodoma. Vilevile, Wizara imekamilisha uundwaji wa Mabaraza ya Wazee katika mikoa ya Geita, Pwani, Rukwa na Njombe na hivyo kufikia lengo la kuwa na jumla ya Mabaraza 20,749 katika Mikoa 26 ya Tanzania Bara. Mabaraza hayo hutumika kama majukwaa ya wazee kwa ajili ya kujadili masuala yanayohusu haki zao pamoja na ushirikishwaji katika masuala yanayohusu maendeleo. Tarehe 17 – 19 Mei 2022, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la HelpAge International tuliwezesha Baraza la Wazee la Taifa kufanya kikao jijini Dodoma kwa lengo

la kukusanya maoni ya mapitio ya Rasimu ya Sera ya Wazee pamoja na rasimu ya Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Mabaraza ya Wazee nchini. Aidha, jumla ya Wazee 1,547,038 wametambuliwa katika Mikoa 26 na kati yao wazee 937,266 wamepatiwa vitambulisho/ Bima ya Afya kwa ajili ya matibabu. Sambamba na hilo jumla ya madirisha 2,335 ya kutolea huduma kwa wazee yametengwa katika hospitali na vituo vya umma vya kutolea huduma za afya kote nchini. Pia, Wizara imeendelea kuratibu maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wazee Duniani yanayofanyika tarehe 1 Oktoba kila mwaka ambapo kwa mwaka 2021 maadhimisho hayo Kitaifa yalifanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa Mkoa wa Dodoma. Jumla ya Wazee 291 kutoka katika Halmashauri nane (8) za Mkoa wa Dodoma walishiriki maadhimisho hayo ambapo Wazee 135 walipatiwa huduma za afya. Natoa shukrani za pekee kwa wadau wa masuala ya wazee wakiwemo HelpAge International na REDESO kwa ushiriki wao mkubwa katika kuwezesha shughuli mbalimbali za wazee. Aidha, naishukuru Wizara ya Afya kuendelea kusimamia upatikanaji wa huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

69. Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi zote za utoaji wa huduma za ustawi jamii zinazofanywa na Maafisa Ustawi wa Jamii nchini, bado tunakabiliwa na changamoto ya upungufu wa Maafisa 22,395 ambayo ni sawa na asilimia 97% ya Maafisa wanaotakiwa kama inavyoonesha katika **Jedwali Na. 4**.

Jedwali Na. 4: Idadi ya Maafisa Ustawi wa Jamii katika Ngazi Mbalimbali

NA.	NGAZI	MAAFISA WANAOHITAJIKA	MAAFISA WALIOPO		UPUNGUFU	
			IDADI	%	IDADI	%
1.	Mkoa	26	26	100	0	-
2.	Hospitali za Rufaa za Mkoa	168	35	20.8	-133	- 79
3.	Halmashauri	1,472	490	33.3	-982	- 67
4.	Hospitali za Wilaya	549	65	11.8	-484	- 88
5.	Kata/Vituo vya Afya	4,494	115	2.56	-4,379	- 97
6.	Kijiji/Mtaa / Zahanati	16,426	9	0.05	-16,417	- 100
<i>JUMLA</i>		23,135	740	3.2	-22,395	- 97

Chanzo: *OR-TAMISEMI*

70. Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa Maafisa Ustawi wa Jamii, Wizara itaendelea kuwasiliana na OR- TAMISEMI pamoja na OR-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili kutatua changamoto ya upungufu wa Maafisa hao hususan katika ngazi ya Kata kwa kuwaajiri kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kadiri bajeti ya Serikali itakavyoruhusu kila mwaka.

Nitoe rai tena kwa Wadau wa Maendeleo yakiwemo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutoa ajira za muda kwa Maafisa Ustawi wa Jamii hususan katika ngazi ya Halmashauri, Kata na Kijiji/Mtaa ambapo kuna upungufu mkubwa ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa afua za kutatua changamoto za ustawi wa jamii nchini.

ENEO LA 4. MAENDELEO YA JINSIA NA UWEZESHAJI WANAWAKE

71. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza ajenda ya usawa wa kijinsia, Wizara ilifanya uzinduzi wa Kamati ya Ushauri ya Kitaifa ya Utekelezaji wa Ahadi za Nchi kuhusu Kizazi Chenye Usawa (*Generation Equality Forum - GEF*) tarehe 16 Desemba, 2021 Jijini Dodoma ambapo Mgeni Rasmi alikuwa **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kamati hiyo ina

wajumbe 25 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar. Pia, Sekretarieti ya GEF imeanzishwa kwa ajili ya kuratibu shughuli za kila siku za Jukwaa hilo. Katika kutekeleza malengo ya Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa, Tanzania imechagua kuwa kinara wa utekelezaji wa eneo la Haki na Usawa wa Kiuchumi. Aidha, Wizara inaendelea kuratibu ukamilishaji wa Andiko la Programu ya Utekelezaji wa Ahadi za Nchi kuhusu Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa ili iweze kuzinduliwa mwishoni mwa mwezi Juni, 2022. Sambamba na hilo, Wizara inaratibu maandalizi ya Mwongozo wa Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi utakaowezesha uundaji na uhuishaji wa Majukwaa hayo kuanzia ngazi ya Kijiji/Mtaa hadi Taifa ambao unatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 30 Juni, 2022. Mwongozo huo utakapokamilika na kuanza kutumika utachochea ufanisi wa utendaji kazi wa Majukwaa hayo na hivyo kuongeza kasi ya jitihada za Serikali katika kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi na kiuongozi. Vilevile, Jukwaa la Kitaifa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi linatarajiwa kuundwa na kuzinduliwa ifikapo tarehe 30 Juni, 2022 baada ya kukamilika kwa zoezi la kuhuisha majukwaa katika ngazi za miko.

72. Mheshimiwa Spika, Wizara imekamilisha Kanzidata inayolenga kuwezesha ukusanyaji na utunzaji wa taarifa zinazohusu wasifu, ujuzi na utaalum wa Wanawake katika nyanja mbalimbali hapa nchini ambapo uzinduzi wake ulifanyika tarehe 8 Machi, 2022 katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani. Kanzidata hii itawezesha utambuzi wa wanawake wenye sifa za kushika nafasi za uongozi na maamuzi ndani na nje ya nchi. Hadi kufikia mwezi Aprili 2022, jumla ya wanawake 978 walikuwa wamejisajili kwenye kanzidata hiyo kupitia <https://twl.jamii.go.tz>. Kanzidata hii inahusisha utunzaji wa taarifa za wanawake wenye wasifu mbalimbali kutoka Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

73. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inalo jukumu la kuratibu maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ambayo hufanyika kila mwaka ifikapo tarehe 8 Machi. Kwa mwaka 2022, Tanzania iliadhimisha Siku hii ambapo maadhimisho ya kimkoa yalifanyika katika Mikoa yote 26 Tanzania Bara. Wizara ilishiriki maadhimisho hayo katika mikoa ya Dodoma, Shinyanga na Arusha. Kaulimbiu ya maadhimisho kwa mwaka 2022 ilikuwa **“Kizazi cha Haki na Usawa kwa Maendeleo Endelevu: Tujitokeze Kuhesabiwa”**. Kaulimbiu hii ililenga kuhamasisha uwajibikaji kwa wote katika kuleta usawa wa kijinsia pamoja na kukumbushana umuhimu wa usawa wa kijinsia katika kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo jumuishi. Kaulimbiu ilitoa fursa ya kutathmini utekelezaji wa Maazimio na Mikataba ya Kimataifa, Kikanda na Kitaifa yenye lengo la kuimarisha jitihada za kuleta amani, usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi. Vilevile, kaulimbiu ililenga kutoa wito kwa wananchi kuona umuhimu wa kujitokeza kuhesabiwa katika zoezi la Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika mwezi Agosti, 2022. Halikadhalika maadhimisho yalilenga kutathmini mafanikio na changamoto katika utekelezaji wa Maazimio ya Ulingo wa Beijing; Malengo ya Maendeleo Endelevu (2030) hususan Lengo Namba 5 linalohusu Usawa wa Jinsia; na Ajenda ya Afrika Tuitakayo (2063) pamoja na kujenga hamasa na ushiriki wa wananchi katika kuchangia na kuleta usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake. Aidha, maadhimisho haya hutoa fursa ya masoko kwa wanawake wajasiriamali ambapo katika wiki ya kuelekea kilele cha maadhimisho kuanzia tarehe 1 hadi 7 huwa ni wiki ya maonesho ya bidhaa zinazozalishwa na wanawake wajasiriamali.

74. Mheshimiwa Spika, Wizara ilishiriki kwenye Mkutano wa Sita (6) wa Kamati Maalum ya Mawaziri wa Umoja wa Afrika wanaoshughulikia masuala ya Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji Wanawake uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia tarehe 1 Machi 2022. Lengo kuu la

mkutano huo lilikuwa ni kuweka mashauriano ya nchi za Afrika kuhusu Mkutano wa 66 wa Kamisheni ya Wanawake Duniani (*Africa-Wide Consultation for the 66th Session of the Commission on the Status for Women - CSW66*). Mkutano huo ulikuwa ni sehemu ya maandalizi ya nchi za Afrika kushiriki Mkutano wa 66 wa Kamisheni ya Wanawake Duniani uliofanyika New York, Marekani kuanzia tarehe 14-25 Machi 2022. Kaulimbiu ya mkutano wa 66 wa Kamisheni ya Wanawake Duniani ni **Kufanikisha Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji Wanawake na Wasichana kwenye Sera na Programu za Kukabiliana na Maafa Yanayosababishwa na Mabadiliko ya Tabianchi na Mazingira**. Katika mkutano huo, ilikubaliwa kuwa nchi za Afrika ziweke mipango ya kitaifa ambayo inashirikisha kikamilifu wanawake kwenye juhudi za kukabiliana na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi na mazingira, kuwezesha ushiriki wa Wanawake na Wasichana kwenye nafasi za uongozi, kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa wanawake na wasichana, kuongeza ufadhili na uwekezaji kwenye miradi ambayo inazingatia usawa wa kijinsia. Pia, nchi za Afrika zimekubaliana kuimarisha uwezo wa Taasisi za Takwimu za Kitaifa katika kukusanya takwimu na kuzitumia kutambua changamoto na fursa za wanawake na wasichana kushiriki katika kazi za uzalishaji kwenye sekta za kilimo na uchumi wa bluu.

Sambamba na mkutano huo, Wizara kwa kushirikiana na Asasi za Kiraia za LANDESA na OXFAM zilifanya Mkutano wa Pembeni (*Side Event*) unaohusu *Promoting Women's Participation and Decision Making in Addressing Climate Change: Tanzania's Village Land Use Planning Framework* ambao ulifanyika tarehe 16 - 17 Machi, 2022 katika ukumbi wa Morena, Jijini Dodoma kwa njia ya mtandao ambapo jumla ya wadau 150 walishiriki mkutano huo.

75. Mheshimiwa Spika, Tanzania kupitia Wizara ninayoiongoza ilipokea mwaliko kutoka Ubalozzi wa Ujerumani kushiriki Mkutano wa G7 uliofanyika Berlin,

Ujerumani kuanzia tarehe 6 - 8 Aprili, 2022. Mkutano huo ulilenga kujadili masuala mbalimbali kuhusu *Uzingatiaji wa Usawa wa Kijinsia na Uthaminishaji Mchango wa Wanawake Wanaofanya Kazi Zisizo na Ujira katika Uchumi wa Familia na Taifa*. Mkutano huo uliratibiwa na Shirika la UN Women kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (ILO). Aidha, katika mkutano huo Tanzania ilipongezwa kwa juhudi kubwa inayoifanya katika utekelezaji wa lengo namba 5 la Malengo ya Maendeleo Endelevu linalohimiza kukuza ushiriki wa wanawake katika uongozi na nafasi za maamuzi na uwezeshaji wanawake kiuchumi na kuweza kuliweka suala la kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi kuwa moja ya vipaumbele vya Taifa.

76. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake ya uwezeshaji wanawake kiuchumi, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo wanawake wajasiriamali ili kuwa na stadi za kufanya biashara. Katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya wanawake wajasiriamali 1,167 wamejengewa uwezo kupitia mafunzo yaliyotolewa katika Mikoa ya Shinyanga, Geita, Katavi na Tanga. Katika mafunzo hayo, wanawake walijengewa uwezo kwa kupatiwa elimu kwenye baadhi ya maeneo kama vile kodi, urasimishaji wa biashara, elimu ya hifadhi ya jamii na elimu ya viwango na ubora wa bidhaa. Pia, mbinu mbalimbali za kukuza mitaji pamoja na kupata masoko ya uhakika ya bidhaa zao zilitolewa kupitia Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO), Taasisi za Fedha na Wakala wa Usajili wa Leseni na Biashara (BRELA). Mafunzo hayo yataendelea kutolewa kwa wanawake katika mikoa yote Tanzania Bara. Aidha, katika kuwezesha wanawake wajasiriamali kupata mitaji ya biashara, Dirisha la Wanawake katika Benki ya Biashara Tanzania (*Tanzania Commercial Bank*) limewezesha mikopo yenye thamani ya **Shilingi 16,138,750,000** kwa wanawake 3,421 wa Tanzania Bara hadi kufikia mwezi Aprili, 2022.

77. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na vitendo vya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati, Wizara imewezesha kuandaliwa na kuzinduliwa kwa Mwongozo wa Uanzishaji, Uendeshaji na Ufuatiliaji wa Dawati la Jinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati. Mwongozo huo ulizinduliwa na **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 25 Novemba 2021 ikiwa ni jitihada za Serikali za kuweka mfumo wa kushughulikia matukio ya unyanyasaji wa kingono na vitendo vya ukatili katika maeneo ya Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati. Hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya Madawati 13 yameanzishwa katika Vyuo 13 kati ya Vyuo 50 vilivyokusudiwa kufikiwa ifikapo Juni 2022. Vyuo hivyo ni; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu cha Iringa, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ruaha, Chuo cha Maendeleo ya Jamii Buhare, Chuo Kikuu cha St. Augustine (SAUT) Mwanza, Chuo cha Mipango (IRDP) Dodoma na Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi.

78. Mheshimiwa Spika, miongoni mwa jitihada zinazofanywa na Wizara katika kuhakikisha Madawati yanaanzishwa kwenye Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati ni pamoja na: -

i. Kuvielekeza Vyuo kuhakikisha kuwa vinateua waratibu, wajumbe na kutenga sehemu maalum kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Dawati;

ii. Kuwajengea uwezo menejimenti za Vyuo na Waratibu wa Madawati ya Jinsia kuhusu namna bora ya uanzishwaji wa madawati hayo; na

iii. Kufuatilia uanzishaji wa Madawati ya Jinsia katika Vyuo vya Elimu ya Juu na Elimu ya Kati ili kufikia lengo tarajiwa.

Aidha, Wizara imeweka mkakati wa kuhakikisha kuwa ifikapo Juni 2022, Vyuho 50 viwe vimeanzisha Madawati ya Jinsia na kuhakikisha yanafanya kazi. Katika kuwezesha hilo, Wizara inaratibu na kufuatilia matumizi ya Daftari lililoandaliwa mahsusi kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za taarifa za vitendo vya ukatili katika Taasisi za Elimu ya Juu na Kati. Vilevile, Wizara imeandaa Kitini cha Mafunzo kwa ajili ya kuwafundisha Waratibu na Wajumbe juu ya namna ya kuendesha Dawati hili.

ENEO LA 5: URATIBU WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI

79. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia usajili, uratibu na ufuatiliaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili yachangie katika kuleta maendeleo ya Taifa. Katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi Aprili 2022, Wizara imesajili jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 1,217 kati ya Mashirika 500 yaliyopangwa kusajiliwa kwa mwaka 2021/22. Ongezeko la idadi ya Mashirika yaliyosajiliwa linatokana na uboreshaji wa mfumo wa usajili unaowezesha wadau kufanya usajili wa Mashirika kwa njia ya kielektroniki. Aidha, elimu inayoendelea kutolewa kwa jamii kuhusu umuhimu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na mchango wake katika maendeleo ya nchi imechangia kuongezeka kwa usajili.

80. Mheshimiwa Spika, Wizara ilifanya zoezi la uhakiki wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa lengo la kupata idadi sahihi ya Mashirika yaliyo hai na yanayotekeleza shughuli zao kwa kuzingatia Sheria Na. 24/2002 ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kuhuisha kanzidata ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 2,479 yalihakikiwa na kutangazwa kwenye tovuti ya Wizara. Aidha, kutokana na Mashirika kuwa mengi na kusambaa nchi nzima, Wizara iliongeza muda wa uhakiki hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2022. Katika kipindi hicho cha nyongeza, jumla ya Mashirika 2,385 yalijitokeza kuhakiki na kufikia jumla ya Mashirika 4,864 yaliyohakiki. Hii imewezesha kanzidata ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuwa na Mashirika 7,533 yaliyo hai

kati ya Mashirika 12,442 yaliyopo kwenye kanzidata ya Mashirika.

81. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanaratibiwa vizuri nchini, Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali imeanzisha Baraza la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ikiwa ni moja ya chombo cha uratibu wa Mashirika hayo. Chombo hiki ni asasi mwamvuli wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Uanzishwaji wa Baraza hilo umerahisisha uratibu wa Mashirika katika ngazi za Mikoa na Halmashauri kwa kuanzisha mitandao katika ngazi hizo, kuwepo kwa Kanuni za Maadili za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali zenye kuimarisha uwazi na uwajibikaji na kuwezesha uwepo wa uwakilishi wa Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Bodi ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Aidha, Baraza kwa kushirikiana na Serikali limewezesha kufanyika kwa Mkutano wa kwanza wa mwaka wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini mwaka 2021. Lengo la Mkutano huo ni kuimarisha ushirikiano baina ya Serikali na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kutambua mchango wa mashirika katika maendeleo ya nchi ikiwa ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2001) na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 Ibara ya 127 (a) na (d). Mkutano huo ulizinduliwa rasmi na **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 30 Septemba, 2021 Jijini Dodoma ambapo jumla ya Mashirika na Wadau 1,448 walishiriki.

82. Mheshimiwa Spika, wakati wa uzinduzi huo, Mheshimiwa Rais aliielekeza Wizara yangu kushirikiana na wadau wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa Uendeleu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kama hatua ya kupunguza utegemezi na kuyawezesha kuwa himilivu. Katika kutekeleza agizo hilo, Kamati ya kitaalam inayohusisha wajumbe 20 kutoka Serikalini na kwenye Mashirika hayo iliundwa mwezi Novemba 2021 ambapo mpaka sasa Kamati hiyo imefanikiwa kuandaa andiko la majadiliano na

ushirikishaji wa wadau wa Sekta mbalimbali zikiwemo sekta binafsi na wadau wa maendeleo. Kupitia andiko hilo, nyenzo za kukusanyia taarifa zimeandaliwa na zimeanza kutumika kupokea maoni ya wadau nchi nzima katika Kanda tano (5) ambazo ni; Kanda ya Mashariki, Kanda ya Ziwa, Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Kati. Pia, Kamati imefanikiwa kuajiri Mtaalam Mwelekezi ili kukusanya na kuchakata taarifa na takwimu kisayansi ambapo jumla ya wadau 1,089 wamefikwa kutoka katika Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 1,015 sawa na asilimia 13.7 ya Mashirika 7,533 yaliyo hai. Hata hivyo, zoezi la ukusanyaji wa maoni ya wadau linaendelea kwa njia ya dodoso mtandao (*KoboCollect*). Aidha, Kikosi Kazi kinatarajia kuendelea kukusanya maoni ya wadau kutoka Sekta Binafsi pamoja na wadau mbalimbali wa maendeleo (DPGs). Vilevile, mchakato wa uandaaji wa andiko la Mkakati wa Kitaifa wa Uendeleo wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali unatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 30 Julai, 2022.

83. Mheshimiwa Spika, Sambamba na uzinduzi wa Mkutano huo, Taarifa ya Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2020 ilizinduliwa ambayo ilibainisha kuwa **Shilingi Trilioni 1.1** zilitumika katika utekelezaji wa miradi ya afya, elimu, hifadhi ya jamii, uwezeshaji kiuchumi, utawala bora, mazingira, maji, jinsia na haki za binadamu ambapo jumla ya wanufaika 49,697,214 walifikwa pamoja na kutoa ajira kwa Watanzania 8,918.

84. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha uratibu, usajili na usimamizi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara imekamaliza ujenzi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa asilimia 100 ambapo umeshaanza kutumika. Aidha, Wizara inaendelea kupitia mfumo huo na kufanya maboresho kwa kila hatua iliyokamilika ili kuwezesha utendaji mzuri wa mfumo huo.

85. Mheshimiwa Spika, Wizara imetoa mafunzo kuhusu Sheria, Kanuni na Miongozo inayosimamia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kupitia mikutano ya wadau na vyombo vya habari. Jumla ya wadau 970 wamefikwa kati wadau 1,000 waliyopangwa kufikiwa kwa kipindi cha mwaka 2021/22 katika mikoa ya Arusha (150), Pwani (125), Songwe (50), Mbeya (50), Mtwara (50), Kinondoni (60), Morogoro (25), Geita (52), Shinyanga (70), Tanga (100), Mwanza (123) Tabora (65) na Simiyu (50). Lengo la mafunzo hayo ni kuyawezesha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo ili kuchangia ipasavyo katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa Taifa.

Aidha, katika kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa Sera ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini, Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali imeanzisha Bodi ya uratibu wa Mashirika hayo. Kwa mwaka 2021/22, Bodi ya nne (4) imewezesha kufanyika kwa zoezi la uhakiki wa Mashirika Tanzania Bara lililoendeshwa kuanzia mwezi Machi 2021 hadi mwezi Machi 2022 na Mkutano wa mwaka wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali uliofanyika kwa mara ya kwanza Septemba, 2021. Vilevile, Bodi imewezesha na kuboresha mazingira ya uwajibikaji na utendaji kazi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ikiwemo ujenzi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

86. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha ushirikiano baina ya Tanzania Bara na Zanzibar juu ya Masuala ya Muungano na Yasiyo ya Muungano, Idara ilishiriki vikao viwili (2) vilivyofanyika tarehe 18 Novemba, 2021 na tarehe 10 Desemba, 2021 ikiwa ni sehemu ya kuimarisha mashirikiano baina ya Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara na Ofisi ya Mrajis wa Asasi za Kiraia Zanzibar. Kupitia vikao hivyo, uratibu na usimamizi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa pande zote mbili (2) za Muungano umeboreshwa hususan katika masuala ya usajili na kuweka utaratibu

wa kutoa barua za utambulisho kwa Mashirika yanayotaka kufanya kazi upande wa Tanzania Bara au Zanzibar.

ENEO LA 6: URATIBU WA UTEKELEZAJI WA MTAKUWWA

87. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) kupitia maeneo nane (8) ya utekelezaji (*Thematic Areas*). Utekelezaji wa MTAKUWWA ulianza mwezi Julai, 2017 na utafikia ukomo mwezi Juni, 2022 na umekuwa ukitekelezwa kwa ushirikiano wa Wizara za Kisekta na Wadau mbalimbali. Baadhi ya mafanikio ya utekelezaji wa Mpango Kazi huu ni kama ifuatavyo: -

(i) Matukio ya ukatili wa kijinsia yaliyoripotiwa katika Dawati la Jinsia na Watoto la Polisi yamepungua kwa asilimia 31 kutoka matukio 42,414 mwaka 2020 hadi matukio 29,373 mwaka 2021 (**Kielelezo Na. 1**). Aidha, matukio ya ukatili wa kijinsia kwa watoto yaliyoripotiwa kwenye Dawati hilo yamepungua kwa asilimia 28 kutoka matukio 15,870 mwaka 2020 hadi matukio 11,499 mwaka 2021 kama inavyoonesha katika **Kielelezo Na. 2**;

(ii) Jumla ya Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto **18,186** kati ya 20,750 (sawa na asilimia 88) zimeanzishwa katika ngazi ya Taifa, Mkoa, Halmashauri, Kata na Kijiji/Mtaa mwaka 2021/22 kutoka Kamati 16,343 zilizoanzishwa mwaka 2019/20 sawa na ongezeko la Kamati 1,843. Kamati hizi zinawezesha kubaini na kushughulikia vitendo vya ukatili nchini kuanzia ngazi ya Kijiji/Mtaa hadi Taifa. Serikali inaendelea kufanya ufuatiliaji ili kuziimarisha na kuziwezesha kutekeleza majukumu yao ipasavyo;

(iii) Hadi mwezi Februari 2022, Serikali kupitia OR-TAMISEMI imetoa mikopo yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 35.55** kupitia asilimia 10 ya Mapato ya ndani ya Halmashauri.

Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni 19.36** zimetolewa kwa vikundi vya wanawake wajasiriamali 2,881. Fedha hizo zimeendelea kuwawezesha wanawake kujiimarisha kiuchumi na kuboresha uchumi wa kaya;

(iv) Hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya Vituo 21 vya Mkono kwa Mkono (*One Stop Centers*) vimeanzishwa katika Hospitali mbalimbali za Serikali kwenye Mikoa 12 ikilinganishwa na Vituo 14 vilivyoanzishwa hadi kufikia mwaka 2020/21. Jumla ya manusura wa vitendo vya ukatili 1,857 walipatiwa huduma jumuishi ikiwemo huduma za kitabibu, polisi, msaada wa kisheria, ustawi wa jamii kupitia Vituo hivyo. Lengo ni kuwezesha utoaji wa huduma hizo katika eneo moja ili kuepusha usumbufu, ucheleweshaji wa huduma, kuharibu au kupoteza ushahidi. Serikali kwa kushirikiana na Wadau itaendelea kuratibu uanzishwaji wa Vituo vya Mkono kwa Mkono katika Mikoa ambayo haijaanzisha Vituo hivyo ikiwemo Mikoa ya Dodoma, Singida, Tanga, Geita, Katavi, Rukwa, Mtwara, Lindi, Ruvuma, Mara, Kagera, Njombe, Songwe na Manyara. Vituo hivi vinarahisisha huduma kwa kumpa fursa manusura kufika katika kituo na kupata huduma za unasihi, utoaji taarifa kwa Afisa wa Polisi na kupata matibabu. Aidha, vinarahisisha upatikanaji wa haraka wa ushahidi unaotokana na vipimo vya kitabibu unaowasilishwa katika Mahakama;

(v) Kuanzishwa kwa Nyumba Salama 10 katika mikoa ya Arusha (3), Iringa (1), Kigoma (1), Mara (2), Manyara (1), Morogoro (1) na Mwanza (1). Nyumba hizi zinatumiwa kutoa huduma za msingi na hifadhi ya dharura kwa manusura wa ukatili nchini. Kwa kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya manusura 493 walihudumiwa kupitia Nyumba hizo. Serikali kwa kushirikiana na Wadau itaendelea kuratibu uanzishwaji wa Nyumba Salama katika maeneo mbalimbali kulingana na uhitaji wake. **Napenda kuishukuru Serikali ya Uingereza kupitia Taasisi ya *British Council* kwa kutupatia msaada wa majengo kwa ajili ya kuanzisha kitengo cha**

kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu huduma ambayo uratibu wake utashirikisha sekta mbalimbali;

(vi) Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma iliratibu kikao kilichowakutanisha wajumbe wa Kamati ya Ulinzi wa Wanawake na Watoto ngazi ya Mkoa ili kujadili utekelezaji wa MTAKUWWA, kukumbushana majukumu ya Kamati ngazi ya Mkoa na kuweka mikakati ya kutokomeza ukatili. Kikao hicho kilifanyika tarehe 15 Februari, 2022 ambapo kilihudhuriwa na washiriki 67.

Aidha, Wizara iliratibu kikao cha Wadau wanaotekeleza afua mbalimbali za kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto kilichofanyika tarehe 26 Februari, 2022 Jijini Dodoma kwa lengo la kuweka Mkakati wa pamoja wa kukabiliana na vitendo vya ukatili katika jamii ambapo Wadau zaidi ya 200 waliweza kushiriki. Maazimio ya kikao hicho yalikuwa ni pamoja na: Kuimarisha Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto ngazi zote ili zitekeleze majukumu yao ipasavyo katika kutokomeza vitendo vya ukatili na kuwezesha upatikanaji wa taarifa na takwimu za matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto; Kuelimisha jamii kupitia majukwaa mbalimbali ikiwemo redio za kijamii, sanaa, vyombo vya habari na wadau ili kuijengea jamii uelewa wa masuala ya Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto; na kuwe na mabalozi wa MTAKUWWA; na

(vii) Wizara iliwezesha kuzinduliwa kwa Kampeni ya **“Twende Pamoja, Ukatili Tanzania Sasa Basi”** katika Mkoa wa Mwanza lengo lilikuwa ni kuimarisha utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) ambapo hadi kufikia mwezi Aprili 2022, Kampeni hii ilitekelezwa katika mikoa mitano (5) ya Dar es Salaam, Mara, Mwanza, Katavi na Kigoma. Mikoa hii imefanikiwa kuzindua mpango wa Kampeni hii kati ya mikoa 12 iliyopangwa kufikia 2021. Kutofikiwa kwa idadi hii kulitokana na athari za UVIKO-19.

88. Mheshimiwa Spika, pamoja na Takwimu za Jeshi la Polisi kuhusu Hali ya Uhalifu na Matukio ya Usalama Barabarani kuonesha kupungua kwa matukio ya ukatili yaliyoripotiwa mwaka 2021 ikilinganishwa na miaka iliyopita, bado tumeendelea kushuhudia matukio ya vitendo vya ukatili mara kwa mara kwenye vyombo vya habari hususan kupitia mitandao ya kijamii. Pamoja na hatua za kila siku za Serikali na wadau mbalimbali kupambana na ukatili kupitia MTAKUWWA, Wizara inaratibu utekelezaji wa kampeni kubwa ya kupambana na ukatili sambamba na kuimarisha mifumo ya kubaini viashiria vya ukatili na kuchukua hatua za kuzuia.

89. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utekelezaji wa MTAKUWWA unafikia ukomo mwezi Juni 2022, Wizara imeanza mchakato wa kufanya tathmini ya Mpango huo kwa lengo la kubaini mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji kwa kipindi cha miaka mitano, changamoto na upungufu wa kimuundo na kiutendaji ulioathiri kufikiwa kwa malengo ya Mpango. Aidha, tathmini inatarajiwa kubainisha masuala ya kuigwa (*best practices*) na kutoa mapendekezo ya namna bora zaidi ya kukabiliana na changamoto na upungufu uliobainika. Matokeo au mapendekezo yatakayobainishwa katika taarifa ya Tathmini ya Mpango yatawezesha kuanza kwa maandalizi ya MTAKUWWA awamu ya pili itakayotoa mikakati mahsusi ya kutokomeza aina zote za ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa miaka mitano ijayo.

Katika hatua ya sasa, Wizara imesaini Mkataba na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) kutoa huduma ya Ushauri Elekezi katika zoezi la Tathmini ya MTAKUWWA sambamba na kuandaa MTAKUWWA II. Hatua za awali ikiwemo kukamilika kwa wasilisho la kwanza yaani "Inception Report" zimekwishafanyika na hivyo maandalizi kwa ajili ya zoezi la kukusanya na kuchakata taarifa kutoka kwa Wadau mbalimbali linaendelea. Tathmini na Maandalizi ya MTAKUWWA II yanatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Septemba, 2022.

D. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

90. Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali, Wizara imekuwa ikisimamia utekelezaji wa majukumu yake kupitia Taasisi zilizochini yake ambazo ni Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Taasisi ya Ustawi wa Jamii.

91. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru imeendelea kutoa mafunzo ya taaluma ya maendeleo ya jamii katika ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada na Stashahada ya Uzamili. Pia, Taasisi imeendelea kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato ili kuboresha shughuli za utoaji mafunzo. Katika mwaka 2021/22, Taasisi ilipanga kukusanya kiasi cha **Shilingi 3,560,574,000** kutoka vyanzo mbalimbali. Hadi mwezi Aprili 2022, Taasisi imefanikiwa kukusanya jumla ya Shilingi **2,669,377,825** sawa na asilimia **75** ya makadirio.

92. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa masomo 2021/22, Taasisi ilidahili wanafunzi 2,800 katika ngazi zote (Ke 1,857 na Me 943) ikilinganisha na wanafunzi 2,492 waliodahiliwa mwaka 2020/21. Aidha, kwa mwaka 2021/22, jumla ya wanafunzi 1,464 (Ke 1,006 na Me 458) walihitimu katika fani na ngazi mbalimbali ikilinganishwa na wanafunzi 1,003 (Me 262 na Ke 741) waliohitimu mwaka 2020/21.

93. Mheshimiwa Spika, Taasisi iliandaa Kongamano kubwa la wanawake tarehe 7 Machi 2022 kuelekea kilele cha Siku ya Wanawake Duniani. Jumla ya washiriki 306 walihudhuria wakiwemo Mabalizi, Mashirika ya Kimataifa, Taasisi za Serikali, Maafisa kutoka Wizara mbalimbali, Wakurugenzi na Maafisa kutoka WMJJWM, Maafisa kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki na wawakilishi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Aidha, Taasisi ilifanikiwa kuandika maandiko na kupata ufadhili wa kiasi cha **Shilingi Milioni 70** kutoka kwa wadau.

94. Mheshimiwa Spika, Taasisi imeandaa programu sita mpya za kitaaluma ambapo programu moja ya kitaaluma ilibadilishana na Taasisi ya Mafunzo ya Serikali za Mitaa (LGTI) – Hombolo. Ushirikiano huu umeongeza idadi ya watumishi wa kitaaluma na wasaidizi wanaofadhiliwa na Taasisi kwa kozi ndefu na fupi. Hadi kufikia mwezi Desemba 2021, wafanyakazi 20 wameanza programu za PhD katika Vyuo Vikuu mbalimbali. Vilevile, wafanyakazi 11 wanaendelea na masomo ya shahada ya uzamili. Pia, watumishi watatu (3) wanahudhuria kozi ya Mhasibu wa Umma Aliyeidhinishwa (CPA) na mmoja anahudhuria kozi ya taaluma ya ununuzi na ugavi. Ili kuongeza umahiri na maarifa ya wafanyakazi kitaaluma, mafunzo ya ndani kuhusu mbinu za utoaji na tafsiri ya mtaala yalifanyika kwa wiki moja Desemba 2021. Aidha, mafunzo kuhusu udhibiti wa msongo wa mawazo yalifanyika kwa wafanyakazi wote ili kuwa na wafanyakazi wenye afya bora wanaofanya kazi. chini ya udhibiti na udumishaji wa utamaduni thabiti, wenye afya mahali pa kazi ambao unafaa kwa ubunifu na tija.

95. Mheshimiwa Spika, Taasisi imeendelea kutekeleza programu ya kuchochea na kuendeleza ubunifu (*innovation*) miongoni mwa wanafunzi kupitia Kituo cha Huduma Tandaa na Ubunifu wa Kidijitali (*Jamii Outreach Digital Innovation Center – JODIC*). Kituo hiki kinatumika kuratibu utekelezaji wa programu za ubunifu wa kidijitali, ushirikishaji jamii na uanagenzi katika kazi pana za Taasisi. Kupitia kituo hicho, Taasisi imetekeleza kazi zifuatazo: -

(i) Taasisi iliandaa Wiki ya Maendeleo ya Jamii kuanzia tarehe 6-11 Desemba 2021. Katika maadhimisho hayo, maonesho yaliandaliwa katika viwanja vya TICD ambapo wadau wakuu walishiriki na kuonesha bidhaa na huduma zao. Pia, vikundi mbalimbali vya wanafunzi wa Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru walionesha bidhaa zao. Maonesho hayo yaliongeza mwonekano wa bidhaa zao, pia kujenga mitandao/muunganisho na

kuboresha ujuzi wa masoko, uuzaji na uwekaji chapa kwa wanafunzi;

(ii) Kuhamasisha na kutoa mafunzo kwa vikundi 17 vya wanawake, vijana na walemavu kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Arusha kuhusu stadi za ujasiriamali;

(iii) Kuanzisha ushirikiano na Kampuni ya Gongali *Model* ambapo Kituo kiliwasilisha andiko la kufadhili shughuli za Kituo (JODIC);

(iv) Kuendesha mafunzo kuhusu uundaji wa vikundi, taratibu za usajili, fursa za mikopo, uuzaji wa kidijitali, unyanyasaji wa kijinsia na ulinzi wa haki za binadamu kwa wanafunzi 49 na viongozi wa vikundi vya kijamii;

(v) Kuadhimisha siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia ambapo shughuli mbalimbali zilifanyika ikiwemo mijadala kuhusu migogoro ya kifamilia inavyochangia unyanyasaji wa kijinsia miongoni mwa wanandoa. Mojawapo ya mambo muhimu yaliyochukuliwa kutoka kwenye mazungumzo hayo ni kutambua kuwa wanaume pia ni waathiriwa wa unyanyasaji wa kijinsia. Aidha, mafunzo kuhusu unyanyasaji wa kijinsia yaliendesha kwa wanawake 500 kutoka Kata za Akheri, Kikwe na Kiutu Wilayani Arumeru. Pia, ilifanyika kampeni ya uhamasishaji juu ya mambo yanayoendeleza unyanyasaji wa kijinsia na hatua za kukabiliana nayo kwa wanafunzi 200 na 300 wa shule za msingi na sekondari mtawalia; na

(vi) Kutoa mafunzo kwa wanafunzi 289 na wafanyakazi wa taaluma 53 kuhusu uanagenzi na stadi za kuajiriwa kwa ajili ya utekelezaji bora wa programu ya uanagenzi. Aidha, Kituo (JODIC) kilifanya uchanganuzi wa upungufu wa ujuzi kwa wanafunzi 289 ili kubaini maeneo yanayofaa kwa programu ya uanagenzi. Vilevile, Kituo kiliendesha zoezi la ufuatiliaji na tathmini kwa wanagenzi 274 waliokuwa waandaaji katika mashirika mbalimbali nchini Tanzania.

96. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii ambayo nayo ipo chini ya Wizara ninayoiongoza ni kwamba Taasisi hii imeendelea kutoa mafunzo katika ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada, Stashahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamili katika fani ya Ustawi wa Jamii na fani nyinginezo zinazoshabihiana nayo. Aidha, Taasisi imeendelea kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato kutoka kwenye vyanzo vikubwa vya mapato ambavyo ni; ada za wanafunzi, tafiti, ushauri elekezi na vyanzo vingine. Katika mwaka 2021/22, Taasisi ilipanga kukusanya kiasi cha **Shilingi 6,356,968,500**. Hadi kufikia mwezi Aprili 2022, Taasisi imekusanya **Shilingi 4,877,734,052** sawa na asilimia 77 ya makadirio.

97. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa masomo 2021/22, Taasisi imedahili wanafunzi 3,234 (Ke 2,104 na Me 1,130) ikilinganishwa na wanafunzi 2,542 (Ke 1,680 na Me 862) waliodahiliwa mwaka 2020/21 sawa na ongezeko la asilimia 27. Kati ya wanafunzi waliodahiliwa mwaka 2021/22, wanafunzi 879 walidahiliwa katika ngazi za Astashahada, wanafunzi 674 ngazi ya Stashahada, wanafunzi 1,586 ngazi ya Shahada na wanafunzi 95 ngazi ya Shahada ya Uzamili. Aidha, katika mwaka 2020/21, Taasisi iliwezesha wanafunzi 2,493 (Ke 1,645 na Me 848) kuhitimu katika fani na ngazi mbalimbali ikilinganishwa na wanafunzi 1,246 (Ke 928 na Me 318) waliohitimu mwaka 2019/20. Kati yao, wanafunzi 938 waliohitimu katika ngazi ya Astashahada, wanafunzi 687 ngazi ya Stashahada, wanafunzi 692 ngazi ya Shahada na wanafunzi 176 waliohitimu katika ngazi ya Shahada ya Uzamili.

98. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Ustawi wa Jamii imeendelea kutoa huduma ya msaada wa kisaikolojia kwa wanafunzi na jamii kupitia Kituo chake cha Elimu, Ushauri na Msaada wa Kisaikolojia kilichokarabatiwa kwa ufadhili wa Shirika la *Korea International Cooperation Agency* (KOICA). Taasisi ilitoa huduma za kisaikolojia na ushauri kwa manusura 345 wa janga la moto katika Soko

la Karume ikiwemo watu wenye mahitaji maalum 150. Kupitia Kituo hiki Taasisi pia imeweza kutembelea shule nne (4) za Wilaya ya Kinondoni na shule moja (1) katika Wilaya ya Mwanaga ili kuelimisha wanafunzi kuhusiana na nidhamu, ufaulu na mahusiano. Vilevile, elimu ilitolewa juu ya viashiria vya ukatili wa kijinsia, stadi za kuepukana na makundi mabaya na matumizi ya dawa za kulevya. Kupitia afua hizo, Taasisi iliweza kuwafikia jumla ya wanafunzi 853 na kutoa huduma za ushauri, unasihi na kisaikolojia kwa wanajamii 1,034 wanaozunguka Taasisi. Yote haya yamelenga katika kuhakikisha malezi na makuzi yanaimarishwa ili kukuza ustawi wa mtu mmoja mmoja, familia na Taifa kwa ujumla.

99. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Ustawi wa Jamii pia imekuwa ikiendesha programu za kushirikisha jamii (*community engagement*), uanagenzi (*apprenticeship*) na ubunifu (*innovation*). Kupitia kituo chake cha ubunifu, Taasisi imeweza kuwajengea ujuzi na uwezo wanafunzi 180 katika muda wa wiki nane (8) ili waweze kutumia teknolojia ya kidijitali kama nyenzo ya kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. Kupitia programu yake ya uanagenzi, Taasisi imeweza kuwaunganisha wanafunzi 11 kupata ajira na kuwezesha wanafunzi wengine 56 kupata nafasi mbalimbali za kujifunza stadi za kazi katika mashirika mbalimbali kwa kipindi cha mwaka 2021/22. Pia, Taasisi kupitia programu yake ya kushirikisha jamii imewapatia vijana 428 wa Manispaa ya Kinondoni elimu na ushauri juu ya namna ya kukabiliana na changamoto za maisha, afya, mahusiano na namna ya kujikwamua na umaskini.

100. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Ustawi wa Jamii iliadhimisha Siku ya Kimataifa ya Ustawi wa Jamii duniani tarehe 15/3/2022 kwa kutoa huduma za ustawi wa jamii bure kwa wananchi. Huduma zilizotolewa ni pamoja na; ushauri wa masuala ya ndoa na mahusiano, masuala ya watoto waliotelekezwa na ushauri wa kisaikolojia. Vilevile, Taasisi iliadhimisha siku hiyo kwa kufanya vipindi

vya luninga kuelimisha jamii juu ya Ustawi wa Jamii na wataalam wa ustawi wa jamii wanavyoweza kusaidia kupunguza changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika jamii.

101. Mheshimiwa Spika, Taasisi imeendelea kufanya tafiti zinazohusu changamoto mbalimbali za kijamii ikiwemo utafiti kuhusu utumiaji wa taasisi za kimila na kijamii kukabiliana na ukatili wa kijinsia na jinsi ya kuondoa unyanyasaji wa kijinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu. Aidha, Taasisi imejielekeza katika kuimarisha elimu ya malezi na makuzi ya watoto kwa kutoa kozi za awali za makuzi kwa walezi wanaolea watoto katika vituo vya SOS vya Arusha, Dar es Salaam na Mwanza. Katika kutambua umuhimu wa elimu ya awali ya malezi na makuzi, Taasisi imeanza maandalizi wa Mtaala wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Watoto (*Early Childhood Care and Development*) ambao utatumika kuwajengea uwezo na uelewa walezi hususan walio katika vituo vya kulelea watoto.

102. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 Ibara ya 80, Taasisi imefanya maboresho mbalimbali katika miundombinu yake ya kujifunzia na kufundishia kama ifuatavyo: -

(i) Taasisi imeendelea kutekeleza mradi wa kujenga maktaba ya kisasa hatua ya nane (phase VIII) na ya mwisho ambapo kazi zilizofanyika ni pamoja na kufunga mfumo wa mawasiliano ya TEHAMA, mfumo wa umeme, kuweka mfumo wa mabomba ya maji, kufunga kiinua (*lift*), ujenzi wa kuta za ndani na kupaka rangi;

(ii) Katika kuimarisha matumizi ya TEHAMA, Taasisi imenunua vifaa mbalimbali pamoja na kujiunga na mtandao wa Serikali (Government Network). Pia, Taasisi imefunga seva ya kompyuta yenye uwezo wa kuruhusu hadi wanafunzi 10,000 kutumia mifumo ya TEHAMA iliyopo kwa wakati mmoja na kuongeza wigo

wa upatikanaji wa mtandao (*Internet Band- Width*) kutoka 12Mbps hadi kufikia 22Mbps; na

(iii) Taasisi imekamilisha ujenzi wa madarasa mawili (2) pamoja na ofisi mbili za wafanyakazi katika Kampasi yake ya Kisangara iliyopo Mwangi Killimanjaro. Madarasa hayo yana uwezo wa kuhudumia wanafunzi 500 kwa wakati mmoja na Ofisi hizo zina uwezo wa kuhudumia watumishi sita (6).

103. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha utendaji kazi na kutoa elimu yenye tija itakayoweza kukuza Ustawi wa Jamii nchini, Taasisi imewafadhili watumishi 32 wanaoendelea na masomo yao katika Shahada ya Uzamivu (PhD), Watumishi sita (6) katika Shahada ya Uzamili (*Master's*) na watumishi 48 katika mafunzo ya muda mfupi (*Short Courses*).

F. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

104. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi, Wizara imeendelea kutekeleza afua mbalimbali za miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi na ukarabati wa majengo na miundombinu katika Taasisi na Vyuo vilivyo chini yake. Kwa kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi mwezi Aprili 2022, Wizara iliweza kupokea kiasi chote cha fedha za ndani za maendeleo kiasi cha **Shilingi Bilioni 4.9** kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Mradi wa Huduma za Ustawi wa Jamii.

Kati ya fedha za ndani zilizopokelewa, **Shilingi Bilioni 3.6** ni kwa ajili ya Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ambapo fedha hizo zimeanza kutumika kwa ajili ya kujenga mabweni mawili, maktaba na ukumbi wa mihadhara katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ruaha, kujenga bweni lenye ghorofa mbili katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba na kujenga bweni lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 600

katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Uyole. Aidha, fedha hizo zimeanza kutumika kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala na darasa moja katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Mlale, kukarabati kumbi mbili za mihadhara (zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 kila ukumbi kwa wakati mmoja) pamoja na kujenga ukumbi wa mihadhara (wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 450 kwa wakati mmoja) katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Monduli. Ujenzi wa miradi hiyo umeanza na upo katika hatua za awali za utekelezaji.

Aidha, kiasi cha **Shilingi Bilioni 1.3** kimeelekezwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo na miundombinu katika Taasisi na Vituo vya Ustawi wa Jamii ikiwemo: ujenzi na ukarabati wa majengo na miundombinu katika Shule ya Maadilisho Irambo, Mahabusu za Watoto za Mbeya, Tanga na Arusha; na ujenzi wa hosteli ya wanafunzi katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii (Kampasi ya Kisangara) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 400 kwa wakati mmoja. Ujenzi na ukarabati katika Taasisi na Vituo hivyo unaendelea.

105. Mheshimiwa Spika, hata hivyo, katika kuunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wizara kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Jamii inaandaa miradi ya maendeleo ambapo kupitia miradi hiyo ifikapo mwaka 2024/25 inatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi Bilioni 2.1**. Aidha, kiasi hicho cha fedha kitaweza kupunguza kwa kiasi kikubwa utegemezi wa Vyuo hivyo kwa Serikali katika uendeshaji wake. Mchanganuo wa miradi hiyo na makadirio ya makusanyo umeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 3**.

G. VIPAUMBELE VYA WIZARA NA BAJETI YA MAPATO, MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2022/23

106. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Wizara kupitia Idara na Taasisi zilizo chini yake itatekeleza

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

vipaumbele nane (8) ili kuboresha utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii: -

(i) Kuratibu afua za kukuza usawa wa kijinsia, uwezesaji wanawake kiuchumi na kiungozi na kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake, watoto na wazee;

(ii) Kukuza ari ya jamii kushiriki katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo iliyoibuliwa ngazi ya jamii;

(iii) Kutambua na kuratibu makundi maalum wakiwemo wafanyabiashara ndogondogo (Machinga) ili kuboresha mazingira ya biashara zao;

(iv) Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Vyuvo vya Maendeleo ya Jamii;

(v) Kuratibu utoaji wa huduma za msingi kwa watu wenye mahitaji maalum, huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa na familia na huduma ya msaada wa kisaikolojia kwa manusura wa majanga mbalimbali na makundi mengine yenye uhitaji katika jamii;

(vi) Kuratibu na kuwezesha upatikanaji wa huduma za ustawi wa jamii kwa wazee;

(vii) Kuratibu na kusimamia afua za upatikanaji wa haki za mtoto, ulinzi na malezi chanya ya watoto; na

(viii) Kuimarisha ushiriki na mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo ya Taifa.

107. Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa hapo juu, Wizara kwa mwaka 2022/23 imekadiria kutumia kiasi cha **Shilingi Bilioni 43.4** zitakazotumika kutekeleza majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na kuwezesha uendeshaji wa ofisi na utekelezaji wa miradi wa maendeleo. Baadhi ya maeneo

yaliyotengewa fedha kwa mwaka 2022/23 ni pamoja na: -

(i) Katika eneo la ukatili na masuala ya usawa wa kijinsia, kiasi cha **Shilingi Bilioni 2.65** kimetengwa kwa ajili ya kuratibu utekelezaji wa afua za kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto ikiwemo Kampeni ya “**Twende Pamoja, Ukatili Tanzania Sasa Basi**”. Pia, fedha hizo zitatumika kwa ajili ya kusambaza Mwongozo wa Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake K i u c h u m i , kuwezesha utekelezaji wa Ahadi za Nchi kuhusu Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa na kuwezesha ushiriki wa wanawake katika Maonesho ya Kitaifa na Kimataifa;

(ii) Kwenye eneo la watoto, kiasi cha **Shilingi Bilioni 2.36** kimetengwa kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa huduma kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na marekebisho ya tabia kwa watoto waliokinzana na sheria, kukarabati Mahabusu za Watoto katika Mikoa ya Mbeya na Arusha, kujenga Mahabusu ya Watoto mpya katika Mkoa wa Mwanza, kuratibu utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Mtoto (2021/22 – 2025/26) na kuanzisha vituo vya kijamii vya malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto;

(iii) Katika eneo la wazee, **Shilingi Bilioni 1.45** zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa huduma za ustawi kwa wazee wasiojiweza katika Makazi ya Wazee 14 na ukarabati wa majengo na miundombinu katika Makazi ya Wazee ya Ipuli na Njoro;

(iv) Kwenye eneo la Taasisi na Vyuo, kiasi cha **Shilingi Bilioni 5.6** kimetengwa. Fedha hizo ni kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo na miundombinu katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Taasisi ya Ustawi wa Jamii (Kampasi ya Kisangara) na Vyuo nane (8) vya Maendeleo ya Jamii;

(v) Eneo la uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali limetengewa kiasi cha **Shilingi Milioni 642.3** kwa ajili ya

ufuatiliaji wa Mashirika 1,000 katika Kanda tano (5), kuendesha Mfumo wa Kielekroniki wa Usajili wa Mashirika, kuwezesha vikao vya Bodi ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, kusajili Mashirika na kuratibu Jukwaa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(vi) Eneo la maendeleo ya jamii limetengewa kiasi cha **Shilingi Milioni 160.2** kwa ajili ya kutekeleza Kampeni ya Kitaifa ya Kuamsha Ari ya Jamii kuhusu ujenzi wa nyumba bora za gharama nafuu kwa kutumia teknolojia rahisi katika mikoa 26 ya Tanzania Bara; na

(vii) Katika eneo la ufuatiliaji na tathmini, kiasi cha **Shilingi Milioni 200** kimetengwa. Fedha hizo ni kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa mipango, programu na miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika Taasisi, Vyuo na Vituo vya Ustawi vilivyo chini ya Wizara.

H. SHUKRANI

108. Mheshimiwa Spika, Wizara imekuwa ikipata ushirikiano mkubwa kutoka nchi rafiki, Mashirika ya Kimataifa na Sekta mbalimbali zinazosaidia na kuchangia katika huduma za maendeleo na ustawi wa jamii.

109. Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii ya kipekee kuzishukuru Serikali za nchi za Marekani, Ujerumani, Ubelgiji, Ufaransa na nchi nyingine ambazo zimeendelea kuisaidia Wizara kwa njia mbalimbali. Aidha, naishukuru Serikali ya Uingereza kupitia Shirika la Misaada la FCDO ambalo limefadhili kazi ya kupokea maoni ya wadau katika maandalizi ya Mkakati wa Kitaifa wa Uendeleu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini.

110. Mheshimiwa Spika, nayashukuru pia Mashirika ya Kimataifa kwa ushirikiano wao waliotoa kwa Wizara. Mashirika hayo ni pamoja na: Mashirika yaliyo chini ya Umoja wa Mataifa (UNICEF, UN-Women, UNFPA, WHO, IOM na UNESCO); Umoja wa Nchi za Ulaya (EU); Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB); USAID; Abbott Fund; na

Global Fund (for HIV, TB na Malaria). Aidha, nazishukuru Taasisi za Kifedha zinazoshirikiana na Wizara ambazo ni pamoja na NMB, CRDB, Stanbic Bank na Benki ya Biashara Tanzania (TCB).

111. Mheshimiwa Spika, nayashukuru Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya ndani ya nchi na Mashirika ya Dini kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Mashirika hayo ni pamoja na; WILDAF, TCRF, TAMWA, TAWLA, TGNP, TAYOA, LSF, Plan International - Tanzania, Kivulini, FSDT, The Aga Khan Foundation, CBM International, Segal Foundation, HelpAge International, Save the Children, World Vision, PACT Tanzania, TradeMark East Africa (TMEA), Equality for Growth (EfG), Landesa, TAWIA, CAMFED, SOS Children's Village Tanzania, C- SEMA; Railway Children Africa, REPPSI, Amani Girls Home, Pelum Tanzania, LHRC, ECPAT, INTERPOL, Haki Elimu, SOS Children Tanzania, TWCC, Compassion International, Care International Tanzania, TECDEN, Pact Tanzania, BAKWATA na CCT.

112. Mheshimiwa Spika, nazishukuru Taasisi mbalimbali za Serikali zikiwemo SIDO, BRELA, NIMR, TBS, Shirika la Posta Tanzania, NSSF, TFS, TASAC, TPA, NHIF, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), TASAF, Jeshi la Polisi Tanzania, Jeshi la Magereza Tanzania Bara na TAKUKURU kwa kuendelea kushirikiana na Wizara yangu. Pia, navishukuru Vyuo vilivyo chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Aidha, nawashukuru wadau wengine waliotoa huduma ya elimu kwa njia za redio, luninga, magazeti na mitandao ya kijamii kuhusu masuala ya maendeleo na ustawi wa jamii. Wadau hao ni pamoja na; Joyce Kiria (kupitia kipindi cha Wanawake *Live*), Mhe. Vicky Kamata (kupitia kipindi cha Wanawake na Maendeleo) na wadau wengine. Vilevile, navishukuru Vyama mbalimbali vya

kitaaluma ikiwemo; CODEPATA, TASWO na Tanzania Bankers Association.

113. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha utekelezaji wa majukumu yangu nikiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, nimepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara. Napenda kumshukuru **Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis (Mb)**, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa ushirikiano anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Pia, naomba kuwashukuru **Dkt. Zainab Abdi Seraphin Chaula**, Katibu Mkuu na **Bw. Amon Anastaz Mpanju**, Naibu Katibu kwa mchango na ushirikiano wao katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, nawashukuru Makamishna, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Wataalam wote wa Wizara kwa utendaji wao mzuri uliowezesha kukamilisha maandalizi ya Hotuba yangu kwa wakati muafaka. Vilevile, kupitia OR-TAMISEMI nawashukuru sana Wakuu wa Mikoa yote, Makatibu Tawala, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri zote na wataalam wote chini ya ofisi zao na pia wadau wote wa sekta mbalimbali wanaohudumia katika maeneo yao.

114. Mheshimiwa Spika, kipekee naomba kuwashukuru Wakuu wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru. Pia, nawashukuru Wakuu wa Vyuo nane (8) vya Maendeleo ya Jamii kwa ushirikiano wao mzuri unaonirahisishia utekelezaji wa majukumu yangu. Natoa shukrani kwa sekta zote ambazo tunashirikiana nazo katika kutoa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii pamoja na wananchi wote kwa ushirikiano wao. Nawaasa waendeleo kuzingatia misingi ya huduma bora na kufanya kazi kwa bidii kwa manufaa ya Taifa letu. Aidha, naishukuru Kamati ya Ushauri ya Kitaifa ya Utekelezaji wa Ahadi za Nchi kuhusu Kizazi Chenye Usawa (*Generation Equality Forum - GEF*) chini ya uongozi mahiri wa **Mheshimiwa Anjellah Kairuki** ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati hiyo.

115. Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii pia kuishukuru familia yangu, hususan mume wangu **Advocate Metusela Gwajima** na watoto wetu pamoja na wote ambao wamekuwa sehemu ya familia yetu kwa uvumilivu wao na kipekee kwa kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa. Aidha, nawashukuru wananchi wote wa Tanzania kwa kuipatia ushirikiano Wizara ninayoismamia wakati wote wa kutekeleza majukumu yangu na pia kwa wao binafsi kuendelea kupambana kuhakikisha maendeleo na ustawi wa jamii kwa usawa wa jinsia huku wakitumia **Simu Namba 116** bila malipo kwa ajili ya kuripoti matukio au viashiria vya ukatili saa 24 kila siku. Aidha, nawahimiza kuendelea kutumia simu zote za wataalam waliopo Wizarani na katika Mikoa na Halmashauri nchi nzima pamoja na namba yangu **0734124191** kwa ajili ya kutoa taarifa za viashiria vya ukatili kama tulivyotangaza kwenye vyombo vya habari na kuziweka kwenye tovuti yetu ya Wizara ambayo ni www.jamii.go.tz.

I. MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA 2022/23

Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2022/23

116. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Wizara imekadiria kukusanya **Shilingi 8,500,000,000** kutokana na ada na tozo mbalimbali za usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, mapato ya ada za mitihani na uuzaji wa mitaala ya Mafunzo ya Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii na mapato mengine.

Matumizi ya Kawaida

117. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Wizara inakadiria kutumia kiasi cha **Shilingi 32,310,981,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 18,169,057,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 14,141,924,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi.

Miradi ya Maendeleo

118. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa shughuli za maendeleo, Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 11,092,080,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 6,900,000,000** ni Fedha za Ndani na **Shilingi 4,192,080,000** ni Fedha za Nje.

119. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2022/23, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (Fungu 53) inaomba jumla ya **Shilingi 43,403,061,000** ili kutekeleza majukumu yake kwa maendeleo na ustawi wa jamii.

120. Mheshimiwa Spika, Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum www.jamii.go.tz.

121. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

VIAMBATISHO

Kiambatisho Na. 1: Idadi ya Watoto Waliosajiliwa na Kupatiwa Huduma katika Vituo 15 vya Mfano vya Kijamii vya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto

NA.	JINA LA KITUO	HALMASHAURI	WAVULANA	WASICHANA	JUMLA
1.	Kongwa	Kongwa	31	44	75
2.	Mbande	Kongwa	28	32	60
3.	Chamwino	Chamwino	37	30	67
4.	Bahi Sokoni	Bahi	35	31	66
5.	Mayamaya	Kondoa	26	23	49
6.	Kidulo	Kondoa	38	32	70
7.	Soro	Kondoa	23	27	50
8.	Chibelega	Bahi	22	30	52
9.	Ngh'ombolola	Bahi	25	27	52
10.	Mundemu	Bahi	28	29	57
11.	Saku	Kondoa	33	29	62
12.	Mlowa Barabarani	Chamwino	22	39	61
13.	Mbagala Kuu	Temeke	44	35	79
14.	Mbutu	Kigamboni	26	32	58
15.	Kimbiji	Kigamboni	08	17	25
	JUMLA		426	457	883

Chanzo: *WMJJWM*

Kiambatisho Na. 2: Wazee Wasiojiweza walio katika Makazi ya Wazee ya Serikali

MWAKA	WANAWAKE	WANAUME	JUMLA
2010	239	375	614
2011	254	324	578
2012	242	330	572
2013	257	334	591
2014	250	332	582
2015	394	333	727
2016	238	207	445
2017	267	247	514
2018	209	240	449
2019	179	204	383
2020	110	179	289
2021	100	167	267
Aprili, 2022	111	160	271

Chanzo: *WMJWM*

Kiambatisho Na. 3: Miradi ya Maendeleo katika Vyuo

Na.	Jina la Chuo	Aina ya Mradi	Hali Halisi ya Mradi Mwaka 2021/22	Kiasi Kinachotaraji wa Kukusanywa Mwaka 2022/23	Matarajio ya Mradi Ifikapo Mwaka 2024/25	Kiasi Kinachotaraji wa Kukusanywa Ifikapo Mwaka 2024/25
1.	Rungemba CDTI	Kilimo cha Parachichi	Chuo kina ekari 25 zenye miti 1,500 iliyopandwa mwaka 2019/20 yenye uwezo wa kuzalisha kilo 150,000 za parachichi ifikapo Desemba 2022. Kila kilo ya parachichi itauzwa Shilingi 2,000/=	300,000,000	Kupanda ekari 70 zitakazokuwa na jumla ya miti 4,200 ya parachichi yenye uwezo wa kuzalisha kilo 420,000 na kilo moja itauzwa Shilingi 2,000/=	840,000,000
		Ufugaji wa Samaki	Chuo kina bwawa la asili lenye ukubwa wa mita za mraba 12,269 lenye uwezo wa kuchukua samaki 245,920 kwa mwaka. Kwa mwaka 2021/22, chuo kimepanda samaki 5,000 aina ya sato ambao watakuwa na kilo 1,250 na kila kilo itauzwa Shilingi 7,000/=	8,750,000	Kufuga samaki 245,920 aina ya sato ambao watakuwa na uzito wa kilo 61,480 na kila kilo itauzwa Shilingi 7,000/=	430,360,000

Kielelezo Na. 1: Idadi ya Watu Waliofanyiwa Ukatili wa Kijinsia na Unyanyasaji kwa kipindi cha mwaka 2017 – 2021



Chanzo: Takwimu za Hali ya Ukatili na Mutekwa ya Usufuria Barabara (2017 – 2021)

Kielelezo Na. 2: Idadi ya Watoto Waliofanyiwa Ukatili wa Kijinsia kwa kipindi cha mwaka 2017 – 2021



Chanzo: Takwimu za Hali ya Ukatili na Mutekwa ya Usufuria Barabara (2017 – 2021)

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja Ilitolewa lamuliwe)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Ahsanteni sana, ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Sasa kabla sijamuita Mwenyekiti nimeletwa majina hapa kuna watu nilisema kama sioni vizuri nadhani nahitaji kubadili miwani kidogo. Kwenye Jukwaa la Spika yupo Ndugu yetu Sophia Simba ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Umoja

wa Wanawake Tanzania na alipata kuwa Mbunge pia, karibu sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Yupo pia Anjellah Kairuki ambaye alikuwa ni Mbunge mwenzetu humu ndani, karibu sana. Karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, karibuni sana Bungeni. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge sana nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii na kwa niaba yake namuona Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete akija kusoma kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati. *(Makofi)*

MHE. SALMA R. KIKWETE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusoma taarifa kuhusu utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza ni utangulizi; awali ya yote napenda kukushukuru kwa kunipa fursa kwa mujibu wa Kanuni 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo Juni, 2020 ili niwasilishe mbele ya Bunge lako tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na maoni, ushauri, mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, naomba taarifa yote ya Kamati iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge yaani *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane kifungu cha 7(1)(a) ya

Kanuni ya 137 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, pamoja ya majukumu ya Kamati hii kama zilivyo Kamati nyingine za kisekta ni pamoja na kushughulikia Bajeti ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge Huduma na Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, katika vikao vyake vilivyofanyika mwezi Machi, 2022 hapa Dodoma, Kamati ilichambua na kujadili bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni za Kudumu za Bunge. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 Kamati ilipaswa kabla ya kuchambua bajeti, kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 kwa lengo la kuona hatua ya utekelezaji wa miradi hiyo ili kuwa katika nafasi nzuri ya kuweza kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea na kukagua miradi miwili iliyo chini ya Wizara hii iliyopo katika Mikoa ya Arusha na Iringa. Miradi hiyo ni mradi wa ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru, Mradi namba 6330, na mradi wa ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba namba hiyo hapo ambayo tumeitaja.

Mheshimiwa Spika, muundo wa taarifa; taarifa hii ya Kamati imegawanyika katika maeneo makuu yafuatayo; kwanza uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti na Maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2021/2022; pili uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023; na tatu, Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, maelezo na uchambuzi kuhusu ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2021/2022; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ilifanya ukaguzi wa baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2021/2022. Ziara za ukaguzi wa miradi ya

maendeleo zilifanywa kwa kuzingatia Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata wasaa wa kukagua mradi wa ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru - Mradi Namba 6330, na mradi wa ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba, namba iliyotajwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya ukaguzi wa miradi hiyo, Kamati ilifanya tathmini na kutoa maoni yake kuhusu miradi hiyo ikiwemo hali ya upatikanaji wa fedha, uchakavu wa miundombinu na upungufu wa watumishi kama inavyoonekana katika Taarifa kubwa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu; uchambuzi wa utekelezaji wa mpango wa bajeti na maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2021/2022; katika vikao vya Kamati vilivyofanyika mwezi Machi, 2022 hapa Dodoma, Kamati ilichambua na kujadili Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum - Fungu 53 kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na kutoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara. Uchambuzi wa Kamati ulikuwa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2021/2022; katika Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni kuhusu Bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto - Fungu 53 kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya iliyokuwa Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, ilijumuisha pamoja na mambo mengine maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati matatu. Pamoja na Kamati kupokea taarifa ya utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati bado iliona kuna maoni mawili ambayo hayakutekelezwa kikamilifu ambayo ni uhaba wa watumishi na uchakavu wa miundombinu ya vyuo na taasisi za maendeleo ya jamii. Kamati itaendelea kuyasisitiza tena masuala hayo kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2021/2022; katika mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara ilipanga kukusanya jumla ya shilingi 6,000,000,000 kutokana na vyanzo mbalimbali ambapo hadi kufikia Februari, 2022, Wizara imefanikiwa kukusanya shilingi bilioni 3.07, sawa na asilimia 51.23 ya makusanyo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla hali ya ukusanyaji wa maduhuli katika Wizara hii siyo ya kuridhisha kwani hadi kufika Februari, 2022 ambapo ni asilimia 66 ya utekelezaji wa mwaka wa fedha, Wizara imekusanya asilimia 51.23 ya kiasi ilichokusudia kukusanya.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa ushauri kwa Wizara kuwa na makadirio yenye uhalisia ili kusaidia utekelezaji mzuri wa bajeti. Maelezo zaidi kuhusu ukusanyaji wa fedha za maduhuli ni kama inavyooneshwa kwenye Kielelezo Namba 1.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina mwaka 2021/2022; Kamati ilijulishwa kuwa katika mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara pamoja na taasisi zake iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 28.7 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, matumizi ya mishahara ni shilingi bilioni 12.98 na matumizi mengineyo ni shilingi bilioni 15.74. Kwa upande wa fedha za maendeleo Kamati ilijulishwa kuwa Wizara iliidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 14.9 kwa ajili ya miradi ya maendeleo; kati ya fedha hizo shilingi bilioni 4.9 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 10 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa hadi kufikia Februari, 2022, Wizara ilipokea kiasi cha shilingi bilioni 18.56 sawa na asilimia 64.6 ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo shilingi bilioni 8.6 sawa na asilimia 66.6 ni fedha kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 9.9 sawa na asilimia 63 ni fedha za matumizi mengineyo (OC).

Mheshimiwa Spika, aidha Kamati ilijulishwa hadi kufikia Februari, 2022, Wizara imepokea fedha za miradi ya maendeleo zenye jumla ya thamani ya shilingi bilioni 5.48 sawa na asilimia 36.8 ya fedha za miradi ya maendeleo

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 4.9 ni fedha za ndani sawa na asilimia 100 na shilingi milioni 580.3 ni fedha za nje sawa na asilimia 5.8. Kielelezo Namba 2 kinaonesha upatikanaji wa fedha kutoka Hazina.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa utolewaji wa fedha za matumizi ya kawaida na imeridhisha na kasi ya utolewaji wa fedha hizo hadi kufikia Februari, 2022 ambacho ni kipindi cha robo ya tatu ya utekelezaji mwaka wa bajeti na tayari Wizara imekwishapokea asilimia 64.6 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa utolewaji wa fedha za ndani za miradi ya maendeleo kwa asilimia 100. Kamati inashauri miradi hiyo iendelee kusimamiwa vema ili kuwaletea wananchi maendeleo kwa wakati. Kwa upande wa fedha za maendeleo Kamati ilifanya uchambuzi wake na kubaini utolewaji mzuri wa fedha za ndani za maendeleo kwa ambazo zimetolewa asilimia 100. Hata hivyo, kamati ilibaini utolewaji mdogo wa fedha za nje za maendeleo ambapo zilitolewa kwa asilimia 5.8 tu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitaka kujua sababu za kutolewa kidogo kwa fedha za nje za miradi ya maendeleo ambapo ilijulishwa ni kutokana na uchelewesho kutoka kwa wadau wanaohusika. Kamati inashauri mawasiliano yaendeleo kufanyika ili fedha hizo zitolewe kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha hapo Juni, 2022 ili miradi iliyopangwa kutekelezwa itekelezwe na kuwapatia wananchi maendeleo.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne; uchambuzi wa mpango wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023; ili kuweza kutekeleza malengo mbalimbali iliyojiwekea katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara iliwasilisha mbele ya Kamati Randama yake yenye kuonesha makadirio ya makusanyo ya maduhuli na matumizi kwa lengo la kuchambuliwa na kujadiliwa na Kamati. Kamati ilifanya kazi hiyo na uchambuzi ni kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka 2022/2023; Wizara kupitia Fungu 53 katika mwaka wa fedha 2022/2023 inakadiria kukusanya maduhuli ya shilingi bilioni 8.5 kutoka vyanzo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yameongezeka kwa shilingi bilioni 2.5 sawa na ongezeko la asilimia 29.4.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliarifiwa kuwa ongezeko hilo la maduhuli linatarajiwa kutoka makusanyo ya ada za vyuo vya maendeleo ya jamii kwa shilingi bilioni 1.1 sawa na asilimia 29.4; ada za usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali shilingi milioni 128.8, sawa na asilimia 19.5; ada za malazi kwa wanafunzi wa vyuo vya maendeleo ya jamii shilingi milioni 765.2, sawa na asilimia 9 ya bajeti yote ya fedha za maduhuli zinazotarajiwa kukusanywa. Kielelezo Namba 3 kinaonesha ulinganisho wa makusanyo ya maduhuli kwa mwaka 2021/2022 na 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makadirio ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kwa mwaka 2022/2023; katika eneo hili Kamati imefanya uchambuzi wa aina mbili kama ifuatavyo; kwanza ni uchambuzi wa Bajeti ya Wizara (Fungu 53); uchambuzi huu unalenga kufanya ulinganisho wa bajeti ya mwaka 2021/2022 na 2022/2023 [Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020] kwa lengo la kuona mwenendo wa bajeti ya Wizara hii.

Katika Randama iliyowasilishwa mbele ya Kamati na Wizara kuhusu makadirio yake ya matumizi kupitia Fungu 53 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako tukufu jumla ya shilingi bilioni 43.4. Kati ya fedha hizo, matumizi ya kawaida yanaombewa shilingi bilioni 32, sawa na asilimia 74.4 na shilingi bilioni 11.09, sawa na asilimia 25.5 zinaombwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa fedha hizo ambao pia unaonekana katika Kielelezo Na. 4 ni kama ifuatavyo: -

i) Mishahara ya Watumishi (PE) shilingi bilioni 14.1 sawa na asilimia 32.5;

ii) Matumizi Mengineyo (OC) shilingi bilioni 18.1 sawa na asilimia 41.8;

iii) Fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo shilingi bilioni 6.9 sawa na asilimia 15.8; na

iv) Fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo shilingi bilioni 4.19 sawa na asilimia 9.6.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wake kwa kulinganisha Bajeti ya Fungu 53 kati ya mwaka 2021/2022 na 2022/2023 na kubaini kuwa kuna upungufu wa bajeti kwa kiasi cha shilingi milioni 222.8 sawa na asilimia 0.51 kutoka shilingi bilioni 43.6 mwaka 2021/2022 hadi shilingi bilioni 43.4 mwaka 2022/2023. Upungufu zaidi unaonekana kwenye fedha za nje za miradi ya maendeleo ambazo zimepungua kwa shilingi bilioni 5.8 sawa na upungufu wa asilimia 58 kutoka shilingi bilioni 10 ya mwaka 2021/2022 hadi shilingi bilioni 4.1 mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha za mishahara kuna ongezeko la shilingi bilioni 1.15, sawa na asilimia 8.17 kutoka shilingi bilioni 12.98 ya mwaka 2021/2022 hadi shilingi bilioni 14.14 mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitaka kujua sababu ya ongezeko hili na iliarifiwa kuwa ongezeko la mishahara linatokana na kuongezeka kwa idadi ya viongozi wakuu wa Wizara walioteuliwa baada ya kuundwa kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum pamoja na ongezeko la nafasi za ajira mpya katika Idara kwa mwaka 2022/23.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuunda Wizara hii na inatoa ushauri kuongeza vifungu vya bajeti vya Wizara hii ili iweze kutekeleza shughuli za maendeleo ya Wizara hii. Aidha, Kamati inatoa wito kwa Serikali kuhakikisha fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo zitolewe zote kwa wakati ili kuboresha ustawi wa wananchi unaosimamiwa na Wizara hii. Kielelezo Namba 5 kinaonesha ulinganisho wa Bajeti ya Fungu 53 kwa mwaka 2021/2022 na 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Bajeti ya Wizara - Fungu 53 kwa kulinganisha na Mpango wa Maendeleo wa Taifa; Kamati ilifanya uchambuzi wa kulinganisha Bajeti ya Fungu 53 dhidi ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2022/2023 kwa lengo la kubaini masuala mbalimbali ikiwemo asilimia ya Bajeti ya Wizara katika Mpango huo (Bajeti ya Taifa) kati ya mwaka 2021/2022 na 2022/2023, lakini pia kuona ni kwa kiasi gani mwenendo wa bajeti hiyo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaathiri bajeti ya Fungu 53.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi huo, Kamati imebaini masuala mbalimbali kama ifuatavyo: -

i) Bajeti ya Fungu 53 kwa ujumla wake kiasi cha shilingi bilioni 43.4 kwa mwaka 2022/2023 ni asilimia 0.10 ya Bajeti yote ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa ya shilingi trilioni 41.06. Bajeti hii imepungua kutoka asilimia 0.11 dhidi ya shilingi trilioni 37.9 ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo ya mwaka 2021/2022;

ii) Bajeti ya Mishahara ya Fungu 53 dhidi ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/2023 imeendelea kubaki kiwango kilekile cha asilimia 0.1 kama ilivyokuwa mwaka wa fedha 2021/2022;

iii) Bajeti ya Maendeleo ya Fungu 53 dhidi ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa imepungua kutoka asilimia 0.9 mwaka 2021/2022 hadi asilimia 0.07 mwaka wa fedha 2022/2023. Kielelezo Namba 6 kinaonesha ulinganisho huo.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

iv) Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2022/2023 ikiwa imeongezeka kwa asilimia 7.5 kutoka shilingi trilioni 37.9 mwaka 2021/2022 hadi shilingi trilioni 41.06 mwaka 2022/2023. Aidha, Bajeti ya Fungu 53 imepungua kwa asilimia 0.5 kutoka shilingi bilioni 43.6 mwaka 2021/2022 hadi shilingi bilioni 43.4 mwaka 2022/2023;

v) Wakati Bajeti ya Mishahara ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa ikiwa imeongezeka kwa asilimia 16.32 mwaka 2021/2022 ikilinganishwa na mwaka 2022/2023, Bajeti ya mishahara ya Fungu 53 imeongezeka kwa asilimia 8.17; na

vi) Wakati Bajeti ya Maendeleo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa ikiwa imeongezeka kwa asilimia 3.5, Bajeti ya Maendeleo ya Fungu 53 imepungua kwa asilimia 25.5.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla kwa mwaka 2022/2023 kuna ongezeko la Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Hata hivyo, upungufu umeonekana katika Bajeti ya Fungu 53. Ongezeko la Bajeti ya Mishahara ya Mpango wa Maendeleo umesababisha pia ongezeko la mishahara ya Fungu 53. Hata hivyo, bajeti ya fedha za Maendeleo ya Fungu 53 imepungua ikilinganishwa na ongezeko la Bajeti ya Maendeleo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa upungufu huo wa Bajeti ya Maendeleo kwa Fungu 53 umetokana na mwitikio mdogo wa wadau wa maendeleo katika kutoa fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tano; maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati; baada ya Kamati kufanya uchambuzi wake na kubaini mambo mbalimbali inatoa ushauri, maoni na mapendekezo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, pongezi kwa kuundwa kwa Wizara. Ni ushauri wa Kamati kwa muda mrefu kwa Sekta hii

ya Maendeleo ya Jamii kuwa Wizara. Kamati inatoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan kuunda Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na kuifanya ijitegemee toka kwa iliyokuwa Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii. Jambo hili limesaidia kufahamu kwa ukaribu changamoto za taasisi zilizo chini ya Wizara hii. Kamati inashauri ni vyema sasa Wizara hii kutengewa fedha za maendeleo za kutosha katika taasisi zake ili kutatua changamoto za muda mrefu za Wizara hii na kuwaletea wananchi maendeleo.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa watumishi; uhaba wa watumishi ni changamoto inayokumba sekta na taasisi nyingi za Serikali nchini. Uhaba wa watumishi hawa unasababisha ucheleweshaji wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara na wakati mwingine kutotekeleza ipasavyo kwa majukumu hayo. Kamati imebaini tatizo hili lipo hata katika Wizara hii. Ustawi wa Jamii katika ngazi mbalimbali hususan Kata, Maafisa hawa ni muhimu katika kutatua changamoto mbalimbali za jamii kama vile huduma za unashahi na ustawi wa jamii.

Kamati imebaini pia kuwepo kwa uhaba wa vitendea kazi kama vile usafiri wa Maafisa Ustawi wa Jamii kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji wa masuala mbalimbali ya jamii hali inayopelekea kushuka kwa ari ya jamii kushiriki kwenye shughuli za miradi ya maendeleo. Kutokana na changamoto hizo Kamati inatoa ushauri ufuatao: -

(i) Serikali iwe na mkakati wa dhati wa kutoa ajira hususan katika Wizara hii ili kuongeza nguvu kazi katika ufuatiliaji wa masuala mbalimbali ya jamii;

(ii) Serikali itenge bajeti kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi vya watumishi wa Wizara kama vile vyombo vya usafiri, kompyuta, nakadhalika ili kuwarahisishia utendaji wa kazi zao katika kutatua changamoto zinazoikabili jamii.

Mheshimiwa Spika, uchakavu wa miundombinu; katika ziara yake ya ukafuguzi wa miradi ya maendeleo ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

taasisi zilizo chini ya Wizara hii, Kamati ilibaini uchakavu wa miundombinu kama vile majengo ya madarasa, Ofisi na mabweni, uchakavu wa barabara na samani. Kamati ilijulishwa pia upo uchakavu wa miundombinu katika Makazi ya Wazee ya Serikali, Makao ya Watoto Kurasini, mahabusu tano za watoto, shule za maadilisho Iramba, taasisi za mafunzo kama vyuo vya mafunzo ya jamii, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii kama Rungemba na uchakavu huo unafanya wanafunzi wasiwe na mazingira mazuri ya kujifunza. Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao: -

(i) Kwa majengo chakavu ambayo yalijengwa muda mrefu, Kamati inashauri Serikali itenge fedha za kutosha ili kujenga upya majengo ya vyuo vya Taasisi zilizo chini ya Wizara hii badala ya kuendelea kukarabati, mfano mzuri ni majengo ya vyuo vya Maendeleo ya Jamii Rugemba;

(ii) Vyuo vilivyo nje ya Mji Serikali iwekeza katika kujenga hosteli kwa wanafunzi ili kuwapunguzia usumbufu wa usafiri kwenda na kurudi chuoni na hivyo kuwafanya wasome kwa utulivu;

(iii) Kamati inashauri Wizara ihakikishe inajenga mabweni kwa wanafunzi wote wa kike na wa kiume; na

(iv) Wizara ihakikishe barabara za kwenda kwenye vyuo vyake na za ndani ya vyuo zitengenezwe na kuwa katika kiwango kizuri ili kurahisisha usafiri kwa walimu, wanafunzi na wadau wengine.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa Asasi Zisizo za Serikali; Kamati inatambua kuwa Wizara hii ndiyo msimamizi mkuu wa Asasi Zisizo za Serikali nchini kupitia Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na. 24 ya mwaka 2002 ikiwa na majukumu yafuatayo:-

(i) Kusimamia utekelezaji wa Sera za Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001, Sheria ya Mashirika Yasiyo Kiserikali namba 24 ya mwaka 2002;

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

(ii) Kuratibu utendaji kazi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kuhakikisha kwamba unakuwa na manufaa kwa nchi na jamii kwa kuzingatia vipaumbele vya maendeleo ya Taifa; na

(iii) Kusajili na kutunza Rejista ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kutunza kumbukumbu za taarifa za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea taarifa ya usimamizi, utekelezaji na mafanikio ya AZISE ambazo baada ya uchambuzi wa taarifa hiyo ilitoa maoni na ushauri ufuatao:-

(i) Kumekuwa na utitiri wa AZISE nchini ambazo nyingine hazifanyi kazi na zimefungwa, Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara hii kufanya uhakiki wa kina ili kuhakikisha AZISE zisizofanya kazi zinafutwa na kubaki na AZISE hai tu. Uhakiki huo ufanyike mara kwa mara ili kubaki na zile hai tu. Aidha, katika uhakiki na usajili wa AZISE, Wizara iwe na taarifa za AZISE zinapofanya kazi na aina ya kazi zinazofanya mahali zilipo;

(ii) Sheria za uanzishwaji wake zinazitaka AZISE kutojihusisha na siasa lakini wakati wa kampeni za uchaguzi kuna baadhi ya AZISE zinajipambanua kisiasa na kufanya shughuli za kisiasa jambo ambalo ni kinyume na sheria za nchi. Kamati inaitaka Wizara kuzichukulia hatua AZISE zenye mrengo huu na kuzisimamia zijikite katika lengo la kusajiliwa kwake;

(iii) Ni matumaini ya Kamati uboreshaji wa kanuni za AZISE zitarahisisha utendaji kazi wa AZISE. Kamati inashauri ni wakati sasa kwa Serikali kutunga kanuni hizo ili kurahisisha shughuli za usajili, usimamizi na uhakiki wa AZISE; na

(iv) Wakati wa usajili wa AZISE Kamati inashauri Serikali kupitia wasajili wasaidizi katika Mikoa na Wizara ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI izingatie ulinganifu wa mgawanyiko, vigezo kama vile kazi inazofanya na eneo la kijiografia. Hii itasaidia kutosajili AZISE nyingi zenye kazi moja katika eneo moja.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba; katika ziara zake Kamati ilitembelea Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba. Kamati ilijulishwa majengo ya chuo hiki ni urithi kutoka kwa mlowezi Lord Baroness na mkewe Chesham ambayo yalijengwa mwaka 1926. Aidha, Kamati iliarifiwa kuwa hiki ni chuo pekee kinachotoa elimu ya maendeleo ya jamii kwa wanafunzi wa kike pekee kutokana na ombi la mmiliki huyo alipokuwa anakabidhi majengo hayo kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla hali ya chuo hiki ni mbaya kutokana na uchakavu wa miundombinu ya mabweni, ofisi za walimu na madarasa ambayo ni majengo yaliyojengwa muda mrefu. Kutokana na hali hiyo Kkamati inatoa maoni na ushauri kama ifuatavyo: -

(i) Kuwe na malengo ya kuendeleza miundombinu ya chuo hiki kwa kuwa majengo yake yamechakaa sana. Kamati inasisitiza ipo haja kwa Wizara kuhakikisha inatoa bajeti ya kutosha kufanya ujenzi wa majengo mapya kwa ajili ya chuo hiki ili wanafunzi wasome kwenye mazingira bora, yenye utulivu na rafiki.

(ii) Kamati ilijulishwa kuwa katika mikakati ya kuongeza mapato ya ndani chuo hiki kimeanzisha kilimo cha parachichi takribani hekari 23. Kamati inashauri kwakuwa zao hilo linastawi zaidi katika eneo hilo, chuo kiongeze ukubwa wa eneo la kulima zao hilo ili kujiongezea mapato hayo. Aidha, Kamati inashauri kuongeza kilimo cha miti ya mbao kwa kuwa inastawi zaidi katika ukanda huo na hivyo kujiongezea kipato hapo baadae;

(iii) Kamati ilijulishwa kuwa chuo kina mahitaji makubwa ya watumishi. Kamati inashauri Wizara ione namna itakavyoweza kutatua changamoto hii ili kuendelea kutoa elimu bora kwa wanafunzi wa chuo hiki; na

(iv) Pamoja na kwamba chuo kimewekeza kwenye kuanzisha miradi ya maendeleo, Kamati inashauri kuelekeza nguvu kubwa katika kufundisha wanafunzi na si vinginevyo.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, sehemu ya sita, hitimisho; napenda kukushukuru tena kwa nafasi uliyonipa ya kuweza kuwasilisha Taarifa hii ya Kamati mbele ya Bunge lako tukufu. Aidha, namshukuru sana Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakinipa na zaidi katika kushiriki vyema katika vikao vya Kamati ikiwemo cha uchambuzi wa bajeti ya Wizara hii. Nawapongeza sana na naomba majina yao yote yaingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe na Naibu Spika, kwa kuendelea kuongoza vyema Bunge letu, hakika ninyi ni viongozi wa mfano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum - Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, (Mbunge), Naibu Waziri - Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis (Mbunge), Makatibu Wakuu wa Wizara hii wakiongozwa na Dkt. Zainab Chaula - Katibu Mkuu, Ndugu Amon Mpanju - Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati wakati wote pamoja na kushiriki vyema katika vikao vya uchambuzi wa bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Katibu wa Bunge, Ndugu Nanelwa Joyce Mwihambi, *ndc* kwa ushirikiano ambao amekuwa akiipa Kamati yetu katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati kiufanisi. Pamoja naye, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, *ndc* na Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia Kamati yetu Ndugu Gerald Magili, Msaidizi wa Kamati Ndugu Jane Ndulesi na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake bila vikwazo. *(Makofi)*

Kipekee tunawashukuru sana Makatibu wa Kamati yetu Ndugu Francisca Haule, Ndugu Happiness Ndalu, Ndugu Emmanuel Mdidi na Ndugu Chacha Nyakega kwa kuendelea kuishauri vyema Kamati na kuhakikisha majukumu ya Kamati

yanatekelezwa bila mkwamo ikiwemo kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum - Fungu 53 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ya shilingi 43,403,061,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA BAJETI YA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 PAMOJA NA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kukushukuru kwa kunipa fursa ili kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa [Nyongeza ya Nane (7) (1) (a) ya Kanuni ya 137 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020], mojawapo ya Majukumu ya Kamati hii kama zilivyo Kamati nyingine za Kisekta ni pamoja na kushughulikia

Bajeti ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii. Katika vikao vyake vilivyofanyika Mwezi Machi, 2022 hapa Dodoma, Kamati ilichambua na kujadili bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni za Kudumu za Bunge. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, Kamati ilipaswa kabla ya kuchambua Bajeti, kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha wa 2021/2022 kwa lengo la kuona hatua ya utekelezaji wa miradi hiyo ili kuwa katika nafasi nzuri ya kuweza kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea na kukagua Miradi miwili iliyo chini ya Wizara hii iliyopo katika mkoa ya Arusha na Iringa. Miradi hiyo ni mradi wa Ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru Mradi Namba 6330, na Mradi wa ukarabati wa chuo cha maendeleo ya jamii Rungemba Mradi Namba 6330.

1.1 MUUNDO WA TAARIFA

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii ya Kamati imegawanyika katika maeneo makuu yafuatayo: -

- a) Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti na Maoni ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;
- b) Uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; na
- c) Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

SEHEMU YA PILI

2.0 MAELEZO NA UCHAMBUZI KUHUSU UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ilifanya Ukaguzi wa baadhi ya Miradi

ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2021/2022. Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo zilifanywa kwa kuzingatia Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata wasaa wa kukagua Mradi wa Ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru, Mradi Namba 6330, na Mradi wa ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba Mradi Namba 6330.

2.1 MIRADI YA UJENZI NA UKARABATI KATIKA CHUO CHA MAENDELEO YA JAMII RUNGEMBA

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa katika mwaka wa fedha 2021/2022 chuo hiki kiliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu kiasi cha **shilingi 500,000,000** kwa ajili ya kutekeleza Miradi mbalimbali kama vile Ujenzi wa bweni lenye ghorofa mbili ambalo likikamilika litakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 216. Aidha Kamati ilielezwa kuwa, Chuo kinaendelea na ukarabati wa Jengo la Utawala. Pamoja na miradi hiyo Chuo kimeendelea na uboreshaji wa miradi mingine ya uzalishaji mali 43 ikiwa ni pamoja na Mradi wa uokaji wa mikate (Bakery). Kamati ilijulishwa kuwa hadi kufikia februari, 2022 tayari fedha hiyo imekwishatolewa yote.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa pia, Katika kuongeza vyanzo vya mapato, Chuo kimeanzisha miradi mbalimbali kwa kutumia fedha za matumizi ya kawaida. Miradi hiyo ni pamoja na mradi wa kilimo cha maparachichi, ufugaji nyuki, ufugaji samaki, na utekelezaji wa programu za ushirikishwaji jamii, ubunifu na uanagenzi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza chuo hiki kwa ubunifu wa miradi ambayo itaongeza pato la ndani la chuo lakini pia itawasaidia wanafunzi kuwa na ujuzi mbalimbali na kuongeza maendeleo. Hata hivyo, pamoja na pongezi hizo kamati imebaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali katika chuo hiki zikiwemo: -

i. Uchakavu wa miundombinu ya chuo; Katika ziara yake kamati ilishuhudia jinsi majengo ya chuo hiki yalivyochakaa kutokana na kuwa ya muda mrefu sana.

ii. Upungufu wa watumishi; Kamati ilijulishwa kuwa chuo hiki kimekuwa na upungufu wa watumishi kama vile, watunza kumbukumbu, wakufunzi na wakutubi. Katika kutatua changamoto hiyo chuo kimekuwa kikitumia wataalamu wa muda na wa kujitolea ili kukabiliana na tatizo hilo. Hata hivyo kamati ilijulishwa utumiaji wa watumishi wa muda umekuwa ukiongeza gharama za uendeshaji wa chuo hiki.

iii. Ukosefu wa fedha za kuendeshea miradi; Pamoja na ubunifu wa chuo katika kuanzisha miradi mbalimbali ya maendeleo ili kuongeza uwezo wao kifedha. Chuo bado kinakabiliwa na ukosefu wa rasilimali fedha za uendeshaji wa miradi hiyo.

2.2 MIRADI YA UJENZI NA UKARABATI KATIKA TAASISI YA MAENDELEO YA JAMII TENGERU

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa, Katika kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia, Taasisi hii imeendelea kutekeleza miradi ifuatayo: -

(i) Ukarabati wa kantini inayotumiwa na wanafunzi na wafanyakazi;

(ii) Jumba la mihadhara na mabweni na nyumba za watumishi;

(iii) Kuweka lami katika maeneo ya chuo, kubadilisha vifaa chakavu katika ukumbi wa mihadhara, hosteli na majengo ya ofisi.

Aidha kamati ilijulishwa kuwa Taasisi imenunua shamba la ekari 4.1 lenye thamani ya **Sh.143,500,000** lililopo katika Kijiji cha Nambala kwa lengo la kujenga Kituo cha Kitaifa cha Ubunifu wa Kidijitali. Shughuli nyingine zilizofayika ni pamoja na, ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kama vile

vifaa vya kuandikia, vipuri 45, kompyuta, printa na fotokopi, samani na ununuzi wa vitabu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakipongeza chuo hiki kwa ujenzi na ukarabati wa miradi hii ya maendeleo. Kamati inaamini miradi hii ikikamilika itawasaidia wanafunzi kusoma kwa utulivu. Ni rai ya Kamati kukamilisha miradi ya taasisi hii kwa wakati ili kuongeza thamani ya mradi na kuwasaidia wanafunzi kusoma kwa utulivu. Hata hivyo kutokana na chuo kuwa umbali mrefu kutoka mjini Kamati inatoa ushauri wa utoaji wa fedha zaidi ili kujenga mabweni ya wanafunzi wa kike na kiume ili kupunguza adha ya malazi.

SURA YA TATU

3.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Mheshimiwa Spika, Katika vikao vya Kamati vilivyofanyika Mwezi Machi, 2022 hapa Dodoma, Kamati ilichambua na kujadili Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (Fungu 53) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na kutoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo mbalimbali kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara. Uchambuzi wa Kamati ulikuwa kama ifuatavyo: -

3.1 UTEKELEZAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Mheshimiwa Spika, Katika taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni kuhusu Bajeti ya Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Fungu 53) kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya iliyokuwa wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, ilijumuisha pamoja na mambo mengine Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati matatu (3). Pamoja na Kamati kupokea Taarifa ya utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati bado iliona kuna maoni mawili ambayo hayakutekelezwa kikamilifu ambayo ni

pamoja na uhaba wa Watumishi na uchakavu wa miundombinu ya vyuo na Taasisi za Maendeleo ya Jamii. Kamati itaendelea kuyasisitiza tena masuala hayo kwenye Taarifa hii.

3.2 UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara ilipanga kukusanya **Shilingi 6,000,000,000** kutokana na vyanzo mbalimbali kama vile ada za Vyuo vya Maendeleo ya Jamii **shilingi 5,400,835,000** sawa na **asilimia 90**; uuzaji wa Mitaala ya vyuo vya Maendeleo ya Jamii **shilingi 40,000,000** sawa na **asilimia 0.6**; usajili na ada za mwaka za *NGOs* **shilingi 531,161,000** sawa na **asilimia 8.85**; uuzaji wa Mitaala ya Taasisi za Ustawi wa Jamii **shilingi 28,000,000** sawa na **asilimia 0.4** na vyanzo vingine **shilingi 4,000**.

Mheshimiwa Spika, Hadi kufikia Februari 2022, Wizara imefanikiwa kukusanya **Shilingi 3,073,691,282** sawa na **asilimia 51.23** ya makusanyo yaliyokusudiwa. Makusanyo hayo yalikuwa katika mchanganuo ufuatao: Ada za Vyuo vya Maendeleo ya Jamii **shilingi 2,850,174,020** sawa na **asilimia 52.77**; Uuzaji wa Mitaala ya vyuo vya Maendeleo ya Jamii **shilingi 4,000,000** sawa na **asilimia 10**; Usajili na ada za mwaka za *NGOs* **shilingi 209,337,262** sawa na **asilimia 39.41**; Uuzaji wa Mitaala ya Taasisi za Ustawi wa Jamii **shilingi 9,000,000** sawa na **asilimia 32.14**; na vyanzo vingine **shilingi 4,000**.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla hali ya ukusanyaji wa maduhuli katika Wizara hii siyo ya kuridhisha kwani hadi kufika Februari, 2022 ambapo ni asilimia 66 ya utekelezaji wa mwaka wa fedha, Wizara imekusanya asilimia 51.23 ya kiasi ilichokusudia kukusanya. Uchambuzi wa Kamati ulibaini makusanyo madogo toka uuzaji wa Mitaala ya Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Taasisi ya Ustawi wa Jamii. Kamati ilijulishwa kuwa makusanyo ya mapato katika Vyuo na Taasisi za Maendeleo ya Jamii hayakufikia lengo kwa sababu ya kutoanzishwa kwa vyuo vipya kwa idadi iliyotarajiwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

ambavyo vingeweza kununua mitaala kwa wingi na kuongeza mapato.

Kamati inatoa ushauri kwa Wizara kuwa na makadirio yenye uhalisia ili kusaidia utekelezaji mzuri wa Bajeti. Maelezo zaidi kuhusu ukusanyaji wa fedha za maduhuli ni kama inavyooneshwa kwenye Kielelezo Namba 1.

Kielelezo Na. 1: UKUSANYAJI WA MADUHULI FUNGU 53 KWA MWAKA 2021/2022

MAELEZO	MAKADIRIO	MAKUSANYO	ASILIMIA
Ada za Vyuo vya Maendelo ya Jamii na mapato mengine	5,400,835,000	2,850,174,020	52.77
Uuzaji wa mitaala wa vyuo vya maendeleo ya jamii	40,000,000	4,000,000	10
Ada za mashirika yasiyo ya kiserikali	531,161,000	209,337,262	39.41
Uuzaji wa mitaala wa Taasisi za maendeleo ya jamii	28,000,000	9,000,000	32.14
Mapato Mengine	4000	1,180,000	29,500
JUMLA	6,000,000,000	3,073,691,282	51.23

Chanzo: Randama ya Wizara fungu 53 (March 2022) na usanifu wa kamati

3.3 UPATIKANAJI WA FEDHA KUTOKA HAZINA MWAKA 2021/2022

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa Katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Wizara pamoja na Taasisi zake iliidhinishwa jumla ya **Shilingi 28,725,929,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Mishahara ni **Shilingi 12,985,672,000.00** na Matumizi Mengineyo **Shilingi 15,740,257,000.00**. Kwa upande wa fedha za maendeleo Kamati ilijulishwa kuwa Wizara iliidhinishwa kiasi cha **shilingi 14,900,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo; kati ya fedha hizo **shilingi 4,900,000,000** ni fedha za ndani na **shilingi 10,000,000,000** ni fedha za nje.

Mheshimiwa spika, Kamati ilijulishwa kuwa hadi kufikia Februari, 2022, Wizara ilipokea kiasi cha **Shilingi 18,565,427,532.81** sawa na **asilimia 64.6** ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo **Shilingi 8,644,991,293.00** sawa na **asilimia 66.6** ni fedha kwa

ajili ya Mishahara na **Shilingi 9,920,436,239.81** sawa na **asilimia 63** ni fedha za Matumizi Mengineyo (OC). Aidha Kamati ilijulishwa hadi kufikia Februari, 2022, Wizara imepokea fedha za miradi ya maendeleo zenye jumla ya thamani ya **Shilingi 5,480,376,200** sawa na **asilimia 36.8** ya fedha za miradi ya maendeleo zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo **shilingi 4,900,000,000** fedha za ndani sawa na **asilimia 100** na **shilingi 580,376,200** ni fedha za nje sawa na **asilimia 5.8**. Kielelezo Namba 2 kinaonesha upatikanaji wa fedha kutoka Hazina.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa utolewaji wa fedha za matumizi ya kawaida na imeridhishwa na kasi ya utolewaji wa fedha hizo hadi kufikia Februari, 2022 ambacho ni kipindi cha robo ya tatu ya utekelezaji mwaka wa Bajeti na tayari Wizara imekwishapokea **asilimia 64.6** ya Bajeti iliyoidhinishwa. Kamati inaipongeza Serikali kwa utolewaji wa fedha za ndani za miradi ya maendeleo kwa **asilimia 100**. Kamati inashauri miradi hiyo iendelee kusimamiwa vema ili kuwaletea wananchi maendeleo kwa wakati. Kwa upande wa fedha za maendeleo Kamati ilifanya uchambuzi wake na kubaini utolewaji mzuri wa fedha za ndani za maendeleo kwa ambazo zimetolewa **asilimia 100**. Hata hivyo kamati ilibaini utolewaji mdogo wa fedha za nje za maendeleo ambapo zilitolewa kwa **asilimia 5.8** tu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitaka kujua sababu za kutolewa kidogo kwa fedha za Nje za Miradi ya Maendeleo ambapo ilijulishwa ni kutokana na uchelewesho kutoka kwa wadau wanaohusika. Kamati inashauri mawasiliano yaendeleo kufanyika ili fedha hizo zitolewe kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha hapo Juni, 2022 ili Miradi iliyopangwa kutekelezwa itekelezwe na kuwapatia wananchi maendeleo.

Kielelezo Na. 2: UPATIKANAJI WA FEDHA FUNGU 53 MWAKA 2021/2022

UPATIKANAJI WA FEDHA FUNGU 53 MWAKA 2021/2022				
MATUMIZI		KILICHODHINISHWA	KILICHOPOKELEWA	ASILIMIA
KAWAIDA	MISHAHARA	12,985,672,000	8,644,991,293.00	66.6
	OC	15,740,257,000	9,920,436,239.81	63
	JUMLA	28,725,929,000	18,565,427,532.81	64.6
MAENDELEO	NDANI	4,900,000,000	4,900,000,000	100
	NJE	10,000,000,000	580,376,200	5.8
	JUMLA	14,900,000,000	5,480,376,200.00	36.78
JUMLA BAJETI		43,625,929,000	24,045,803,733.00	55.1

Chanzo: Randama ya fungu 53 (Machi 2022) na Usanifu wa Kamati

SEHEMU YA NNE

4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 imejiwekea Malengo mbalimbali kwa kuzingatia Mipango na Sera za Kitaifa na Kimataifa ambazo ni Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025); Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26); Ilani ya Chama cha Mapinduzi (2020); Malengo ya Maendeleo Endelevu (2030); na Ajenda ya Afrika Tuitakayo (2063). Wizara pia imetekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sera ya Maendeleo ya Jamii (1996), Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000), Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2001), Sera ya Taifa ya Wazee (2003), Sera ya Maendeleo ya Mtoto (2008) pamoja na Sheria ya Mtoto Sura ya 13 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019, Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2002), Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (2017/18 – 2021/22) na Ajenda ya Kitaifa ya Kuwekeza katika Afya na Maendeleo ya Vijana Balehe (2021/22 - 2024/25).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ni kama vifuatavyo: Kukuza ari ya jamii kushiriki katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo; Kuratibu wafanyabiashara wadogo (Machinga); kuboresha mazingira ya biashara zao; Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Taasisi ya Ustawi wa Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii; Kuratibu utoaji wa huduma za msingi kwa watu wenye mahitaji maalum wakiwemo manusura wa majanga mbalimbali; Kuratibu na kuwezesha upatikanaji wa haki na huduma za ustawi wa jamii kwa wazee na watoto; Kufanya kampeni ya Kitaifa ya kuhamasisha jamii kubadili mtazamo na kutumia fursa za kiuchumi zilizopo kwa ajili ya wanawake na makundi mbalimbali katika jamii kujajiri; Kuimarisha uwezesaji wa wanawake kiuchumi kwa kutoa mafunzo ya ujasiriamali, mikopo yenye masharti nafuu na kuwezesha upatikanaji wa teknolojia wezeshi; Kuingiza masuala ya jinsia katika Sera, Mikakati, Mipango, Miongozo na Bajeti za Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia; Kuhamasisha ushiriki wa wanawake katika ngazi za uongozi na nafasi mbalimbali za maamuzi; Kuratibu afua za kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake, watoto na wazee; Kuimarisha mifumo ya malezi, ulinzi na maendeleo ya watoto na familia; Kuratibu utekelezaji wa huduma jumuishi za Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Watoto kwa watoto katika umri wa miaka 0-8; Kuratibu utekelezaji wa Ajenda ya Kitaifa ya Kuwekeza katika Afya na Maendeleo ya Vijana Balehe (2021/22 - 2024/25); Kuratibu utekelezaji wa Ajenda ya Malezi (*Parenting Agenda 2019 – 2030*) ijulikanayo kama “Familia Bora Taifa Imara; na Kuimarisha ushiriki na mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika katika Maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Ili kuweza kutekeleza malengo haya pamoja na majukumu mbalimbali, Wizara iliwasilisha mbele ya Kamati, Randama yake yenye kuonesha Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli na Matumizi kwa lengo la kuchambuliwa na kujadiliwa na Kamati. Kamati ilifanya kazi hiyo na uchambuzi ni kama ifuatavyo: -

4.1 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA 2022/2023

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia **Fungu 53** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 inakadiria kukusanya maduhuli ya **Shilingi 8,500,000,000**. Fedha hizi zinatarajiwa kukusanywa kutoka vyanzo mbalimbali ambavyo ni pamoja na ada za Vyuo vya Maendeleo ya Jamii **shilingi 6,600,560,000**; uuzaji wa Mitaala ya Maendeleo ya Jamii **shilingi 40,000,000**; ada ya malazi kwa wanafunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii **shilingi 765,235,000**; usajili na ada za mwaka za *NGOs* **shilingi 660,000,000**; na uuzaji wa Mitaala ya Vyuo vya Ustawi wa Jamii **shilingi 15,000,000**.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya Uchambuzi wake kwa kulinganisha Makadirio ya Makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ambapo Wizara ilikadiria kukusanya **shilingi 6,000,000,000** dhidi ya yale ya mwaka 2022/2023 ambapo **shilingi 8,500,000,000** zinatarajiwa kukusanywa. Baada ya uchambuzi huo Kamati imebaini kuwa makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 yameongezeka kwa **shilingi 2,500,000,000** sawa na ongezeko la **asilimia 29.4**.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliarifiwa kuwa ongezeko hilo la maduhuli linatarajiwa kutoka makusanyo ya ada za vyuo vya maendeleo ya jamii kwa **shilingi 1,119,725,000** sawa na **asilimia 29.4**; ada za usajili wa mashirika yasiyo ya kiserikali **shilingi 128,839,000** sawa na **asilimia 19.5**; ada za malazi kwa wanafunzi wa vyuo vya maendeleo ya jamii **shilingi 765,235,000** sawa na **asilimia 9** ya bajeti yote ya fedha za maduhuli zinazotarajiwa kukusanywa. Kielezo Namba 3 kinaonesha ulinganisho wa makusanyo ya maduhuli kwa mwaka 2021/2022 na 2022/2023

Kielelezo Na. 3: ULINGANISHO WA MADUHILI 2021/2022 NA 2022/2023 - FUNGU 53

MAELEZO	2021/2022	2022/2023	ASILIMIA %
Ada za vyuo	5,400,835,000	6,600,560,000	18.1
Uuzaji wa mitaala ya maendeleo ya jamii	40,000,000	40,000,000	0
Ada ya malazi	0	765,235,000	100
Usajili wa NGOs	531,161,000	660,000,000	19.52
Uuzaji wa mitaala ya vyuo vya ustawi	28,000,000	15,000,000	-46
Jumla	6,000,000,000	8,500,000,000	29.4

Chanzo: Randama ya fungu 53 (Machi, 2022) na Usanifu wa kamati

4.2 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2022/2023

Mheshimiwa Spika, Katika eneo hili Kamati imefanya uchambuzi wa aina mbili kama ifuatavyo: -

a) Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara (Fungu 53)

Mheshimiwa Spika, uchambuzi huu unalenga kufanya ulinganisho wa bajeti ya mwaka 2021/2022 na 2022/2023 [Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020] kwa lengo la kuona mwenendo wa bajeti ya Wizara hii. Katika Randama iliyowasilishwa mbele ya Kamati na Wizara kuhusu makadirio yake ya matumizi kupitia Fungu 53 kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi Sh.43,403,061,000**. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida yanaombewa **Shilingi 32,310,981,000.00** sawa na **asilimia 74.4** na **Shilingi 11,092,080,000.00** sawa na **asilimia 25.5** zinaombwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa fedha hizo ambao pia unaonekana katika kielelezo Na. 4 ni kama ifuatavyo: -

i) Mishahara ya Watumishi (PE) **Shilingi 14,141,924,000** sawa na **asilimia 32.5**;


ii) Matumizi Mengineyo (OC) **Shilingi 18,169,057,000** sawa na **asilimia 41.8**;

iii) Fedha za Ndani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo **Shilingi 6,900,000,000** sawa na **asilimia 15.8**; na

iv) Fedha za Nje kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo **Shilingi 4,192,080,000** sawa na **asilimia 9.6**.

Kielelezo Na. 4: BAJETI (FUNGU 53) 2022/2023

BAJETI (FUNGU 53) 2022/2023



Chanzo: Randama ya tungu 53 (Machi 2022) na Usanifu wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wake kwa kulinganisha Bajeti ya **Fungu 53** kati ya Mwaka 2021/2022 na 2022/2023 na kubaini kuwa kuna upungufu wa Bajeti kwa kiasi cha **Shilingi 222,868,000** sawa na **asilimia 0.51** kutoka **Shilingi 43,625,929,000** mwaka 2021/2022 hadi **Shilingi 43,403,061,000** mwaka 2022/2023. Upungufu zaidi unaonekana kwenye fedha za nje za miradi ya maendeleo ambazo zimepungua kwa **shilingi 5,807,920,000** sawa na upungufu wa **asilimia 58** kutoka **shilingi 10,000,000,000** ya mwaka 2021/2022 hadi **shilingi 4,192,080,000** mwaka 2022/2023.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Kwa upande wa fedha za mishahara kuna ongezeko la **shilingi 1,156,252,000** sawa na **asilimia 8.17** kutoka **Shilingi 12,985,672,000** ya mwaka 2021/2022 hadi **Shilingi 14,141,924,000** mwaka 2022/2023. Kamati ilitaka kujua sababu ya ongezeko hili na iliirifiwa kuwa ongezeko la mishahara linatokana na kuongezeka kwa idadi ya Viongozi Wakuu wa Wizara walioteuliwa baada ya kuundwa kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum pamoja na ongezeko la nafasi za ajira mpya katika Idara kwa mwaka 2022/23.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuunda Wizara hii na inatoa ushauri kuongeza vifungu vya Bajeti vya Wizara hii ili iweze kutekeleza shughuli za maendeleo ya wizara hii. Aidha kamati inatoa wito kwa Serikali kuhakikisha fedha zinazoidhinishwa kwaajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo zitolewe zote kwa wakati ili kuboresha ustawi wa wananchi unaosimamiwa na Wizara hii.

		2021/2022	2022/2023	ONGEZEKO/UPUNGUFU	%
KAWAIDA	MISHAHARA	12,985,672,000	14,141,924,000	1,156,252,000	8.17
	OC	15,740,257,000	18,169,057,000	2,428,800,000	13.36
	JUMLA	28,725,929,000	32,310,981,000	3,585,052,000	11
MAENDELEO	NDANI	4,900,000,000	6,900,000,000	200,000,000,000	28.98
	NJE	10,000,000,000	4,192,080,000	-5,807,920,000	-58
	JUMLA	14,900,000,000	11,092,080,000	-3,807,920,000	-25.5
JUMLA BAJETI	JUMLA KUU	43,625,929,000	43,403,061,000	-222,868,000	-0.5

Chanzo: Randama ya fungu 53 (Machi 2022) na Usanifu wa Kamati

b) Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara (Fungu 53) kwa Kulinganisha na Mpango wa Maendeleo wa Taifa

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa kulinganisha Bajeti ya Fungu 53 dhidi ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/2023 kwa lengo la kubaini masuala mbalimbali ikiwemo asilimia ya Bajeti ya Wizara katika Mpango huo (Bajeti ya Taifa) kati ya mwaka 2021/2022 na 2022/2023, lakini pia kuona ni kwa kiasi gani mwenendo wa bajeti hiyo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaathiri bajeti ya Fungu 53.

Mheshimiwa Spika, Katika uchambuzi huo, Kamati imebaini masuala mbalimbali kama ifuatavyo: -

i) Bajeti ya **Fungu 53** kwa ujumla wake kiasi cha **shilingi 43,403,061,000** kwa mwaka 2022/2023 ni **asilimia 0.10** ya Bajeti yote ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa ya **Shilingi 41,063,915.000,000**. Bajeti hii imepungua kutoka **asilimia 0.11** dhidi ya shilingi **37,980,601,000,000** ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo ya mwaka 2021/2022;

ii) Bajeti ya Mishahara ya **Fungu 53** dhidi ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/2023 imeendelea kubaki kiwango kilekile cha **asilimia 0.1** kama ilivyokuwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

iii) Bajeti ya Maendeleo ya **Fungu 53** dhidi ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa imepungua kutoka **asilimia 0.9 mwaka 2021/2022** hadi **asilimia 0.07** Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, Kielelezo Na. 6 kinaonyesha ulinganisho huo.

Kielelezo Na. 6:

ULINGANISHO WA BAJETI YA FUNGU 53 DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2021/2022 NA 2022/2023

ULINGANISHO WA BAJETI FUNGU 53 DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2021/2022			
MATUMIZI	BAJETI KUU YA TAIFA	BAJETI FUNGU 53	% FUNGU 53
MISHAHARA	8,150,509,000,000	12,985,672,000	0.1
OC	4,189,199,000,000	15,740,257,000	0.3
MAENDELEO	14,977,615,000,000	14,900,000,000	0.9
MFUKO MKUU WA SERIKALI	10,663,278,000,000	-	-
JUMLA	37,980,601,000,000	43,625,929,000	0.11
ULINGANISHO WA BAJETI FUNGU 53 DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2022/2023			
MATUMIZI	BAJETI KUU YA TAIFA	BAJETI FUNGU 53	% FUNGU 53
MISHAHARA	9,740,753,000,000	14,141,924,000	0.1
OC	4,493,456,000,000	18,169,057,000	0.4
MAENDELEO	15,521,341,000,000	11,092,080,000	0.07
MFUKO MKUU WA SERIKALI	11,308,365,000,000	-	-
JUMLA	41,063,915,000,000	43,403,061,000	0.10

Chanzo: Mpango wa Maendeleo wa Taifa, Randama Fungu 53 (Machi 2022) na Usanifu wa Kamati.

iv) Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2022/2023 ikiwa imeongezeka kwa **asilimia 7.5** kutoka **Shilingi Trilioni 37.9** mwaka 2021/2022 hadi **shilingi Trilioni 41.06** mwaka 2022/2023. Aidha Bajeti ya Fungu 53 imepungua kwa **asilimia 0.5** kutoka **shilingi bilioni 43.6** mwaka 2021/2022 hadi **shilingi bilioni 43.3** mwaka 2022/2023;

v) Wakati Bajeti ya Mishahara ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa ikiwa imeongezeka kwa **asilimia 16.32** mwaka 2021/2022 ikilinganishwa na mwaka 2022/2023, Bajeti ya mishahara ya **Fungu 53** imeongezeka kwa **asilimia 8.17**; na

vi) Wakati Bajeti ya Maendeleo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa ikiwa imeongezeka kwa **asilimia 3.5**, Bajeti ya Maendeleo ya Fungu 53 imepungua kwa **asilimia 25.5**.

Mheshimiwa Spika, Kwa ujumla kwa mwaka 2022/2023 kuna ongezeko la Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Hata hivyo upungufu umeonekana katika Bajeti ya Fungu 53. Ongezeko la Bajeti ya Mishahara ya Mpango wa Maendeleo umepelekea pia ongezeko la Mishahara ya Fungu 53. Hata hivyo Bajeti ya Fedha za Maendeleo ya Fungu 53 imepungua

ikilinganishwa na ongezeko la Bajeti ya Maendeleo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa upungufu huo wa Bajeti ya Maendeleo kwa Fungu 53 umetokana na mwitikio mdogo wa wadau wa maendeleo katika kutoa fedha hizo.

SEHEMU YA TANO

5.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kufanya uchambuzi wake na kubaini mambo mbalimbali inatoa ushauri, maoni na mapendekezo kama ifuatavyo: -

5.1 PONGEZI KWA KUUNDWA KWA WIZARA

Mheshimiwa Spika, Ni ushauri wa Kamati kwa muda mrefu kwa sekta hii ya Maendeleo ya Jamii kuwa Wizara. Kamati inatoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais kuunda Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na kuifanya ijitegemee toka kwa iliyokuwa wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii. Jambo hili limesaidia kufahamu kwa ukaribu changamoto za Taasisi zilizo chini ya Wizara hii. Kamati inashauri ni vema sasa Wizara hii kutenga fedha za maendeleo za kutosha katika Taasisi zake ili kutatua changamoto za muda mrefu za Wizara hii na kuwaletea Wananchi Maendeleo.

5.2 UHABA WA WATUMISHI

Mheshimiwa Spika, Uhaba wa watumishi ni changamoto inayoikumba Sekta na Taasisi nyingi za Serikali nchini. Uhaba wa watumishi hao unasababisha ucheleweshaji wa utekelezaji wa mujukumu ya Wizara na wakati mwingine kutotekeleza ipasavyo kwa majukumu hayo. Kamati imebaini tatizo hili lipo hata katika Wizara hii. Kwa mujibu wa taarifa za Wizara upungufu wa Maafisa Ustawi wa Jamii katika ngazi mbalimbali hususan Kata; Maafisa hawa ni muhimu katika kutatua changamoto mbalimbali za jamii kama vile huduma za unasihi na ustawi wa jamii.

Kamati imebaini pia kuwepo kwa uhaba wa vitendea kazi kama vile usafiri wa maafisa ustawi wa jamii kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji wa masuala mbalimbali ya jamii hali ilinayopelekea kushuka kwa ari ya jamii kushiriki kwenye shughuli na Miradi ya Maendeleo. Kutokana na changamoto hizo kamati inatoa ushauri ufuatao: -

i. Serikali iwe na mkakati wa dhati wa kutoa ajira hususan katika Wizara hii ili kuongeza nguvukazi katika ufuatiliaji wa masuala mbalimbali ya jamii.

ii. Serikali itenge Bajeti kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi vya watumishi wa wizara kama vile vyombo vya usafiri, kompyuta na kadhalila ili kuwarahisikia usafiri na kuifikia jamii kiurahahi na kutatua changamoto zao.

5.3 UCHAKAVU WA MIUNDOMBINU

Katika ziara zake za ukaguzi wa miradi ya maendeleo ya Taasisi zilizo chini ya Wizara hii, kamati ilibaini uchakavu wa miundombinu kama vile majengo ya madarasa, ofisi na mabweni; uchakavu wa barabara na samani. Kamati ilijulishwa pia upo Uchakavu wa miundombinu katika Makazi ya Wazee ya Serikali, Makao ya Watoto Kurasini, Mahabusu tano za Watoto, Shule ya Maadilisho Irambo, Taasisi za mafunzo kama Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii kama Rungemba na Uchakavu huo unafanya wanafunzi wasiwe na mazingira mazuri ya kujifunzia. Kamati inatoa maoni Na ushauri ufuatao: -

i. Kwa majengo chakavu ambayo yalijengwa muda mrefu mno, Kamati inashauri Serikali itenge fedha za kutosha ili kujenga upya majengo ya vyuo na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii badala ya kuendelea kukarabati. Mfano mzuri ni majengo ya Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba.

ii. Kwa vyuo vilivyo nje ya mji, Serikali iwekeze katika kujenga hostel kwa wanafunzi ili kuwapunguzia usumbufu wa usafiri wa kwenda na kurudi chuoni na hivyo kuwafanya wasome kwa utulivu.

iii. Kamati inashauri Wizara ihakikishe inajenga mabweni kwa wanafunzi wote wa kike na wa kiume ili kupunguza adha ya ukosefu wa malazi kwa wanafunzi.

iv. Wizara ihakikishe barabara ya kwenda kwenye vyuo vyake na za ndani ya vyuo zitengenezwe na kuwa katika kiwango kizuri ili kurahisisha usafiri kwa walimu, wanafunzi na wadau wengine wa vyuo.

5.4 USIMAMIZI WA ASASI ZISIZO ZA SERIKALI

Mheshimiwa Spika, kamati inatambua kuwa Wizara hii ndio msimamizi mkuu wa Asasi Zisizo za Serikali (AZISE) nchini kupitia Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na. 24 ya mwaka 2002 ikiwa na Majukumu yafuatayo: Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya Mwaka 2001 na Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na. 24 ya mwaka 2002; Kuratibu utendaji kazi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kuhakikisha kuwa unakuwa na manufaa kwa nchi na jamii kwa kuzingatia vipaumbele vya maendeleo ya Taifa; Kusajili na kutunza rejista ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali; na Kutunza kumbukumbu na taarifa za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Kamati ilipokea taarifa ya usimamizi, utekelezaji na mafanikio ya AZISE ambapo baada ya uchambuzi wa taarifa hiyo ilitoa maoni na ushauri ufuatao: -

i. Kumekuwa na utitiri za AZISE nchini ambazo nyingine hazifanyi kazi na zimefungwa, Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara hii kufanya uhakiki wa kina ili kuhakikisha AZISE zisizofanya kazi zinafutwa na kubaki na AZISE hai tu; Uhakiki huo ufanyike mara kwa mara ili kubaki na zile hai tu. Aidha Katika uhakiki na usajili wa AZISE, Wizara iwe na taarifa ya AZISE zinapofanya kazi na aina ya kazi inazofanya mahali ilipo;

ii. Sheria za uanzishwaji wake inazitaka AZISE kutojijhusisha na siasa lakini wakati wa kampeni za uchaguzi kuna baadhi ya AZISE zinajipambanua kisiasa na kufanya shughuli za kisiasa jambo ambalo ni Kinyume na Sheria. Kamati inaitaka Wizara

kuzichukulia hatua AZISE zenye mlengo huu na kuzisimamia zijikite katika lengo la kusajiliwa kwake.

iii. Ni matumaini ya Kamati uboreshaji wa kanuni za AZISE zitarahisisha utendaji kazi wa AZISE. Kamati inashauri ni wakati sasa kwa Serikali kutunga kanuni hizo ili kurahisisha shughuli za usajili, usimamizi na uhakiki wa AZISE nchini;

iv. Wakati wa usajili wa AZISE Kamati inashauri Serikali kupitia wasajili wasaidizi katika Mikoa na Wizara ya OR - TAMISEMI izingatie ulinganifu wa mgawanyo/vigezo kama vile kazi inazofanya na eneo la kijografia. Hii itasaidia kutosajili AZISE nyingi zenye kazi moja katika eneo moja.

5.5 CHUO CHA MAENDELEO YA JAMII RUNGEMBA

Mheshimiwa Spika, katika ziara zake kamati ilitembelea Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba. Kamati ilijulishwa majengo ya chuo hiki ni urithi kutoka kwa mlowezi Lord Baroness na mkewe Marion Lady Chesham ambayo yalijengwa mwaka 1926. Aidha Kamati iliarifiwa kuwa hiki ni Chuo pekee kinachotoa elimu ya Maendeleo ya Jamii kwa wanafunzi wa kike pekee kutokana na ombi la mmiliki huyo alipokuwa anakabidhi majengo hayo kwa Serikali. Kwa ujumla hali ya chuo hiki ni mbaya kutokana na uchakavu wa miundombinu ya mabweni, ofisi za walimu na madarasa ambayo ni majengo yaliyojengwa muda mrefu. Kutokana na hali hiyo kamati inatoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

i. Kuwe na malengo ya kuendeleza miundombinu ya chuo hiki kwa kuwa majengo yake yamechakaa sana. Kamati inasisitiza ipo haja kwa wizara kuhakikisha inatoa bajeti ya kutosha kufanya ujenzi wa majengo mapya kwa ajili ya Chuo hiki ili wanafunzi wasome kwenye mazingira bora na utulivu.

ii. Kamati ilijulishwa kuwa katika mikakati ya kuongeza mapato ya ndani chuo hiki kimeanzisha kilimo cha maparachichi katika hekari 23. Kamati inashauri kwakuwa zao hilo linastawi zaidi katika eneo hilo, chuo kiongeze ukubwa wa eneo la kulima zao hilo ili kujiongezea mapato

hayo. Aidha kamati inashauri kuongeza kilimo cha miti ya mbao kwa kuwa inastawi zaidi katika ukanda huo na hivyo kujiongezea kipato hapo baadae.

iii. Kamati ilijulishwa kuwa chuo kina mahitaji makubwa ya watumishi. Kamati inashauri Wizara ione namna itakavyoweza kutatua changamoto hii ili kuendelea kutoa elimu bora kwa wanafunzi wa chuo hiki.

iv. Pamoja na kwamba chuo kimewekeza kwenye kuanzisha miradi ya maendeleo; Kamati inashauri kuelekeza nguvu kubwa katika kufundisha wanafunzi na si kwenye mradi pekee.

SEHEMU YA SITA

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru tena kwa nafasi uliyonipa ya kuweza kuwasilisha Taarifa hii ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, namshukuru sana Makamu Mwenyekiti - Mhe. Aloyce John Kamamba, Mb pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakinipa na zaidi katika kushiriki vyema katika vikao vya Kamati ikiwemo cha uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii. Naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa majina kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Aloyce John Kamamba, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Eng. Samweli Hhayuma Xaday Mb - Mjumbe
5. Mhe. Husna Juma Sekiboko, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Tecla Mohamedi Ungele, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Kassim Hassan Haji, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Francis Leonard Mtega, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Latifa Khamis Juakali, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Kabula Enock Shitobela, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb - Mjumbe

13. Mhe. Bernadeta Kasabago Mushashu, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Neema Kichiki Lugangira, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Mussa Ramadhani Sima, Mb - Mjumbe
17. Mhe. George Ranwell Mwenisongole, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Dkt. Paulina Daniel Nahato, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Salome Wycliffe Makamba, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Abdallah Dadi Chikota, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Khamis Kassim Ali, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Khalifa Mohamed Issa, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Hassan Zidadu Kungu, Mb - Mjumbe
24. Mhe. Nashon William Bidyanguze, Mb - Mjumbe
25. Mhe. Hamisi Shabani Taletale, Mb - Mjumbe
26. Mhe. Prof. Kitila Alexander Mkumbo - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe na Naibu Spika, kwa kuendelea kuongoza vyema Bunge letu. Hakika ninyi ni viongozi wa mfano.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum - Mhe. Dkt. Doroth Onesphoro Gwajima (Mb), Naibu Waziri - Mhe. Mwanaidi Ali Khamis (Mb), Makatibu Wakuu wa Wizara hii wakiongozwa na Dkt Zainab Chaula - Katibu Mkuu, Ndg. Amon Mpanju - Naibu Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati wakati wote pamoja na kushiriki vyema katika vikao vya uchambuzi wa bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Katibu wa Bunge - Ndg. Nenelewa Joyce Mwiambi, *ndc* kwa ushirikiano ambao amekuwa akiipa Kamati yetu katika kutekeleza majukumu ya Kamati Kiufanisi. Pamoja nae, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, *ndc* na Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia Kamati yetu Ndugu Gerald Magili, Msaidizi wa Kamati Ndg. Jane Ndulesi na Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake bila vikwazo. Kipekee tunawashukuru sana Makatibu wa Kamati yetu Ndg. Francisca Haule, Ndg. Happiness Ndalul, Ndg. Emmanuel

Mdidi na Ndg. Chacha Nyakega kwa kuendelea kuishauri vyema Kamati na kuhakikisha majukumu ya Kamati yanatekelezwa bila mkwamo ikiwemo kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum - **Fungu 53** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 jumla ya **Shilingi 43,403,061,000**.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja.

Stanslaus H. Nyongo (Mb),

MWENYEKITI

KAMATI YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII

30 MEI, 2022

SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge tumesikia maoni ya Kamati inayohusika na Wizara hii na sasa tunaanza uchangiaji, ninayo majina ya Waheshimiwa Wabunge walioomba fursa ya kuchangia kwenye hoja hii. Tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, atafuatiwa na Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu ajiandae.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia katika Wizara hii. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutupa afya njema na kibali cha kusimama mahali hapa.

Mheshimiwa Spika, lakini namshukuru sana na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan kwa maono yake makubwa kuanzisha Wizara hii mama ambayo inashughulika na ustawi wa jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katia hotuba ya bajeti ya Wizara hii iliyoko mbele yetu kuna vipaumbele kadha wa kadha ambavyo wameviweka. Moja ya kipaumbele ni kuendelea kuimarisha huduma za ustawi wa jamii na haki kwa familia na watoto ikiwemo malezi ya kambo na kuasili, malezi makuzi na maendeleo ya jamii, lakini zaidi ni kuhakikisha kwamba kuna kuwa na maendeleo ya awali, ulinzi na usalama kwa watoto dhidi ya vitendo vya ukatili.

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu hivi karibuni kumekuwa na wimbi kubwa la ukatili wa kijinsia, ukatili wa kingono, ukatili wa kifikra, lakini ukatili wa kimwili. Ukiangalia hasa katika Mkoa wa Shinyanga inaonesha kabisa ni dhahiri kwamba kuna ukatili mkubwa wa kijinsia. Ukiangalia takwimu inaonesha kwamba kutoka Juni, 2020 hadi Disemba, 2021 ukatili wa kingono kwa watu wazima umekuwa na matukio karibia 217; lakini kwa watoto ukatili wa kingono watoto jumla 661 wamefanyiwa ukatili wa kingono. Katika hiyo idadi ya watu wazima 217 ambao ni wanawake kwa wanaume waliyofanyiwa ukatili wa kingono, kesi ambazo zilipelekwa Mahakamani ni 149 kati ya 217 na ambazo zilipelekwa Makamani zikahukumwa ni kesi 80 peke yake. Hii inasikitisha sana, watu wazima 217 lakini watoto 661, kesi ambazo zimepelekwa Mahakamani ni 149 tu na ambazo zimekuja kuamuliwa kesi 80 hii haikubaliki. Tatizo ni nini, hapa kuna tatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jamii yetu imekuwa ikinyanyasika katika ukatili wa kijinsia, ukatili wa kingono, ukatili wa kimwili, lakini ukatili wa kihisia. Kesi zinapelekwa Mahakamani na ukizingatia sheria hii ya watu wanaofanya ukatili hasa la suala zima la wanaobaka, wanaolawiti, wanaofanya vitendo vyovyote vile vya unyanyasaji wa kingono, sheria inampa dhamana mhusika, wakishawekewa dhamana wanatoroka, kesi zinapotelea hewani.

Ngingomba Mheshimiwa Waziri kama inawezekana sheria inawa-*favor*wale watu ambao wanafanya uhalifu, basi sheria iletwe hapa Bungeni tuweze kurekebisha. Kwa sababu kama mtu anahujumu uchumi, anakuwa hana dhamana, je,

anayehujumu uhai wa mtu inakuwaje, hili halikubaliki. Tunajenga kizazi ambacho kinakuwa na maisha magumu, angalia watoto wa mitaani walivyo wengi, ukitafuta historia ya hawa watoto ni wengi ambao wamenyanyasika majumbani na watu ambao wanawanyanyasa hawa watoto au wanawafanyia vitendo vya ukatili ni watu ambao wanatuzunguka, wanaweza wakawa ni ndugu zetu, wanaweza wakawa ni majirani, wanaweza wakawa ni walimu. Lakini anapobainika ya kwamba amefanya ukatili akafikishwa kwenye chombo cha sheria anahaki ya kupata dhamana. Akishapata dhamana, amewekewa dhamana na watu wanne anatoroka, anakwenda kusikojulikana, huko kusikojulikana ni wapi ambako hawezi kupatikana.

Mheshimiwa Spika, ninafikiri kuna umuhimu wa sheria hii kubadilishwa ili hawa watu ambao wanaowabaka watoto wetu, ambao wanafanya ukatili kwa jamii wasiwe na dhamana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kule Shinyanga mwaka huu mapema mtoto wa mwaka mmoja na miezi 11 alifanyiwa ukatili wa kingono na baba yake wa kambo. Mtoto akaharibika vibaya, *Shinyanga Government* pale ikashindwa kumtibu ikampeleka Bugando. Lakini huyu mtu aliyefanya unyama huu bado ana haki ya kupata dhamana, kweli akipata dhamana akakaa nje anajua kabisa kwamba ninathibitika nilifanya huu ukatili atabaki, si atakimbia. Vitendo vimeongezeka na ndiyo maana tunajenga jamii ambayo inakuwa ina ukatili, ukiangalia wale watoto wako mitaani Dar es Salaam au hapa Dodoma, wanavuta unga, wanavuta gundi ni kwa sababu ya malezi na ukatili ambao yumkini wamefanyiwa kule nyumbani.

Mheshimiwa Spika, tunatakiwa tuziangalie sheria zetu vizuri, kuangalia ni kwa nini wanapata hiyo *favor* ndiyo ni haki na ninajua wanasheria sasa hivi wanaoshughulika na haki za binaadam wanajitahidi sana kuhakikisha kwamba inakuja sheria ya makosa yote kuwa na dhamana, lakini kwa kosa la ukatili wa kijinsia kwa watoto na wanaume na wanawake halikubaliki hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa pia nizungumzie kidogo kuhusu suala zima la mikopo ya wanawake, vijana pamoja walemavu. Kwa kweli tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuhamasisha na kuendelea kuhakikisha kwamba fedha kwa ajili ya mikopo ya wanawake, fedha kwa ajili ya mikopo ya vijana, lakini na watu wenye makundi maalum - walemavu wanapata. Niwapongeze sana, sana Wakurugenzi wa Mkoa wa Shinyanga, sisi Shinyanga katika *10 percent* ya mikopo hii ambayo wanapewa watu wenye makundi maalum nikiwa na maana ya wanawake, vijana pamoja na watu wenye ulemavu jumla ya shilingi bilioni 18 zimeweza kutolewa katika Mkoa wetu wa Shinyanga hadi kufikia Februari, 2022.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nawapongeza sana Wakurugenzi pamoja na Waheshimiwa Madiwani kuhakikisha kwamba wanasimamia hizi fedha, ili wanawake waweze kunufaika ni zaidi ya asilimia 91 ya mapato ya ndani kwa kweli ni kazi na ni hatua kubwa sana. Lakini nimpongeze Rais pia kwa kuwajali Wamachinga amewaweka katika *group* la makundi maalum, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais na tunasikia siji ilikuwa tarehe ngapi pale, aliweza kusema kwamba atawapa shilingi milioni 10 wamachinga Tanzania nzima kila Mkoa. Kwa kweli hili ni suala la kumpongeza ni jinsi gani ambavyo anawathamini wananchi wake, ni jinsi gani ambavyo anataka kila mtu ajikomboe kiuchumi kwa kweli tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini ningependa kuishauri Wizara ya Maendeleo ya Jamii, hii mikopo pamoja na kwamba inatolewa na haya makundi, lakini kule vijijini sina hakika kama hii mikopo kule vijijini inawafikia walengwa wengi. Mikopo mingi hii inatoka kwenye vile vikundi vya mjini ambavyo watu tayari wanauielewa wa nini wanafanya au tayari wameshaanza biashara zao.

Ningeomba mjielekeze katika sehemu ambazo ziko pembezoni kule wanawake wana uhitaji, wanawake wanataka kufanya biashara lakini hawajui waanze kufanyaje hiyo biashara.

Mheshimiwa Spika, tungeomba Wizara kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii ambao wako kule pembezoni waweze kuwafikia wanawake wengi, waweze kuwafikia vijana wengi, waweze kuwafikia watu wenye ulemavu ili basi waweze kujikimu na wao waweze kufanya biashara. Lakini ningepomba hili suala la kujenga vituo vya wamachinga ninaomba Serikali ilichukue kwa uzito mkubwa. Tumeona baadhi ya mikoa mfano hapa Dodoma kuna sehemu ambapo inajengwa hilo soko la wamachinga kwa kweli ni soko zuri. Basi hata mikoa mingine iweze kuiga huo mfano, ihakikishe kwamba wamachinga wanatengewa sehemu nzuri, wanaweza kufanya biashara zao bila kubugudhiwa, wanaweza kuendelea kuongeza pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kunipa hii nafasi ninaomba Wizara hii iwajali pia wale watu ambao ni wanasaikolojia. Tunajua watu wakishafanyiwa ukatili wa kijinsia, wakishafanyiwa ukatili wa kiuchumi, wakifanyiwa ukatili wa aina yoyote ile kisaikolojia wanakuwa hawako vizuri. Kuna hawa watu ambao wamesoma wako barabarani, hawajapata ajira...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Haya ahsante sana Mheshimiwa kengele ya pili imeshagonga.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Spika, wanasaikolojia tunaomba waajiriwe ili kupunguza tatizo. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Shally Josepha Raymond atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mheshimiwa Amina Daud Hassan ajiandae.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ninakuomba kwa huruma ya kiti kabla sijaanza mchango wangu, nitoe pole kwa wazazi wa kijana William Manento Elifuraha aliyepoteza maisha hapo *UDOM*

akiwa katika matibabu. Yeye ni kijana aliyekuwa mwaka wa tatu katika ndaki ya elimu na ninapozungumza hapa sasa hivi waliondoka jana kusafirisha. Kwa hiyo, wale ni eneo ninalotokea, nasikitika nao na pia nawapa pole. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sasa niingie kwenye mchango, awali ya yote namshukuru Mungu kwa kutupa uhai wote na kuweza kuwa hapa kuongelea mambo ya maendeleo. Leo tunaongelea eneo ambalo ni mtambuka. Tunaposema Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ni Wizara ambayo inagusa kila mahali. Lakini nichukue fursa hii kipekee kabisa kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuona umuhimu kurejesha Wizara hii. Hii Wizara ni nyeti na inahitajika sana kwa sababu inagusa maeneo yote. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nianze tu na masikitiko kwamba bajeti iliyosomwa hapa ya kiwango hicho cha shilingi bilioni 43.4 kwa Wizara kubwa kama hii na mpya ninaiona kama ni ndogo, lakini basi kwa vile tumeshapita katika mchakato wote na inaonekana, nimpongeze sana Dkt. Dorothy Gwajima kwa wasilisho lake na inaelekea inakwenda kufanya kazi. Lakini nimpongeze pia Naibu Waziri pamoja na timu yao ya Katibu Mkuu na wote ambao anafanya nao kazi. Leo nitazungumzia zaidi kwenye eneo moja tu la maendeleo ya jamii kwa sababu, nikianza kutangatanga huko nitapotea njiani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, waajiriwa hawa wa maendeleo ya jamii katika lugha nyepesi ningeweza nikawaita *social engineers*. Kuna ma-*engineer*wa ujenzi (*civil engineers*), kuna *technical engineers*, kuna *electrical engineers* na kadhalika, lakini hawa ni *social engineers* kwa sababu bila hao hakuna linalofanyika chini kwenye jamii. Lakini nimesikitika tu kwamba katika kwenda sasa kuchukua mafunzo wanakwenda wakipungua na katika wasilisho la Mheshimiwa Waziri amesema wako wachache na hata hawatoshlezi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niombe sasa Serikali itoe kibali maalum kwa wale ambao wamehitimu na wako mitaani wote waajiriwe na sio lazima waajiriwe Serikalini, hawa wanatakiwa wawe katika kila taasisi lazima kuwe na Afisa Maendeleo ya Jamii. Kwa nini nasema hivyo, kwenye maji kama ni kwenye Taasisi za Maji lazima wawepo, waweze kuwafundisha watu utumiaji mzuri wa maji na jinsi ya kutunza maji na pia kutunza vifaa vya maji. Lakini ukienda benki lazima wawepo wawafundishe watu jinsi ya kutunza fedha waende, kuna benki mpaka sasa hivi zina shilingi bilioni tisa za *dividend* zimekaa tu hakuna wachukuaji kwa sababu hawajaelimishwa kule chini. Wangukuwa na Afisa Maendeleo ya Jamii na hapa nazungumzia CRDB, wangeshatoa elimu watu wao wakaenda kutoa elimu watu wakaja kuchukua *dividend* zao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini pia hata kwenye elimu na kwingineko tatizo ninaloliona/changamoto kubwa, hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Mkoa hawana Idara yao, wao wako wame-*hang* mahali. Sasa hili ni tatizo kubwa mno wao wako chini ya mtakwimu na wanapokuja sasa kwenye *level* ya kutoa maamuzi wao wanapelekewa na hao, watanisahihisha watakapokuja kutoa, lakini nina uhakika nalo kwa sababu hata mimi katika kusoma kwangu mambo mengi nilichukua pia Diploma ya *Community Development*, najua jinsi gani *cadre* hiyo inanyanyasika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini naomba basi twende mbele zaidi tunapokuja kwenye halmashauri kazi zao ni nyingi mno Maafisa Maendeleo ya Jamii. Tukizungumza marejesho ya ile asilimia kumi inayotolewa na Serikali 4-4-2 tunasema kila siku ni *revolving funds*, lakini hazirudi lakini wako mbali, utoke mjini au utoke makao makuu mpaka ukafike kijijini kule.

Kwa hiyo, siku hizi pia kuna hizi simu wanaingia kwenye simu wanauliza marejesho hawawezi kwenda, labda waombe gari kwa RAS na kama kuna mitihani waombe gari kwa Afisa Elimu, waombe gari kwenye Idara ya Afya, waombe gari ni lini sasa tutawapatia magari. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nikiangalia hii bajeti ya leo ya shilingi bilioni 42 nimechukua Randama mezani, sijaona kwenye maendeleo kama kuna fedha za kununua magari naomba sana hili jambo lifikiwiwe. Lakini nimechukua mimi Ilani ya CCM imezungumzia vizuri sana kwenye ule ukurasa wa 279 na hii nataka niseme wazi ni Wizara ya Muungano, ni Wizara kubwa sana, ndani ya TAMISEMI ukiuliza Wizara zote mtasema Elimu, mtasema sijui nini, lakini hii ni kubwa mno.

Mheshimiwa Spika, nawaomba sana yaani naiomba Serikali yangu sikivu iangalie sasa baada ya kutupa Wizara kamili iangalie inakwenda kuiwezesha vipi, lakini pia nataka niombe hata hao wafadhili waiangalie kwa jicho la pekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inapokuja kwenye *NGOs* nipongeze *NGOs* zote Tanzania, zimejitahidi sana kutoa elimu kwenye eneo hili, zimejitahidi sana kuelimisha makundi mbalimbali, lakini inapokuja sasa Ofisa Maendeleo ya Jamii anakwenda kukagua *NGO* na *NGO* hiyo haiko karibu, yule mwenye *NGO* atamuwezesha. Sasa unapowezeshwa na mtu yule ukaenda kukagua wewe unakwenda kufanyaje sasa kusema hii ni hapana. Hapo hakuna rushwa ila kuna huruma, wewe umeniwezesha nimetoka mjini, labda nimetoka Dodoma ninakwenda kukagua kule mbali kabisa yaani sijui ni Kata gani ya mbali kabisa huku Dodoma. Halafu nafika naona mambo hayapo hivi nakujaje mimi kumpa alama za chini! Sio kitu kirahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mimi ninaombi maalum chenji ya zile fedha za *Covid-19* kama kwenye maeneo mengine, ikiweko ile ya Maliasili wataona kwamba wanahitaji Ofisa Maendeleo ya Jamii naomba wapatiwe. Kwa nini nikasema ile chenji zile fedha zilishagawiwa kwa maeneo muhimu, lakini kuna hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii wangetakiwa sasa watumike, kwa sababu mnavyotuletea viosa mikono mabomba na nini bila Maafisa Maendeleo ya Jamii kupita na kuingia kwenye kaya, kuingia kwenye makanisa, kuingia kwenye misikiti kuelimisha watu nani anakwenda kutoa hiyo elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naongea kwa uchungu nikisema kwamba hata ukija kwenye *political issues, economic issues* mimi kila siku nasimama hapa naomba vifaranga vya kuku, naomba mitamba ya ng'ombe lakini Maafisa Maendeleo ya Jamii wao ndio watakwenda kule kuwaambia mkifuga...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Kengele ya pili hiyo Mheshimiwa.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naunga hoja mkono asilimia 100 na ninawaomba wenzangu wote tuunge hoja mkono na tuzidi kwenda nao ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge niwaombe wakati mnachangia muwe mnatazama hapa mbele nikiwasha kisemeo, ndio maana huwa inabidi uzungumze na kiti na usimuangalie Waziri wala Naibu Waziri. Ukishaona nimewasha malizia sentensi uunge mkono hoja kama unaunga kama huungi basi unawasilisha.

Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Daud Hassan, Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq ajiandae.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi asubuhi ya leo na mimi kuwa miongoni mwa wachangiaji kwenye bajeti ya Wizara hii mpya ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

Awali ya yote nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan na kumpongeza kwa maono yake ya kuirejesha Wizara hii, kama walivyosema waliotangulia na umuhimu wa Wizara hii tumeuona namna ambavyo Mheshimiwa Waziri nikupongeze

Dkt. Gwajima na Naibu Waziri wako na watendaji wote kwa kazi nzuri na mchakamchaka mliouanza mara baada ya kuundwa kwa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze kwenye mpango kazi wa Taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto ambao unatarajia kukamilika Juni, 2022 na kwa mujibu wa maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake wanatarajia kufanya tathmini ya kina ya mafanikio ya mpango huu. Pamoja na kwamba inaonesha mpango huu umepunguza matukio ya ukatili kwa wanawake na Watoto, lakini ninadhani kuna haja kama Taifa kujipanga kuangalia namna gani ya kushirikiana pamoja na Wizara na Serikali kupunguza matukio ya ukatili. Ukiangalia takwimu zinatisha kwa Januari, 2019 mpaka sasa matukio ya ukatili jumla yake yalikuwa kama 29,000, lakini miongoni mwao matukio ya kubakwa kama 19,000 ni kama asilimia 70 na katika hayo yaliyofikishwa mahakamani ni kama asilimia 75. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo unaona yapo baadhi ya matukio pia hayafikishwi mahakamani, lakini yaliyohukumwa ni kama asilimia 67. Kwa hiyo naunga mkono kama alivyosema mmoja wa wachangiaji kwamba tatizo hili ni kubwa na katika moja ya changamoto hasa matukio ya kulawiti watoto wa kiume zaidi ya 3,000 kati ya 3,260 asilimia 94. Pamoja na maendeleo yanayofanyika Serikali inafanya vizuri kwenye sekta mbalimbali, lakini sekta hizo maendeleo haya yanaweza yakawa hayana maana, kama tunaandaa kizazi cha watoto wengi wanabakwa kama tunaandaa kizazi cha watoto wa kiume wengi wanalawitiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba sana Serikali nilikuona Mheshimiwa Waziri Gwajima unavyoshirikiana na Wizara zingine mfano Mambo ya Ndani, mfano Wizara ya Katiba na Sheria kama pana mapungufu mbalimbali ya kisheria, kwa sababu adhabu ya miaka 30 ipo, kifungo cha maisha ipo, lakini haipiti wiki haujasikia tukio la kubakwa, kulawitiwa na vipigo na kinachosikitisha zaidi matukio haya sasa yameambukiza ndani ya familia. Unamkuta baba anabaka watoto, wake baba analawiti watoto wake,

mjomba, kaka nadhani tumuombe Mwenyezi Mungu atuwezeshe na viongozi wa dini muendeleo kukemea haya matukio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na hayo jamii/wazazi hasa wanawake tumrudie Mwenyezi Mungu tutafakari namna ya malezi ya vijana wetu. Nalisemea hili kwa uzito kwa sababu na kwa hisia kubwa tunaanza kuwa na hofu unapokuwa na watoto wa kike, wa kiume humuamini hata jirani, humuamini mume wako, humuamini ndugu yako, tunakwenda wapi? *(Makofi)*

Kwa hiyo, naiomba Serikali hata pale tutakapokuwa na tafakuri au tulete adhabu zaidi, tunaanza kufikiria au hawa wanaume tufanyeje au wahasiwe? Nadhani tunahitaji kuangalia haiwezekani kwa hiyo nadhani tunaomba Watanzania, hebu tuangalie hebu tutathmini kwa nini kila siku matukio yanajitokeza? Tuiombe mahakama iende mbele kutenda haki. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili nilikuwa naangalia hotuba pia ya Wizara hii pamoja na mambo mbalimbali, lakini kama alivyosema Mheshimiwa Mama Shally upo upungufu mkubwa wa watumishi. Naiomba Serikali tunaona juhudi za Mheshimiwa Rais hata jana zimetangazwa ajira zaidi ya 1,000 na amekuwa mama ambaye anatoa ajira amevunja rekodi, lakini tunamuomba kwa dhamira yake namna gani anavyoguswa na matukio ya ukatili wa kijinsia aitazame Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii kuweza kuipa kibali mahususi. Kwa ajili ya Maafisa Maendeleo ya Jamii ambako kuna upungufu wa zaidi ya asilimia 43, lakini kwa Maafisa Ustawi wa Jamii ambako kuna upungufu wa asilimia zaidi ya 90. Hawa Maafisa ndio watakaosaidia kuelimisha jamii namna gani katika sekta mbalimbali, lakini kuongoza mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na hilo naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo ameunda kamati ya kumshauri masuala ya kijinsia, lakini

sambamba na hilo kuchagua eneo mahususi la haki na uwezeshaji wa wanawake. Tumeona kwenye masuala ya haki hivi karibuni mtandao wa haki umempa Tuzo naona ambavyo alivyoanza. Lakini kwenye masuala ya uwezeshaji wanawake tunamshukuru sana kwa kuendelea kusimamia halmashauri zetu kutoa mikopo ya asilimia 10 lakini kuelekeza kwenye miradi ya kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasimama hapa kuushukuru uongozi wa Mkoa wa Pwani Mkuu wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wote mkoa wetu umetoa zaidi ya shilingi bilioni tisa, lakini kwa mwaka huu wa fedha zaidi ya shilingi bilioni tatu Mheshimiwa Gwajima ulikuja katika Mkoa wetu umeona namna gani pia tumejipanga kwenye majukwaa ya uwezeshaji. Tunayo majukwaa 1,700 tumeshayasajili, tunaelekea kuunda kiwanda tunaelekea kutoa mchango kwenye jukwaa la uwezeshaji wa wanawake kiuchumi kitaifa; na jitihada zote zimechangiwa na kiongozi wetu mahiri Katibu Tawala wa Mkoa *Engineer* Mwanaasha. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuwapa nafasi wanawake mahiri wakiwemo Mawaziri, Naibu Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala na Wakurugenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi wawakilishi wa wanawake katika maeneo mbalimbali tunaona kazi zao, tunatembelea miradi, tunaona namna wanavyochakarika. Kwa hiyo, naomba huu mwongozo unaoandaliwa wa namna ya kuzisajili hayo majukwaa uendeleo, tuna matumaini makubwa kutokana na shughuli mbalimbali za kiuchumi na fursa anazozitafuta Mheshimiwa Rais wanawake wamejipanga vizuri kuzisubiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kama kuna wakati wamepata ari zaidi ni wakati huu ambapo pia Mheshimiwa Rais mwenyewe Mama Samia anaongoza kwa mfano, na ndio maana amekuwa miongoni mwa watu 100 wenye ushawishi hapa duniani na tumeona kazi yake ambayo imepitia katika ushawishi wake kukubalika katika siasa za

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Kimataifa, siasa za ndani ya nchi, maridhiano na kazi inayoendelea.

Kwa hiyo, nimalizie kwa kuwashukuru sana Wizara hii tunakuomba Mheshimiwa Gwajima tumekuona unapambana na *panya road*, Wizara yako ni mtambuka tunakuombea upate watumishi wengi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Naibu Waziri na Katibu Mkuu lakini pia suala la wamachinga mnavyolisimamia na ujenzi wa masoko mahususi haya. Tunaipongeza Mkoa wa Dodoma na mikoa yote mingine Mwanza, Mbeya, Dar es Salaam namna ambavyo wanawapanga wamachinga, na tunawaomba wamachinga hususani wamachinga wa kike muwe na imani na Serikali hii inajipanga ili muweze kukaa maeneo mazuri.... *(Makofi)*

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Kengele imeshagongwa Mheshimiwa Subira, ahsante sana.

MHE. SUBIRA K. MGALU: ... kutoa mchango wenu.

Mheshimiwa Spika, naomba kushukuru naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana.

Mheshimiwa Amina Daudi Hassan, atafuatiwa na Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mheshimiwa Shukrani Elisha Manya ajiandae.

MHE. AMINA DAUD HASSAN: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie katika hoja ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kuweza kusimama katika Bunge lako hili tukufu ikiwa ni mara yangu ya kwanza nikiwa na afya njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika Taifa letu. Vilevile nimpongeze Waziri na Naibu wake pamoja na watendaji wake kwa kazi nzuri wanayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mimi nichangie kuhusu ukatili wa watoto mitandaoni; tumeona mara nyingi *video* za utupu zikisambazwa katika mitandao ya kijamii na matukio mbalimbali ya *video* na ngono za watoto na wanawake zikisambazwa katika mitandao ya kijamii kwa makusudi kabisa. Udhalilishaji huu unaleta madhara ya kisaikolojia na kusababisha hata kifo au kupoteza mwelekeo wa maisha katika jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukatili huu wa wanawake na watoto unaonekana kuathiri makuzi na mila za desturi zetu za jamii ya Kitanzania. Udhalilishaji huu umeonekana ni fimbo ya kuwapigia wanawake pindi wanapoomba ajira au nyadhifa fulani kwa makusudi au kwa wivu au kwa wivu wa mapenzi. Kwa mfano, baadhi ya wasanii, wanamuziki na maigizo wanawake hapa nchini hudhalilishwa katika mitandao yao ya kijamii wao wenyewe, haya ni matukio yasiyo ya kawaida.

Ninaiomba Serikali iangalie vizuri na iweke sheria kali kwa wale ambao wanahusiana na kadhia hii. Ntoa wito kwa Serikali na asasi za kiraia kuzungumzia madhara na vitendo kama hivi vya ukatili wa kijinsia na kutoa elimu hasa katika kizazi cha sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu wamachinga; naipongeze Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwamba kwa kulitambua kundi hili la wamachinga kwamba ni wafanyabiashara wadogowadogo

ambao ndio wanaoleta pato katika Taifa letu. Sambamba na hilo nampongeza sana Rais kwamba wamachinga wawekewe maeneo rafiki ili waweze kufanya biashara zao bila ya kubughudhiwa na mtu yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendeleo kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa dhamira yake na makusudi na mapenzi yake kwa Watanzania kwamba ameamua kutoa shilingi milioni 10 kwa kila Mkoa ili waweze kuwaendeleza wamachinga ambao ni wafanyabiashara wadogo wadogo kati yao na wanawake humo wamo, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya, Mheshimiwa Profesa Patrick Aloyce Ndakidemi ajiandae, lakini Mheshimiwa Toufiq kabla hujaanza kutoa mchango wako, Waheshimiwa Wabunge wapo wageni walioingia baada ya tangazo la wageni.

Kwanza ni wanafunzi 75 na walimu watano wa Chuo cha Uhasibu kutoka Mkoani Singida, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wengine kutoka *East Africa Tv* ambao ni watangazaji wa *EATV* kipindi cha Dadaz, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia watangazaji kutoka *Clouds FM* ambao ni watangazi wa kipindi cha Leo Tena, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa ataendelea Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia hoja iliyopo

mbele yetu, hoja ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

Mheshimiwa Spika, nami pia naomba niungane na wenzangu wote waliotangulia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuona umuhimu wa kuiunda upya tena Wizara hii na tumeona kabisa faida ya kuundwa Wizara hii na tunaona viongozi ambao wamekuwa wakifanya kazi katika Wizara hii jinsi wanavyofanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia niendeleo kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa sana ambayo wanaifanya, lakini pia kuandaa bajeti hii. Mimi naomba nijikite katika masuala mawili, kwenye suala la ukatili, lakini sambamba na hilo, uanzishwaji wa madawati ya jinsia katika vyuo vya elimu ya juu na elimu ya kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzagu wengi wamezungumzia, mimi pia naomba nipongeze mikakati mbalimbali ya Serikali ya kuhakikisha ukatili unatokomezwa kwa mpango mkakati yaani wa MTAKUWWA ambao dhamira ya mkakati huu ni kuhakikisha kwamba, ukatili dhidi ya wanawake na watoto unapungua kwa asilimia 50 ifikapo Juni, 2022. Nina taarifa kuwa tathmini ya mkakati huu iko kwenye *stage ya consultant* kwamba wako kwenye *inception report*, naamini kabisa ripoti hii itakapotoka itatuonesha hali halisi ya ukatili ilivyo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa nane wa taarifa hii umezungumzia kuendelea na kampeni ya kutokomeza ukatili; nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa kweli hata hivyo kama walivyozungumza wenzangu kumekuwa na ukatili wa kingono, ukatili wa vipigo, kuuawa wanawake na wenza wao au waume pia, kuchomwa moto kwa watoto, lakini pia ukeketaji, usafirishaji haramu wa watoto, ubakaji na ulawiti. Ukweli ni kuwa ukatili umekithiri kupita kiasi, na pia, kwa kuwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

vyombo vya habari vimekuwa vikitoa taarifa mbalimbali, matukio yamekuwa yakiripotiwa, utakuta kwamba baba, ndugu wa karibu, wanabaka na kulawiti.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano, hivi karibuni kuna matukio ambayo yameripotiwa, mfano Mkoa wa Kilimanjaro kuna mume amemuua mkewe mbele yam toto wake wa miaka minne. Sasa je, huyu mtoto akikua akili yake itakuwaje?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo ni tatizo, lakini pia kuna mwanaume ambaye amemuua mke wake kwa kumpiga risasi saba, hili tukio limetokea hivi karibuni. Sambamba na hili tarehe 5 Mei, 2022 kuna mfanyakazi kuke Dar es Salaam wa baa aliuawa na mpenzi wake. Tarehe 26 Machi mtoto alinyongwa, lakini sambamba na hilo kuna baba ambaye alimvunja mtoto wake shingo kwa kushindwa kusoma, sasa sijui yeye amesoma kiasi gani mpaka akamuue mtoto wake!

Mheshimiwa Spika, lakini pia unaona kwamba, tunawapa ndugu zetu, rafiki zetu kuweza kutusaidia kutulelea watoto wetu, kuna mama mkubwa naye amemuua mtoto wa mdogo wake. Kwa hiyo, haya mambo kwa kweli, yanatisha.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, ukurasa wa nne wa hotuba hii pia umezungumzia kuhusu utekelezaji wa MTAKUWWA ambao ulianza Julai, 2017 na utafikia ukomo mwaka 2022, lakini bado kesi zinaonekana zinaripotiwa, nyingine hazifikikiwi uamuzi. Kwa hiyo, taarifa pia inaendelea kusema kwamba, pamoja na matukio kupungua kutoka 42,414 mwaka 2020 hadi kufikia 29,373 mwaka 2021, lakini pamoja na takwimu hizo tunazozipata bado ukatili upo.

Kwa hiyo, matukio haya tunayapata kwa sababu ya Serikali kufanya kazi kubwa sana ya kuelimisha jamii ili kusudi iweze kutoa taarifa. Kwa hiyo, naendelea kuipongeza Serikali, lakini wito wangu ni kwamba inabidi lazima elimu iendeleo kutolewa ili kusudi jamii iweze kuachana na matatizo haya ya ukatili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilitaka kulizungumzia pia, katika shule zetu. Katika baadhi ya shule nako sio salama kwenye madarasa kwa sababu, kuna baadhi ya watoto ambao madarasa ya juu wamekuwa wakiwalawiti watoto wa madarasa ya chini, na hili jambo nalo inabidi lazima tuliangalie kwa kuona jinsi gani tunaielimisha hii jamii jamani kwa sababu hawa watoto inawezekana kuna baadhi ya tabia wanazirithi kutoka katika nyumba zao au katika familia zao. Kwa hiyo, ni budi sasa ifikie wakati jamii ibadilike.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ushauri wangu ni kwamba kwanza niseme Tanzania bila ukatili inawezekana. Kila mtu akichukua nafasi yake, kila mtu kuanzia kwenye ngazi ya familia tuhakikishe kwamba tunawalea watoto wetu vizuri ili kusudi tuweze kupambana na ukatili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ushauri wangu Sheria ya Kanuni ya Adhabu kuhusu mimba zinazotokana na kubakwa na ndugu wa damu, yaani mahirimu akiwemo baba, mjomba, kaka, baba mkubwa, iangaliwe upya ili iwaondolee sonona wale mabinti na kama itafaa ujauzito huo utolewe na wataalam.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nililokuwa napenda kupendekeza wazazi wa kiume wanaotelekeza watoto wao wawajibishwe, kwa sababu hii pia inasaidia sana kwenye suala zima la ukatili kwa sababu, baadhi ya akinamama wanashindwa kuwalea watoto wao.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine naomba nishauri, sheria iangalie jinsi ya kushughulikia madalali wanaosafirisha wasichana wa kazi, kwa sababu wasichana wa kazi nao wamekuwa wakipata madhifa sana huko wanakokwenda. Wengine wanauawa, wengine wanapewa mimba na kufanyiwa ukatili wa aina mbalibali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri mwingine, Serikali iangalie jinsi ya kutoa ulinzi na usalama kwa wanawake na watoto ambao wanatetea haki za binadamu. Kwa sababu kuna

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

wengine huwa wanapewa vitisho ili kusudi wasiweze kwenda kutekeleza majukumu yao hasa na wale ndugu wa wahanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri mwingine ni kwamba vyombo vya kupambana na rushwa vifuatilie mienendo ya kesi za ukatili wa ngono na ubakaji, kwani kesi nyingi zinapoteza ushahidi, kwamba hawa watu ambao wanafanya hivi vitendo vya ukatili mara nyingi wengine wanakuwa na uwezo wa kipesa au ndugu zao kwa hiyo, inafikia wakati kwamba, haki inakiukwa kwa hiyo, wale ambao ni waathirika wanashindwa kupata haki yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine nilikuwa nashauri Serikali ione umuhimu wa kujenga nyumba salama za wahanga wa ukatili iwapo mtu atafanyiwa ukatili asirudi nyumbani, kwani akirudi nyumbani ndugu watakwenda pale wamrubuni, ili kusudi aweze kubadilisha mawazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watoto wapewe mafunzo ya kujilinda mapema; kwamba tuwafundishe watoto wetu katika ngazi...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Naomba nimalizie. Tuwafundishe watoto wetu ili kusudi waweze kujilinda...

SPIKA: Sekunde 30 muda wako umeshaisha.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Patrick Aloyce Ndakidemi, Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo ajiandae.

MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia katika hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, na cha kwanza kabisa niweze kumpogeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi ambavyo aliona vema kuweza kuunda tena Wizara hii kwa sababu Wizara hii inashughulikia mambo mtambuka, lakini ni kweli kwamba inashughulikia ustawi wa jamii yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ustawi wa jamii yetu una uhusiano mkubwa sana na ustawi wa mama na mtoto; na mimi asubuhi ya leo ningependa kukita mchango wangu juu ya lengo la Wizara ambalo linasema kuendelea kuimarisha huduma za ustawi wa jamii na haki kwa familia na watoto, ikiwemo malezi ya kambo na kuasili, watu, walezi wa kuaminika, malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto, ulinzi na usalama kwa watoto dhidi ya vitendo vya ukatili pamoja na huduma za utengamao katika familia.

Mheshimiwa Spika, na ni kwa nini niulete mchango wangu kuhusiana na hili lengo?

Mheshimiwa Spika, mimi napenda kuamini kwamba changamoto katika jamii tunaweza tukawa tunaangalia ukatili unaokuja kutokea baadae, lakini chanzo cha mambo yote haya tungetambua kwamba yanaanza katika familia. Na kwa jinsi hiyo malezi ya mtoto, elimu ya malezi ya mtoto inapaswa kutolewa katika jamii yetu tangu wazo la kutaka kuwa na mtoto linapotungwa katika mawazo ya wenzi wanaotarajiwa; na ni kwa sababu mapungufu ya elimu hii ndio chanzo cha kupata hata watoto ambao baadae tunakuja kuwaita watoto wanaokaa katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Wizara inapotengeneza sera kwa sababu najua ni Wizara mpya, lazima ione umuhimu wa kufikisha elimu hii kwa jamii nzima ili kwamba jamii sasa iweze kujua kwamba, tunapokuwa tunatarajia kupata watoto maana yake tunaambatana na wajibu. Na jamii ifikie

mahali itambua kwamba wajibu wa malezi ya watoto ni wajibu usiohamishika na hasa watoto wanapokuwa miaka *zero* mpaka miaka 11, ni wajibu usiohamishika. Maana mara nyingi pia unakuta katika jamii yetu tunapenda kuamini kwamba mtoto atazaliwa, atapelekwa kwa ndugu yake fulani, hapana, *this is non transferable responsibility*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, na kama ni *non-transferable*, elimu hii inapaswa kuwaendea watu wote wanaotarajia kuwa na watoto hapo mbeleni, maana yake baba na mama; na wajibu huu, mimi ningependekeza hata mimba inapokuwa imetungwa na kama binti anapaswa kwenda kliniki basi na yule baba naye aende kliniki akapate elimu hii asisingizie kwamba, ni majukumu, hapana. Kama anafanya kazi mahali pa kazi, waajiri watoe ruhusa baba waende kliniki wakapate elimu ya malezi ya watoto. Na kwa sababu gani nasema hivi? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine kama Taifa tumeongelea hali ya udumavu. Hali ya udumavu inatokana na kutokuwa na lishe bora wakati wa mimba. Sasa unakuja baadae kuhangaika, elimu ya msingi, elimu ya awali, sijui *tuition*, *tuition* itafanya nini kama mtoto alidumaa wakati wa mimba? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, habari ya lishe bora lazima iwe ni elimu ambayo itapelekwa kwa watu wote wahusika. Na mimi kwa kuongelea habari ya *non transferable* kama jukumu la malezi, hata inapofikia kuongea habari ya elimu tunayoitoa, hivi kuna sababu ya mtoto wa miaka sita kwenda *boarding*? Akalelewe na nani? Na *matron* na hao.

Mheshimiwa Spika, sasa tunakuta kwamba tunshindwa kujenga *bond* kati ya baba na mama mhusika anakwenda kujenga *bond* na *matron*, anakwenda kujenga *bond* na mtu ambaye hamfahamu. Kwa hiyo, unakuta hata mtoto anapokua hana *bond* na wazazi wake, lakini tuko hapa kwenye mitaala yetu ya elimu tunapendekeza shule za *boarding* za watoto wadogo, si sawa, si sawa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunapokuwa tunajadili msingi wa ustawi wa jamii mimi napendekeza ndani ya Bunge lako tukufu, nimesema sentensi ambayo nitairudia tena; wajibu wa malezi yam toto mchanga kwa wazazi wake *is non transferable*, na kama ni *non transferable* maana yake si *matron* wa chekechea au wa shule ya awali ambaye ana jukumu la kulea mtoto wako. Na kwa msingi huo tujadili kama kweli ni sahihi kuwa na shule za kulea watoto katika umri ule mdogo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, elimu hii ikifikishwa napendekeza ifikishwe kwa namna zote, sasa hivi njia za kidijitali yawezekana ni za msingi sana kupeleka elimu hii. Kwa hiyo, Wizara iweke sera itakayohakikisha kwamba elimu hii inawafikia Watanzania wote ili tuweze kuwa na jamii ambayo ina ustawi.

Mheshimiwa Spika, ninaelewa muda wangu si mrefu sana niongelee jambo la mwisho katika ustawi wa jamii yetu. Ni kweli kwamba tunapenda burudani, sasa ninamfikiria mtoto mdogo aliyezaliwa yuko mahali fulani nyumbani, halafu katika jamii hiyo kuna *club* kubwa inayopiga muziki mdundo wake mpaka saa nane usiku na kuna mtoto mdogo hapa ambaye ngoma zake za masikio sidhani kama zinaweza kuhimili huo muziki. Lakini watoto wako majumbani, kuna wazee wenye *pressure* majumbani, kuna wazee ambao wanatamani utulivu lakini ngoma inadunda mpaka saa nane usiku, inasambaa kilometa tano kutoka ukumbi wa mahali ilipo, si sawa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba nikutolee tu mfano unatoka hapa Dodoma unakwenda Mbeya unakwenda kwa ajili ya kuhudumia wananchi wako, halafu usiku huo unaofika umefika saa nne usiku unatamani uwe na masaa manane ya kulala, halafu ngoma inarindima usiku mzima, kesho utakuwa tayari kwa ajili ya kazi, hapana. (Makofi)

Kwa hiyo, ili tuweze kuwa na ustawi wa jamii teknolojia ya kuzuia muziki ipo, burudani tunaipenda ni kweli, lakini ikomee masaa ambayo jamii inapohitaji ustawi wa afya ya

akili kama balozi anavyosema watu wapumzike ili tuweze kuwa kesho yake kutayarishwa kwa ajili ya kufanyakazi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo napendekeza tunapoongelea ustawi wa jamii yetu pia hebu watoa burudani watuburudishe tunapenda, lakini watuachie muda tupumzike sisi, wazee, wenye *pressure* na watoto wetu wadogo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Patrick Aloyce Ndakidemi, atafuatiwa na Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu ajiandae.

MHE. PROF. PATRICK A. NDEKIDEMI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana nami nitoe shukrani zangu za pekee kwa kunipa fursa mwanamme wa pili kuchangia katika hoja hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza sana Rais wetu kwa kuona umuhimu wa kuiondoa idara hii kutoka Wizara ya Afya na kuifanya idara kamili na niendeleo kwa kumpongeza sana Waziri wetu Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima na Naibu wake Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis kwa kazi nzuri pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, mimi nitaanzia pale alipomalizia mwenzangu Profesa Manya kwamba wazee, nataka nichangie kuhusu wazee. Wazee wako kwenye kundi maalum katika hii Wizara lile kundi maalum linajumuisha wazee, vijana, machinga na watu wenye ulemavu. Sasa mimi ngoja niongelee wazee kwa sababu na mimi ni mzee na hawa wazee hawajapata mtu wa kuwasemea kwa sauti kubwa huku Bungeni kwa sababu moja kubwa muhimu kwamba labda sisi Wabunge wazee ambao tuko huku tunakimbizana kutetea hoja za kwenye Jimbo, akinamama wanatetea hoja

zao, kwa hiyo hawana mwakilishi huku lakini leo ngoja niwaongelee. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, wazee ni watu muhimu sana kwenye jamii yetu, tuki-define wazee ni mtu mwenye miaka kuanzia 60, 70 na hata kwenye vitabu vitakatifu vya Qurani na vya kikristu wanasema wazee tuwaangalie ni kundi muhimu sana. Wazee ni amana kubwa na ni utajiri katika Taifa letu, hawa wazee wameshirikiana na Mwenyezi Mungu kwenye kuhakikisha kwamba sote tuliopo hapa tumeumbwa tukawa watu na tuko huku duniani, kwa hiyo hii ni kazi nzuri ambayo wazee wetu wamefanya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na haya wazee kwenye nchi yetu ya Tanzania wamekuwa na busara kubwa sana. Rais wetu wa kwanza aliyetuletea uhuru Mwalimu Nyerere aliwashirikisha wazee, walimpa busara na kuhakikisha kwamba wanamshauri mpaka tukapata uhuru. Kwa hiyo, kile chochote tunachoringia nchi hii sasa hivi, majivuno yetu naomba tuwahusishe wazee kwamba wamefanya *contribution* kubwa sana kwenye mafaniko ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika sensa ya mwaka 2012 idadi ya wazee hapa nchini ilikuwa takribani milioni 2.5 ambapo wakinamama walikuwa milioni 1.3 na wazee wanaume walikuwa milioni 1.2. Idadi hii ni ndogo ukilinganisha kwamba Tanzania yetu ina watu karibu milioni 45 wakati wanahesabiwa mwaka 2012. Kwa hiyo, idadi ya wazee ni kama 5.6% tu; kwa nini idadi hii ni ndogo? Idadi hii ni ndogo kwa sababu zifuatazo; kwanza kabisa wazee wengi kule vijijini na mijini ambapo tumeshaona vijana wengi hawana kazi siku hizi wana umaskini mkubwa wa hali ya juu na wengi wao hawana hata pesa ya kununua chakula.

Mheshimiwa Spika, pia wazee wengi kule vijijini wanakumbwa na magonjwa ya uzee kama tezi dume kwa wanaume, kansa za matiti kwa akinamama, kansa za vizazi, magonjwa ya *pressure* na magonjwa mengine kisukari na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Waziri amesema kwamba wameshatambua wazee kama milioni 1.5 kwenye hotuba yake na wameshawapatia bima za afya, hiyo tunashukuru sana, lakini kusema ukweli hizi huduma wazee hawazipati kama ambavyo tungependa iwe na kutokana na hali hii mbaya ya kwamba wazee hawapati huduma wameishia kuuza rasilimali zao. Kwa mfano mzee anaona niuze shamba au niuze nyumba niliyokuwa nayo kwa sababu watoto wengi hawana uwezo wa kuangalia wazee, anauza shamba, anauza gari, anauza nyumba ili aokoe maisha yake asife, kwa hiyo hiyo ni changamoto.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine kubwa ni kwamba wazee wengi wameshatelekezwa kule kwenye jamii, watu wengi siku hizi hawawaangalii sana wazee na hatumlaumu mtu, labda ni kwa sababu za kiuchumi na kipato sio cha kueleweka. Pia kwenye maeneo mengine kuna mauaji ya ukatili kwa wazee wetu, mtu ameshalitumikia Taifa letu hili lakini anaishia kuuawa kikatili kabisa kwa mambo ya kishirikina na kandalika.

Mheshimiwa Spika, changamoto hizi ambazo nimezitaja hapo juu zimesababisha hawa wazee wetu wafe mapema, wanakufa mapema kabla ya wakati wao. Sisi kama Watanzania na Taifa la Kitanzania nimuombe Waziri wetu ni jukumu letu sasa kuhakikisha tunawaangalia hawa wazee wapate huduma zao ili wasife mapema kama ambavyo imezoeleka huko.

Mheshimiwa Spika, wajibu wa kuwalea wazee uko kwenye vitabu vitakatifu, Qurani inasema tuwaangalie wazee na hata Biblia zinasema tuwaangalie wazee kwa hiyo ni wajibu wetu. Mimi niipongeze sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wao wameshaanza kuwapa pensheni wazee kule. Kule wazee wanapata pensheni kidogo na mzee hahitaji kitu kikubwa ukienda kule kijijini anakuomba naomba pesa kidogo ninunue sukari. Kwa hiyo, tukianza hata na kuwapa kilo mbili za sukari hawa wazee wetu najua tutafika mahali na mambo yatakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi nyingine kama za Botswana, Swaziland, Seychelles, Mauritius, Afrika Kusini zimeshaanza kutoa pensheni kwa wazee kuwatunza wazee wao na nchi kama Kenya, Uganda na Zambia ziko kwenye mchakato wa kuhakikisha pia wanawapa wazee wao pensheni kwa nini sisi watazania tusifanye hicho kitu jamani na siyo wengi watu milioni 2.5 tushindwe kuwapa kilo moja au mbili ya sukari.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba nitoe ushauri wangu kwa Serikali. Ushauri wa kwanza kuna sera ya wazee iliwekwa tangu mwaka 2003 naiomba Serikali ishirikiane na wadau wengine ikiwepo *Help Age* ni Shirika la Kimataifa linalosaidia sana mambo ya wazee warekebishe ile sera iendeane na wakati wa sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, kitu cha pili ninaishauri Serikali mwarobaini wa hii kitu sera tumeshaitunga tutunge sheria ya wazee mtu ambaye hatatekeleza sheria basi atachukuliwa hatua. Kwa hiyo namuomba Waziri uhakikishe kwamba sheria ya wazee ipo kwa sababu tangu hii sera itoke mwaka 2003 mpaka leo bado hamna sheria ya wazee.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ushauri wangu naomba chonde chonde huku Bungeni wazee hatuna wawakilishi ikiwezekana zile nafasi wazee kwa sababu ni kundi maalum nao wapatiwe wawakilishi wao waje huku Bungeni waje waongeelee mambo ya wazee. Mimi hapa napambana na Jimbo, wale wengine wanapambana na mambo ya akinamama na kadhalika, vijana wanapambana na mambo ya vijana kwa hiyo wazee ingependeza nao wapate uwakilishi huku Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ikiwezekana naishauri Serikali kama ikiwezekana tupawe pensheni hawa wazee hela kidogo tu ya kununua sukari nao ili maisha yaende mbele; na ushauri wangu mwingine ni kuhusiana na Bima ya Afya napendekeza iwe bima itakayoweza kuwasaidia hawa wazee wapate huduma zote bure, siyo anakwenda anaambiwa hii dawa haipo kwenye bima, hapana, bima

kama tunasema wazee hawa milioni 2.5 wanapata bima basi wapate huduma zote za kiafya.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali watokomeze kabisa hii tabia ya kumaliza vizee vyetu, wazee unakuta tu labda ana *pressure* ya macho yamekuwa mekundu anaambiwa ni mchawi wanamua. Kwa hiyo naomba kabisa Serikali isimame kidedea ihakikishe tunawalinda wazee wetu. Wazee ni utajiri, wazee ni tunu ya Taifa letu naomba tuwaheshimu, tuwahudumie kama Taifa na kwa kufanya hivyo tutapata baraka kwa Mungu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Patrick Aloyce Ndakidemi, lakini Waheshimiwa Wabunge nitoe ufafanuzi kidogo hamna kundi kwenye jamii ambalo mambo yake hayasemwi hapa Bungeni, yameshaulizwa maswali kadhaa na Wabunge kadhaa na mfano mmoja ni Mbunge huyo hapo nyuma yako hapo. Hilo suala la Bima kwa wazee alishaliuliza humu ndani Mheshimiwa Bahati Ndingo na Waheshimiwa Wabunge wengi ningekuwa na takwimu hapa kama ningejua huo mchango, lakini mchango wako ni wa muhimu sana, ila sasa haimaanishi kundi la wazee halina wasemaji humu ndani wapo wengi tu wanaolitetea hilo kundi na pia Waheshimiwa Wabunge natambua kwenye maeneo yenu kwa sababu kama idadi hii ndiyo ya wazee nchi nzima, naamini kila mmoja wetu kwenye majimbo yetu tukichukua hatua kuhusu hawa wazee tutaweza kufika hatua ambayo hakuna mzee atakayekuwa anakufa kwa kukosa huduma zile za msingi kabisa kama za kilo mbili, kwa sababu kama wapo milioni tano na sisi Wabunge humu tuko wangapi tukigawana kila mtu kwenye eneo lake akajaribu kuwasaidia wale wazee ambao hawajiwezi, bila shaka tunaweza kulipeleka Taifa letu mahali. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kila Mbunge aanzie kwenye sehemu yake kutoa zile huduma za kawaida kabisa ambazo anauwezo wa kuwasaidia wazee hao ili kutambua mchango wao, lakini

upande wa Serikali Mheshimiwa Mbunge ameshatoa ushauri kwao, lakini sisi Wabunge lazima tuchukue hatua pia katika maeneo yetu ya kuwahudumia wazee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, atafatiwa na Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu, Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko ajiandae.

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye Bunge lako tukufu kuchangia kwenye Wizara hii nyeti, Wizara muhimu sana ya akinamama. Awali ya yote ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais mama Samia Suluhu Hassan kwa kuunda hii Wizara muhimu sana kwa ajili ya wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanawake wa Tanzania nzima wanatambua sana na wanalijua hili, wanapokuwa wajawazito wanajua Serikali ipo, watajifungua salama na bila gharama yoyote. Kwa bahati mbaya sana kumezuka tatizo ambapo wanawake wanajifungua siyo wote, wanawake wengine watapata bahati mbaya ya kujifungua watoto wakiwa na mgongo wazi, wanawake wale wanakuwa hawajajiandaa chochote kuhusu masuala ya fedha kwamba watatokewa na hilo tatizo.

Lakini tatizo hilo mtoto akizaliwa ana mgongo wazi anapelekwa hospitali, anafanyiwa *operation* kwa gharama ya shilingi 500,000 mpaka shilingi 1,000,000 wanawake wale uwezo huo wanakuwa hawana. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri alichukue hili kwa umakini sana, hili tatizo ni la Tanzania nzima hasa wanawake wa Mkoa wa Mbeya wamepata matatizo makubwa sana juu ya kujifungua watoto wenye mgongo wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitafurahi sana na nitashukuru endapo Mheshimiwa Waziri atalizingatia hili kuangalia namna gani watapunguziwa gharama ama kuimaliza kabisa gharama za matibabu hayo ya kutibu watoto hao. Ninaipongeza sana Serikali na ninaishukuru sana kwa namna

ambavyo wametoa fedha kwenye halmashauri zetu zile asilimia 10. Ile asilimia 10 ni kwa ajili ya wanawake 4%, vijana 4% na kundi la walemavu 2%.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kuishauri Serikali juu ya hili, ninaomba sana kwenye 10% ile iongezwe iwe 15%. Asilimia 15 kwa maana ipi? Asilimia 15 ili kwa wanawake maana wanawake wana majukumu mengi sana, wana mzigo mkubwa sana wa kutunza na kulea familia, ninaomba kwenye 15% hiyo 9% iende kwa wanawake, 3% iende kwa vijana, 3% iende kwenye kundi la walemavu. Ninamaanisha kwamba mwanamke hata mtoto mdogo maadamu amezaliwa ni mwanamke ni kama anaanzia majukumu yake hapo.

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Spika, ninamaanisha kwamba kundi la vijana watoto wa kike nilikuwa naomba hao waingie kwa upande wa wanawake, nina maana kwamba mabinti hao wakiingia kwenye kundi la wanawake mpaka sasa hivi hiyo fedha inaonekana kama ni ya 4% ni ya wanawake, lakini pia tunakuwa na mabinti huko ndani, kwa hivyo wasichana waingie kwenye kundi la wanawake kwenye mkopo huo ambapo 9% iwe wanawake wakijumuisha na mabinti, vijana lakini vijana ambao ni wa kiume wapate 3% ninamaanisha kwamba mama endapo atasikia mtoto wake anaumwa ambaye ni kijana, mama ndiyo anashughulikia mwanzo mwisho, siyo kwamba atam-charge kijana kwamba nipe fedha zako....

SPIKA: Mheshimiwa Suma kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Jackson Kiswaga.

T A A R I F A

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Spika, ninapenda kumpa taarifa mzungumzaji kwamba katika lile kundi kubwa la vijana, pia wapo akinamama humo na nina

wasiwasi aina ya mchango huu wakati mwingine unaweza ukatugawa namna unavyowasilishwa kwa sababu pia kundi la vijana ni kubwa, lakini ndani ya vijana pia wapo wakinamama humo. Kwa hiyo ndiyo hiyo nilipenda kumpa taarifa ahsante sana.

SPIKA: Ndiyo maana niliacha amalizie ile hoja yake kama umemsihiliza vizuri anataka hiyo asilimia iongezeke halafu hao mabinti waondolewe kwenye hiyo 4% wanayopewa pamoja na vijana wengine waingie kwenye wanawake. Kwa hiyo, ukitaja wanawake wote wawe kundi moja, ndiyo hoja yake ndiyo maana nilitaka umsihilize amalize halafu ndiyo umpe taarifa.

Kwa hiyo, hoja yako wewe ndiyo ambayo kidogo inaweza ikaleta mushkeli yeye anaenda na hoja yake ya kuongeza asilimia.

Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo.

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa ufafanuzi huo na hilo ndiyo lilikuwa lengo langu sana kwamba vijana wa kiume watakapokuwa wamebakiwa na hiyo 3% naamini itawatosheleza sana kwa sababu tutakuwa tumeondoa kundi kubwa la vijana kwa maana mabinti zetu kuingia kwenye kundi la akinamama.

Ninasema hivi kundi la wanawake liongezewe asilimia hizo kwa sababu mama anabeba majukumu mengi sana. Anabeba majukumu ya baba, anabeba majukumu ya hao vijana, anabeba majukumu ya watoto wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, mama ana huruma sana kwa watoto kwa baba kwa wamama na kwa kila mtu hivyo basi nitashukuru sana hili likichukuliwa uzito kwamba wapewe akinamama kwa maana ya 15%; ninaomba sana mumshawishi, mshauri hizo halmashauri iongezeke iwe asilimia 15 nasisitiza 9% iwe kwa wanawake, 3% kwenye kundi la vijana wetu lakini 3% kwenye kundi la walemavu nitashukuru sana hili kama litabebwa kwa uzito.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa sana hapa nchini hasa kwetu mkoa wa Mbeya, anapokuwa akiishi ama wakioana baba na mama wanaishi pamoja, wanaanza kutafuta tangu shilingi moja pamoja baba na mama, lakini mwisho wa siku ikatokea mama ametangulia mbele ya haki baba atasononeka yeye pamoja na familia, lakini maisha yataendelea atakuwa tu burudani raha mustarehe hasumbuliwi na mtu yoyote.

Mheshimiwa Spika, lakini ikatokea amefariki baba ghafla kwa maana ya mume shida inaingia kwenye familia, shinda inaingia kweli kweli, anajitokeza baba hafahamiki kwenye hiyo familia anasema mimi ndio baba mkubwa, mimi ni mdogo wake, mimi ndio natakiwa niwasimamie, kwenye kusimamia mali kuzitafuta walikuwa tu baba na mama na watoto wao wakimuomba Mungu wafanikiwe kwenye hiyo familia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini watu wanajitokeza *from nowhere*, watoto hawa hawawajui wanasema unasikia mimi ndio baba yako mkubwa, mimi ndio baba yako mdogo hawawafahamu wametokea wapi? Mbona akifariki mama hawa watu hawajitokezi kuja kumbuguzi baba kwenye hiyo familia. *(Makofi)*

Nilikuwa ninaomba sana kule kwetu Mkoa wa Mbeya wanawake wajane wanasumbuliwa sana na haya, hivyo basi nilikuwa naomba sana kushauri Serikali ijaribu kuweka kama sio kuweka moja kwa moja kwa maana ya kutokujaribu, iweke mawakili kila Halmashauri ambao watakuwa wanawasaidia wanawake wajane ambao wanapatwa na matatizo kama haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii sheria naona iliangalia upande mmoja, unajua kwenye familia yamkini mama ndio mtafutaji mkubwa, baba ni msimamizi sawa kama kiongozi mkubwa kwenye hiyo familia, lakini akifariki baba ni shida, ni shida ni shida. Hivyo basi hiyo sheria kama ilikuwa imewekwa miaka ya nyuma sana kwamba baba ndio hatakiwi kusumbuliwa endapo mke atakuwa ametangulia mbele ya haki, hiyo

sheria naomba ibadilishwe, hiyo sheria naomba ibebe uzito kote kote kwamba mama na baba wanakuwepo pale wanakuwa wanatafuta fedha pamoja, kwa ajili ya familia hivyo basi asisumbuliwe mwanamke yeyote pindi baba atakapokuwa ametangulia mbele ya haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanawake wana majonzi makubwa sana, naona taa umeiwasha.

SPIKA: Muda umeisha.

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Spika, nilikuwa nimalizie kidogo

SPIKA: Sekunde 30 malizia.

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana hivyo basi nitashukuru sana kama Serikali italichukulia hili kwa uzito mkubwa kuangalia mama anavyoteseka, mama anavyosumbuliwa na Mheshimiwa Rais ameunda hii Wizara kwa makusudi mazima kabisa ili tuendelee kuwatetea wanawake hapa ndani na katika kuwatetea hawa wanawake ninaomba mlibebe muwasaidie wanawake wanaoonewa pindi wanaume zao wanapokuwa wamekufa...

SPIKA: Haya ahsante sana.

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Spika, maana analia mara analia mara mbili analia msiba wa baba/wa mme wake analia msiba wa kupokonywa mali zake zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri kuna jambo ambalo siku hizi kama linaanza kuzoeleka hivi, kuna watu wanatoa huko mafunzo mbalimbali hasa wanawake wanatoa mafunzo wanaita wanawake huku, wanaita huku

wengine kwa mgongo wa dini, wengine mafunzo ya ujasiriamali na mambo kama hayo, mambo wanayofundishwa wanawake kule yanaleta athari kwenye hili jambo analolisema Mheshimiwa Suma Fyandomo. *(Makofi)*

Kwa sababu wanawake tunapenda sana mafunzo, kwa hiyo akiitwa huku anakwenda, akiitwa kule anakwenda. Sasa ninyi kama Wizara mpya mjaribu kuyatazama hayo pia na hao wanaotoa mafunzo wao wenyewe hawana mafunzo kwenye jambo lolote, wanajianzishia tu hoja, wanawake hivi, wanawake vile, basi wanawake wanajua ndio hivyo mwendo. Sasa tunafika mahali tunakutana na changamoto kubwa kama hizi, hilo nalo nadhani Wizara hii mlitazame sana hawa wanawake huko wanapotosha mabinti zetu, wanapotosha wanawake na baadaye changamoto zinakuja kuwa kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu atafuatiwa na Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko tutamalizia na Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza. *(Makofi)*

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU: Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi nikushukuru kwa ajili ya kunipa nafasi hii, lakini pia na mimi nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuona umuhimu wa kuanzisha Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, lakini pia nimpongeze Waziri pamoja na wenzie wote kwa kazi kubwa ambayo wameanza kuifanya kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, mimi leo naomba niongelee watoto wa kiume; tangu uumbaji Mungu alivyounda utaratibu kila kitu kina namna ya kuongezeka na katika baraka ambazo Mwenyezi Mungu alizitoa kwa viumbe alivyoviumba tukiwepo wanadamu alisema tukaongezeka, tukatiishe, tukazalishe na tukatawale, hivi ni vitu ambavyo Mwenyezi Mungu, lakini sasa tunakwenda kuongelea pale kwenye kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa wanadamu au mbegu ya wanadamu Mwenyezi Mungu ameiweka ndani

ya mtoto wa kiume, hakuna namna utabisha hilo. Na hata katika wanyama mbegu yao ya kuongezeka ipo ndani ya yule mnyama wa kiume, kwenye samaki hivyo hivyo yaani kwenye viumbe vyote ni hivyo. Sasa watu wote wenye afya nzuri ya akili wanaitunza mbegu kuliko kituo chochote, mkulima yeyote mwenye busara anaitunza mbegu yake vizuri kuliko kitu chochote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na ndio maana mimi siwezi kuwa mshabiki wa kwamba mwanaume akifanya kosa ahasiwe kwa sababu mwisho Watanzania tutakosa mbegu na tukikosa mbegu tukaenda kuagiza kutoka nje sio Watanzania; na tukiitwa mbinguni kule tutaonekana Taifa letu liliisha siku nyingi sisi ni Taifa lingine. Sasa ninachotaka kusema, namna ambavyo tunaangalia watoto wetu wa kiume nchi hii sio sawa, naomba Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii alichukue ile ni mbegu, tukianza kwenye *level* ya familia tuangalie namna tunavyowalea watoto wetu wa kiume. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mbegu unajua inaweka kwenye kihenge inatunzwa vizuri isibunguliwe, lakini leo kwenye *level* ya familia ukiangalia mtoto wa kike ameweka karibu kabisa na chumba cha baba na mama ili hata akitoka usiku washtuke wamlinde, mtoto wa kiume amewekewa chumba banda la uani huko, arudi hakurudi hakuna anayejua. Leo hii kwenye familia tunasema kwamba hawa ndio vichwa vya familia, lakini ukiangalia namna tunavyowalea sio kuja kuwa vichwa, ndio maana kunatokea mgongano sasa hivi, huwezi kutegemea kumlea mfalme halafu ukamlea kilezilezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo hii tuangalie wengi hapa tunaweza tukawa tunaangalia kwenye Azam pale sinema ya Ertugul angalia Ertugul jinsi alivyo m-*raise* Ottoman, alivyompeleka vitani, alivyomsimulia kwamba wewe ni mfalme, alivyomfundisha na kumpa mbinu, alivyomlisha, alivyompeleka shule na kumpa maarifa ya kwamba yeye ni mfalme, lakini sivyo tunavyowalea watoto wetu wa kiume. Leo hii tunaanza kuwapa sifa za ufalme kabla hajafika kwenye kuwa mfalme, mtoto wa kiume anapendelewa,

anapewa vitu hata akiumia tu wakati mwingine anahitaji faraja alie, amwambie mama mimi nimefanyiwa kitu kibaya leo watoto wetu wanalawitiwa kwenye majumba kwa sababu ameshaambiwa mtoto wa kiume halii lili, mtoto wa kiume hasemi semi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo anasindwa hata kujieleza tatizo lake, leo hii ukienda mitaani waliojaa ni watoto wa kiume, sio wa kike, wameachwa, leo hii tukienda kwenye elimu tukianza kuweka kipaumbele hapa tunaweka kipaumbele cha kujenga *hostels* tunajenga za wanawake sio za watoto wa kiume.

Mheshimiwa Spika, sisi tunaangalia *equality* hatuangalii *equity*, sasa huyu unayetegemea aje kuwa kichwa leo hii twende kwenye *style* tunavyowaozesha watoto wetu, watoto wa kike wanaitwa wanapewa *kitchen party* wanapewa mafunzo...

(*Hapa kengele illia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji*)

MHE. CONSTATINE J. KANYASU: Mheshimia Spika, Taarifa.

SPIKA: Kengele imeshagongwa muda wake umekwisha, sekunde 30 malizia.

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU: Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema lazima sasa tubadilishe *style* ya kuangaia watoto wetu wa kiume na kuwapa haki sawa kwenye elimu, kwenye matibabu kwenye mafunzo kwenye kila kitu ili tuanze kuwa na kichwa kilichoenda shule, kama tunajua ile ndio mbegu yetu lazima tuitunze kwa ubora wote bila kuangalia kwamba ...

SPIKA: Haya ahsante sana.

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU: ... hawa ni watu wa aina gani, ahsante naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Haya ahsante sana siku nyingine nitakupa nafasi ufafanue huyo anayeitwa kichwa na mwanamke sasa yeye ni nani sehemu yake kwenye mwili kaa tu Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, siku nyingine utatueleza mwanamke sehemu yake ni ipi.

Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko atafuatiwa na Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza. (*Makofi*)

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi kuchangia bajeti hii lakini awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa busara na maamuzi magumu aliyoyafanya kuiweka sekta hii kwenye Wizara kamili, ni jambo kubwa sana na ni jambo la kupongezwa.

Mheshimiwa Spika, mpaka Mheshimiwa Rais anafanya maamuzi ya kusimamisha Wizara hii kuwa Wizara kamili ameangalia mambo mengi, ameona nchi yetu inahitaji ustawi wa hali ya juu na tukiangalia kwenye mazingira yetu tunapotoka tunaona sehemu kubwa ya changamoto zinazokabili Taifa letu ni maendeleo ya Jamii, nataka niseme jambo moja kuna usemi kwamba siasa hapo ulipo; *politics is local*. Siasa ya nchi yetu *locality* yetu, changamoto zetu ni changamoto za mwanamke na mtoto wa kike, hizo ndizo changamoto kubwa ambazo tunaza Tanzania na nitasema kwa nini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, watu na wachangiaji wengi hapa wamezungumzia masuala ya ukatili wa kijinsia wamezungumzia namna ambavyo watoto wetu wananyanyasika kwenye maeneo mbalimbali, lakini nataka niseme ukweli watoto wengi wanaopata hayo manyanyaso ni watoto wa maskini, sijaona mtoto wa tajiri au pengine sio wengi ambao wanapitia kwenye hayo manyanyaso na hii ni sababu ya umasikini. Kama tunataka kutatua changamoto ya unyanyasaji wa kijinsia, ukatili wa aina yoyote, jambo la kwanza kabisa ni kuziimarisha familia zetu kiuchumi. Leo tunazungumzia suala la kusimamisha mawakili kwenye Halmashauri kwenye Idara ya Maendeleo ya Jamii ili

kumsaidia mwanamke anapolia na mirathi apate msaada wa kisheria, mtoto wake anapobakwa apate msaada wa kisheria, lakini hii ni nini ni kwa sababu familia zetu nyingi ni maskini, wenye uwezo wa kusimamisha mawakili watetezi, wanasheria kwenye mahakama zetu ni wale ambao wana uwezo wa kifedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nini niishauri Serikali; kwenye Halmashauri zetu tuna asilimia 10 tuliyotenga kwa ajili ya kukopesha vijana, kinamama na watu wenye ulemavu, lakini hile fedha haitoshi, niombe sana Serikali na niombe Wizara hii, iangalie namna nzuri ya kuweza kuweka mikopo ya akinamama na hususani akinamama kwenye Halmashauri zetu ili familia zetu ziweze kuimarisha kiuchumi, waweze kusimamia vizuri malezi kwenye familia zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, malezi na mmomonyoko wa maadili kwa namna nyingi na kwa maeneo mengi umesababishwa na akinamama na akinababa kuhemea mpaka usiku wa manane kuwaacha watoto peke yao, watoto wengi ambao unaambiwa wameenda kulelewa na familia nyingine na baba mkubwa na shangazi ni wale ambao unakuta kwenye familia baba, mama ameenda kuhemea anashinda shambani, anarudi usiku, baba anaenda kutafuta anarudi usiku, muda wa kuzungumza na watoto kwenye familia hakuna wote wanakwenda kuhemea. Sasa namna nzuri ni kuimarisha hizi familia kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano Wilaya ya Lushoto, Wilaya ya Kilindi, Wilaya ya Handeni ni Wilaya ambazo zipo pembezoni Wilaya hizi makusanyo yake hayafiki hata shilingi bilioni 1.5 kwa mwaka, mapato ya ndani ukisema hata utenge asilimia 10 haifiki hata shilingi bilioni moja kwa mwaka, lakini akinamama ni wengi, nini sasa kifanyike maana yake Serikali i-*subsidize* hiyo *ten percent*, iongozee kwenye zile Wilaya za pembeni kuwawezesha akinamama wengi zaidi kuweza kupata mikopo ya bei nafuu na hili liendane sambamba tumekuwa na wimbo wa muda mrefu wa Benki ya Wanawake Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mpaka tunavyozungumza sasa hatujaona *effectiveness* ya hiyo Benki ya Wanawake Tanzania imewakopesha akinamama vijijini huko wangapi, imewawezesha kubadiisha maisha ya akinamama wangapi, hii bado halijaleta tija ningeomba sana ningeishauri Wizara hii iangalie namna nzuri ya kutenga fungu maalum kwa ajili ya kuwakopesha akinamama hasa akinamama maskini ambao wapo Wilaya maskini ambazo zipo pembezoni ambapo mapato yao hayafanani kama Wilaya za mjini, halmashauri zao zina mapato madogo ambayo ukitenga hiyo *ten percent* haiwasaidii akinamama kuwainua kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna jambo la dawati la kijinsia na mwaka jana niliuliza swali la msingi humu ndani, kuna sababu gani lile dawati la kijinsia kukaa polisi? Familia zetu tunafahamiana akinamama na Watoto wengi wanaogopa kwenda kwenye vituo vya polisi, dawati lile lingesogezwa kwenye huduma ya maendeleo ya jamii, kwenye ustawi wa jamii, hospitali matukio mengi yangeripotiwa na tungepata namna nzuri ya kushughulikia hayo matukio na mwisho wa siku jamii yetu ingestaarabika.

Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya muda naunga mkono hoja, nashukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia machache katika hii bajeti ya Ustawi wa Maendeleo ya Wanawake Jinsia na nini na nini lina neno refu mimi sijaielewa vizuri. *(Kicheko)*

SPIKA: Haya ngoja nikusaidie, inaitwa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, nimefuatilia kwa karibu sana hotuba ya Waziri, lakini pia nimefuatilia kwa kwa karibu sana maoni ya Kamati, hotuba hiyo na maoni ya Kamati hakuna mahali wameongelea Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake yaani ile *Women Development Fund*. Waziri hakusema popote na hata kamati haikusema popote. Mfuko huu upo katika Wizara hii na unatoa mikopo katika halmashauri, je, naomba niulize mfuko huu upo au mfuko umekufa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, CAG ametuambia mwaka 2020/2021 mfuko huu ulipanga kutoa mikopo ya shilingi milioni 450 lakini Serikali haikutoa chochote katika mfuko yaani *one hundred percent* na kama Serikali haitoi fedha katika mfuko huu, huu mfuko ukoje na unaendaje? Maana yake tutaongea mikopo ndani ya Halmashauri ile ya *ten percent* lakini huu mfuko naona Wizara imekaa kimya na hata Kamati imekaa kimya. Tungependa kupata ufafanuzi kwamba je mfuko huu upo au umekufa. Mfuko huu ulipanga kutoa mikopo, lakini mfuko huu licha ya kupanga mikopo, lakini sekretarieti yake ilikuwa inapaswa kukusanya madeni ya shilingi milioni 300 lakini amekusanya shilingi milioni 20.6 ambayo ni asilimia saba tu. Kwa hiyo inaonekana hata *sekretarieti* yake haifanyi kazi vizuri, kwa hiyo, kuja haja ya Serikali kurudia kuupanga upya mfuko huu ili na wenyewe uweze kusaidia katika kutoa mikopo kama halmashauri zinavyofanya.

Mheshimiwa Spika, siwezi kuchangia bila kwenda kwa wazee, yamesemwa mengi katika wazee na tumechangia sana kuhusu mambo yao, nashukuru kila mtu anawaona wazee jinsi anavyowaona. Kitu cha kwanza ninachokiona *perception* ya Watanzania au raia na wananchi kwa ujumla juu ya wazee ni kama imefifia katika miaka fulani, lakini mimi napenda kusema Serikali imejitahidi kusaidia wazee kufanya mambo mbalimbali ikiwemo kuwapa tiba bure, lakini watu ambao wana uhakika wa kuweza kutunza wazee ili waweze kupata matunzo yao ni watoto wao pia wanapaswa kufanya hiyo kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi napendekeza Serikali hii ije na muswada, baada ya kufanya *need assessment* tunaweza

kuangalia mahitaji ya wazee, baadaye ukaja muswada ambao unawa-*task* watoto kuweza kutunza wazazi wao, na wanaweza kutunga sheria ambayo kwa wale watoto wanapata kazi sehemu ya mishahara yao inaweza ikakatwa ikapelekwa moja kwa moja kwenye akaunti za wazazi wao. Kwa hiyo mimi naona kwamba twende na hiyo muda ni mchache. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naona niongee kuhusu *TASAF*; *TASAF* ni Mfuko wa Maendeleo ya Jamii ambao upo chini ya Wizara ya Utumishi na kadhalika, lakini mfuko huu kwa sababu ni wa maendeleo ya jamii uangalie namna ya kurudishwa katika Wizara hii, kwa sababu huu mfuko unaangalia wanawake vijana yaani wale *young women* pamoja na wale wasichana wanaopevuka yaani *adolescent* ambao wanaweza kupata fedha kwa ajili ya kuendeleza mambo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini mfuko huu hautoi fedha kwa ajili ya wanawake hawa kwa sababu hata ukiwapa hakuna mtu wa kuusimamia, utasimamia vizuri kama huu Mfuko wa *TASAF* ambao unahusu haya makundi maalum, wazee, wanawake, vijana pamoja na hawa wasichana wanaopevuka wakipewa fedha kwa ajili ya miradi yao midogo wanayotengeneza, basi mtu wa kusimamia vizuri mfuko huu ni Wizara hii ambayo kwa kweli na mimi ninapenda kumshukuru Rais ambaye amerudisha Wizara hii ambayo kutokuwepo kwake kwa kweli kulichagiza mambo machafu sana kufanyika ndani ya nchi pamoja na ubakaji na mambo mengine ya udhalilishaji.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha kwanza kwa siku ya leo, niwataje wachangiaji ambao tutaanza nao mchana Mheshimiwa Jumanne Kishimba, Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, Mheshima Asya Sharif Omar, Mheshimwia Tauhida Cassian Gallos na Mheshimiwa Aysharose Mattembe

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

na wengine tutaendelea kuwataja kadri muda utakavyokuwa unakwenda.

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo hapa, niwakumbushe tena Waheshimiwa Wabunge tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge kwamba mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa 7.00 mchana Waheshimiwa Wabunge wote tuelekee ukumbi wa Msekwa na Mafunzo haya ama semina hii Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshatangulia huko, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge niwaombe tukitoka tu hapa tuelekee huko kwa ajli ya mafunzo haya.

Baada ya kusema hayo nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11:00 jioni leo.

(Saa 7.00 mchana Bunge Lilitishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 Jioni Bunge Lilitirajia)

SPIKA: Waheshimiwa tukae. Katibu.

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

(Majadiliano Yanaendelea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, wakati tukienda mapumziko mafupi nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Jumanne Kishimba, Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila atafuatiwa na Mheshimiwa Asya Sharif Omar, Mheshimiwa Tauhida Gallos ajiandae.

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi kuchangia kwenye Wizara hii ambayo ni mpya kwetu. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa

Waziri hasa kwa dawati la jinsia ambalo linasaidia sana hasa majimbo yetu ambayo yana watu wengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala sasa hivi linatutuzia sana hasa vijijini na sielewi kama suala hili ni sheria au ni utaratibu na uzuri Mheshimiwa Waziri alikuwa Waziri wa Afya kwa muda mrefu kidogo. Suala hili linaleta mgongano sana hasa kwenye jamii zetu za kienyeji, suala la kwenda na kinamama wajawazito na wanaume zao kliniki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unaposema mtu wa kijijini aende na mke wake kliniki unaleta taharuki kubwa sana kwa sababu kwa mila zetu na kwa dini zingine unaruhusiwa kuoja wanawake mpaka wanne na huwezi kuwaoa kwa wakati mmoja. Sasa kama mtoto wako wa kwanza wa mke wa kwanza ana mimba na huyu wa kiume naye mke wake ana mimba na mke wako mdogo ana mimba; je, mtakwenda wote kliniki na siku ya kliniki ni siku moja tu kwa wiki itawezekana? Lakini kwa mila zetu mimba kwetu siyo ugonjwa, ila inapokuwa limetokea tatizo ambalo ni mara chache sana na hata mimba ukiwa unamsalimia mtu mjamzito kawaida huwa tunamuuliza tu vipi mwenye mzigo ameutua au bado? Anasema bado hajatua mzigo, siyo ugonjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa pole pole inaanza kuwa kero, kule kwangu Kahama yamewekwa mabango ya watu kukodisha wanaume wa kwenda nao kliniki kwa sababu wanaume wanakataa na je, sheria hiyo ni sheria *model* gani? Wewe ni mwanasheria, anayeenda kuadhibiwa pale hospitali ni yule mwanamke, lakini atatakiwa aje na mume sasa mwenye kosa ni mwanaume aliyekataa na kwa mila za kwetu mtu anakataa anasema mbona hii kitu sisi hatutaki anayeteseka ni mwanamke, matokeo yake inasababisha mpaka vifo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu huyu mama hana uwezo wowote wa kujieleza, tuelewe watu wetu tunaowaongoza ni watu wa hali ya chini sana, tunapopewa utaratibu na wazungu lazima tuwe tunauliza wazungu jamani

hiki kitu unakipeleka kule Afrika na hasa kwetu Tanzania wataweza watu wetu wa kule kijijini kufanya hiki kitu? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, humu ndani kuna Wabunge akinamama na wengine ni wajawazito, ukimuuliza tu humu ndani kwamba hii mimba shemeji ni nani hamsalimiani mwezi. (Makofi/Kicheko)

Sasa watunga sheria hawataki kuitekeleza, tena unamuuliza tu na ninajua kama ingekuwa wanafanya hivyo Wabunge tungeona wamejirusha kwenye *WhatsApp* sijaona hata siku moja Mbunge mjamzito amejirusha kwenye *WhatsApp* akiwa kwenye *bench* la kliniki na mumewe. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri inawezekana ni sababu kubwa pia inayosababisha kuwepo kwa mlundikano wa kesi kwenye dawati la jamii, maana yake unapokodishiwa mke na jina anaenda kuandika yule mume, je, ikitokea yule mtoto akazaliwa yule mume aliyekuwa anampeleka mke akamkatalia mtoto, utafanyaje? Haitawezekana, tumuombe Mheshimiwa Waziri alitizame kwa makini sana hili suala linasumbua mno.

Mheshimiwa Spika, suala lingine tumesema kujifungua akinamama ni bure, lakini ukweli siyo bure, sasa hivi imezuka kama iliyokuwa kwenye shule imehamia hospitali, anaambiwa aje na vitenge *pair* saba, aje na beseni, aje na *gloves*, anaambiwa vitu vingi sana. Kwa hali ya sasa ya maisha ya kijijini na hali ya watu wetu ni sahihi kweli na je, watoto wa sasa hivi ndiyo wamebadilika?

Ni kitu gani kimetokea hapa katikati ambacho mtoto wa sasa hivi anahitaji vitu vingi namna hiyo na uzuri Mheshimiwa Waziri yeye ni daktari, ajaribu kutueleza kimetokea kitu gani hapa katikati maana yake akifika pale hospitali kama hana vile vitenge, aidha, atoe rushwa au aambiwe kanunue vitenge kwenye eneo lile, lakini kitenge kipya kinaweza kubeba mtoto mchanga kweli? Haiwezekani, ni lazima iwe nguo iliyotumika.

Kwa hiyo, tumuombe Mheshimiwa Waziri aliangalie sana hilo suala kwa sababu linatupa wakati mgumu sana na hasa sisi kwenye majimbo ambayo yana watu wengi sana kwa ajili ya shughuli za migodi na ukulima na ufugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpaka miaka ya 1985 wagonjwa walikuwa wananywea dawa hospitali, ilikuwa mtu hawezi kupewa vidogo ili aende akanywe nyumbani na wakati ule hospitali zilikuwa mbali mbali na barabara hazikuwepo, pikipiki hazikuwepo, teknolojia haikuwa hiyo, lakini kwa utafiti hata ukiangalia leo asilimia 70 au 60 ya dawa watu hawamalizi dozi wanakunywa, wakipona wanaziacha mle ndani, kwa nini Serikali isirudishe utaratibu wa zamani ili wagonjwa wa vijijini wakanywee dawa hospitali ili kusudi inawezekana dawa nyingi tunapoteza bure na tunakataa kuwatibu watu bure. Kwa sababu mimi ninafhamu mtu mpaka leo anaweka *alarm* kwenye simu ya kujikumbusha kunywa dawa hasa wagonjwa wale ambao ni wa kisukari au *pressure*, lakini wagonjwa wengine baada ya kuwa wamepona hasa kijijini mgonjwa anapimwa kwa kuweza kunywa uji, ukinywa uji tu ukamaliza au ukala wanakwambia twende shambani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa hiyo, madawa mengi yanashinda tu kule ndani, kwanini sasa Serikali isiruhusu watu wakanywee dawa hospitali ili mimi kama nimeandikiwa sindano tano, mimi ni mtu wa kijijini nikichomwa mbili nikaona nimepona, mimi siendi, maana yake hata ukinipa dozi nyumbani kwani wewe unakuja kunithibitishia mimi kama nazimaliza, hakuna mtu anayenifuata kama nimemaliza dawa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tungemuomba kwa kuwa sasa zahanati ni ni nyingi na barabara ni nzuri na ni kila kijiji turudishe huo utaratibu kwa sababu pia utatuondolea mgogoro wa dawa *fake* na kama dawa zitanywewa pale hospitali sidhani tena kama kutakuwa na kesi ya dawa *fake* na itakuwa vizuri zaidi kwa sababu ukweli kabisa wote tunafhamu kwamba dawa nyingi sana zinabaki majumbani hasa huu tumepita muda wa corona mtu ananunua dawa

hii akinywa vitatu, amepona *typhoid* mpaka inadawa 50 lakini mtu anakunywa nusu siku ya tatu anaachana nazo, kwa hiyo, zipo tu ndani. Kwa hiyo, inaweza ikaisaidia hata Serikali pia kupunguza baadhi ya gharama bila sababu yoyote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kumalizia tu nimuombe Mheshimiwa Waziri aliangalie hili suala kama labda tulijaribie kwenye maeneo ya ndugu zetu labda Tanga na Pwani ili wao waruhusiwe kwenda na wake zao, lakini sisi kule ni ngumu, huwezi kuwa unatoka kulima, utoke kulima na siku ya kliniki ni moja, je, nani atalinda mpunga shambani haitawezekana, maana hamuwezi kwenda wote kliniki mkapangane kweli kwenye fomu wewe na watoto wako na mkwe wako, mpangane hapo kweli na nguo zenyewe za shida aangalie tu kama mimba ina tatizo aniite mimi mwanaume ili mimi niende siku hiyo kwa *special* maana yake haiwezekani mimba zote zina matatizo. *(Makofi)*

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila atafuatiwa na Mheshimiwa Asya Sharif Omar, Mheshimiwa Tauhida Gallos ajandae.

MHE. NEEMA G. MWANDABILA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia katika Wizara muhimu hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mengi yanayoendelea katika Wizara hii ambayo kwa kweli nisiposema ninakuwa kama sijitendei haki. Nimpongeze Mheshimiwa Gwajima na timu yake wamekuwa wakiendelea

kupambana sana kwa kuwafikia wananchi hadi ngazi ya chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijachangia nilipenda nitumie *forum* hii kuwashukuru vijana wawili katika Mkoa wa Songwe; Mshomari na Sam Midadadi ambao kiupekee wamenitungia wimbo maalum nikiwa kama dada yao ambao imewapendeza wao kwa jitihada zao na bidii yao na fedha kuona wamuimbe dada Neema. Kwa hiyo ninawashukuru sana popote walipo wapokee shukrani zangu za dhati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nijielekeze katika kuchangia katika wizara hii na ningependa nianze na kipengele cha Ustawi wa Jamii; tunaona katika takwimu tulizoletewa tuna upungufu wa asilimia 97 ya Maafisa Ustawi wa Jamii katika nchi yetu na kimsingi uhitaji au umuhimu wa hawa Maafisa Ustawi wa Jamii unaonekana kutokana na ongezeko la vitendo vya ubakaji, ulawiti, mauaji na pia utelekezaji wa familia ambao umekuwa ukiendelea kwenye jamii yetu. Hivi ni viashiria vya msingi vya kuonesha kabisa kwamba watu hawapo salama afya ya akili ya vijana wengi, wazee wengi na akina baba wengi huko kwetu na wanawake wengi kwa ujumla yaani jamii kwa ujumla haipo salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilitamani sana kusema neno hili si kwa maana ya kwamba labda nina maana mbaya ila naona kwamba kitendo cha kutokuwa na Maafisa Ustawi wa Jamii inaonesha Serikali kwa namna moja au nyingine imeamua kuhalalisha vitendo hivi vya ubakaji, ulawiti na mauaji na utelekezaji wa familia kwa kutokuwa na mkakati maalumu wa kuhakikisha Maafisa Ustawi wa Jamii tunakuwa nao wengi wa kutosha. [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]

Mheshimiwa Spika, na...

SPIKA: Mheshimiwa Neema ngoja ngoja kidogo. Hiyo sehemu ya maneno uliyoyasema hapo kwanza yafute halafu uchangie upya hiyo sehemu maana siwezi hata kuyarejea.

Kwa hiyo, yaondoe hayo maneno wewe mwenyewe halafu anza kuchangia upya ili pengine ukitumia lugha nyingine tutaelewa vizuri.

MHE. NEEMA G. MWANDABILA: Mheshimiwa Spika, naomba niyaondoe maneno kama ulivyoniambia ila ninataka niseme nini? Nataka niione dhamira ya Serikali kuhakikisha inatoa ajira kwa Maafisa Ustawi wa Jamii kwa wingi zaidi ili changamoto hizi za ubakaji, ulawiti, mauaji na utelekezaji wa familia zinazoendelea katika jamii yetu viweze kupungua. Tunaamini kabisa na tunafahamu kwamba Maafisa Ustawi wa Jamii ndiyo watu wenye elimu ya kuweza kufanya *counselling* kwa watu wetu na ndiyo watu wanaoweza kusaidia kubadili mwenendo na tabia ya jamii yetu na kufuatilia kwa ukaribu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninataka kuiomba Serikali kupitia *forum* hii kwamba wahahakishe Maafisa Ustawi wa Jamii wanaajiriwa wanakuwa wengi na mimi sidhani au sielewi ni kwanini Serikali haiipi kipaumbele kada hii kwa sababu hata ukiangalia mara leo wapo Afya, mara leo wapo Maendeleo ya Jamii, sijui kesho watakuwa wapi. Kwa hiyo ninatamani kwamba kada hii ya Ustawi wa Jamii ipewe kipaumbele na ikiwezekana itengenezewe sheria maalumu ya kuilinda taaluma hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo niseme tu hata kiwango cha bajeti kinachotengwa kwa Wizara hii kinaonesha kabisa dhamira ya Serikali kupambana na vitendo hivi bado haijawa wazi sana. Ninatamani kuona kwamba katika Wizara ambayo ingekuwa inapewa kipaumbele ni pamoja na hii kwa kutengewa fedha ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kwenda kwenye eneo la maendeleo ya jamii hususani kwenye hii ya mikopo inayotolewa kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Tunaona ni pesa nyingi inatengwa na tunaona kabisa ubunifu wa miradi unaoendelea kwenye halmashauri si toshelevu, si mzuri kwa maana gani naongea maneno haya

tungekuwa na watu wa ku-*design* miradi wazuri tusingekuwa tunaona ya kwamba *projects* zinazoendelea ununuzi wa pikipiki tu, bajaji tu kila siku tunatamani kuona kwamba Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii wanakuja na mkakati wa kuajiri wataalamu wa ku-*design* miradi watakaowafundisha jamii yetu wanawake, vijana na hao watu wenye ulemavu ili kuepuka miradi ya aina moja kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunajua kabisa uelekeo wa nchi yetu ulikuwa ni viwanda na hatutajua miradi hii kupitia mifuko ya wanawake yaani kuna miradi gani ambayo mpaka sasa hivi wameweza kuifanya ambayo inaonyesha kabisa uelekeo wetu niwaviwanda. Vikundi vipewe fedha ya kutosha, lakini pia uelekeo ungeendana na hii Sera ya Viwanda ingependeza zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna kitu kingine ambacho nilitamani kukiongelea kuna kundi ambao lipo kwenye jamii, hawa mabinti wengine ambao walibakwa wengine ambao walilaghaiwa kwa namna moja au nyingine unakuta wamepata watoto, malezi ya watoto hawa mara nyingi yanakuwa yanayumbayumba. Ninatamani katika eneo hili la maendeleo ya jamii wangukuja na mkakati maalumu wa kuangalia namna ya kuwajengea uwezo hawa mabinti ili wawe na uchumi ambao ni *stable*, lakini mbali zaidi tunaamini kwamba wakijengewa uwezo hata utapiamlo kwa watoto wetu utakuwa haupo, hawa watu wote watakuwa wana uhakika wa chakula lakini na uhakika wa huduma zingine kama mavazi, malazi na matibabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho nimekiona katika eneo hili la mikopo hii mpaka sasa hivi ni muda mrefu tumekuwa tukiendelea kutoa mikopo, lakini *impact assessment* ya mikopo hii haipo na ukiangalia mpaka sasa hivi ukiwauliza ni wanawake wangapi wamejikomboza kutoka kipato kipi kwenda kipato kipi au ni vijana wangapi walikuwa na uchumi huu saa hizi wapo uchumi huu taarifa hizi hazionekani. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kupitia *forum* hii, Bunge hili tukufu nilitamani kuiomba Wizara wakafanye *assessment* tuweze kujua tulipokuwa na tunapoelekea ili hata unaposema tunatoa pesa nyingi iwe kweli ni pesa nyingi lakini zenye tija kwa wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kitu kine ambacho nilitamani kukiongelea zaidi ni katika hili suala la ulinzi wa mtoto; tumekuwa tunaona ni kwa namna mbalimbali ambazo kila mwananchi, kila mtanzania anapambana kulea mtoto wake anavyojua yeye naniwapongeze kwa *forum* ambayo wameianzisha yakuwa na vituo vya malezi ya watoto katika kila kijiji na ninasikitika tu kwamba vituo vya mfano vyote vipo Dar es Salaam na vingine vinaletwa Dodoma. Mimi nadhani kama mfano ungeanzia kwa kila angalau yaani hata kwa angalau kila kanda kukawa na kituo kimoja ingependeza zaidi kwa sababu tungekuwa tunaendelea kuinua Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi niseme tu, kwa hili nawapongeza na ninaamini kupitia Bunge hili tukufu hiki tutakiona na kukipa kipaumbele na kuhakikisha kila kijiji Tanzania inakuwa na hizi *centers* za kulelelea watoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nashukuru sana kwa nafasi ya kunipa kuweza kuongea. (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Asya Sharif Omar atafuatiwa na Mheshimiwa Tauhida Gallos, Mheshimiwa Aysharose Mattembe, ajiandae.

MHE. ASYA SHARIF OMAR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza nichukue nafasi hii nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii ya mara ya pili kusema tunakupongeza wewe binafsi kwa namna unavyoliendesha Bunge hili tukufu, tunakuombea kwa

Mwenyezi Mungu aendelee kukulinda na tunasema tupo pamoja na wewe, mwanamke anaweza na ndiyo maana ukaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo, mimi nianze kuchangia na kuchangia nianze kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu lakini na Rais wetu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa namna wanavyoendelea kutuongoza katika nchi hii katika nyanja mbalimbali za kimaendeleo, kiuchumi, kijamii na kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nianze kuchangia hoja yangu kwenye wizara hii kwenye suala zima la ukatili wa wanawake na suala la uzalilishaji wa kijinsia wakiwemo watoto.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba wanawake wengi wanakabiliwa na suala la udhalilishaji wa kijinsia ikiwemo ukatili na ukatili huu ambao wanapata wanawake wengi ikiwemo kutekelezwa na familia, na hii hutokea pale baadhi ya wanaume wanaposahau wajibu wao wakawaacha wanawake hawa na mzigo wa watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanawake hawa wengi wanapatwa na vilema kutokana na ukatili unaoendelea kwa baadhi ya maeneo katika nchi yetu. Wanawake hawa pia wananyang'anywa mali ambazo wamezichuma pamoja na mwanaume ambaye walifunga ndoa. Kufuatia hali hii mimi nina ushauri wangu kwa Wizara husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza naiomba Serikali kuwajengea uwezo wanawake hawa kielimu ya uthubutu ili wanawake hawa sasa waweze kuvunja ukimya. Wanawake wengi wamekuwa kimya sana, wamekuwa wanaogopa. Sasa kuogopa kwao hii inapelekea wanapata maumivu makali ya kunyanyaswa bila ya sababu ya msingi. *(Makofi)*

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, niombe Serikali kupitia Wizara hii kuwachukulia hatua wale wote ambao wanahusika na udhalilishaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto. Ni dhahiri kwamba wanawake wanateseka kwa kulea watoto peke yao, lakini inapelekea kuwa na ongezeko kubwa la watoto mtaani kwa sababu watoto hao wanakosa matunzo ya baba na mama na wanasahau kwamba mwanamke yule hakuweza kuzaa peke yake, alizaa kwa ushirikiano na baba. Lakini leo cha kushangaza sijui inakuwaje mwanamke huyu anatekelezwa na watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe sana Serikali impe nguvu mwanamke anapofika kwenye vyombo vya maamuzi ili kuweza kupata haki ya kuwatunza Watoto, lakini pia kuendelea kufurahia maisha yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema kwamba wakati umefika wa wale wote wanaozalilisha watoto na kuwatumikisha wakiwa na umri mdogo kufunguliwa kesi maalum. Kuna wimbi kubwa la baadhi ya watu kuwaaajiri Watoto au niseme ajira za watoto. Hili wimbi ni kubwa sana, hata hapa Dodoma tumejionea baadhi ya maeneo kuna watu wanawaaajiri, tukiwauliza anakwambia mama ndiyo amenipeleka kule mimi nifanye kazi za majumbani. Kiubinadamu haielekei, mtoto ana miaka 12/13/14 mtoto wa mwenzio unakwenda kumtuma, hasomi. Hivi kweli kama ni wa kwake angefanya hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Wizara husika jambo hili msilifumbie macho, mlichukulie hatua kwa sababu ni jambo lipo na linaathiri nguvu kazi. Lakini naendelea kusema watoto wana haki ya kuishi, watoto wana haki ya kusoma, watoto wana haki ya kusikilizwa, watoto wana haki ya kucheza. Lakini yote haya leo hawayapati, baadhi yao hawayapati; na hawayapati kwa sababu watu wamekosa imani, lakini watu wanajaribu.

Naamini Serikali yetu sisi iko imara na uwezo uko wa kuweza kushughulikia watu wa aina hii ili wasiweze kutuharibia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo kabla sijaunga mkono hoja. Nasema kwamba, naomba nimnukuu Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu kwa kauli yake ambayo ameisema hivi karibuni kwamba; "sasa umefika wakati tupaze sauti zetu kila mtu kwa nafasi yake, alipo popote kuhakikisha kwamba tunapinga vitendo hivi vya ukatili wa kijinsia...." (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Malizia Mheshimiwa sekunde 30.

MHE. ASYA SHARIF OMAR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nakushukuru, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Haya ahsante sana. Mheshimiwa Tauhida Gallos Nyimbo atafuatiwa na Mheshimiwa Aysharose Mattembe. Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa ajiandae.

MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia Wizara ya Wanawake, Jinsia, Wazee na Watoto. Kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu. Mheshimiwa Rais wetu amechukua kwa namna ya kipekee ndani ya Taifa letu kuangalia kwa namna na jicho la kipekee wanawake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia niwapongeze walioteuliwa kupewa nafasi hii, muda bado tunao, tutawapa pongezi za ufanyaji kazi nafikiri baada ya miaka miwili au mitatu, kwa sasa tuwapongeze kwa kuteuliwa. Lakini pia tukiwa kama wenzenu tuna imani kubwa kwamba mtafanya kazi vizuri na tunaamini kwamba tutafika pale ambapo Mheshimiwa Rais anatarajia tufike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la ubakaji; leo takribani Wabunge wako wote waliosimama hususan wanawake wamezungumzia suala la ubakaji. Ndani ya Taifa

letu suala la ubakaji limekuwa suala la simanzi na kilio hususan kwa akinamama. Tunafika wakati wanawake tunaulizana maswali, hivi kinababa hawatusikii, hawaoni, hawajui au kwao wanaona ni jambo la kawaida? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulitegemea kuona Wabunge wanaume wakiungana nasi katika suala zima la kulizungumzia suala la ubakaji, na nilitegemea hili kwa sababu suala zima la ubakaji watoto wanaobakwa wamo ndani ya majimbo yao. Hili kwao limekuwa la Viti Maalum na wakati suala la ubakaji ni kwa Taifa zima na wanaobakwa ni watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tanzania Bara kuna mwenzangu mmoja alizungumza akasema takribani sasa imekuwa tukio kila wiki la suala la ubakaji. Kwetu sisi Zanzibar si mambo hayo, imekuwa takribani kila siku kuna suala la ubakaji. Tumeamua sasa Wabunge tupaze sauti zetu, tunaamini, tuishauri Serikali yetu kwa namna ya kipekee Mheshimiwa Waziri liangalieni. Wakati unamuomba Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Mwinyi atengeneze pacha wako hakusita, haikuzidi siku mbili au siku tatu kwa upande wa Zanzibar naye Mheshimiwa Rais alitupatia Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mategemeo yetu hasa sisi tunaotoka Zanzibar utafanya kazi na Waziri wa Zanzibar kuangalia changamoto iliyoikabili Tanzania yetu hususan kwenye suala la ubakaji na unyanyasaji. Wanawake wamekuwa na matatizo makubwa kila unapopita ndani ya nchi hii. Kila unapokwenda suala ni moja tu, sisi tukiwa kama viongozi tunaowakilisha mikoa yetu, huna unapokwenda kukanyaga ukafanya mkutano usikute wanawake wanalia wanasema ubakaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna ajenda tunayoweza kwenda kuizungumza nje. Unapokwenda kuzungumza suala ni moja tu Mheshimiwa Waziri ni ubakaji, tushirikiane tuone tunatatua vipi tatizo hili. Kuna mambo mengine mazuri, tunaweza tukawa nayo huku kwa upande wa Tanzania Bara

tukayapeleka Zanzibar yakafanyiwa kazi kutatua tatizo, lakini kuna upande wa Zanzibar yakaletwa huku. Zanzibar kuna eneo la Pemba, kuna eneo la Mkoani kuna eneo kwa ajili ya suala hili wameweka mkakati kunaitwa mkono kwa mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkono kwa mkono kwamba lile tatizo linatatuliwa askari polisi yuko hapo hapo, yuko daktari, akitoka kwa daktari mtoto anaingia kwa askari na tatizo linatatuliwa. Takribani tatizo hili kusuasua kwake hasa ni kwenye kupoteza ushahidi. Mtoto anavyofanyiwa tukio lile, anapochukuliwa kwenda kupelekwa kituoni, akirudishwa kwa daktari ushahidi umepotea. Hayo Mheshimiwa Waziri mnaweza kuyachukua na kuona tunawezaje kuendelea kuboresha kuona kazi tunaweza kuzifanya vipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini suala la unyanyasaji; takribani kila mwanamke leo aliyesimama Mbunge kazungumzia suala la mirathi, suala la haki ya mwanamke anayoipata. Ingawa suala hili pia lipo katika kisheria na kwa upande wa dini pia. Lakini Mheshimiwa Waziri angalia maeneo mahususi, mama amewapa nafasi amejua mtamshika mkono, mtampa nguvu. Tuangalie kama wanawake masuala haya tunayatatua vipi. Pamoja na ugumu uliokuwemo ndani ya mila zetu, ndani ya dini zetu, ndani ya tamaduni zetu lakini bado tuna fursa ya kuwasaidia wanawake wa Tanzania ili haya mambo yaende kwa utaratibu, yaende kwa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri kuna mfuko wa asilimia 10; mfuko wa asilimia 10 ni kwa wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum. Mheshimiwa Waziri fedha zipo, sisi tumo kwenye Kamati ya LAAC fedha tunazona. Kuna halmashauri ziko Tanzania hii hii zimekusanya mamilioni ya pesa, vijana waliokuwepo maeneo yao hawajui kama kuna huo mfuko. Mheshimiwa Waziri tunaishauri Wizara yako ijikite kwenye kuwaelimisha wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inawezekana vijana wengi na wanawake wanakosa fursa kwa sababu hawazielewi hizo fedha. Waliokuwepo ndani ya halmashauri zetu wamezikalia hawazitungumzi, hawatoi elimu, hawatoki kwenda kuwaambia watu kwamba fedha zipo, Serikari ina pesa inaweza kuwakopesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwanamke mwenzetu, Mheshimiwa Waziri lichukue, unapokwenda kwenye mikutano yazungumzeni, halmashauri ina fedha kwa ajili ya wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum. Fanya tathmini ukutane na Waziri wa TAMISEMI, angalia kila halmashauri ina shilingi ngapi? Kuna fedha zimelimbikizana miaka mitatu, minne, mitano hazijaenda kwa walengwa. Tatizo ni mipango iliyokuwepo ndani ya halmashauri yetu ni mipango mibovu ndio maana zinashindwa kufanyiwa kazi ipasavyo. Mheshimiwa Waziri kwa kuwa tunaamini uwezo wako wa kufanya kazi hatuna mashaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine kuna nyumba za kulelea wazee. Si jambo baya, muda huu tunamuda mkubwa wa kukushauri, muda huu tuliokuwa nao wa kukushauri ili tuweze kuona Wizara yetu inafanya kazi vizuri. Kuna nyumba za kulelea wazee, kuna mtu hapa alitutolea mfano kusema kwamba Zanzibar zipo, kweli Zanzibar ipo, na mara nyingi nilikaa nikajaribu kuangalia kwa upande wa Tanzania...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS: Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Aysharose Mattembe atafuatiwa na Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa. Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji ajiandae.

MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii

muhimu kwa ajili ya maendeleo ya wanawake. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anazozifanya na kuona umuhimu wa kuwa na Wizara hii ya wanawake na makundi maalum ambayo uwepo wake imesaidia sana kutatua kero na changamoto za wanawake ambao ndiyo walezi wa familia na jamii kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, dada yangu Dorothy Gwajima, Naibu wake Mwanaidi Ali, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote kwa kazi nzuri wanayoifanya kuhakikisha wanatatua changamoto za makundi maalum, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo napenda kulichangia ni Maafisa Maendeleo Jamii na uwezeshwaji wa wanawake kiuchumi; Maafisa Maendeleo Jamii ni watu muhimu sana katika jamii na napenda niseme kwamba ni *changes agency* ambao wanabadilisha *mindsets* katika jamii, lakini wamekuwa wakisahaulika sana, Serikali imekuwa haiwapi kipaumbele. Wamekuwa wakifanya kazi kwenye mazingira ambayo siyo rafiki, lakini pia hawana vitendea kazi na nyenzo nyingine muhimu za kuwasaidia kufanikisha majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kumekuwepo na matukio mbalimbali ya ubakaji kwa watoto wa kike lakini pia ulawiti kwa watoto wa kiume na vitendo vingine ambavyo kwa kweli havipendezi sana katika jamii yetu. Endapo viongozi hawa, Maafisa Maendeleo Jamii hawa wangeweza kuwezeshwa vizuri vitendea kazi na nyenzo nyingine muhimu kama ambavyo Maafisa Ugani wameweza kuwezeshwa pikipiki na vitendea kazi vingine wangeweza kufanya kazi kwa ufanisi na kuweza kuyafikia makundi mengi sana katika jamii, kuwapa elimu juu ya lishe bora, malezi bora lakini pia kuwapa

elimu juu ya jambo hili muhimu ambalo liko mbele yetu sensa na makazi ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niishauri Serikali iwaangalie sana Maafisa Maendeleo Jamii hawa, kama wenzangu walivyotangulia kusema ni watu ambao wanagusa karibia kila sekta, wakiwezeshwa wataweza kuyafikia makundi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika Mkoa wangu wa Singida kuna uhaba mkubwa sana wa Maafisa Maendeleo Jamii hususan katika Kata, wale Maafisa Maendeleo Jamii ambao wako Wilayani kutokana na jioografia ya Mkoa wa Singida hawawezi kufika kila sehemu. Maeneo ambayo wanaweza kufika ni maeneo machache sana. Lakini endapo kutakuwa na Maafisa Maendeleo ya Jamii katika kila kata wataweza kuielimisha jamii na vitendo hivi mfano vya ukatili wa kijinsia ukiwepo wa kubaka watoto, ulawiti wa watoto wa kiume, mmomonyoko wa maadili, wataweza kuielimisha jamii na mambo hayo yataweza kupungua sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kulichangia ni uwezeshwaji wa wanawake kiuchumi; ni ukweli usiopingika, ukimwezesha mwanamke umeiwezesha jamii. Lakini ipo mikopo ambayo inatolewa katika halmashauri, mikopo ya asilimia 10; wenzangu wametangulia kusema, mikopo hii haitoshi kabisa, lakini pia imekuwa ni mikopo ambayo haina tija. Mfano kikundi kina watu 15, wanapewa kiasi cha shilingi milioni tatu, wanaishia kugawana laki mbili, mbili. Hapo tija iko wapi? hakuna tija yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikari ni vyema sasa kuiangalia na kuitathimini mikopo hii na kuangalia njia bora zaidi za kuweza angalau kuwapa mradi. Mfano mradi wa kufuga kuku au mradi wa kulima mbogamboga au mradi hata wa kufuga nyuki pamoja na kuwapa mafunzo. Jambo hili lingekuwa linatija sana kwa wanawake ambao hawa wanawake ndiyo walezi wa jamii na walezi wa familia lakini wamekuwa wakiangalia matibabu, wamekuwa wakilipa hata ada za watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuishauri Serikali ni vizuri sasa kukawepo mkakati mahususi wa kuangalia namna bora zaidi, kwa sababu nimejaribu kuangalia hapa kwenye bajeti, lakini sijaona mahali popote ambapo kuna mkakati mahususi wa kupinga hivi vitendo vya ukatili wa kijinsia hususani ubakaji wa watoto wa kike ambao wamekuwa watoto *innocent*, hawana hatia, hawajui, wanakuwa wanaharibika kisaikolojia. Naishauri sana Serikali kuweko na mkakati wa kitaifa wa kuweza kuendesha kampeni ya kuzuia ukatili wa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja na nawapongeza sana viongozi wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya na nakupongeza wewe kwa kuliendesha Bunge letu vizuri. Nakushukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa atafuatiwa na Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji. Mheshimiwa Dkt. Paulina Nahato ajiandae.

MHE. AGNES M. MARWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuchangia Wizara hii adhimu. Kwanza nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na timu nzima, lakini nimpongeze zaidi Mheshimiwa Rais kwa kuwateua watu hawa kwa sababu naamini kabisa yeye ana maono, ameona kwamba watatuvusha katika Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwa kuangalia kwenye suala la mikopo zile asilimia 10. Kuna hili suala la asilimia 10 kuna suala la umri ambao umri wenyewe unaanzia miaka 18 mpaka 34. Hiki kipindi cha sasa kwa umri ule wa nyuma uliokuwa unaanzia miaka hiyo ilikuwa ni sahihi, lakini ukiangalia mbele zaidi vijana wa sasa mpaka miaka 45 bado ni vijana.

Mheshimiwa Spika, lakini pia miaka 18 mpaka hii miaka 34 wengi wao wanakuwa ni wale vijana ambao bado wanatabia zile zinaitwa tabia za utoto zaidi. **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Kwa hiyo, ukiangalia kuanzia hapo miaka 36 mpaka miaka 45 kundi hili ndiyo kundi ambalo lina maono kwa ajili ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi binafsi ningeishauri Serikali basi iongeze umri kutoka umri ule wa miaka 18 mpaka 34 sasa ifikie kwenye miaka 45 ili kusudi hata hii mikopo wanapopewa wapewe watu wanaojifahamu wanaojielewa, ili kusudi kuleta tija katika jamii yetu lakini katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna hili suala la bajeti kwa kweli mimi nimuombe tu Mheshimiwa Waziri na timu yake msione aibu kwenda kuomba bajeti na kurudi mara mbilimbili kuomba bajeti na mkirudi kwetu sisi Wabunge basi tutawapitishia kwa sababu Wizara hii ni muhimu sana na nimtambuka na haswa kwa jamii yetu kutokana na mambo mbalimbali. Kwa kweli bajeti hii ni kidogo sana, haiwezi kukidhi mahitaji au uwitaji wa bajeti hii au uhitaji wa eneo hili kutokana na kwamba shughuli zake ni nyingi sana na hasa ukizingatia kama hivi unavyoona hali ya sasa hivi ni mbaya mbaya sana. Lakini bado hao hao Maafisa Maendeleo ya Jamii hawana usafiri na saa nyingine pia wanaleta usumbufu sana kwetu sisi Wabunge wanatuomba wakati sisi wenyewe na sisi wenyewe ni tia maji maji, kwa hiyo wanakuja kutuomba pesa za usafiri na nini suala ambalo tunaamini kabisa Wizara ikitengewa bajeti ya kutosha basi na wo watapata usafiri na vitendea kazi vingine ili kusudi boresha mambo mbalimbali katika wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia walivyotangulia kusema Wabunge wenzangu kwenye hili suala la mikopo midogo midogo; hii mikopo nafikiri sasa imekuwa ni tatizo kubwa sana kwa sababu ukienda sehemu nyingi wengine wanashindwa kurudisha mikopo, lakini wengine wanacheleweshwa, lakini wengine pia hawaendelei, kila siku wanakuwa pale pale ni kwa nini basi? Ni kwa sababu hii mikopo wanapopewa ni midogo sana kwa mfano shilingi milioni tano unawapa watu 10 ukigawanya nafikiri ni kidogo sana. Mimi kwenye somo la hesabu nilikimbia umande nafikiri mkiangalia mkipiga hapo

hesabu mtaona kwamba ni pesa kidogo sana, kwa hiyo ni pesa ambazo hazitoshelezi kwa ajili ya mtu au mjasiriamali kujiendeleza kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine na ndiyo maana wengine sasa wanaishia kula nyumbani, lakini kwa wale wenzangu na mimi wanaishia kwenda kununua *carolight*, anaona kwamba sasa mbona hii hela ni kidogo sana mimi itabidi nikapendeze, labda nitairudisha lakini sasa inakuja kutokea anashindwa hata kuirudisha. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi niishauri Serikali hii pesa inatakiwa iongezwe, huu mkopo *at least* basi wawe wanapewa kwa awamu lakini wapewe fedha ya kutosha kwa mfano hao watu 10 wanaweza kupewa awamu ya kwanza hiyo milioni tano halafu tena wakaangaliwa awamu nyingine wakaongezewa tena milioni tano, tena wakaja wakaongezewa kidogo ili kusudi ile mikopo iwe na tija na hasa kwa Watanzania. Tunamshukuru sana mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa upendo wake anaotunyeshwa kwa Watanzania na hasa Watanzania wajasiliamali wadogo na wanawake kwa mikopo aliyoitoe ya milioni 10 kila mkoa ombi langu au ushauri wangu kwa Serikali; mikopo hii ili iwe na tija iende ikasimamiwe vizuri kwa sababu huko kwenye Wilaya zetu au mikoani kwetu huko huwa kuna ile hali ya wanasiasa kuingilia mikopo hii wanapoingilia mikopo hii wanaweza ukakuta kuna kikundi cha shangazi, mjomba, bibi, babu unakuta yuko Mheshimiwa Meya tayari kawandaa ndugu zake au kawaandaa kikundi fulani anajua hapa sasa hapa hiki kikundi huyu Agnes ani-*support*, huyu ndiyo mpiga debe wangu hawa wapiga debe na wengine hawapati lakini hiyo siyo nia ya Mama Samia Watanzania wote mnapaswa kujua Mheshimiwa Wetu Rais hajali itikadi ya mtu, itikadi ya chama, wala kuangalia huyu mtu katokea sehemu gani yeye ametoa pesa imsaidie kila Mtanzania. Kwa hiyo, wale watendaji wabovu mimi niombe tu Mheshimiwa Waziri nenda kashughulike nao, lakini sasa ufanyike ufuatiliaji wa kina, kwa sababu pesa hizi ukizifuatilia kwa undani zaidi utakuta ziko kwa hao hao viongozi ambao ni viongozi wetu wa pale manspaa na nipesa ambazo vikundi vingi vinalalamika sasa unajuliza kwamba kwa nini vikundi vingi vinalalamika...

MHE. LUCY T. MAYENGE: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Agness kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Lucy Mayenga.

T A A R I F A

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kumpa taarifa itakuwa ni vizuri sana *Hansard* iweze kukaa vizuri ni Mheshimiwa Agnes mchangiaji wetu akaweka rekodi vizuri Maafisa ya Maendeleo ya Jamii ni watu ambao tunawategemea sana kwenye halmashauri zetu, wanatufanyia kazi kubwa sana kwa hiyo ni vizuri tu labda nadhani aweke vizuri rekodi kwamba siyo kwamba wanaomba omba, labda pengine mtu akiwa na jambo anaweza akahitaji msaada wa hapa na pale; hilo moja lakini lingine Mheshimiwa Rais akutoa fedha hizo milioni 10 kwa ajili ya mikopo huko kwenye halmashauri zetu, ahsante sana ni vizuri aweke rekodi vizuri isiye ikaonekana kwamba kuna vitu ambavyo tunaviweka havijakaa sawa.

SPIKA: Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa unaipokea taarifa hiyo.

MHE. AGNES M. MARWA: Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa hiyo na hapo hapo nimesahisha kutokana na maneno yake. Lakini tu mimi niseme tu...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Sekunde 30 kengele ya pili imegonga.

MHE. AGNES M. MARWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana haya yote pia katika hii wizara maendeleo ya jamii michezo pia ni furaha kwa maana hiyo kwa furaha hii mnyama kule Mwanza tulimpiga chini na sasa tunasema furaha ipo basi katika maendeleo ya watu nashukuru sana, Yanga oye. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Agnes neno oye humu ndani nilishalitolea maelekezo. Lakini jambo lingine la kufanyiwa marekebisho kidogo hawa vijana wanaopata mikopo halmashauri na umri alioutaja Mheshimiwa Agnes amesema neno moja hivi maana huwa naletewa malalamiko hapo baadaye.

Vijana hawa wanaopewa mikopo halmashauri ni wale vijana ambao wamefanyiwa tathmini na kwamba ile mikopo wanastahili. Kwa hiyo, hakuna wale wanaopewa mikopo wakiwa na utoto fulani, hiyo tunaiondoa ya utoto.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamuita Mwantumu Dau Haji atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Paulina Nahato, Mheshimiwa Tecla Ungele ajiandae.

MHE. MWANTUMU DAU HAJI: Mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii niliyoipata hivi sasa hivi na kuichangia wizara hii iliyombele yangu na kwa mara yangu ya pili Bunge hili lako tukufu kuendelea kuchangia hii leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia kuwa na hali ya uzima na afya na kunijalia kwamba hivi sasa nimesimama niweze kuichangia Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Rais Mheshimiwa wangu Samia Suluhu Hassan kwa kuupiga mwingi. Hii Wizara nasema ilikuwa ina Wizara ambayo imo pamoja na Wizara ya Afya, lakini Rais wetu akaamua kuitenga baina ya Wizara ya Afya na Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii makusudi ili iweze kufanya kazi vizuri. Kwa hiyo mama nampongeza sana na hao watu ambao aliwaweka hapa Mheshimiwa Waziri na Naibu wake wanafanya kazi vizuri ili waweze kufika hapo mbele tunapopataka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuendelea kuchangia, mimi niendeleo kuchangia kwanza kuhusu suala la wanawake; wengi Wabunge wenzangu wamechangia mambo mengi

mambo mazuri tu ambayo wamechangia na kila atakayesimama hapa anachangia masuala ya wanawake na watoto kuhusu unyanyasaji pamoja na ubakaji.

Mheshimiwa Spika, sisi wanawake tuliokuwemo humu ndani ya nchi au ndani ya Tanzania hii kwa kweli tunapata matatizo makubwa sana na kuna wanawake waliokuwemo ndani ya majumba wanaangaika usiku na mchana na hali zao duni na masikini wengine wameolewa, lakini na wengine wanakuwa wajane.

Mheshimiwa Spika, mwanamke mwenye mume hivi sasa amekaa kwa mumewe kusema kwamba mimi naomba stara ili nisitirike, nitazame hatma yangu inapokwenda. Mwanamke huyu anakwenda zake kuuza machungwa au mboga au anakwenda kwenye ujasiriamali wake kujitafuta riziki, mwanamke huyo akirudi pengine maji hana ndani akayatafute, mwanamke huyo hana chakula cha kula ameshanunua huko alikokwenda kuuza matunda yake, anakuja anapika mboga yake, anaupika ubwabwa wake anamaliza shughuli zake na anategemea mume wangu hapa akija nije nimfurahishe.

Mheshimiwa Spika, mwanamke akishapika chakula kile na jinsi wanawake sisi tunavyowapenda wanaume basi Mwenyezi Mungu alivyotujalia sisi wanawake tunawapenda wanaume, nisifiche hili neno lipo mwanamke anapika chakula anaiweka sahani nzuri kaipamba wali, ule wali anaupika kule kwetu kule kwetu linaweka tandu juu, analichukua tandu anamwekea mumewe pale kaipika mboga yake vizuri kaiweka pale kila kitu chake ile kitu kimetokana na mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, anakuja mume anakamkaribisha vizuri mumewe wanakuja wanakula pale ila wenyewe wanaendelea kuzungumza mazungumzo yao baina ya mwanamke na mwanaume ndani ya nyumba, lakini bado wanawake wananyanyasika yote hayo anayoyafanya haonekani kama yeye yule mwanamke si lolote si chochote. Mwanaume anaweza akatafuta nyumba ya pili au ya tatu

mkewe aliye ndani aliyemuwekea lile tandu akaona si lolote si chochote. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Wizara hii naiomba, hii Wizara yako leo au wizara yetu naiyomba hiki kitu kiwasimamie wanawake vizuri kiwajengee uwezo wanawake na kama kuna uwezekano mimi nazungumza siku zote wapate mafunzo ili hawa wanawake wajue jinsi ya kukaa ndani na kuhusu familia zao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, la pili hilo nalizungumzia kuhusu watoto wetu jinsi wanavyonyanyasika ndani ya nyumba, ndani ya maeneo, ndani ya shughuli zao wanakokwenda.

Mheshimiwa Spika, kuna wengine watoto wananyanyasiwa kwenye shule au vyuoni. Walimu wao wenyewe wanawanyanyasa watoto lakini mbaya zaidi inayosikitisha baba yake mtu aliyemzaa kashawekea tandu na mkewe, jioni yake anakwenda kumfanyia kitendo kibaya mwanae mweyewe aliyemzaa. Kweli hii haki? Hii inakuwa si haki anafanya kitendo kilichokuwa si kizuri kwa yule mwanae au watoto wake anawafanyia mambo yasiyokuwa na maana na anamfanyia yule mwanamke kwa juu ya mapenzi aliyonayo haoni hasikii kwamba mimi huku mume wangu ataingia ubavu wa pili aende akawadhuru wale watoto kwa vitendo vibaya. Kalala buheri kwa masaa ishirini mwanamke hana habari baba mtu anakula vitu kwa mtoto.

Mheshimiwa Spika, kweli hili suala ni haki hii Mwenyezi Mungu kweli yupo radhi kufanya vitendo kama hivi? Kwa hiyo, jamani Wizara itusaidie kwa sababu akienda akisema mtoto anatishwa.

Mheshimiwa Spika, juzi tu hapa mtoto kalawitiwa na baba yake mbele na nyuma, akamwambia huna ruhusa ya kusema na ukimwambia mama yako basi sikununulii dhahabu wala sikupi herein, wala sikupi nyumba mtoto kashindwa kusema anamwambia nitakuchinja au nitakuua ukisema kafanya tendo hilo mwanamke kuja kugundua kaenda kusema kwa mama kamwambia wewe mama kampiga

mwanamke kapigwa mpaka kasema hiki nini! Mtoto yule keshamuhangaikia na baba kutambulika kakimbia dunia hii unakimbia unaenda wapi? Ameshakamatwa na sasa hivi yupo kwenye mikono ya sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sheria ya watoto ambao wananyanyasika ingawa imewekwa kwa mtu mbakaji atiwe ndani kwa muda wa miaka 30, mimi naiona hii kidogo na kama atapewa hii miaka 30 huyu mbakaji huyu kama atapewa hii miaka 30 basi ahasiwe kwa ile sindano, akishahasiwa kwa ile sindano yule atakuwa hana nguvu na atakapotoka huku nje adabu atakuwa kaipata kwa muda wa miaka 30, kahasiwa hana nguvu, hana kitu chochote amekaa yeye kama boya, mtu kama huyo anakuwa anaitwa chapa upunga ulale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja asilimia mia moja. Ahsante sana kwa ruhusa yako, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji. Sasa nimuite Mheshimiwa Dkt. Pauline Nahato, atafuatiwa na Mheshimiwa Tecla Ungele, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, ajiandae.

MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi na mimi nikachangie katika Wizara hii. Awali yayote napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipatia nafasi na mimi kusimama mbele kuchangia katika Wizara hii muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, mimi napenda kumshukuru sana Rais wetu mpendwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa maono aliyoyapata ya kuweza kuanzisha Wizara hii. Wizara hii ni muhimu sana, Wizara hii ilipokuwa katika Wizara ya Afya ilikuwa ni kubwa mno kiasi kwamba akili yote au *concentration* yote ilikuwa katika masuala ya afya, lakini leo Wizara hii inajitegemea na mimi sina mashaka na Dkt. Gwajima pamoja na Naibu Waziri pamoja na timu nzima ni

wachapakazi. Kwa hiyo, kwa hilo naipongeza sana wizara hii kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la ukatili wa kijinsia limeongelewa sana kwa hisia kali na suala hili la ukatili wa kijinsia huwanyima wanaume na wanawake na watoto kufurahia haki zao za msingi ambazo kimsingi ni haki ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, katika takwimu za Benki ya Dunia ambayo ilitolewa Aprili, 2022 imeonesha kwamba Tanzania ina asimilia 40 ya wanawake wote wameathiriwa kimwili au kijinsia na ambapo kati ya hao asilimia 14 wameathiriwa kwa kingono.

Mheshimiwa Spika, takwimu hizo hizo za Benki ya Dunia zinaonesha kwamba wanakwake wa umri kati ya miaka 15 mpaka 49 walifanyiwa ukatili huo na wenzi wao. Takwimu inaendelea kusema kwamba kwa wastani asilimia 30 ya wasichana chini ya miaka 18 walifanyiwa ukatili wa kingono.

Mheshimiwa Spika, hili suala ni zito, ukatili wa kijinsia ni jambo zito, ni jambo zito kwa sababu haliathiri tu maumbile, linaathiri hisia za wote wanaoathirika na mtu akiathirika kisaikolojia na kihisia ni rahisi sana kufanya mambo ambayo hakuyapenda kuyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aina za ukatili ambazo zinafanyika katika nchi yetu mojawapo ni ukatili wa kimwili kwa mfano mtu kupigwa au kujeruhiwa, nyingine ni ukatili wa kingono ambapo mtu huingiliwa bila ridhaa yake, inaweza ikawa ndani ya ndoa au ikawa nje ya ndoa, lakini kama hakuna ridhaa basi pia huo ni ukatili wa kingono, lakini pia kuna ukatili wa kisaikolojia, ukatili wa kisaikolojia; ni pale ambapo mtu anaumizwa kihisia na kujisikia vibaya na kutokufurahia Maisha, lakini ukatili mwingine ni ukatili utokao na mila na desturi zilizopo katika jamii zetu hizo ni kwa mfano kutokumiliki ardhi na wengi waathirika ni wanawake na nyingine ni ukeketwaji wa wanawake, nyingine ni ndoa za kulazimishwa, nyingine

ni wajane katika mila mbalimbali kurithiwa lakini nyingine ni mauaji ya vikongwe wasiokuwa na hatia kwasababu mbalimbali. Lakini vilevile ni uuaji wa watu wenye ulemavu na nyingine ambayo pia ni ya ajabu ni miiko ya vyakula, kwa mfano wanaume hula chakula cha aina fulani na wanawake hawaruhusiwi kwa mfano kuku mapaja na nini wanaume ndiyo wanakula huo pia ni unyanyasaji wa kijinsia lakini vilevile hata ndoa ya mkeka pia ni unyanyasaji wa kijinsia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala kubwa linaloonekana hapa pia ambalo linachangia ni tatizo lipo ndani ya familia; ndoa zinakufungwa lakini baada ya muda panakuwa hakuna mawasiliano, baba na mama hawaongei miezi sita, mwaka watoto itakuwaje? Na hawa watoto ndiyo sisi huenda humu ndani na sisi wazazi wetu walifanya hivyo au babu zetu walifanya hivyo, baba kivyake, mama kivyake, baba anampiga mama, watoto wanaona, baba anamtukana mama watoto wanaona, watoto wanatukana, watoto wanaona, watoto hawaweze kuwapiga wazazi, mwisho wa siku watoto wanaamua kuondoka nyumbani na kwenda kutafuta maisha sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini lambo muhimu sana pia katika tafiti nyingi zimefanyika hata hawa wazazi hawajui jinsi ya kuongea na watoto wao. Hawajalelewa katika mazingira ya kuongea na watoto, hawajui waongee na watoto wapi, hawajui waongee na watoto lini, hawajui mbinu gani watumie kuongea na watoto. Watoto hawana uhuru na wazazi, watoto wamesema hawana uhuru ukiwauliza watoto wanasema ni afadhali akaongee na mwalimu na je, hata hawa walimu wameandalia. *(Makofi)*

Kwa hiyo hili jambo Wizara ilianganalie, wazazi wapewe semina ya kutosha kuongea na watoto wao. Wazazi wanaishi na watoto wenyewe warekebishe tabia zao, lakini wawe karibu na watoto ili waongee nao. Watakapoongea na watoto watajua shida zao na mtoto atakuwa na furaha, hatokimbia nyumbani, hatoenda mitaani hata kama familia kiuchumi siyo nzuri mtoto atashiriki katika masuala ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na muda naomba niongee suala moja muhimu sana. Suala hili ni kuhusu hivi vituo vya kulelea watoto. Vituo viko vingi lakini naomba kuishauri Serikali, hivi vituo miongozo yake haieleweki watu wanakurupuka wanaanzisha vituo, miundombinu haijakaa vizuri, wataalam wa kutosha hawapo na hivyo unakuta wapo tu wanaanzisha vituo watoto wanalala chini, watoto mara wanakosa mlo, watoto wanapigana, watoto hivi, wataalam hakuna, na kadhalika. Hivi vituo viangaliwe, vigezo vya kutosha, *checklist* iwepo ili hivi vituo viwe vituo kweli vitakavyoleta watoto watakavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa ninaomba tu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Dakika 30 muda wako umeisha Mheshimiwa.

MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Tecla Ungele, atafatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Judith Kapinga ajiandae.

MHE. TECLA M. UNGELE: Mheshimiwa Spika, ahsante, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunipatia uhai.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nakupongeza kwa kazi kubwa unayofanya kuongoza Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuona umuhimu wa kuwa na Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Amewateua Mawaziri Dkt. Dorothy Gwajima na msaidizi wake Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis na Katibu Mkuu Dkt. Zainabu Chaula na timu yao ingine yote mpaka

kule kwenye halmashauri wanaendelea vizuri kufanya kazi kubwa, kwa kweli ni wapambanaji timu yetu hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, napenda kujikita kwenye maeneo mawili na kama si matatu; la kwanza matukio kadhaa ya unyanyasaji wa watoto yameendelea kutolewa taarifa siku hadi siku, kila siku kunavyokucha mikoa yote, pembe zote za nchi hii, yanatisha sana na hii ni changamoto kubwa sana wakati mwingine najjuliza hapa ni nini? Ni changamoto ya afya ya akili ama ni kitu gani au ni mazingira magumu ya hali ya uchumi ni kitu gani. Hivyo takwimu mbalimbali zimetolewa kila mikoa na zinajulikana, lakini mimi nakuja na jambo la ushauri kwa Wizara hii. Kwenye miaka ya 1980s mpaka 1990s tulikuwa na changamoto kubwa kweli ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI na ilionekana kwamba suala hili ni la kiafya tu, na kwa kweli tulihangaika sana ilivyoonekana ni *health sector* peke yake washughulikie masuala ya UKIMWI, lakini pale ilipokuja kujulikana kwamba suala hili ni *cross cutting*, ni mtambuka ikaja ikarudishwa kwenye jamii na zikaanzishwa Kamati mbalimbali za kudhibiti UKIMWI kuanzia ngazi ya Taifa mpaka ngazi ya vijiji, tukaona kumbe suala la maambukizi ya virusi vya UKIMWI si matibabu peke yake lakini pia hata maambukizi yake yanaenda kwenye *social culture issues*. Kwa hiyo, inahitajika jamii ihusike mpaka kule kwenye ngazi. (Makofi)

Kwa hiyo, hata hapa naona kuna mazingira fulani yanayoendelea na hili suala la mambo ya unyanyasaji wa kijinsia, yakionekana ya ubakaji na mengineyo yanayofanana na hayo. Suala hili inabidi sasa muda umefika tuangalie jinsi ya kulitatu, tulirudishe kwenye jamii na wanaohusika sana kwenye jamii yetu ni wale wa Idara ya Maendeleo ya Jamii wanahusika, wanakubalika sana kwenye ngazi ya jamii. Tulirudishe suala hili kwenye ngazi ya jamii ili uhusike na itakavyoendelea hivyo, basi elimu itolewe kwa kila jamii kuanzia ngazi ya kaya, familia na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo itaonekana huu ukimya tunaouona hata humu ndani tumeendelea kupiga debe hii ni sisi wakina mama tu ndani tangu imeanza

kuchangiwa, sijaona akina baba kuna nini hapa? Kwa hiyo hapa tayari kuna tatizo *social culture issues*, mambo ya kijamii, mambo ya tamaduni zetu, kuna nini katika suala hili la ubakaji na mengineyo yanayofanana na hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini pia niendeleo kwenye makazi ya wazee; tumeona kuna makazi 14 ya wazee nchi nzima na bado kuna wazee 271 tu wako maeneo hayo. Lakini mimi nilikuwa na angalia angalizo kama haya makazi tunasikia huduma zao bado siyo nzuri, hazitoshelezi na kweli Serikali haiwezi ikakidhi huduma zote za wazee. Sasa nini kifanyike, mimi nilikuwa nashauri kwamba huko tunakoenda ni vizuri kabisa huduma hizi za wazee ikapewa sekta binafsi na iruhusiwe kama kuna watu binafsi wanaweza wakaanzisha makazi ya wazee iruhusiwe ili wenye uwezo basi watalipia, kama wafanyakazi wanaweza wakatunza pensheni zao ikatunzwa kule baadaye wanapokuja kumaliza kazi wakiwa na umri mkubwa zaidi wanahamia kwenye makazi yale na huduma zao na fedha zao zinakuwa zimetunzwa kule, ni jambo linawezekana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lingine nilikuona naona bajeti ya Wizara hii. Tumeenda kwenye taasisi mbalimbali ya Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii kwa mfano kule Rungemba kunahitajika miundombinu ile irekebishwe.

Kwa hiyo, tunaomba bajeti katika *item* ya maendeleo iendeleo kupewa kipaumbele, ipewe fedha kubwa ili marekebisho mbalimbali ya vyuo yawezekane ili kwenye vyuo vile kuwe mahali pazuri pa kujifunza na kufundisha walimu wetu na hata vijana wetu wanaotoka mahala pale. Kwa kufanya hivyo jamii yetu itakuwa na hali nzuri tukiboresha maendeleo ya jamii na kila jambo litawezekana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, atafatiwa Mheshimiwa Judith Kapinga, Mheshimiwa Halima James Mdee ajiandae.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi kuchangia. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuianzisha hii Wizara ya Maendeleo ya Jamii kwani ilipokuwa pamoja na Afya niliona kama ilikuwa inamezwa.

Mheshimiwa Spika, tena niwapongeze sana wanawake wote wa Tanzania, kwa kweli wanawake sasa hivi hakuna mwanamke aliyelala. Hata ninyi wanaume mliyo humu ndani mnajua wake zenu wanafanya kazi, hakuna mwanamke aliyelala, kwa hiyo nawapongeza sana. Na wanawake wengi wamejitolea sana kufanya usindikaji, kufanya biashara mbalimbali, wanafanya kazi kweli, tatizo nilikuwa naomba Wizara waone jinsi ya kuwapatia mafunzo ya biashara wanawake kwa sababu wengi wanaanzisha biashara bila ya kupata mafunzo. Wapate mafunzo ya biashara pamoja na ujasiriamali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikiendelea hapo hapo nimekazia kuwa wapatiwe mafunzo ya biashara pamoja na ujasiriamali. Wanawake wamejitoa sana, hakuna mwanamke aliyelala sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ninasema ni asilimia nne kwa akinamama. Kwa kweli hawa akinamama wanarudisha mikopo yao vizuri sana na wanaitumia, lakini wanawake ukweli wamenituma wanasema kuwa hii asilimia nne haitoshi. Kwa hiyo, tuangalie pamoja na kushirikiana na Wizara zingine jinsi ya kuona tufanyeje ili ionekane hizi asilimia nne ambao wanapewa hawa akina mama, pamoja na vijana, pamoja na makundi ya watu wenye ulemavu ionekane kuwa kweli inafanya kitu ambacho kinaonekana kweli kweli kuwa ni kitu chenyewe.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwenye usindikaji; akinamama ambao wamejikita sana ni masoko waweze kutafutiwa masoko na waweze kuonyeshwa kuwa wafanye vitu ya vyakula ambacho kina *quality* kweli. Wakati mwingine vyakula havina *quality* unakuta kuwa *TBS* inawababaisha, kwa hiyo tuangalie tuweze kuwasaidia hawa akinamama.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine na mimi nawaunga mkono akinamama wote waliongelea kuhusu ukatili wa akinamama pamoja na watoto. Unaona kwa kweli ni mambo haya wanafanya kwa kweli, tunaomba wajirudi akina baba kuacha kufanya ukatili kwa watoto wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninaloongelea ni watoto wa mitaani; tutaongelea watoto wa mitaani mpaka lini na yenyewe tuweke mtazamo jinsi ya kukatiza kuachana na kuongelea mambo ya watoto wa mitaani. Wizara pamoja na Afisa Maendeleo tukiwa pamoja na Ustawi wa Jamii tuone jinsi ya kuwaangalia hawa watoto waache kwenda kwenye mambo ya mitaani.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo halijaongelewa humu ni jukwaa la akinamama; majukwaa ya akinamama namshukuru Mheshimiwa Rais Samia ameanzisha majukwaa ya akinamama tangu alipokuwa Makamu wa Rais. Lakini mpaka sasa hivi haya majukwaa ya akinamama hawajui yanafanya nini, wapo tu, hawana uwezeshwaji, wanaendelea tu. Kwa hiyo, naomba sana wangepewa Mwongozo wangeliweza kufanya vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo naomba kuliongelea ni vituo vya wazee; nilitembelea vituo vya wazee vya Morogoro, Kituo cha Fungafunga pamoja Chasi. Unakuta kuwa vituo vya wazee wanamuomba Mheshimiwa Waziri na Naibu awatembelee, hawajawatembelea kwa sababu kuna matatizo mengi, lakini viongozi wengine tumekwenda ndiyo sababu tunayachangia. Unakuta hao wazee wanaishukuru kwanza Serikali inawapatia chakula, ila kwa chakula wanapongeza. Lakini kuna tatizo unakuta hawa wazee majengo yao ni mabovu, kwa hiyo nilikuwa naomba haya majengo yaweze kukarabatiwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine wazee hao wengine siyo wazee sana kwa sababu kuna na vijana ambao wameumwa ukoma, hawana vidole, wamekatika vidole na nini nao wako humohumo. Wanaomba Kituo cha

Fungafunga waweze kupatiwa uzio kwa sababu wazee wanatoroka wanakwenda mjini.

Jambo lingine wanashukuru kuna ma-*nurse*, lakini kuna tatizo moja wakipata magonjwa dawa hazitoshi, kwa hiyo wanaomba wapatiwe dawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo naongelea hapohapo ni maji; wana tatizo la maji naongelea Fungafunga ya Morogoro, kwa hiyo ushauri wangu waweze kupewa maji kusudi na na wenyewe waweze kutumika vizuri.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni watumishi; nikija kwenye watumishi, kuna watumishi wa Ustawi wa Jamii ambao inabidi wa wasaidie. Watumishi ni wachache kiasi wazee wengine hawajiwezi kabisa.

Kwa hiyo, naomba muwaongeze watumishi. Hapo hapo kuna watumishi wengine wamekaa muda mrefu kwenye ngazi hiyo hiyo kuanzia mwaka 1999 hajapandishwa cheo chochote, yuko palepale, kwa hiyo, naomba muwaangalie na wenyewe waweze kuonwa kuwa wanafanyiwa mambo mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu uhaba wa watumishi kwa ujumla na wajibu wao, maendeleo ya jamii ni watu wazuri na inabidi waweze kufanya kazi zao vizuri, waweze na wenyewe kupewa vitenda kazi kama Wizara zingine walivyopewa vitendea kazi kama pikipiki na nini. Kwa sababu masuala yote kwa Afisa Maendeleo ya Jamii ambaye anajijua masuala yote ya lishe yako kwako, masuala yote ya ujenzi wa vyoo yako kwake, masuala yote ya nini kusudi waweze kufanya kazi zao vizuri naomba Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii waweze kuangaliwa kwa vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Kwa hayo niliyoyaongea, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Judith Kapinga, atafuatiwa na Mheshimiwa Halima James Mdee, Mheshimiwa Minza Mjika ajiandae.

MHE. JUDITH S. KAPINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi, awali ya yote ningependa nimpongeze Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuunda Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Kwa kweli ni jambo lenye tija sana na kwa dhati ya moyo wangu naomba nimpongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna tofauti kubwa kati ya ubakaji na ulawiti kwa watu wazima na ubakaji na ulawiti kwa watoto, na tofauti ni kwamba mtu mzima ana haki ya kuipigania haki yake, anaweza kuipigania haki yake kwa sababu nguvu anazo, utashi anao na maarifa anayo. Sasa hii ni tofauti kwa mtoto mdogo kwa sababu mtoto hawezi kupigania haki yake, haki ya mtoto inapiganiwa kwa utashi wa mzazi wake ama mlezi wake, na hapa ndipo ambapo tatizo linakuja kwa sababu ili haki ya mtoto iweze kupiganiwa inategemea utayari wa mzazi wa kupigania haki hiyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mzazi anaweza akachagua mambo tofauti tofauti, kwanza anaweza akachagua aipiganie, lakini la pili anaweza akachugua asipiganie, la tatu akipewa mpunga anaweza akaamua akae kimya. Lakini kama yeye mwenyewe anahusika na matendo ya ukatili hataipigania haki hiyo kabisa. Sasa hapa lazima Wizara ikae na Wizara nyingine ambazo zinahusika ili kuweka mambo sawa. Na lazima wakubali kuweka uwekezaji kwa Maafisa Maendeleo wa Jamii. Nasema hivyo kwa sababu gani, Afisa Maendeleo ya Jamii ndiyo mtu kati ambaye anaweza kulinda haki ya mtoto na akamshurutisha mzazi atafute haki ya mtoto wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafahamu tutasema kwamba labda kuna tatizo la fedha na nini, lakini ulinzi wa haki ya mtoto unategemea hapa tutafanya uwekezaji wa aina gani. Lakini niende mbele zaidi kwenye kuishauri Wizara, sasa hivi

hali ilivyo, namna ambavyo mashtaka yanaendeshwa ya masuala ya ubakaji na ulawiti kwa watoto yanaendeshwa sawasawa na mashtaka ya ubakaji na ulawiti kama ilivyo kwa watu wazima. Sasa hapa pia kuna tatizo lingine kwa sababu Mahakama inatuambia kwamba ushahidi mzuri unatoka kwa yule mtu ambaye amefanyiwa ukatili yeye mwenyewe na hapa tunamzungumzia mtoto mdogo yaani namna anavyotoa ushahidi wake lazima aseme alivyofanyiwa kile kitendo kwa maneno mahsusi yanavyotumika. Na akisema vile ambavyo sivyo ushahidi unapungua thamani yake. Sasa ukiangalia kwa mila zetu na desturi zetu za Kitanzania kwa maadili tuliyokuza nayo watoto wetu yale maneno kutamka ni ngumu sana. Kwa sababu mtoto lazima atamke zile nyenzo za kimwili zilizotumika kumfanyia uhalifu ambazo hata mimi mwenyewe binafsi siwezi kuzitamka. *(Makofi)*

Sasa nafahamu Mahakama inatumia utashi mara nyingine watoto wakishindwa kusema bado wanatumia utashi walionao kwa ajili ya ku-convict hawa watuhumiwa. Lakini lazima tuiweke kwenye sheria, lazima utaratibu wa kushughulikia matatizo ya ulawiti na ubakaji kwa watoto uwe tofauti kabisa na kifungu cha kushughulikia ubakaji na ulawiti kwa watu wazima kwa sababu watoto kama alivyo mtoto kama yeye mwenyewe hawezi kujipigania. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi namshauri Mheshimiwa Waziri akakae na Waziri wa Sheria na Katiba waone namna ya kutofautisha haya mambo. Namwambia yeye kwa sababu yeye ndiyo analinda ustawi wa watoto katika Taifa letu. Kwa hiyo bila kuweka mambo sawa hapa naona kidogo kutakuwa na mushkeli.

Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kushauri kuhusiana na ulinzi wa mtoto, hapa kwa muda mrefu tumeongelea kuhusiana na watoto kubeba mabegi mazito mgongoni na yalishatolewa maelekezo, lakini kinachosikitisha bado watoto wanabeba mizigo mikubwa sana wakienda shuleni na inahatarisha afya zao. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nimuombe Mheshimiwa Waziri kwa sababu yeye ndio anahusika na ustawi wa mtoto, yeye ndio anamlinda mtoto wa Kitanzania, naomba afanye jambo katika hili. Shule zetu zinaweza zikaweka utaratibu mzuri watoto wasibebeshwe mlima wa madaftari, ma-*counter book* na mlima wa vitabu migongoni mwao tunaharibu afya ya hawa watoto. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala langu la mwisho ni kwenye ulinzi wa afya ya mwanamke. Afya bora ya mwanamke ni uwekezaji kwa Taifa letu kwa sababu mwanamke anatomika kama nyenzo ya maendeleo kwenye mambo mengi sana. Ninachosikitika suala la utoaji wa mimba holela mtaani limeachiwa kupita maelezo. Takwimu zinatambia wanawake 400,000 kila mwaka wanatoa mimba mtaani na asilimia 70 wanatumia nyenzo ambazo sio za kiafya. Wanatumia nyenzo ambazo sio za madaktari wenye sifa, ni asilimia 30 tu wa mjini ambao watakwenda kwa madaktari wenye sifa.

Sasa masuala ya utoaji huu wa mimba inawezekana tusiyaongee sana, lakini wanawake 400,000 kwa mwaka ni wanawake 1,100 kila siku wanatoa mimba kwa njia zisizo salama.

Mheshimiwa Spika, sasa tunaomba ulifanyie kazi hili suala, nafahamu kuna *situation* ambazo zinaruhusiwa mwanamke aweze kutoa mimba, lakini kuna mambo ambayo tunaweza tukayaboresha. Kuna mazingira magumu ambayo tunaweza tukaboresha ili masuala ya utoaji wa mimba huko mtaani, pasipo kutumia nyenzo sahihi yaweze kupungua na yaweze kuhalalishwa yakafanywa katika hospitali zetu. Kwa mfano, kwa sababu sasa hivi tunaambiwa takwimu karibu wanawake 1,000,000 kila mwaka wanapata mimba zisizotarajiwa, sasa tuone tunaboresha vipi ili wanawake wasikimbillie kule mtaani kwenye nyenzo ambazo sizo na waende wakafanye katika mahali ambapo panastahili kiafya katika suala hilo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Halima James Mdee atafuatiwa na Mheshimiwa Minza Mjika, Mheshimiwa Jacqueline Msongozi Ngonyani ajiandae.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, nashukuru na mimi nichangie Wizara hii muhimu na nilikuwa nadhani kwamba ni muhimu Mheshimiwa Waziri akatufanya Watanzania tukajua kwamba hii ni Wizara muhimu; mosi, inahusika na maendeleo ya jamii kwa mantiki ya kwamba jamii nzima ya Tanzania; pili, ni jinsia maana yake ni (ke) na (me) maana kuna watu wanafikiria ni Wizara ya Wanawake; tatu, wanawake wenyewe na makundi maalum ambayo ndio vijana, watoto, watu wenye ulemavu na wazee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesema niyaseme haya kwa sababu yamezungumzwa hapa na wachangiaji wengi sana, namna gani kumekuwa na ongezeko la ubakaji na kulawitiwa kwa watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa napitia taarifa za *UNICEF* ambazo zinatambia ili Waziri najua hizi taarifa unazo lakini ni msisitizo tu, ili ujue jukumu lililokuwa mbele yako kwa sababu watoto wako chini yako. Watanzania kwa idadi yetu tuliyonayo sasa hivi watoto chini ya umri wa miaka 18 kwa mujibu wa *UNICEF* ni milioni 29.7; kwa hiyo, kwa lugha nyingine *population* ya Tanzania asilimia 50 ya Watanzania wote ni watoto chini ya miaka 18. Sasa tunaambiwa huyu mtoto tusipomlinda akiwa mtoto ndio anavyokuwa mtu mzima kuna vituko mbalimbali huko vinatokea, alizungumza Profesa hapa asubuhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Wizara hii tusichukulie kama Wizara ya mzaha mzaha, ni Wizara ambayo mmepewa majukumu makubwa ya kulea Taifa. Katika hao watoto milioni 29 mimi leo nitamzungumzia mtoto wa kike ambao wako milioni 14.7. Tunaambiwa kati ya nchi ambazo zina kiwango cha juu cha ndoa za utotoni Tanzania tunaongoza, ni miongoni mwa nchi ambazo tuna kiwango cha juu cha ndoa za utotoni. Tunaambiwa kati ya watoto watano wa kike; wawili wanaolewa kabla hawajatimiza miaka 18. Sasa tujjulize

katika hawa watoto milioni 14.7 kwa mnaojua mahesabu kama ndani ya watano hao ukiwagawanya kiwatano/watano kila watano wawili wanaolewa chini ya miaka 18 Taifa linakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unajua maendeleo ya Taifa yanahitaji jinsia ya (me) na jinsia ya (ke) zifanye kazi kwa pamoja tuweze kwenda mbele. Waziri unajua kizazi cha sasa sio kama kizazi cha mababu zetu na mabibi zetu, vijana wa sasa tunataka mtoto wa kike ajitume na mtoto wa kiume ajitume mnawaza nini kwa watoto hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaambiwa mikoa mitatu bora takwimu zinatufanya tuangalie namna gani tunakwenda kutatua tatizo. Mikoa mitatu bora ambayo kati ya wasichana watano wawili wanaolewa chini ya miaka 18, Shinyanga asilimia 56, Tabora asilimia 58, Dodoma asilimia 51 tunakwenda wapi?

Mimi niombe Serikali juzi nilikuwa napitia maana Tanzania ni Mjumbe wa Baraza la Umoja wa Mataifa wa Haki za Binadamu katika hilo Baraza ni la Kidiplomasia ndio, lakini mnajitathmini kwa namna gani haki za binadamu zinatekelezwa kwenye nchi husika? *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa Halima Mdee dakika moja malizia. *(Makofi)*

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, ni masikitiko yangu dakika moja; katika maeneo ambayo tunataka Waziri hili ulijibu katika maeneo ambayo Tanzania imeweka *pending*, hajakubali bado kuyafanyia kazi; mosi, ni eneo la ndoa za utotoni; pili, ni eneo la masuala ya mirathi sote tunajua wakina mama wanavyoumia kuhusiana na mirathi; tatu, ku-*deal* na sheria hizi *Customary Laws* (Sheria za Kimila) zinazonyima wanawake wa Kitanzania kumiliki ardhi. *(Makofi)*

Sasa kwa sababu ninajua Waziri unajua nataka uniambie kwa nini Watanzania kwenye vikao vya Kimataifa huko vya haki za binadamu masuala ya mtoto wa kike na masuala ya wanawake sio kipaumbele; na kama jibu ni tofauti niambie mna taarifa gani tofauti na hii taarifa ya Umoja wa Mataifa ya Baraza la Umoja wa Mataifa linalohusiana na haki za binadamu. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Halima Mdee nakushukuru sana. Mheshimiwa Minza Mjika atafuatiwa na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi Ngonyani, Mheshimiwa Selemani Jafo ajiandae. *(Makofi)*

MHE. MINZA S. MJIKA: Mheshimiwa Spika, ahsante napenda nishukuru sana kwa kunipatia muda huu, lakini vilevile nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili ya wema wake wa pekee ambao ametufanyia katika siku hii ya leo. *(Makofi)*

Awali ya yote nimshukuru sana Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan ambaye anafanya kazi kubwa kwa ajili ya Taifa letu hili. Mama yetu anapambana, anakimbia huku na kule kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu, tunamshukuru sana na zaidi ya yote tunamuomba kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumlinda na kumpatia afya njema. Lakini vilevile nipende kuwashukuru akinamama hawa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayofanya. Mama Gwajima na Naibu wako tunakuona sana unavyofanya kazi tunakuomba afya njema na uendelee kuifanya kazi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, basi kulingana na muda wetu mimi napenda niseme sehemu tatu tu; sehemu ya kwanza napenda kuongelea habari ya hawa watu wabakaji. Hakuna watu wananiumiza roho kama hao. watoto wa kike wananyanyaswa sana na vijana wa kiume wananyanyaswa sana, lakini nikiangalia hatima yake naona kama vile yaani hawafanyi makosa makubwa. Mtu yule anatakiwa achukuliwe hatua kama vile anavyochukuliwa muuaji kwamba ameua, apewe sheria kali ya kukaa gerezani hata miaka 20 ili ajifunze kule, kwa sababu mtu anapofanya hivyo wanawaathiri sana watoto wetu wa kike. Wanawaharibu

watoto wetu, wanakosa amani na wanakatisha njozi zao kwamba alitaka asome pengine amefanyiwa jambo baya na bado likashindikana hata kutatulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kingine niseme kuna Mheshimiwa Kapinga kasema mtoto hawezi akaongea maneno yale mahakamani, ndio maana unajikuta kwamba ukisema mahakamani kwamba nilitendewa jambo baya unaambiwa jambo gani hilo baya litaje. Sasa mtoto hawezi kutaja kwa asili yetu sisi Watanzania. Tunaomba watu kama wale washughulikiwe, hata msamaha wa wafungwa unaotolewa wakati mwingine Disemba wakati wa sikukuu, Rais watu kama hao wasitoke ashauriwe kabisa watu hao waendeleo kukaa gerezani kwa sababu kosa wanalolifanya ni kubwa lakini unaona mtu kafanya kosa kubwa kama lile unashangaa baada ya miezi mitatu minne unamuona mtaani. Sasa linachukuliwa ni jambo la kawaida kabisa, lakini akipewa adhabu moja tu miaka 20 akakaa gerezani anatoka kule alishachoka hawezi kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana hilo mlíchukue pamoja na Waziri husika wapewe adhabu za kutosha na wasitoke kwa msamaha wa Rais watu wa namna ile kifungo chao wapigwe miaka 30 akae mle ajifunze. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naingia kwa upande wa wamachinga. Ninapenda nimshukuru sana Rais wetu amewakumbuka vijana wetu kupata sehemu maalum za kufanyia kazi kwa kweli kwa hilo ninampongeza sana. Vile vile, wameitisha mkutano hapa vijana wetu wamepata semina mbalimbali, jinsi ya kuchukua mikopo na mikopo ile waitumieje, kwa hilo tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende upande mwingine wa wakina mama kweli mikopo wanapata lakini ile mikopo haitoshelezi. Nilikuwa naomba wenzangu wameongea hapa ninashukuru mimi niliona bora iwe asilimia 16 kwa mchanganuo ufuatao; asilimia 10 wanawake na wasichana wapate asilimia 10; lakini asilimia tatu wapate vijana, lakini

asilimia tatu tena wapate walemavu; hiyo itapendeza kidogo. Kwa hiyo, mtu atachukua kitu ambacho ni kikubwa na anaweza akafanya kazi. *(Makofi)*

Kwa upande wa wanawake ninapenda niseme kwamba hakuna mtu anafanya biashara kama mwanamke, mwanamke ni mjasiriamali wa kweli, akipewa mafunzo ya kutosha mwanamke hakosei na anafanya kazi kwa bidii zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, basi mimi naomba kulingana tu na kwamba hatuna wataalam wa kutosha tunaomba Serikali iongeze hawa maafisa maendeleo ya jamii, ili kwamba watu kabla hawajapata mkopo wakina mama wapewe semina mkopo ule ni wa kufanyia nini na ufanyeje lazima ajue. Lakini mtu anaweza akachukua mkopo siku hiyo hiyo anakwenda kujengea nyumba, anakwenda kununua *cement* anaanza ujenzi wa nyumba, marejesho atatoa wapi? Fedha ya mkopo sio ya kujengea, fedha tunayojengea ni ile inayotengwa kwenye mzunguko yaani ile faida inapopatikana basi iendelee kwenye shughuli za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini unakuta mtu anachukua mkopo, anaingia kufanya sehemu zingine ambazo haziko muhimu na akinamama hawa tunaona wana majukumu mengi. Kina mama kweli tuna majukumu sana yaani kama ni kwenye familia mama anachukua majukumu asilimia 85 baba anachukua tu asilimia 15. Kwa maana hii mama atachukua mkopo akishachukua mkopo chakula cha nyumbani ni mama, mboga ni mama, watoto kwenda shule ni mama, *uniform*, viatu ni mama, baba hana habari tena hususani kule kijijini hawana habari kabisa. Baba anajua *issue* ni kulewa tu, hana mambo mengine anamsumbua mama, hiyo ni kweli wala msibishe, ninasema kitu ambacho nimekifanyia utafiti ni kweli, baba anakunywa anarudi anataka chakula huku nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba wakina mama hawa wasaidiwe na kingine ninapenda niseme kwamba tunapowapa mkopo basi mkopo ule utolewe kwa wakati.

Kwa mfano, mtu anataka mkopo alime nyanya, nyanya inalimwa kuanzia mwezi wa nne na kuendelea huko kwenye kiangazi...

MHE. HAMISI S. TALETALE: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Simuoni Mbunge aliyesimama.

MHE. HAMISI S. TALETALE: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Taletale.

SPIKA: Mheshimiwa Hamisi Taletale.

T A A R I F A

MHE. HAMISI S. TALETALE: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wakina baba sio wakina baba wote ambao hawajali watoto zao, mimi nasimama nafasi ya baba na mama pia, ahsante. *(Makofi)*

MHE. MINZA S. MJIKA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana hiyo naipokea lakini ni kwa baadhi ya akina baba...

SPIKA: Mheshimiwa Mjika.

MHE. MINZA S. MJIKA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema sio akina baba wote.

SPIKA: Mheshimiwa Mjika, subiri kidogo.

MHE. MINZA S. MJIKA: Mheshimiwa Spika, bee.

SPIKA: Mheshimiwa Minza Mjika unaikubali taarifa hiyo?

MHE. MINZA S. MJIKA: Mheshimiwa Spika, naikubali sio kwa akina baba wote wanaofanya hayo matendo kama nilivyosema kwamba hususani wengi kule vijijini. Mimi natoka Simiyu nawaelewa ndugu zangu kule, lakini sio kwamba wote sio wote nalitambua hilo.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine wakina mama wapewe mkopo kwa muda muafaka. Anapoomba mkopo kwamba pengine anataka kuanzisha biashara yake apewe kwa muda muafaka, lakini anapocheleweshwa kupewa mkopo anajikuta sasa anakuwa nje ya matarajio yake na hafanyi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, ninapenda niongee juu ya hili jambo kwamba wakina mama wapate muda mzuri wa kuweza kufundishwa ujasiriamali kama nilivyosema hakuna kitu kinapotosha kama hicho. Inapofika marejesho wakina mama wengi tunaona jinsi wanavyohangaika wanakimbia huku na huku kumbe hawakupata shule nzuri kabla ya kuchukua mkopo wao.

Mheshimiwa Spika, basi kwa hayo yote ninapenda nishukuru ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Jacqueline Msongozi Ngonyani atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Jafo, Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamisi ajiandae.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ambayo inahitaji shilingi bilioni 44. Kwa uchache tu kwamba hii shilingi bilioni 43 kwa Wizara hii nyeti kabisa bado ni ndogo sana sana, ilitosha tu iongezeke. Nilikuwa natarajia kwamba Wizara hii ije na maombi ya kuanzia shilingi bilioni 800 huko shilingi bilioni 900 kama Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, jukumu la kulea watoto wetu ni la kwetu sisi wenyewe kama wazazi, lakini pia wamesema Wabunge wengine kwamba mtoto kama mtoto hawezi kujisemea mwenyewe. Ni dhahiri shahiri kwamba mtoto anaweza akakosa hata lishe, lakini asiseme, hata kama anahitaji mahitaji maalum bado akashindwa kusema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakumbuka nikiwa mdogo enzi ya Mwalimu nchi yetu ikiwa bado changa sana na ni masikini lakini wazazi wetu walikuwa wakienda kwenye masuala ya kliniki watoto wanapopimwa wanapoodoka walikuwa wanaondoka na maziwa ya unga, walikuwa wanaondoka na mkate vitu kama hivyo.

Sasa mimi naomba Wizara hii pia mama yetu Dkt. Gwajima hebu iboreshe hii Wizara na vitu kama hivi viweze kufanyika *at least* kuwe na motisha kwa mtoto, hata ikifika tarehe ya mtoto kwenda kliniki mtoto mwenyewe wakati mwingine mwenye umri wa miaka mitatu/minne akaweza kukumbusha. Waweze kupata motisha mbalimbali kama maziwa, *blueband* na nini na mambo mbalimbali. Hata hivyo ninaamini kabisa wewe ni jembe kweli kweli, unaweza ukaandika na maandiko na nini Wizara yako ikaendelea kupata misaada kama hiyo na ikaenda kutolewa kwenye zahanati na vituo vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, liko jambo ambalo liko kwenye jamii yetu ambalo limejitokeza sana, wako baadhi ya wanaume/akina baba, wanadhulumu haki za watoto kwa kunyonya maziwa ya mama ambayo mtoto ndio alipaswa anyonye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili limejitokeza katika mikoa mbalimbali niombe Wizara ifanye utafiti yako majibaba yanafakamia maziwa ya watoto wanawanyonya wale wake zao wanaonyonyesha. Badala ya mtoto anyonye maziwa yale na kupata ile lishe basi baba anakwenda ananyonya; na kuna mtu ameniongezea nyama hapa akaniambia hivi kwamba yale maziwa ya mama kwanza yana virutubisho sana wako baadhi ya akina baba wamegundua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia yale maziwa ya mama yanasaidia kukata *hangover* ya walevi ambao wanakuwa wamekunywa pombe na yanasaidia kukata hiyo *hangover*. Kwa hiyo, niombe sana Wizara iweke mpango mzuri na itoe elimu ili akina baba hawa wasiwadhulumu watoto haki zao. *(Makofi)*

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie pia suala la kisiasa; kumekuwa na ukatili mkubwa sana wa kijinsia kwenye masuala ya kisiasa kwa wanawake ambao wanachipukia kwenye masuala ya siasa, hususan hata sisi Wabunge wanawake humu ndani, tumekuwa tukinyanyapaliwa kwenye maeneo yetu tunapofanya shughuli zetu za kisiasa. Kwa hiyo, huu ukatili Wizara imejipangaje kuhakikisha kwamba inatusaidia sisi wanawake tunaokua kisiasa kwenye maeneo mbalimbali, ili tuweze kufanya shughuli zetu za kisiasa bila kufanyiwa ukatili, ikiwemo ukatili wa kwenye mitandao?

Mheshimiwa Spika, maana Mbunge mwanamke anaweza akasema jambo hapa na Mbunge mwaname akasema jambo hilo hilo, lakini utakuta Mbunge mwanamke ananyanyapaliwa kwenye mtandao, anatumkanwa matusi makubwa makubwa ya nguoni. Tunaomba Wizara muone namna gani ya kusaidia jambo hili ili lisiendelee kujitokeza kwa sababu, sisi sote ni Watanzania na ni jamii moja.

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie ukatili wa kingono...

MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: ...jamani naombeni leo sina... Naomba Taarifa kaeni nazo, leo hii naomba. Nina mambo mahususi sana hapa. Nina jambo mahususi sana la kuchangia. Tafadhali kaka yangu nakuheshimu, nakupenda sana. (*Kicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ramadhan Ramadhan.

T A A R I F A

MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN: Mheshimiwa Spika, naomba nimpe Taarifa mzungumzaji, mama yangu kwamba wako wasichana na wanawake wengi wamekata tamaa kuendelea na shughuli za siasa kwa sababu ya

unyanyapaa anaoendelea kuusema. Kwa hiyo, naomba nimpe Taarifa kwamba, hilo tatizo kweli ni kubwa na lazima hatua zichukuliwe. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, unaipokea Taarifa hiyo?

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika, ahsante, naipokea sana, ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie ukatili wa kingono; Wabunge wenzangu wengi wamechangia hapa kuhusiana na ukatili wa kingono kwa wanawake. Ni kweli kabisa ukatili wa kingono katika nchi yetu ya Tanzania umeshamiri sana, lakini mimi nitaliongelea jambo hili kitofauti kidogo.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya UKIMWI na kwa kuwa ni Mjumbe wa Kamati ya UKIMWI, nitazungumza jambo ambalo linahusiana na suala la maendeleo ya jamii, lakini pia nitahusianisha na suala la ngono ambalo linaungana pia na suala la UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, hapo unanipoteza unaponyanyua nyanyua *microphone*, naona kama unataka unikatishe. Naomba sana tafadhali.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Dakika moja, malizia. Dakika moja malizia.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika, dakika moja.

Mheshimiwa Spika, wako wanaume ambao hawataki kufanya tohara na kwa misingi hiyo wanataka kuwaingilia wanawake kwa maana ya kuwapa huduma hiyo bila kufanya tohara. Sasa mimi nitoe wito kwa Watanzania wote wanawake wenzangu kwamba suala la mwanaume

ambaye hajafanya tohara kushirikiana naye ni hatari kwa afya yako na niseme tu kwamba inasababisha saratani ya shingo ya kizazi. Kwa hiyo, haifai kabisa kwa matumizi ya binadamu na wakatae kutoa huduma hiyo endapo kama atamkuta mwanaume hajafanyiwa tohara kwa sababu inasababisha saratani ya shingo ya kizazi. Ahsante sana. (Makofi/Kicheko)

SPIKA: Eeh, huu unaitwa mtihani.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. MARTHA N. GWAU: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ukatili kwa wadada wa majumbani ambao wamekuwa wakisaidia familia nyingi majumbani maarufu kama *house girl*; ni muhimu kuweka mkazo na kutoa elimu kwa jamii hususani kwa familia ambazo zinawachukulia wadada wa kazi kama watumwa na kuwatumikisha kinyume na utaratibu na maelewano.

Mambo kadhaa ambayo wanapitia na kuwa yanahitaji kuangaliwa kwa ukaribu ni kama ifuatavyo; kwanza ni mishahara yao ilipwe kwa wakati na kiwango kiwe elekezi ili kusaidia wadada wa majumbani wapate haki zao; pili muda wa ufanyaji kazi na kupata hata siku moja ya mapumziko tofauti na sasa kuna baadhi ya familia wanawafanyisha kazi siku saba za wiki na bila mapumziko.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Maafisa Maendeleo ya Jamii wakawaelemisha wadada wa majumbani kuhusu haki zao za msingi na ni wapi wakaripoteni endapo watapata kunyanyaswa na waajiri wao na hasa suala la ukatili kwa kutaka kulazimishwa na baba tendo la ndoa kwa madai asipokubali atafukuzwa kazi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naomba kuwasilisha.

MHE. ZUENA A. BUSHIRI: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inavyoongozwa na Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan; nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia kuhusu wanawake wanaovyonyanyasika kwa kutelekezwa na waume wao; kumekuwa na tabia ya wanaume kutelekeza wake zao na watoto na kusababisha watoto kukosa haki zao za msingi kama elimu, chakula, malazi na mapenzi ya wazazi wao wote. Wanawake wanaotelekezwa kwanza wanaathirika kisaikolojia na kusababisha hata kukosa malezi bora. Niishauri Serikali kutunga sheria kali ili kudhibiti hali hii.

Mheshimiwa Spika, nichangie pia kuhusu suala la nyumba za kulelea wazee nchini. Tunao wazee wengi sana ombaomba ambao hawana uwezo katika Taifa letu, wazee hawa wengine hawana nyumba bora za kuishi wengine hawana chakula, nguo na kadhalika. Niiombe Serikali kwanza ihakikishe kila mkoa kunakuwa na nyumba za kulelea wazee za kutosha kulingana na idadi ya wazee waliopo katika mkoa husika ili kuwasaidia wazee ambao wanahitaji kulelewa.

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa kuchangia suala la ukatili kwa wanawake na watoto. Kumekuwa na wimbi kubwa la wanaume kupiga wake zao na watoto hata kupelekea kupata ulemavu, niiombe Serikali itunge sheria kali ili kudhibiti ukatili huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja.

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya. Pia nimpongeze Waziri Mheshimiwa Dorothy Gwajima pamoja na timu yake kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa wayumshi katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Mandeleo ya Jamii ya Ufundi

husususan Mabughai, Lushoto na Misungwi, Mwanza; vyuo vya ufundi na vyuo vya maendeleo ya jamii, Uyole, Buhare na vingine hauoni uhaba huo unapelekea vyuo kutumia fedha nyingi kwa kutumia wakufunzi wa muda na hata kurundikana kwa masomo. Mwalimu mmoja anahudumia wanafunzi zaidi ya 100 jambo hili linashushia hadhi ya utoaji wa mafunzo.

Mheshimiwa Spika, kwa nini watumishi wengi wanavikimbia vyuo vya maendeleo ya jamii badala ya kuvikimbilia kufanya kazi, sababu watumishi wetu hufuata maslahi vyuo vingine ama taasisi nyingine. Pia miundombinu chakavu na hali duni ya vifaa vya karakana na maabara na hata uchakavu wa vyombo vya usafiri, kwa mfano magari yote ni ya tangu mwaka 2009.

Pia kuna uhaba wa hosteli vyuoni; kwa kuwa vyuo vya maendeleo ya jamii na watoto havina hosteli, niombe Serikali itenge fedha za kutosha ili vyuo vyetu vijengewe hosteli ili watoto wetu wajisikie kuwepo kwenye vyuo kwa ustawi wao na kuwalinda na unyanyasaji na endapo watakaa mtaani hawatatimiza ndoto zao.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na unyanyasaji wa kijinsia katika maeneo yetu ya kazi, hii imefikia hatua mbaya zaidi mpaka kupelekea wananchi kuwalinda wahalifu hao. Niishauri Serikali itenge dawati la kutoa elimu ya mambo mabaya kama haya ili kuonesha kabisa tabia hii iliyokithiri hasa mijini.

Pia kuna haja ya kuangalia *pension* za wazee hawa hasa kwa wale ambao hawana uwezo wa kufanya kazi na pia kuna hawa walemavu hasa wanaoishi vijijini kwani walemavu hawa hawafikiwi na huduma yoyote inayowahusu wao, badala yake huduma hii huishia kwa walemavu waishio mijini tu.

Mheshimiwa Spika, niombe Serikali iwape usafiri Maafisa Ustawi wa Jamii ili waweze kuwafikia walemavu hawa wanaoishi vijijini, kwani nao wana haki kama hawa wenzao wanaoishi mijini.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali iongeze fedha kwenye Wizara hii ili iweze kutimiza malengo yake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. GHATI Z. CHOMETE: Mheshimiwa Spika, naipongeze sana Wizara kwa juhudi kubwa iliyoanza nayo tangu imeanzishwa.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia kwa kuigawa Wizara hii ili kuwafikia wananchi kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuishauri Serikali katika kundi hili la mabinti walemavu na mabinti walemavu wanaofichwa na wazazi wao kwa kudhania kuwa ulemavu ule hawezi kupata elimu wala kufanya kazi yoyote.

Mheshimiwa Spika, niombe tutoe elimu kwa jamii ili itambue kuwa watoto hao wanaweza kusoma na kuisaidia jamii yao. Lakini pia wanawake walemavu watambuliwe kwa idadi yao kupitia Kata, Wilaya mpaka Mkoa ili wawezeshwe kwa kupatiwa miradi rafiki kwao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ndoa za utotoni, kumekuwa na ndoa za utotoni sana katika jamii yetu, naishauri Serikali itenge fedha kwa ajili ya kutoa elimu inayohusu madhara ya ndoa za utotoni na kushirikiana na mashirika yanayotoa elimu na yanayopinga ndoa za utotoni kwa mfano kule Mkoani Mara Shirika kama Masanga, *Hope for Girls* yamekuwa ni mashirika yanayotoa elimu inayohusu madhara ya ndoa za utotoni ili Taifa letu liwe na vijana wenye elimu na afya njema.

Mwisho naishauri Serikali kuviboresha Vyuo vya Maendeleo ya Jamii kama vile Chuo cha Buhare kilichopo mkoani Mara na vingine vingi nchini ili viendeleo kufanya vizuri zaidi.

MHE. ESTHER E. MALLEKO: Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza nichukue nichukue nafasi hii kumpongeza sana Rais Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuitenganisha Wizara hii na Wizara ya Afya, hakika ameitendea haki ili iweze kusimamia maendeleo ya jamii, kwa kuwa Wizara hii imebeba mwanga wa vizazi vyetu kwa maana jinsia wazee, watoto, na makundi maalum ndio ukamilifu wa maisha ya mwanadamu.

Mheshimiwa Spika, tukielekea kupitisha bajeti hii muhimu ni ukweli usiopingika nchi yetu imepitia vipindi kadhaa vya udhalilishaji wa kijinsia hasa kwa na watoto katika maeneo mbalimbali. Kiukweli katika dunia ya sasa watu wameshabadilika kutoka kwenye dhana ya unyanyasaji wa kijinsia, badala yake wanapigania kuyakuza makundi mbalimbali kwa kuyaongezea nguvu na uwezo hasa wanawake na watoto.

Mheshimiwa Spika, tafiti za hivi karibuni zilizotolewa na Jeshi la Polisi nchini ambao ni chombo kinachohusika kupokea matukio mengi ya unyanyasaji wa kijinsia inaeleza kuwa mpaka Juni, 2021 tayari watu 15,131 walikuwa wamefanyiwa ukatili wa kijinsia hasa wanawake waliouawa katika ndoa. Pia ripoti iliyotolewa Septemba, 2021 na Jarida la Afrika kuhusu hali ya ukatili wa kijinsia Tanzania imeonesha kuwa asilimia 46 ya wanandoa hufanyiwa ukatili wa kimwili na asilimia 32 walifanyiwa ukatili wa kisaikolojia na asilimia 13 wanafanyiwa ukatili wa kingono.

Mheshimiwa Spika, Mungu ameliwezesha Taifa letu kwa kulionesha kuwa mwanamke anaweza kufanya mambo makubwa yanayobeba na kuiheshimisha jamii kwa kutupa Rais mwanamke Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ambaye anatupa tafsiri kuwa mwanamke sio kiumbe anayestahili kunyanyaswa, bali anastahili kuungwa mkono na kufunguliwa milango ya fursa. Sasa inasikitisha sana kuona namna Taifa letu linavyojipambanua juu ya kuheshimu nafasi ya mwanamke na haki za Watoto, lakini jamii zetu zimekuwa kimya juu ya ukatili huu unaojitokeza.

Mheshimiwa Spika, sasa Wizara ihakikishe inaimarisha uelewa wa Watanzania juu ya kulinda haki za watoto na wanawake kila mahala sambamba na kuwawezesha wanawake na watoto kuweza kujitambua. Kuwe na madawati katika shule za msingi na sekondari yawepo kusaidia watoto hawa kutoa taarifa kwenye mazingira rafiki maana wengine wanaogopa kwenda polisi kwa hofu.

MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO: Mheshimiwa Spika, wanaaikolojia hueleza maana ya maisha kuwa ni mchakato wa binadamu na jamii yake kusaka na kutunza furaha, yaani tunafanya mambo yote haya ya maendeleo katika nyanja zake zote ili hatimaye tupate furaha kama mtu mmoja mmoja, jamii na hatimaye Taifa. Kiwango cha furaha katika nchi ni kigezo na kiashiria muhimu sana katika kupima ubora wa maisha katika jamii na nchi husika. Ni kwa sababu hii kila mwaka hutolewa taarifa ya dunia kuhusu kiwango cha furaha katika kila nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya mwaka 2022 iliyotolewa na taasisi inayojihusisha na kupima kiwango cha furaha duniani ya *Gallup World Poll* wastani wa kiwango cha furaha katika nchi yetu kilikuwa ni 3.623 (kiwango cha juu ni 10.0), tukiwa ni miongoni mwa nchi kumi duniani ambazo watu wake wanaonesha kiwango cha chini cha furaha. Nchi zngine ni Burundi (3.775), Yemen (3.658), Tanzania (3.623), Haiti (3.615), Malawi (3.6), Lesotho (3.512), Botswana (3.467), Rwanda (3.415), Zimbabwe (3.145) na Afghanistan (2.523). Taarifa hii inapatikana <https://dmerharyana.org/world-happiness-index/>

Mheshimiwa Spika, ukisoma majukumu ya jumla ya Wizara hii utaona kuwa jukumu la msingi la Wizara hii ni *kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya kuleta furaha na kuamsha matumaini kwa jamii na kwa mtu mmoja mmoja*. Na mimi katika mchango wangu ninataka nichangie maeneo mawili ambayo ninashauri Wizara ichukue hatua kadhaa za kiseru na kisheria katika kuleta furaha kwa jamii yetu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Kuhusu haja ya kinga jamii wa wazee; kwa kuzingatia makadirio ya idadi ya watu (*population projections*) ya NBS, Tanzania inakadiriwa kuwa na watu 61,280,743 na inatarajiwa kuwa na watu 67,036,280 ifikapo mwaka 2025. Kati ya idadi hii ya watu, wazee[1] ni watu 2,801,541 kwa mwaka 2022 (*sawa na asilimia 4.6*) na inatarajiwa kuwa 3,038,267 mwaka 2025. Hawa ni Watanzania ambao kwa nyakati tofauti waliwahi kuitumikia nchi yetu ama katika nafasi za kuajiriwa au kujajiri au katika mashamba huko vijijini.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha pia kwamba katika nchi yetu *zaidi ya asilimia 80* ya wazee wanaishi vijijini na wakiwa huko wanalazimika kufanya kazi zozote ili waendeleo kuishi. Wengi wao hawana msaada. Aidha, takwimu zinaonesha kuwa wazee ndio wanaotunza watoto yatima; asilimia 40 ya watoto yatima Tanzania wanatunzwa na wazee ambao nao wanahitaji kutunzwa.

Mheshimiwa Spika, takwimu nyingine muhimu ni kwamba ni *asilimia 6.5* pekee ya wazee nchini Tanzania ndio wanaopokea malipo ya uzeeni (pensheni). Wazee walio wengi hawana msaada hasa kufuatia kuanza kuvunjika kwa mfumo wa familia jamii (*extended family*) kwenda katika mfumo familia ya kibaolojia (*nuclear family*). Aidha, tafiti zinaonesha kuwa kiwango cha umaskini kwa kaya zenye wazee nchini kipo juu kwa *asilimia 22.4* zaidi ya wastani wa kitaifa!

Kutokana hali yao, wazee wengi wanakabiliwa na ukosefu wa usalama wa kifedha, wapo katika hatari zaidi ya kuugua magonjwa sugu, na wanakabiliwa na upweke.

Mheshimiwa Spika, nini kifanyike? Ninapendekeza tutekeleze kinga jamii (*social protection for all*). Mwaka 2010 Serikali ilifanya utafiti mzuri sana unaoitwa *Achieving income security in old age for all Tanzanians: a study into the feasibility of a universal social pension*. Pamoja na mambo mengine, utafiti ulipendekeza kulipa wazee kinga ya jamii kwa kiwango cha shilingi 16,586. Kwa bei ya leo hii inaweza ikawa sawa na *shilingi 28,586*. Kwa idadi niliyoeleza hapo juu hii ni sawa

na shilingi bilioni 80 kwa mwezi sawa na shilingi bilioni 961 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, nini faida ya kinga jamii kwa wazee? Katika mpango wetu wa maendeleo wa tatu wa miaka mitano (2021/22-2025/26), pamoja na mambo mengine, tumejijwekea lengo kuwa ifikapo mwaka 2025/2026 tuwe tumepunguza idadi ya watu maskini (wanaoishi chini ya mstari wa umaskini) kutoka *watu milioni 26.4 mwaka 2020/2021 hadi watu milioni 20.2 mwaka 2025/2026*. Lengo hili sio dogo kwa kuzingatia kuwa pamoja na kwamba uchumi uliendelea kukua vizuri hadi kufikia hatua ya uchumi wa kati wa chini, ukuaji huu haukwenda sambamba na kupungua kwa idadi ya watu maskini. Ukweli ni kwamba idadi ya watu maskini iliongezeka kwa watu takribani milioni mbili katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, faida za hatua ya kutoa kinga ya jamii kwa wote ni kubwa. Ukiacha kuongeza furaha kwa wazee wetu hawa, tafiti zinaonesha kuwa hatua hii itapunguza kiwango cha umaskini miongoni mwa wazee kwa asilimia 57.9. Aidha, hatua hii itasababisha kuwaondoa *watu zaidi ya milioni 1.5 katika wimbi la umaskini wa kutupa*. Kwa maneno mengine, hatua hii itasaidia sana katika kufikia malengo tuliojiwekea katika mpango wetu wa maendelea katika kupunguza idadi ya watu maskini. Tayari nchi nyingi zimechukua hatua hii na matunda yanaonekana. Nchi jirani ya Kenya walitumia taarifa yetu ya utafiti na sasa wanatekeleza mpango huu. Nchi zingine Afrika ni pamoja na Mauritius, Lesotho, Afrika Kusini, Eswatini, Zambia, na Uganda wapo katika majaribio.

Mheshimiwa Spika, haja ya kuondoa zuio la kutafuta furaha wakati wa asubuhi na mchana; juzi nikiwa Dar es Salaam nilipata malalamiko kutoka kwa mmoja wapiga kura wangu kutika katika Kata ya Makubiri. Mpiga kura huyu ni daktari wa binadamu anayefanya kazi katika kitengo cha *mortuary* katika moja ya hospitali za Serikali katika Mkoa wa Dar es Salaam. Mara nyingi huingia usiku na kutoka asubuhi. Kwa utaratibu aliojiwekea, kila anapotoka asubuhi

hupitia baa iliyopo karibu na nyumbani kwake na kunywa bia sita kabla hajaenda nyumbani kulala. Alilalamika kuwa kila anapopita baa na kunywa hukamatwa na askari na huachiwa baada ya "mazungumzo". Aidha, mwenye baa pia hukamatwa na kuachiwa katika mazingira hayo hayo.

Mheshimiwa Spika, siku ya Ijumaa tarehe 20 Mei, 2022 nilikutana na wafanyabiashara zaidi ya 200 kutoka katika Jimbo la Ubungo kwa lengo la kusikiliza kero na ushauri na kupokea maagizo yao kuhusu mambo ambayo wangependa niyawakilishe hapa Bungeni. Moja ya malalamiko makubwa yanafanana na ya daktari niliyemwelezea hapo juu kwamba wafanyabiashara katika jiji la biashara wanazuiwa kufungua biashara asubuhi na kuzuiwa kufanya biashara baada ya saa sita usiku! Baada ya kufuatilia na kuzungumza na baadhi ya Maafisa Biashara na maaskari wanaosimamia utaratibu huu, nimebaini kuwa tunayo Sheria ya Vileo (*The Intoxicating Liquors Act, 1968*) ya mwaka 1968. Katika kifungu cha 14, sheria imeweka muda wa kuuza vileo ambapo ni kuanzia saa sita mchana hadi saa sita usiku kwa siku za kazi. Ni wazi kuwa sheria hii imepitwa na wakati ukizingatia kuwa ilitungwa mwaka mmoja baada ya kutangazwa kwa Azimio la Arusha na wakati huo nchi ikijulikana kuwa ni nchi ya wakulima na wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, sasa ni muhimu sheria hii na zingine zinazopangia watu muda wa kufurahi ziangaliwe. Kawaida majiji duniani kote huwa yanafanya kazi saa ishirini na nne na kuna watu ambao wanafanya kazi usiku na kupumzika mchana. Tunaweza kuzipa mamlaka za Serikali za Mitaa zikatunga sheria ndogo kutokana na mazingira yao kulikoni kuendelea kuwa na sheria moja ambayo inakwaza sana biashara na kuondoa furaha za watu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003, dhana 'mzee' hutafisiriwa kwa kuzingatia umri mkubwa, majukumu aliyonayo na hadhi ya mtu katika jamii. Katika maoni yangu haya ninazingatia umri wa mtu ambapo kwa mujibu wa sera hii mzee ni mtu yeyote mwenye umri wa miaka 60 na kuendelea. Kigezo kikubwa ni

kwamba katika umri huu binadamu huanza kupungukiwa nguvu za kufanya kazi.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Spika, naungana na Watanzania wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa baraka kwa kuijalia nchi yetu amani, utulivu, mshikamano, ustawi wa jamii na kutuepusha na majanga mbalimbali yanayotokea mara kwa kote duniani.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kwa niaba ya wananchi wote wa Jimbo la Mbulu Mjini kutoa pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan - Rais wetu mpendwa kwa jinsi anavyoiongoza nchi yetu na kusimamia utekelezaji wa Ilani ya CCM 2020 – 2025.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Wizara hii, Naibu Waziri wa Wizara, Mheshimiwa Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa jinsi mnavyoitendea haki Wizara hii kwanza kwa kutusikiliza sisi wawakilishi wa wananchi na kutatua changamoto mbalimbali tunazowasilisha kwenu, hongereni sana na Mungu awabariki.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naungana na viongozi wenzangu kutoa pole nyingi kwa familia zilizopata misiba mbalimbali ya kuwapoteza wapendwa wao kuanzia kwa viongozi wote, watendaji na Watanzania wote Mwenyezi Mungu atujalie hali ya ustahimilivu katika kipindi hiki, sote kwa pamoja tunaziombea roho zao kwenye ufalme wa mbinguni usio na mwisho.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa mchango wangu kupitia mapendekezo ya hotuba ya Wizara hii na taarifa ya Kamati yetu ya Bunge; kwanza tunaipongeza Serikali yetu kwa kutoa fedha za ndani kwa ajili mipango ya maendeleo. Hata hivyo kwa kuwa Wizara hii mpya tunaiomba sana Serikali iongeze bajeti ya Wizara hii kwa kuwa ina mahitaji makubwa ya miundombinu, watumishi na

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

vitendea kazi mbalimbali na kuendelea kutumia utashi wa kushawishi kupata fedha za nje kwa wadau.

Pili, kwa kuwa Wizara imeundwa kuna umuhimu mkubwa sana kufanya mapitio ya sheria zilizoko na mpya ili kusimamia na kuwezesha utendaji wa Wizara yetu kukabiliana na masuala mbalimbali kama vile wingi wa watoto wa mitaani na ndoa zinazotelekezwa na haki za mirathi na wajane.

Mheshimiwa Spika, tatu, Serikali iwaelekeze asasi za kiraia wapitishie mipango kazi yao kwenye vikao vya Mabaraza ya Madiwani, *DCC* na *RCC* kwa ajili ya kupata vipaumbele na kufanikisha mahitaji muhimu na mtambuka katika maeneo hayo.

Aidha, Wizara iandae mafunzo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii kwa ngazi za Kata na Wilaya katika ratiba zake kila mwaka. Pia Serikali iangalie uanzishwaji wa Mabaraza ya Wazee kwa ngazi ya Mkoa, Wilaya, Kata na Vijiji kurahisisha uratibu wa matatizo na changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naunga hoja mkono asilimoa mia moja na naomba kuwasilisha.

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu Dkt. Dorothy Gwajima na Naibu wake Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, wazee ni amana na utajiri wa jamii; wazee ni wadau wa kwanza walio Shirikiana na Mwenyezi Mungu katika kazi ya uumbaji. Wazee ni wadau muhimu wa malezi na makuzi ya watoto na vijana na Taifa letu kwa ujumla. Wazee ni watunzaji wa mapokeo hai na wanayo misingi ya jamii na mambo wanayopaswa kuwarithisha vijana.

Mheshimiwa Spika, wazee ni walezi kwa watoto na vijana; wazee ni urithi, amana na utajiri kwa jamii kwani uzoefu na busara zao ni ushuhuda wa kinabii kwa siku hizi.

Mheshimiwa Spika, wazee ni sehemu muhimu sana kwa jamii yoyote ile. Uzoefu na busara za wazee ni kiungo na hamasa kwa maisha ya wanajamii.

Mheshimiwa Spika, wazee wa Kitanzania wamelitumikia Taifa kwa muda mrefu tena kwa namna mbalimbali ikiwemo kuwaletea na kuhakikisha wanapata mafanikio ambayo tunajivunia sasa. Tanapaswa tutambue kwamba wazee hao wamelitumikia Taifa kwa muda mrefu. Tena wamechangia mafanikio makubwa ambayo Tanzania inajivua kwa wakati huu!

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto mbalimbali za maisha ya uzeeni bado wazee wa Tanzania wana nafasi na mchango mkubwa kwa ustawi wa jamii. Wazee ni alama ya utimilifu wa maisha ya mtu na jamii katika ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, Tanzania ilikuwa na jumla ya watu 44,929,002 ambapo wazee walikuwa 2,507,508 (ambapo wanawake walikuwa 1,307,358 na wanaume 1,200,210) sawa na asilimia 5.6%. Kwa idadi hii Tanzania ina wazee wachache.

Mheshimiwa Spika, sababu za uchache wa wazee katika jamii yetu ni kama zifuatazo; hapa nchini Tanzania katika maeneo mengi hasa yale ya vijijini, uzee umeambatana na umaskini, magonjwa na unyanyapaa unaohusishwa na uchawi. Vitu hivi vimekuwa ni sababu ya kuwatenga na kuwakosea heshima wazee katika baadhi ya jamii zetu za Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, wazee wa Tanzania wanakabiliwa na changamoto mbalimbali, ikiwemo; wengi wanakabiliwa na umaskini wa hali na kipato vijijini na mijini, na baadhi hukosa hata fedha za kununua chakula; wazee katika umri

wao, wengi wao wanakumbana na changamoto za magonjwa ya wazee (tezi dume, kisukari, kansa ya kizazi na aina nyinginezo za kansa, shinikizo la damu); upatikanaji duni wa madawa na vifaa tiba kwa wazee na wanapokumbana na changamoto hizi na kukosa msaada, wazee huishia kuuza rasilimali zao kama mashamba na nyumba ili kupata huduma muhimu ambazo hawana uwezo kuzigharamia.

Mheshimiwa Spika, pia baadhi yao kutelekezwa na jamii inayowazunguka na mauaji ya kikatili kwa kisingizio cha imani za kishirikina.

Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa wazee pamoja na uchache wao, kunaashiria uhitaji wa ongezeko la huduma mbalimbali kwa wazee. Kutokana na ukweli huu, tunahitaji kuzingatia sana jinsi nchi yetu itakavyoshughulikia matatizo ya watu wetu kuzeeka.

Mheshimiwa Spika, hii ni kutokana na ukweli kwamba hata muumba wetu alionesha kuwajali wazee na hata dini zetu mbili kubwa hapa nchini za uislamu na ukristo zinatuelekeza kuwapenda, kuwajali na kuwatunza wazee.

Mheshimiwa Spika, wajibu wa kuwahudumia au kuwasaidia wazee ni wa kila mmoja. Tuna jukumu kama Taifa au kila mmoja wetu katika jamii kuwashukuru, kuwaenzi na kuwabariki wazee kutokana na mchango wao katika ustawi wa Taifa letu. Hii ni pamoja na kuwapatia kipato kila mwisho wa mwezi ili wewezi kujikimu.

Mheshimiwa Spika, jambo kama hili linafanyika huko Zanzibar na nchi nyingine Kusini mwa Jangwa la Sahara kama vile Botswana, Lesotho, Mauritius, Namibia, Seychelles, *South Africa* na Swaziland. Mataifa haya yamefanikiwa kuwapatia wazee wao pensheni, na nchi nyingine kama Kenya, Uganda na Zambia ziko kwenye mchakato.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali isikwepe jukumu la kuwatunza wazee kwa sababu nguvu zao za uzalishaji mali zimepungua kutokana na kazi waliyoifanya wakiwa vijana

kwa ajili ya maendeleo na ustawi wa familia zao na Taifa kwa ujumla. Tunao wajibu wa kuwajali wazee wetu kwa hali na mali ikiwa ni sehemu ya matunda ya uwajibikaji wao kwetu na kwa Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, hivyo, ninatoa ushauri ufuatao kwa Serikali; kwanza, Serikali iboreshe Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003 kwa kushirikiana na wadau; sheria inayosimamia masuala yote ya wazee iaandaliwe na kuanza kutumika mara moja; kama ilivyo kwa makundi yote maalumu (vijana, walemavu na akina mama), wazee wapatiwe nafasi za uwakilishi kutetea maslahi yao katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ianze mchakato wa kuwalipa *pension* wazee wetu ambao hawana msaada wa aina yoyote ule wa kipato. Jambo hili jema na lenye baraka linatekelezwa huko Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, pia wazee wapatiwe bima ya afya inayoweza kupambana na changamoto zote za kupambana na magonjwa ya uzeeni ili wazee wafaidi huduma hizo kama ilivyokusudiwa kwenye sera wa kuwapatia huduma za afya ya mwaka 2007; Serikali ihakikishe mafao ya wastaafu yanalipwa kwa wakati ili kuwaondolea wazee usumbufu wa kufuatilia; Serikali na wananchi wote kwa ujumla kulinda na kutetea haki za wazee, ikiwemo kuthamini mchango, uzoefu na ushiriki wao kwa maendeleo ya Taifa; Serikali iendelee kutekeleza mkakati wa Kitaifa wa kutokomeza mauaji ya wazee na kuhakikisha wazee wanalindwa dhidi ya ubaguzi, uonevu, ukatili na mila potofu na wasiokuwa na msaada, Serikali na wadau mbalimbali waangalie jinsi ya kuwasaidia wale wasiokuwa na makazi, tiba na msaada wa mahitaji ya msingi.

Mheshimiwa Spika, nchini Tanzania kuna Sera ya Wazee iliyotungwa mwaka 2003 lakini hadi sasa haijatumwa sheria ya kusimamia utekelezaji wa sera hiyo. Sheria ya kuwalinda wazee ndio itakuwa muarobaoni wa changamoto za maisha wanazokabiliana nayo hasa ya kiuchumi na afya kwani wanapoishiwa nguvu za uzalishaji, hukosa mahitaji ya msingi anayostahili binadamu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, licha ya Tanzania kuwa na sera ya Taifa inayotaka wazee wasiojiweza kupatiwa matibabu bure, lakini utekelezaji wake bado ni wa kiwango cha chini na baadhi ya maeneo, wazee wamelazimika kuingia mifukoni kwa ajili ya kununua dawa. Wengi ya wazee hao wanasema Sera ya Taifa ya mwaka 2007 inayofungua milango kwa wazee wasiojiweza kupatiwa matibabu bure haitekelezwi ipasavyo na kwamba baadhi ya Waganga Wafawidhi wa Mikoa na hata wale wa Wilaya wamekuwa wakiwatoza fedha licha ya sera hiyo kueleza bayana.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutunga Sheria ya Masuala ya Wazee Na. 2 ya mwaka 2000; kuweka utaratibu wa kuwapatia pensheni jamii na vitambulisho vya kupatiwa huduma mbalimbali wazee wenye umri wa kuanzia miaka 70.

Mheshimiwa Spika, hapa kwetu Tanzania wazee ni utajiri, hatutakiwi kuwatenga wala kuwadharau bali wanabaki kama miamba na walezi wakuu wa mila, desturi na tamaduni njema katika jamii yetu. Katika harakati za kupigania Uhuru wa Taifa letu, Mwalimu Nyerere alielekezwa na wazee mbinu za kutumia na hatimaye tukapata uhuru. Kutokana na umuhimu wa wazee, hata Maraisi wa awamu zote zilizopita wakiwa na jambo huwaita wazee na kuteta nao. Pamoja na umuhimu wao, inasikitisha kuona kwamba wazee hawajaangaliwa kama kundi maalumu kwenye Taifa letu na wanasahauliwa katika maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango - Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa - Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya

Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Serikali katika utekelezaji wa sera ya maendeleo ya jamii ikienda sambamba na ustawi wa jamii na maendeleo endelevu, na hii ni mojawapo ya nguzo kuu katika utayari wetu wa ushindani wa kimataifa (*national competitiveness*). Bajeti hii inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 ambayo ni kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Spika, Shule ya Maadilisho ilianzishwa mwaka 1972 baada ya Serikali kubadili matumizi ya miundombinu iliyokuwepo kutoka Kikosi cha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na kuwa shule ya kulelea/kuadili vijana watukutu wanaolazimika kutengwa na jamii kufuatia vijana husika kufanya makosa mbalimbali katika jamii. Kwa sasa shule bado ina vijana wachache chini ya 30 ambao wanalelewa/kuangaliwa/kuadiliwa wakiwa chini ya uangalizi wa wafanyakazi 16. Majengo mbalimbali pamoja na yale ya shule ya msingi yaliyopo hapo hayatumiki kikamilifu. Kwa upande wa shule ya msingi, idadi ya wanafunzi ni 102 ukilinganisha na uwezo wa shule hiyo wa zaidi ya wananafunzi 350. Pamoja na miundombinu mbalimbali zipo ekari zaidi ya 448 ambazo zinaweza kutumika kwa ajili ya shughuli za mafunzo ya kilimo na pia kukipatia chuo mahitaji yake ya msingi ya chakula na shughuli nyingine za maendeleo. Kutokana na mabadiliko ya kijamii kuna umuhimu mkubwa wa kuboresha matumizi ya hii shule kuwa Chuo cha Maendeleo ya Jamii na ufundi na pia eneo la Kituo cha Afya.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali kuboresha matumizi ya Shule ya Maadilisho iliyopo Irambo, Kata ya Ulenje, Wilaya ya Mbeya kuwa eneo maalum ili kuanzisha mafunzo ya maendeleo ya jamii, ufundi na hivyo kuiwezesha nchi kutumia nguvu kazi na rasilimali ya vijana kikamilifu na kwa ajili ya maendeleo ya jamii na uchumi wa nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa shule hii ya sasa, eneo hili liwe kwa ajili ya Shule na Chuo cha Ufundi na Maendeleo ya Jamii pamoja na jamii yote ya Kata ya Ulenje na Tanzania yote.

Mheshimiwa Spika, ombi hili limejikita katika ukweli kwamba kwa kutoa elimu ya maendeleo ya jamii na ufundi kwa vijana, Tanzania itakuwa inaongeza ajira na pia ueledi kwa vijana katika kujenga nchi hasa kutokana na ukweli kwamba nguvu kazi kubwa iko katika vijana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MAIMUNA S. MTANDA: Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iangalie na kufuatilia ili kulinda afya ya watoto wadogo wanaokwenda kwenye vituo vya kulelea watoto wadogo. Wapo baadhi ya wamiliki wa vituo hivyo ambao wamepata vibali isivyo halali kwani nimeshudia watoto wakirundikwa kwenye vyumba visivyokidhi haja kiafya wakati wa mchana wanaposubiri wazazi kuwafuata. Wanarundikwa kwenye vigodoro, wanalazwa kama samaki. Fuatilieni vituo hivyo hususani mkoa wa Dar es Salaam, hali si rafiki.

Mheshimiwa Spika, watoto hawa wengi ni kati ya mwaka mmoja hadi miaka minne, lakini cha kushangaza vituo hivyo vinachanganywa na watoto wa umri wa miaka mitano hadi sita wanaotakiwa wawe *pre-school*. Matokeo yake ni watoto wadogo wanaweza kulawitiwa na hawa watoto wenye umri usiotakiwa kuwa kwenye hivi vituo vya kulelea watoto. Tunaomba Maafisa Ustawi wa Wilaya wafuatilie na kukagua kwa kushtukiza vituo hivi.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima (Mb), Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum; na pongezi kwa Naibu Waziri Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis (Mb). Pia nampongeza Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu 10% inayotolewa na Halmashauri kwa ajili ya mkopo, nashauri ipatikane *system* maalum itakayohusika kusimamia vizuri ukopeshaji na ukusanyaji wa madeni kama ilivyo kwa mabenzi. Pia vituo vya ushauri nasaha hakuna. Serikali ifungue dirisha maalum *either* kwenye vituo vya afya au ofisi za kata ili kusaidiwa. Familia nyingi zina changamoto za kifamilia, zinaumwa lakini hazina pa kukimbilia (*counselling centres*).

Mheshimiwa Spika, uhamasishaji wa maendeleo ya jamii upewe mwongozo maalum na wafanye mikutano ya hamasiki mara kwa mara. Pia umeanza unyanyapaaji wa wazee hata kuwasemasema bila heshima.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa fursa ya kuchangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, ushauri kuhusu uanzishaji wa Madawati ya Jinsia katika Taasisi za Vyuo Vikuu na Vyuo vya Kati, niipongeza Serikali kwa kuanzisha madawati haya. Mwongozo huu utasaidia wanafunzi kupata ushauri na pia inaweza ikawanusuru changamoto za msongo wa mawazo, kuu na kujua, rushwa ya ngono na masuala mengine ya ukatili. Ushauri wangu mwongozo huu uwe *popularized* katika vyuo vyote. Pia wanavyuo wote wafahamishwe kuhusu mwongozo huu. Pia Serikali iongeze bajeti ya maendeleo Fungu 53 katika pesa ya maendeleo ili kuleta ufanisi.

Mheshimiwa Spika, ushauri kuhusu ukatili kwa watoto; watoto wafundishwe kutoa taarifa na wasiogope vitisho wanapofanyiwa ukatili watoe taarifa, pia wazazi/walezi wawe wanakagua watoto wao kuona kama wamefanyiwa ukatili na kuchukua hatua za mapema.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja.

SPIKA: Mheshimiwa Selamani Jafo kwa dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri Mwanaidi Ali Khamis. Mtoa Hoja ajandae.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, kwanza awali ya yote nami naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayofanya, lakini nimpongeze sana dada yangu Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima kwa kazi kubwa aliyoifanya pamoja na Naibu wake shemeji yangu hapa Mheshimiwa Mwanaidi Khamisi, kwa kweli Wizara hii wanaitendea haki.

Mheshimiwa Spika, yangu mimi ni machache tu; kwanza kifupi tu kabla sijakuja katika hoja ya ufafanuzi naomba Wabunge tuungane kwa pamoja wa pande zote, wanaume na wanawake, katika kuisaidia hii Wizara kwa sababu naona kuna mambo ya msingi mengi sana na yanataka ushirikiano wa kila mmoja wetu, sio kazi ya Wizara peke yake.

Ni jambo la kila mmoja, aidha mwanamke ama mwanaume, kuisaidia jamii yetu kwa hiyo, tunakazi kubwa sana kuisaidia nchi yetu na dada yangu Mheshimiwa Gwajima naomba nikwambie, sisi wote tutakupa ushirikiano na timu yako ilimradi kazi ya wananchi iweze kufikiwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, nilitaka nitoe ufafanuzi wa jambo moja tu hapa, kaka yangu Mheshimiwa Profesa Shukrani hapa alizungumza suala zima la kelele na mitetemo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli, jambo hili limeleta kero maeneo mengi na tumezungumza athari zake mwaka jana tulipokutana takribani Mawaziri tusiopungua nane. Leo hii kuna watu wengine ambao wana magonjwa ya *pressure* wanapoteza maisha kwa ajili ya kelele za muziki katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya taarifa za kiafya zinasema kuna watoto wengine wanakuwa viziwi kabisa, hawawezi kusikia kwa ajili ya kelele, lakini kwa bahati mbaya nyingine kuna watu wengine wametafuta ujauzito kwa nguvu kubwa sana, lakini mwisho wa siku ujauzito unapotea kwa ajili ya kelele na mitetemo. Bahati mbaya sana jambo hili tumelipigia kelele wakati wote na hata ninyi wengine mnafahamu, wote humu ni watu wazima, hata watu wengine *network* hazifanyi kazi vizuri kwa ajili ya kelele na mitetemo, tulilizungumza hili wazi tukasema hivi ilimradi watu waelewe nini madhara ya kelele na mitetemo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaamini watu kwa ujumla ni kwamba tutaungana pamoja. Kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004, Sura Namba 191 ambapo kifungu cha 230(2) na Kanuni zake za Januari, 2015, tumetoa maelekezo jinsi gani jambo hili sasa tuweze kulirekebisha.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2020 takwimu zinaonesha kwamba taarifa ziliripotiwa za maeneo sumbufu zaidi ni 840. Mwaka 2021 tulikuwa na taarifa rasmi 450 na mwaka huu toka mwezi Julai, 2021 mpaka leo hii tumekuwa na taarifa 156; kwa hiyo, *trend* inaonesha kidogo angalao kidogo sasa watu wameanza kufanya *compliance* ya sheria, lakini hata hivyo bado changamoto ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie *forum* hii kumuelekeza mkurugenzi wetu wa *NEMC* na timu yake kanda zote waendeleo kuchukua hatua. Hatua hizi ziko za aina mbili; kwanza, tumetoa melekezo kwamba taasisi yetu iendeleo kutoa elimu jinsi gani madhara ya kelele na mitetemo ambavyo yanaweza yakaleta athari kubwa sana katika jamii yetu, hili ni moja.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili, natoa maelekezo hapa tena kwa mara nyingine kwamba taasisi yetu sasa ifuatilie maeneo yote yaliyokuwa sumbufu hasa majengo ya starehe. Tumewaambia watu kwamba hata ukiwa na nyumba ya starehe unapaswa kuhakikisha

unaweka *sound proof*. Kwa hiyo, Mkurugenzi wa NEMC, Dkt. Gwamaka hakikisha maeneo yote yenye baa zote ambazo ni *open bars* zinapiga muziki funga na chukua hatua, sheria lazima ichukue mkondo wake, lazima tuliokoe Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini tulikaa na viongozi wa dini tukiwaomba kwamba kupitia taasisi zote za jumuiya za kidini, sasa kuna bahati mbaya sana baadhi ya taasisi chache za dini zimekuwa zikiwa zinaleta usumbufu wa hali ya juu zaidi. Katika hili tumeelekeza wenzetu viongozi wa dini kupitia jumuiya zote hizi sasa wahakikishe na waendeleo kutoa maelekezo kwa sababu, tuna imani taasisi za dini ndio zingekuwa za kwanza kurekebisha katika maisha ya watu.

Mheshimiwa Spika, imani yetu kubwa kwa sababu, tumeamua kusimamia sheria, nikuhakikishie kama maoni ya wajumbe wote waliozungumza, tutaendelea kusimamia sheria na sasahivi tunaona *trend* inapungua. Imani yetu tutafika mahali pazuri, niwaombe Watanzania tutekeleze Sheria ya Mazingira ya mwaka...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamisi, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Karibu uchangie. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu kuchangia hoja za Wabunge ambazo wamezitoa leo tarehe 30/05/2022. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia nimshukuru Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniadini, kunituwa kuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ili kumsaidia kazi katika Wizara hii. Pia, nimshukuru Mheshimiwa Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana vizuri na kutusaidia katika Wizara yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nimshukuru Mheshimiwa Dorothy Gwajima, Waziri wangu ambaye ananielekeza vizuri na kunisimamia katika kuelekeza maelekezo yote katika kuendesha Wizara hii. Bila kumsahau Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutuendeleza ili kuhakikisha kwamba Serikali yetu inakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niipongeze Kamati ya Kudumu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa michango yao na ushauri na maoni katika kuboresha na utendaji wa majukumu ya Wizara. Niishukuru Kamati tunajitahidi kuzingatia maoni na ushauri katika kutekeleza majukumu ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana wewe pamoja na Naibu wako kwa umahiri wenu wa kuliongoza Bunge hili. Pia nisikose kuwashukuru Wenyeviti ambao wanasaidia kuliongoza Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nikishukuru chama changu cha CCM kwa kunipa heshima kuwa Mbunge na hii leo nipo hapa kama Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

Pia nishukuru UWT kuanzia ngazi ya shina hadi mkoa, mkoa hadi Taifa, bila kuwasahau akinamama wa Mkoa wa Kusini ambao wameniheshimisha leo kuwapo hapa Bungeni na Taifa likaniadini kuniwezesha kuongea hapa katika Bunge hili tukufu. *(Makofi)*

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba nitamke kuwa kuunga mkono hoja hii iliyowasilishwa kwa asilimia mia moja

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kujibu hoja za Wabunge; kwanza tumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mimi katika hoja hizi za Wabunge nitajikita katika sehemu nne; wamachinga, malezi na makuzi ya watoto, wazee na wafanyakazi wa ustawi wa jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara yetu ina sera kama tano, Sera ya Maendeleo ya Jamii ya mwaka 1996, Sera ya Maendeleo ya Wanawake ya mwaka 2000, Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008 na Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001 na Sera ya Taifa ya Wazee.

Mheshimiwa Spika, tunakuja katika wamachinga; kwanza tumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuona umuhimu wa watu hawa ili kuendesha biashara zao ndogo ndogo katika Taifa hili. Napenda nimpongeze kwa upendo mkubwa aliokuwa nao katika Taifa hili, Mheshimiwa Rais ameunda Wizara hii kuhakikisha kwamba anataka kurejesha mila na desturi za Watanzania ili kuwe na utamaduni ambao tunautokea. Hivi sasa mila na desturi zote ambazo zina mmomonyoko mkubwa kwa hiyo, ameona umuhimu wa kuunda Wizara hii ili kuhakikisha kwamba yale yote ambayo tulikuwa tunapewa na wazee wetu waliotangulia basi tunayaleta na kuyafanyia kazi kuhakikisha nchi yetu hii inakuwa salama salmini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wamachinga, Waheshimiwa wamechangia masuala mbalimbali kuwa maeneo Rafiki ili wafanye biashara zao bila kubughudiwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi na Halmashauri na viongozi wa SHIUMA tunaendelea kutenga na kuboresha

miundombinu ya maeneo waliyotolewa kwa ajili ya shughuli za wamachinga. Pia tumshukuru Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoa shilingi milioni kumi-kumi kwa kila Mkoa kuhakikisha kazi zao zinakwenda vizuri, ili kutimiza malengo yao waliyokuwanayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, wamachinga tunao vizuri na tunaendelea kusikiliza changamoto zao kuhakikisha kwamba taratibu zote za kifisi zinakamilika ili waweze kuwa na taasisi ambayo itakuwa mfano katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma za wazee; napenda kulithibitishia Bunge lako tukufu kuwa Serikali imeheshimu na inatambua kuwa wazee ni hazina kubwa ya rasilimali katika umuhimu na ustawi wa jamii wa maendeleo ya Taifa. Aidha, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 imeweka misingi ya kibinadamu kuwaheshimu na kuwathamini wazee.

Katika kuhakikisha kuwa wazee wanapata haki zao na huduma za msingi, Wizara imefanya mapitio ya Sera ya Wazee ya mwaka 2003 na kuandaa mikakati ya utekelezaji wa kuwezesha utungaji wa sheria hiyo kuhusu pensheni ya wazee, mafao kwa watumishi wastaafu kulipwa kwa mujibu wa sheria ya kuanzishwa na mfuko husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha kulingana na mgawanyo wa majukumu suala hili lilitolewa ufafanuzi na Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana na Watu Wenye Ulemavu. Aidha, Serikali inatambua umuhimu wa kuanzisha mpango wa pensheni katika jamii kwa wazee wote.

Mheshimiwa Spika, pendekezo na mpango huu umeandaliwa na kuwasilishwa katika vikao vya maamuzi ambavyo vimetoa maelekezo ya masuala ya kufanyiwa kazi ili kuweka mifano mizuri na endelevu pale mipango itakapokamilika. *(Makofi)*

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, kuhusu wazee na makazi yao; Wizara inaendelea kutoa huduma na matunzo ya makazi 17 ya wazee yanayowezeshwa, mfano Nunge, Kibirizi, Njoro, Kolandoto, Ngeha, Bakumbi, Ipuli, Fungafunga, Mazangwe na Nandanga na mikoa mbalimbali ambayo inapewa huduma hizi za wazee. Hadi kufikia Machi, 2019 wahudumu katika makazi hayo ni 510 ambapo wana ndugu kuwatunza katika jamii hii. Huduma zinazotolewa katika makazi hayo ni pamoja na chakula, malazi na huduma za matibabu.

Mheshimiwa Spika, vilevile wazee wanaendelea kupewa huduma mbalimbali, Serikali ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ya Awamu ya Sita inatoa fedha kila mwezi shilingi milioni 76.247 kwa ajili ya chakula. Vilevile inatoa fedha shilingi milioni 76.247 kwa ajili ya kuendeleza makazi kila mwezi. Vilevile Wizara inatoa vifaa tiba kwa ajili ya kupewa matatizo ya afya yanayowasumbua wazee hao.

Mheshimiwa Spika, wazee wanarudishwa kutoka nje ya makazi ili wasitumike vibaya. Kwa hivyo, Serikali yetu inawaenzi wazee na inawathamini kwa kila hali na mali ambazo wanahitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako tukufu niwaombe Waheshimiwa Wabunge wote wazee wanahitaji malezi, na sisi sote tumelelewa na wazee hawa na ndio maana leo tuko hapa na tunasimama imara kuwatetea wazee wetu hawa, kwa hivyo, wazee wanapokuwa washakuwa na hali ambayo hawajiwezi basi tuwaelimishe wananchi wetu katika majimbo yetu huko ili waweze kuwaenzi wazee wetu hawa kuhakikisha kwamba, nao wanafaidika na nchi yao, sio kuwapotezea na kuchukuliwa na Serikali. Pale tunapowachukua katika Serikali haina budi tu inabidi tuwalee wazee hawa kwa hivyo, tuwasaidieni wazee wetu, wazee ni tunu, wazee ni kila kitu katika maisha yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Maafisa wa Maendeleo ya Jamii...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Dakika moja, malizia Mheshimiwa.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi wamechangia kuhusu maafisa hawa. Naamini Serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, tutahakikisha kwamba tunawaajiri na kuwapa malezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, muda ni mdogo, michango yote mingine ataelezea Mheshimiwa Waziri kutokana na nafasi yake. Mimi nashukuru sana, niwashukuru Wabunge wote ambao wamechangia Wizara yetu hii. Ni imani yetu kwamba tutafanya kazi kwa uadilifu na michango yote ambayo mliyotupa tutaitekeleza kuhakikisha Wizara yetu hii inakuwa kama Mheshimiwa Rais alivyoitathmini.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo yote naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, kazi iendelee. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamuita mtoa hoja nadhani wote tutaafikiana na hoja hii kwamba Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamisi amependeza sana leo. *(Makofi)*

Sasa nimuite mtoa hoja Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum aje ahitimishe hoja yake.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuhitimisha hoja niliyowasilisha mbele ya Bunge lako tukufu siku ya leo tarehe 30 Mei, 2022.

Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla ambao wametoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania ambao wamekubali kabisa na kuona Wizara hii ilikuwa imechelewa ilitakiwa ianze siku nyingi sana ili haya yote ambayo yanatukuta hapa leo yangeweza yakawa yamerudishwa nyuma kwa kasi kubwa kwa sababu tungekuwa na mikakati hii tuliyonayo leo mfano ya malezi na makuzi ya watoto tusingekuwa na kizazi ambacho kina ukatili mwingi namna hii hivi leo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kila jambo linakuja kwa wakati wake, tunashukuru kwa maono yake na tumepokea pongezi hizi, tutazifikisha ili aone kwamba Bunge lako tukufu limeelewa tafsiri ya uamuzi wake mkubwa kwa maslahi ya Taifa letu kwa miaka 50 na miaka 100 mbele.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa ushauri na kuisimamia Wizara yangu kwa umakini mkubwa, ushauri na maelekezo yao yamesaidia katika kuboresha utendaji wa Wizara hii hadi hapa ilipo. Wizara yangu inathamini sana michango yote iliyotolewa naomba nilithibitishie Bunge lako tukufu kuwa tutaifanyia kazi na majibu yote ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge hapa tutaziwasilisha kwenye ofisi yako ili waweze kuzisoma na kuelewa tumezitendeaje haki na kwa sababu hii ni *process* inaendelea ya Bunge tunaamini kadri tunavyokwenda mbele watakuja kuona kwamba tumezitendea haki.

Mheshimiwa Spika, nachukua tena fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia hoja yangu niliyoiwasilisha leo Bungeni, michango yao ni mizuri sana ina lengo la kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara lakini kuboresha tija na ufanisi wa maisha ya wataanzania kwa mingi ya vizazi vijavyo. Jumla ya Waheshimiwa Wabunge nimehesabu hapa 39 wamechangia hoja yangu ambapo kati yao 25 wamechangia kwa kuzungumza na hapo hapo Wabunge 14 wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana pia Mheshimiwa Jafo naye namuongeza anakuwa wa 26 aliyechangia hapa

akizungumzia athari nzima ya masuala ya mazingira tunayoishi katika nyanja za makelele na mitetemo jinsi gani inaweza kuathiri afya za Watanzania pamoja na watoto pamoja na wazee na wagonjwa hatimaye tukawa na akili ambazo siyo njema sana tukaanza kusababisha matukio makubwa makubwa na tukakosa tumeyatoa wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika michango iliyotolewa ipo inayotoa ushauri na mengine ni maswali na Waheshimiwa Wabunge waliochangia nimewaorodhesha naomba kwa kibali chako nitakapowasilisha taarifa yangu kwa maandishi niunganishe orodha yao.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nitoe maelezo na ufafanuzi wa baadhi ya hoja zilizoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja yangu na nikiri kwamba leo Bunge limeweza kuona ukubwa na unyeti wa hii Wizara kiasi kwamba huenda hii siku moja ikawa haitoshi ya kujadili hoja zote hizi maana hapa mambo ni mengi. Lakini nimebaini baadhi ya Wabunge bado hawajaelewa *profile* ya hii Wizara napenda kusema kwamba ni Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Kwenye makundi maalum hapa tunao watoto, tunao wazee, tunao wajane na wamachinga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hawa vijana na walemavu wako kwenye Wizara nyingine iliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ingawa sisi kama Serikali mambo yanaingia huku na kule, kijana anaweza akaibuka akawa ni mmachinga, lakini bado kijana anaweza akawa bado kijana akawa tena mjane hivyo. Kwa hiyo, tunafanyakazi kwa pamoja nilikuwa nataka niweke tu sawa hili jambo hapa ili ninapojibu twende pamoja.

Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba hoja zimetolewa za kutosha nikiangalia katika *pillar* ya *governance* nimeona hapa Wabunge wameongelea jinsi gani uendeshaji wa Idara za Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii zilivyo kule kwenye halmashauri. Kwa sababu bila wao kuwa na nguvu kule tunaweza tukasema sisi huku tunaongea sana tunatengeneza miongozo na Sera nyingi lakini kule chini

utekelezaji *tone* yake ikabadilika kutokana na kwamba zile *powers* hawana ambazo zingekuwa zinaakisi ukubwa wa tatizo ambalo mmelijadili leo hapa.

Mheshimiwa Spika, mmeongelea masuala ya watumishi; upungufu wa watumishi kwa upande wa Ustawi wa Jamii pamoja na Maendeleo ya Jamii kitu ambacho hawa sasa ndiyo *engine* au hawa sasa ndiyo chachu ya kutengeneza jamii kule ikae sawa hata Wizara ya Elimu ikija, Wizara ya Afya ikija ya Kilimo ikija ya Nishati ikute jamii imeandaliwa kifikra kuweza kupokea haya mambo. Nashukuru kwamba mmelijua hili jambo na nina imani kwamba *full council* zetu zingekuwa zinajadili kwenye *tone* hii tungeweza kusukuma zaidi maamuzi na vipaumbele vya halmashauri kiasi kwamba tukapunguza changamoto hizi nyingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mmeona jinsi *multi-sectorial approach* ilivyo kwenye Wizara yangu kwamba sisi ni *coordinator* ni kama *airport* ya Amsterdam tunakaa pale tunapokea kila ndege inatua inaondoka, inaondokaje inategemea na Wizara yangu imewezeshwa vipi kuweza kuzipokea hizi ndege zinazo-*take off* pamoja na kuondoka, kwa hiyo, tunaamini kwamba imekuwa ni shule pia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye masuala ya uwezeshaji wa vitendea kazi kwa hawa maafisa wachache waliopo mmeweza kuona vizuri jinsi ambavyo tunahitaji kufanyakazi kubwa kuwawezesha hilo tumelipokea. Lakini pia mkiangalia sasa hivi kwenye upande wa miundombinu yao ya ufanyaji kazi bado ni changamoto mmechangia vizuri sana mmeweza kwenda kwenye upande wa huduma jinsi gani watatoa huduma kwenye maeneo mbalimbali bado ni changamoto inayotokana pia na wao kutowezeshwa.

Mheshimiwa Spika, mmechambua vizuri kuhusu jamii jinsi ambavyo ina nafasi pia kwenye masuala haya yote, kwa sababu jamii kama jamii ina mambo mengi yanaendelea ndani yake inategemea na utayari wao kuweza kuyatoa na kuyaibua kwenye vikao vyao halali kuanzia kata, kijiji tarafa

mpaka Wilaya mpaka mkoa ndivyo hivyo ambavyo tunaweza kama Serikali kuyafanyia kazi kwa urahisi yote hii inaonyesha kwamba tunahitaji dawa ya jamii ambayo ni Afisa Ustawi wa Jamii tunahitaji Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa ridhaa yako naomba nijikite kwenye ukatili. Ukatili imekuwa ni sauti leo imevuma sana humu ndani na imegusa wengi sana, nafurahi kuona kwamba sauti hii imevuma sana kwangu mimi kama Waziri mwenye dhamana na kwa niaba ya Serikali haya ni mafanikio makubwa kwa sababu sasa ule mpango wetu wa MTAKUWWA unaoratibiwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu wa kutokomeza ukatili kwa wanawake na watoto ndiyo unafanyakazi na umefanikiwa sana. Nasema hivyo kwa sababu zamani matukio haya yalikuwa hayaripotwi kabisa kila mtu alikuwa anaona aibu anayaficha hayakuwepo. Lakini baada ya MTAKUWWA kuanza mwaka 2017 na 2018 na inaisha Juni, 2022 Kamati zimeundwa mpaka ngazi ya kijiji na kule kwenye mitaa zimeanza sasa kuchukua *role* yake ya kuelimisha jamii, jamii imepata *confidence* ya kuanza kuripoti hivi vitu.

Mheshimiwa Spika, *topic* hii ni kubwa peke yake Mungu anisaidie niimalize ili niende na nyingine, lakini nafikiri ingetoshwa siku mbili.

Waheshimiwa Wabunge, walio wengi wamezungumzia ukatili dhidi ya wanawake na watoto na kwamba vitendo vya ukatili vinaendelea kushamiri katika jamii na wanaofanya ni ndugu wa karibu. Utafiti wa *UNICEF* pamoja na Serikali mwaka 2021 Januari - Desemba umeonyesha kwamba 60% ya ukatili huu tunaongea hapa unafanywa majumbani kwetu wakiwepo wazazi wetu, ndugu, wajomba na watu tunaowaamini huko huko tena usiku mwingi, unaamka mtoto kakatiliwa au mtoto wazazi wameondoka wameenda kwenye shughuli nyingine kakatiliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kuna mmomonyoko wa maadili mkubwa sana na kukosa imani ya Kimungu na hofu

ya Mungu katika jamii zetu huku ndani. Jambo ambalo ni kichaka cha mtihamu mkubwa na hakihitaji sana fedha nyingi kupambana na hiki kitu, kinahitaji mioyo ya uzalendo na watu walioguswa wanaosema hili hapana kila mtu kwa nafasi yake apaze sauti ili masikio ya Watanzania yakisikia na macho ya Watanzania yakiona, asilimia 50 ya tatizo linaondoka kwa sababu wakatili sasa watajiona hawako salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha Waheshimiwa Wabunge wametoa ushauri mbalimbali katika kutatua changamoto hii ya ukatili. Serikali katika kushughulikia changamoto hii naomba niisemie kwamba imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na vitendo hivi ikiwemo kuanzisha Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto kuanzia ngazi ya Taifa, mkoa, halmashauri, kata, kijiji na mtaa.

Mheshimiwa Spika, Kamati hizi uzuri wake ukiziangalia zina kila mtu mle ndani kama ni kwenye kijiji kuna kiongozi wa Serikali ya kijiji pale kuna walimu, kuna watu wa afya, kuna ASASI za kiraia pale pale kuna viongozi wa dini, pale pale kuna wanawake, pale pale kuna vijana, pale pale kuna watu maarufu, pale pale kuna polisi jamii na nilishukuru Jeshi la Polisi sana kwa kuzingatia hii ajenda limepeleka vijana wa polisi tena *graduates* zaidi ya 4500 katika kata zetu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hii inaonesha jinsi gani Serikali inafanya kila jitihada kuweza kuhakikisha kule jamii inaamka kwenye zile kamati kuna Maafisa Maendeleo ya Jamii pamoja na Maafisa Ustawi wa Jamii. Lakini sasa changamoto tuliyonayo katika kupambana na hiki kitu kamati nyingi zimeundwa zinakuwa haziko hai, hata zile zilizojengewa uwezo. Ukienda kwenye *full council* zetu nyingi unakuta hii taarifa haiko itokanayo na utendaji wa hii kamati.

Kwa hiyo, tunapokwenda kujenga uwezo tunadhani kwamba sasa tutaagiza *full council* zote na vikao vyote vya halmashauri viagize kuwe na *chapterya* taarifa hizi za ukatili ili watu waweze kuwajibika na kuona kwamba ni muhimu hii ajenda iende mbele kama kipaumbele chao.

Mheshimiwa Spika, lakini Serikali haijaishia hapo imeimarisha Madawati ya Jinsia Jeshi la Polisi na hapa mmechangia kwamba tuone namna gani jinsi ya kuyaondoa pale, kwa sababu suala hili ni la Kiserikali tutaenda kujadili chini ya uratibu wa Wizara yangu, lakini kwa ridhaa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tuone tunafanyaje. Aidha, kuwaelimisha watu wasiogope au kama inabidi hivyo ndivyo hii tathmini inayofanyika ituambie kwamba tuyapeleke eneo gani ili mwitikio uwe mkubwa zaidi.

Lakini pia ukiacha hizi Madawati ya Jinsia Jeshi la Polisi tumeanzisha vituo vya mkono kwa mkono (*one stop centre*) katika hospitali zetu mbalimbali na zoezi linaendelea na hivi vinakuwa vinatoa huduma jumuishi za kitabibu msaada wa kisheria na ustawi wa jamii kwa manusura wa ukatili na niseme hapa kuna tabia ya jamii kuficha ushahidi; wanakatiliwa, wanaanza kwa kusema huyu ni babu, huyu ni mjomba utapata laana wewe mtoto nyamaza.

Mheshimiwa Spika, kipindi tunapokuja kusikia kinyemela tunakwenda kuwapeleka kwenye haya madawati ushahidi umefutika. Nilitembelea Dawati la Chanika Dar es Salaam, akasema yule Afande yuko pale anaitwa Christina kwamba sisi tumepokea kesi nyingi sana na 99.9% zilizofika kwa wakati zilikwenda mahakamani zikashinda kesi.

Sasa shida inakuwepo imechangiwa hoja hapa kwamba mahakama saa nyingine zinachelewesha kesi nikaenda mpaka kule nikaenda mpaka Polisi nikaambiwa kwamba sasa unapeleka kesi haina ushahidi watu wameamua kupatana zirudi nyumbani wakamalize kindugu. Lakini wengine wamehongana hapo katikati, wengine wamekimbia wametoweka, lakini wale wanaofanikiwa kufika kwenye vituo hivi ushahidi ukachukuliwa asilimia 99.9 kesi zao zimekwenda haraka sana na wameweza kushinda na watu kila siku tunasikia wamefungwa miaka 30, wamefungwa miaka mingapi, hizi ni hatua ambazo Serikali inafanya. Hivyo jamii tunaomba ichukue wajibu wake kutoa msaada kwenye hii mifumo ambayo imeshaanzishwa ili tuweze kwenda sawa katika kufikia ufanisi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, lakini ukiacha hilo, tunazo nyumba salama, tunao watoto wengi waliofanikiwa kwenda nyumba salama waliweza kuepuka ukatili. Tatizo nyumba salama tunakubali bado ni changamoto na ni zoezi ambalo tumepanga kuendelea kuziongezea sambamba na utoaji elimu katika jamii zetu.

Mheshimiwa Spika, naomba tuseme kwamba kwenye vyuo vikuu nako ni mtandao wa ukatili upo lakini Serikali imefanikiwa kuanzisha madawati ya jinsia kwenye hivi vyuo vikuu pamoja na vyuo vya elimu ya kati. Hatujaishia hapo kwenye shule za msingi pamoja na shule za sekondari kule tunakwenda kuzindua kwenye siku ya Mtoto wa Afrika tarehe 16 Juni, Mabaraza ya Watoto yanakwenda kuzinduliwa pale, lakini Madawati ya Jinsia yanakwenda kuzinduliwa pale, klabu za watoto zitazinduliwa pale. Kwa hiyo, watoto wakikatiliwa nyumbani baba na mama hamna muda wa kusikiliza watakwenda kuyasema shuleni, lakini pale shuleni tunaweka utaratibu Maafisa wa Ustawi wa Jamii hata kama ni wachache tutaomba na wa kujitolea waliostaafu wawe wanakwenda pale kuwaimarisha hawa tupate mpaka *matron* wanaoweza kuongea na hawa watoto ili waweze kufunguka na kusema mambo ambayo mengine hawawezi kuyasema kule majumbani kwao.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kufanya kampeni ya twende pamoja ya ukatili sasa basi, lakini tumeiboresha hii kampeni tumetangaza na tutatangaza tena kesho fomu maalum ya wazalendo wote wapambanaji popote walipo wakienda kwenye *google* ukaandika SIMAUJATA. SIMAUJATA ni Shujaa wa Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii Tanzania, tumepata vijana wengi, muitiko ni mkubwa baada ya kutoa hizi elimu za mara kwa mara wanasema tunataka kwenda mstari wa mbele, sisi tumeshachoka kukatiliwa na kuona watu wanakatiliwa, wanajisajili.

Mheshimiwa Spika, itakuwa sasa kila mtaa tunaangalia tumemsajili nani wenzetu wa utalii wametengeneza Jeshi lao la USU na sisi tunatengeneza Jeshi la SIMAUJATA, waende mstari wa mbele, mlango kwa

mlango, mkiona wanapita kwa baiskeli wameweka redio kama ndugu zangu wa Kolomije mfungue milango, watakuwa wanasema kile tulichowalisha maneno ili wananchi wasikie waweze kuona hatuwezi ku-*afford* kuwa na mabilioni ya pesa ya kununua magari kwenda kule, kuna vita vingine ni vya kizalendo tu na moyo katika kulitetea Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hata ninyi Wabunge mlioko hapa wanawake kwa wanaume mnaombwa mjiunge kwenye hiyo kampeni, lakini niseme vita hii inasemwa sana kwenye *centre* ya uadui tunaona jinsia ya kiume inainuliwa pale. Wale wanaume siyo wote ni wanaume wachache lakini wanaume wengi walio wazuri ni kama vile wamekubali haya mambo yaendeleo, hatuoni *forum* zao tunaona ma-*kitchen party* ya akinamama, tunaona majukwaa ya akinamama ya *VICOBA*, tunaona akinamama wanahangaika, tunataka kuona wanaume wanainuka wale waliobarikiwa wenye hekima wanasema kwa wanaume wenzao hapana hii haikubaliki wawakemee tunakimbiza mtu kaiba kuku anakwenda kusitiri njaa tunamshughulikia kweli kweli, lakini tunaacha mbakaji tunamstriri na wababa wapo, matumbo yabebe Watoto, yazae Watoto, wabakwe akinamama, wabakwe watoto wa kiume, wabakwe wa kike hii haikubaliki. Akina baba mko wapi? Wakina baba wazuri mko wapi? (*Makoff*)

Mheshimiwa Spika, dunia sasa inachukua *direction* ya mkakati wa *He for She*; *He for She* maana yake ni kumnyanyua mwanamme atakayekuwa mfano wa nembo ya Taifa ambapo wanaume wengine wakimuangalia wanamuona kwamba sisi mbona kama vile siyo wanaume, tumchoreje mwanamme wetu wa jamii ya Kitzania ambaye yuko mbali na ukatili, ni baba wa familia, ni mbeba maono ya familia na wengine wote wakimuangalia wanaona aibu, watakimbia wataogopa. Leo wakati na wabakaji wanabeba nembo ya kiume wanaifanya ndiyo nembo ya sura ya mwanaume wa Tanzania, wanaume naomba muwakatae, amkeni mtualike kwenye vikao vyenu tuje tufungue vikao vya akinababa vinavyosema mwanamme kibaka wewe siyo mwanamme, wanaume

wamekuwa na moyo mdogo akiudhiwa na mwanamke anamimina risasi saba kwenye kichwa cha mwanamke, ameuawa kule Shinyanga, ina maana wanaume kama ni viongozi wa familia mioyo imekuwa midogo kiasi hicho hasira kidogo umeua hasira kidogo umekomoa hii siyo sawa bebeni uanaume msembe hapana kwa wenzenu wanaowaharibia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, leo tukisema wanawake wanaweza maswali yanakuwa mengi, sasa imeanza *profile* kubadilika, wanaume mnakwenda *down* na mnapelekwa na wenzenu wachache simameni kwenye nafasi zenu Mungu alizowapa, musimamie uanaume wa heri na baraka na furaha na amani kwenye maisha ya watoto hawa wa kike na wa kiume, kwa sababu silaha za kubakia sasa mmepewa nyinyi sisi tutafanyaje wanaume kataeni tuko pamoja na ninyi tupambane na wale wachache. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, inaumiza sana na hapa ndiyo sehemu ya kusema ili tubebe *spirit* ya kitaifa, hili halina hata chama kipi, halina cha imani ipi, halina cha itikadi gani, ni jambo la kitaifa lazima tuende pamoja. (Makofi)

Vilevile Wizara inafanya tathmini ya utekelezaji wa MTAKUWWA kwa kipindi kilichopita kama tulivyosema, tutasubiri hiyo tathmini, lakini *aluta continue* vita lazima ianze mlango kwa mlango tupeane ushirikiano wakati tunaisubiri tathmini hiyo mbele ya safari. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tunao mashujaa wengine wamejiandikisha na walikuja hapa Bungeni leo watu wanajitokeza kwa wingi, tunao vijana wa *Pink Tie* ambao wanaongozwa na *Pink Tie Foundation* hawa ni akina Lillian Mwashu huyu ni mtumishi wa Mungu, akina Salma Dakota, akina Furaha Dominick tunao vijana akina Jacob kutoka Mara wamesajili *Safe Network* kwa uchungu kutokana na mambo haya haya na wanabeba ajenda kweli siyo suala la mwanamke tu ni suala la mtoto wa kiume pia. (Makofi)

Tunao *Wanawake Live* akina Joyce Kiria, tunao wengi na wengine siwezi kuwataja hapa, hii inaonesha kwamba sindano imeingia dawa, imeingia sasa ari ya vijana ya kuona kwamba Taifa linatokomea inachemka, utafanyakazi ya kurudisha nyuma na wakatili hawataweka makao makuu ya shetani mwa ukatili Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze sasa tunafanyaje maana yake nyuma ya ukatili pia tuna ajenda ya uchumi huku chini, tuna agenda ya mila ya desturi ambazo ni *area* pia zimewekwa kwenye MTAKUWWA, lakini tuna masuala ya kisheria niseme kwamba suala hili la hizi programu mbili za kulea watoto wetu malezi na makuzi ya awali ya mtoto tumeisema hapa tumeanza na vituo 20 Dodoma na kumi Dar es Salaam na 15 vimeanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, huu ni mwanzo tu vilikuwa vya majaribio, lengo ni kwenda nchi nzima, hapa nitoe wito kwa akinamama na akinababa ambao wanapenda kuhakikisha watoto wetu sasa wanaanza kukuwa vizuri tujitokeze, tunachangia harusi, tunachangia vitu vingi vituo hivi ni shilingi 10,000,000 hadi 13,000,000 tufanya *force account*, tuona tunafanyaje viende kwa kasi sana tunao wadau wanatusaidia, lakini na sisi Serikali tunaweka fedha pale, lakini na jamii ya wapenda maendeleo katika *spirit* ile ile ya kuchangia mambo yaende kwa kasi tujipange ndugu zangu hakuna kuchelewesha mtoto ukimchelewa leo kesho amepotea, vituo hivi vinatakiwa vijengwe nchi nzima na kazi inaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, natoa tu wito huu kwa ajili ya kuongezea kasi lakini Serikali mpango wake vishuke ilipo zahanati kama ni kwenye kata kuna hicho kituo ilipo zahanati kwenye kijiji kuna hicho kituo, ilipo shule kuna hicho kituo, walimu watapatikana ndugu zangu kuwalea wale watoto sio kazi kubwa sana hauhitaji ma-*degree* mengi, hawa hawa tulionao tutaanza nao wakati taaluma hiyo ya saikolojia na vitu vingine vikiendelea kukuwa sambamba na wanaustawi wa jamii wetu wanatengeneza sheria yao kwa hiyo tutakuwa mpaka na kliniki za wana ustawi wa jamii kama tulivyokuwa

na kliniki za zahanati au vituo vya afya au za kiuuguzi ili waweze na wenyewe kusajiliwa kama ni *private* au kama *government* waweze kuwafikia wananchi popote kule walipo wakati huko tukiendelea kuajiri wa Serikali ili kufikia ile asilimia tunayoihitaji.

Mheshimiwa Spika, usawa wa kijinsia niongelee...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri dakika tatu malizia kengele ya pili imeshagonga.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimia Spika, usawa wa kijinsia tumesemea sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan yeye ni kinara katika haki na usawa wa kiuchumi ambapo jukwaa hilo alilizindua mwaka jana tumesema, andiko linakamilika maana yake ni kwamba ukiacha mikopo ya asilimia 10 mmeisemea sana tunakwenda kuboresha tutaongea na Serikali maana yake ni agenda mtambuka.

Mheshimiwa Spika, tutakuwa na haya Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi ambapo fedha zitakuja, wadau wanatuunga mkono, tutakuwa na madirisha ya posta yanaendelea kuwepo, tutakuwa na mikopo mingine ile ya *Women Development Fund* iliulizwa hoja hapa sio kwamba umefutwa ilitekelezwa kutoka mwaka 1996 hadi 2017, kukatokea changamoto fulani zikahitaji mwongozo utengenezwe, mwongozo unakamilika Serikali itatoa maelekezo jinsi ya kupata fedha na kuendelea kutoa hiyo mikopo kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, masuala ya uwezeshaji kiuchumi katika usawa wa kijinsia yanazingatiwa sana na kufika mwezi wa Julai tutakuwa tumeshaweza kuzindua andiko hili ambazo tumeagizwa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yameulizwa hapa na hapa niseme kwamba wasajili wasaidizi wapo kwenye halmashauri na mikoa yetu walikuwa wanachangamoto ya kukosa fungu la kutekeleza majukumu yao lakini mwongozo wa uratibu wa pamoja na mashirika hayo umeshaandaliwa na umetoa majukumu kwa mamlaka ya Serikali za Mitaa kuratibu ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa katika mamlaka hiyo. Ntoa rai kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kutenga fungu kwa wasajili hawa ili waendeele kutekeleza majukumu yao ya uratibu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mambo ni mengi sana lakini kama vita hii tumeikubali ya kuliokoa Taifa letu naomba halmashauri/*full council* zikae kwenye usukani, taarifa ya kila mwezi inayokuja ikijadiliwa kwa mapana kama ilivyojadiliwa kwenye Bunge lako tukufu, hawa wakatili sio kwamba hawana akili wanajua vizuri wataondoka wenyewe.

Kuhusu suala la ukatili wa mitandaoni tumeshasema tunaandaa sasa kikosi kasi kimeshaandaliwa na sheria itafanyiwa mapitio, sheria zetu huenda ni nzuri sana miaka 30 ni mingi mno lakini saa *enforcement* yake inategemea mwitikio wa jamii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini tathmini ya MTAKUWWA itakapokuja itatuambia kama ni suala la kisheria hatutasita kulileta Bungeni mje mlijadili tuone tunafanyaje, lakini wakati huo jamii yetu twende tukaifungue kwa nguvu zetu zote unatokea ukatili vyumbani kwao sauti zifike hadi vyumbani kwao, mtu afike redio aiweke *siting room* aseme nimekuja hodi kama ni mtaani watu wasikilize hizi taarifa ili wawe *empowered* kuweza kuwa na *confidence* ya kupambana na hayo mambo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ningetamani kuendelea kusema hadi kesho, lakini naona muda hauniruhusu naomba kuwasilisha na naomba kutoa hoja. (Makofi)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono na sasa tutaendelea.

Katibu.

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI: Kamati ya Matumizi.

SPIKA: Kamati ya Matumizi.

KAMATI YA MATUMIZI

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae.

Katibu.

NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge tunajielekeza katika kitabu cha pili cha matumizi ya Kawaida Fungu 53 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Ukurasa wa 367.

KITABU CHA PILI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 53 – Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management.....Sh. 3,117,056,000*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki kina mshahara wa Waziri na ninayo orodha hapa ya Wabunge ambao wanataka ufafanuzi juu ya jambo moja mahsusi la kisera. Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi.

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwanza kabisa niungane na Naibu Waziri Mwanaidi Ali Khamisi kutambua thamani ya wazee nchini kote, lakini pia kwa kuzingatia Sera ya Wazee ya mwaka 2003 inatambua ushiriki wa wazee kwenye vikao kuanzia ngazi ya vijiji, kata, wilaya na mkoa na kwa kuwa kwa sasa kumekuwa na ushirikishwaji mdogo wa wazee kushiriki kwenye vikao hivyo kwa maana ya ngazi nilizoitaja huku. Sasa nini kauli ya Serikali katika suala hilo la ushiriki wa wazee kwenye vikao katika ngazi hizo nilizoitaja? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Iddi Kassim acha nikupe nafasi kwenye ngazi hiyo ukisema unataka kauli ya Serikali sijajua inatusaidia nini kwenye ngazi hii Hoja yako ni ya kiseru kwamba wazee washiriki kwenye vikao.

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, vikao

SPIKA: Sasa huo ufafanuzi unaotafuta ndio nakupa nafasi hebu elezea unataka ufafanuzi kuhusu.

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka mpango mkakati wa nini sasa Serikali imeweka kuhakikisha kwamba wazee wanashirikishwa vyema kwenye vikao hivyo.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri ufafanuzi mkakati wa Serikali wa kuhusisha wazee kwenye vikao.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa swali hili zuri naomba nitoe ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi kirefu wazee hawa walikuwa wanaishi kama kiunaharakati hawakuwa na *forum* nzuri sana ya kuweza kutoa sauti zao na kujadili mambo yao ana kwa ana na Serikali. Ni katika kipindi cha Serikali ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ambapo tumefanikiwa kuunda mabaraza mengi sana kwenye ngazi ya halmashauri

na ngazi ya mkoa na sasa tumezindua Baraza la Wazee la Taifa limeshapewa mafunzo, limeshaka vikao, limepitia sera yao ambayo tulikuwa tukii-*draft* muda mrefu sana limepitia mwongozo wa uendeshaji wao na sasa wapo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila tunapojadili chochote wao wenyewe wanakuwapo hatupeleki kitu mbele bila kuwepo *forum* hii ya baraza la wazee la kitaifa sambamba na mabaraza ya mikoa yote na halmashauri zote. Kwa hiyo, haki zao, vipaumbele vyao na kero zao zinashughulikiwa kikamilifu na Serikali.

MWENYEKITI: Haya ahante sana Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi maana yake ameridhika.

Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, nilitaka tu kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwamba mambo mengi yanayofanywa na Wizara hii yanatekelezwa na Wizara nyingine kwa mfano wengi wanaongelea asilimia 10 ipo TAMISEMI; kuna suala la TASAF lipo Utumishi, kadha wa kadha.

Sasa je, Wizara hii ina mpango gani wa kuwa na *oversight role* ili kuhakikisha kwamba yale yanayofanyika na hizi Wizara nyingine wataweza kuyajua, kuyafanyia tathmini, kuainisha lakini pia kutoa ripoti kwa Bunge kuona namna gani ambavyo...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Neema Lugangira, kwanza huwa ni jambo moja, halafu sasa humo kwenye sera umechanganya mambo mengi ili yeye aeleze. Sasa sijaelewa kama hiyo ulitaka kutoa kama mifano, ama ulikusudia kusemaje, ili nijue ninamwongoza vipi Mheshimiwa Waziri kutoa ufafanuzi jambo lazima liwe mahsus moja la kisera.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru jambo ambalo ninahitaji Mheshimiwa Waziri atolee ufafanuzi ni namna gani ambavyo Wizara yake itahakikisha

inafanya tahmini na *oversight role* ya michango ya Wizara nyingine kwenye afua ambazo zinachangia katika Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum? Ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwasababu unajua hii Wizara yako ni mpya, kwa hiyo watu tukisoma tu lile jina tunapata picha kwamba mambo yanaingia mengi humo, kwa hiyo hoja ya Mheshimiwa Mbunge anataka kujua kwa sababu yanaingia humo mambo mengi ambayo yanatoka sehemu nyingine, Wizara yako ina mpango wa kutengeneza kama sera hivi kwamba mambo hayo sasa yatakuwa yanaulizwa kwenu ama itakuwaje, kwa sababu ni Wizara mpya, kwa hiyo toa ufafanuzi tu huo wa jumla.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa swali zuri la Mheshimiwa Mbunge, ni kweli Wizara hii *nature* yake ni mtambuka kwa sababu kule kwenye jamii kila sekta inakwenda inaifikia jamii na sisi kama Maendeleo ya Jamii tunakuwa *responsible* kusema kwamba jamii/tunatoa *feedback* sasa kwa Serikali kwamba jamii kweli imeridhika na mikakati yetu tupo vizuri. Hivyo kupitia uongozi wa Mheshimiwa Waziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hasa katika masuala haya ya kutokomeza ukatili tumeona kwamba Wizara yetu imepewa *coordination role* ambayo ina kamati tekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kupitia mwongozo huu wa MTAKUWWA tunao *u-revise* tutapeleka mapendekezo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ili wale *ma-focal person* wa MTAKUWWA waliopo kila Wizara waweze pia kuwa wana tu-*inform roles za implementation za policies* hizi zinazogusa Maendeleo ya Jamii kule ikoje na ikimpendeza Waziri Mkuu baadhi ya vitu vingine ambavyo tulikuwa tujibu sisi moja kwa moja kwa wakati wa sasa maana wakati ule Wizara haikuwepo basi tuweze kupewa, lakini pia tuwe *responsible* kupeleka taarifa hii kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ili waweze kuona picha nzima inayokwenda kule chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye Halmashauri pia maana nilitokea kule kwenye *full council* wataalam pia waende na *spirit* hiyo ili waweze kupata wale Maafisa Maendeleo ya Jamii kitu gani kinaendelea wasiwe wanaacha achwa hivi peke yao, tutawasilisha pendekezo hilo tuone tunapata maelekezo gani ya Serikali, ahsante. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Neema pia naona ameridhika. Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, mimi naomba ufafanuzi sina nia ya kuchukua shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya nchi ni kuondoa umaskini kwa kuwawezesha wananchi kupitia mifuko mbalimbali, na inavyoonekana mfuko ambao unachangamkiwa na unaoeleweka kwa wananchi ni ule wa halmashauri wa asilimia 10 yaani nne kwa wanawake, nne kwa vijana na mbili kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilitaka kujua hatma ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake yaani *Women Development Fund* mfuko huu upo chini ya Wizara na unapewa fedha na Serikali Kuu na hadi sasa Serikari haitoi fedha, na kama Serikali kuu haitoi fedha ni kwamba mfuko huu haufanyi kazi lakini pia Wizara yenyewe imeshindwa kukusanya madeni ya mfuko huu. Kwa hiyo ningependa kupata ufafanuzi Serikali itueleze hatma ya Mfuko huu wa Maendeleo ya Wanawake. (Makofi)

MWENYEKITI: Haya Mheshimiwa Waziri wa Fedha naona umesimama, katika kusimama kwako utatupa ufafanuzi kama huo mfuko umeshahamia kwenye Wizara hii ya Wanawake ama bado.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa sababu Wizara ndio imeundwa, bado wanafanya *re-organization* baadhi ya *votes* ambazo ilikuwa

kwenye maeneo mengine ili ku-*consolidate* kazi ambazo zipo kwenye Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo moja tu la faraja ambazo nilitaka kumpa *assurance* Mheshimiwa Mbunge ni kwamba hivi karibuni Rais wetu alichaguliwa kuwa *champion* wa uwezeshaji wa wanawake ambao wapo kwenye shughuli za uzalishaji na shughuli za biashara na mpaka sasa amesha-*mobilize resources* zikiwepo NMB pamoja na taasisi nyingine za kifedha ambazo zinalenga kwenye kutunisha mfuko ambao utaenda kuwawezesha wanawake kuweza kupata mikopo pamoja na mitaji kuwezesha biashara zao ziweze kufanikiwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na taarifa rasmi tutaitoa tutakapokuwa tunatoa kauli ya Serikali kwenye hotuba kubwa ya Serikali. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tumebaki na dakika kumi tumalize siku yetu ya leo kwa hivyo tunaingia kwenye utaratibu wa kupitisha mafungu yote kwa pamoja.

Katibu!

NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 53 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

KITABU CHA PILI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 53 – Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum

Kifungu 1001 – <i>Administration and Human Resources Management</i>	Sh. 3,117,056,000
Kifungu 1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i>	Sh. 612,484,000
Kifungu 1003 – <i>Policy and Planning Unit</i>	Sh. 771,132,000
Kifungu 1004 – <i>Internal Audit Unit</i>	Sh. 394,300,000

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Kifungu1005 – <i>Government Communication Unit</i>	Sh. 271,260,000
Kifungu 1006 – <i>Procurement Management Unit</i>	Sh. 491,436,000
Kifungu 1007 – <i>Information and Communication Technology</i>	Sh. 272,812,000
Kifungu 1008 – <i>Legal Service Unit</i>	Sh. 306,652,000
Kifungu 2001 – <i>Community Development Institutes</i>	Sh. 11,448,780,000
Kifungu 2002 – <i>Community Development</i>	Sh. 956,920,000
Kifungu 3001 – <i>Gender Development</i>	Sh.935,185,000
Kifungu 3002 – <i>Children Development</i>	Sh.716,220,000
Kifungu 4001 – <i>Non- Government Organizations</i>	Sh.1,208,124,000
Kifungu 5001 – <i>Social Welfare Division</i>	Sh.10,808,620,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu, vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitabu cha Maendeleo Fungu 53 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

KITABU CHA NNE

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 53 – Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum

Kifungu 1003 – <i>Policy and Planning Unit</i>	Sh.473,270,000
Kifungu 2001 – <i>Community Development Institutes</i>	Sh. 5,300,000,000
Kifungu 2002 – <i>Community Development</i>	Sh. 0
Kifungu 3001 – <i>Gender Development</i>	Sh. 1,833,210,000
Kifungu 3002 – <i>Children Development</i>	Sh. 1,574,000,000
Kifungu 5001 – <i>Social Welfare Division</i>	Sh. 1,911,600,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu, vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge Lilitarejea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae. Mtoa hoja taarifa.

T A A R I F A

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge Kifungu cha 123(3)(a) na (b) naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake, naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. na sasa nitawahoji.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwa)
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

SPIKA: Ahsanteni sana.

Nitumie fursa hii kumpongeza sana Waziri Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima pamoja na Naibu Waziri wake na watendaji wote wa Wizara hii muhimu ambayo Wabunge hapa kwa michango yao mmepata picha kwamba na wao wanaithamini sana Wizara hii na sasa wameweza kupitisha mafungu kama mlivyokuwa mmeomba na kwa hivyo niwatakie kila ka kheri katika utekelezaji wa yale mliyoyahidi

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

katika hizi fedha ambazo Bunge limeithinisha kwamba mnaweza kwenda kuzitumia kila la kheri katika kushughulika na changamoto tulizonazo kwenye jamii.

Waheshimiwa Wabunge, pia niishukuru sana Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Huduma chini ya Mheshimiwa Stanslaus Nyongo pamoja na Makamu wake na Wajumbe wote wa Kamati hii tunawashukuru sana kwa kuisimamia vizuri Wizara hii na mpaka imefika sehemu ambapo wanaweza kufanya kazi. Sasa baada ya kuomba fedha Bungeni kwa hiyo tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Lakini pia Wajumbe wa Kamati mbalimbali ambao wamepata nafasi leo ya kuchangia na wengine wamechangia kwa maandishi mambo mazito mliyoyasema hapa yote yamechukuliwa na Mheshimiwa Waziri kwa uzito huo huo mliousema na yatafanyiwa kazi na yale ambayo hakupata nafasi ya kufanua hapa kwa mujibu wa utaratibu wetu msiwe na wasiwasi majibu ya kila hoja iliyotolewa hapa yataletwa.

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge pia niwashukuru kwa mawazo yenu mlioishauri Serikali katika kuhakikisha Wizara hii inatimiza jukumu lake ambalo Mheshimiwa Rais ameiunda kwa ajili hiyo.

Kwa hiyo nichukue fursa hii kutangaza sasa kwamba Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yamepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Yalipitishwa na Bunge)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mambo machache la kwanza kabisa ni kuhusu *parking* ya magari. Waheshimiwa Wabunge tu-*park* magari tulipoelekezwa tusi-*park* sehemu nyingine, leo imetokea changamoto lakini kwa kuwa

hatujawahi kupata changamoto huko nyuma nalazimika kutoa huu ufafanuzi kwa sababu yanaweza kutokea mambo fulani hivi yakaleta jambo ambalo pengine Mbunge asingependa litokee kwa namna hiyo. Lakini hata sisi kwa ajili ya usalama wetu tu-*park* sehemu tulizoelekezwa, tusi-*park* sehemu nyingine yoyote ile.

Jambo lingine ambalo nimependa nilizungumzie leo ni kuhusu uwasilishaji wa jumla Waheshimiwa Mawaziri wakati mwingine mkiwa mnasoma zile hotuba unakuta na taarifa za ziada unazotaka kuzisema, lakini wakati huo huo mwanzoni ulishasema hotuba yako yote iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. Kwa hiyo sisi taarifa tutakayokuwa nayo ni ile hotuba yako uliyotukabidhi kwamba iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge na yale ya ziada unayokuwa umeyatoa hapa ama ufafanuzi unaokuwa umeutoa hapa wakati wa kusoma hotuba ile asubuhi unakuwa hauingii kwenye taarifa rasmi za Bunge kwasababu hatuwezi kuwa sasa na taarifa mbili, tunaingiza ile moja uliyoleta kwa maandishi. Nimeona nilisema hilo tena kwa mara ya pili ili tuwe tunaenda sawa.

Jambo la tatu hili nataka Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii lakini pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali amesema hapa Mheshimiwa Waziri nilikuwa nasikiliza kwa makini kwamba kesi zile ambazo watu wamewahi kwenda kutoa taarifa na ushahidi ukachukuliwa mapema na hivyo amesema asilimia 99.9 kesi hizo zikipelekwa mahakamani zinaenda kwa ule mtindo wa kumfanya yule aliyefanya kosa kuwa na hatia.

Sasa hilo ningependa utusaidie takwimu hizi kidogo zinanipa mimi wasiwasi kwasababu leo nilikusudia kukisema kifungu hiki ambacho ndio maana nimekutaja Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kifungu cha Sheria inayohusu Ushahidi kifungu namba 127(2) ushahidi wa mtoto mdogo aliyefanyiwa ukatili huo tunaosema. Kifungu hiki kina tafsiri nyingi sana huku Mahakamani na wewe Mwanasheria Mkuu wa Serikali tunakuomba utusaidie ili zile tafsiri siziendele kuwa nyingi na siziendele kugongana kwa sababu kifungu hicho kipo kwenye sheria, kama ipo changamoto tuletewe hapa

tukibadilishe, wananchi tunaowawakilishi hawafurahi mtu ambaye wanao uhakika kwamba alifanya kosa halafu kunatokea matundu kwenye ushahidi wa mtoto, halafu huyo mtu anatolewa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sisi ambao humu ndani sawa wanasheria tupo na huko nje wapo na kwenye jambo hili kesi zipo nyingi kwa hiyo siyo kesi moja hizo kesi zote zikipitiwa ni rahisi kujua changamoto ipo wapi, lakini ukizipitia mimi kwa hizo chache nilizozipitia changamoto ipo kwenye hiki kifungu 127. Kwa hivyo Mwanasheria Mkuu utusaidie sheria hii Waheshimiwa Wabunge tuifanyie marekebisho kwa sababu changamoto nyingi zilizokuwa zinasemwa hapa kuhusu ushahidi wa watoto, watu wanatolewa kule ndani, anaweza asitoke kule kwenye ngazi ya chini ambapo ndio amepelekea mara ya kwanza, lakini ataenda Mahakama Kuu wanaweza wakamkuta na hatia ama wasimkute na hatia. *(Makofi)*

Ataenda Mahakama ya Rufani atatolewa kule tutakutana naye mtaani kwanini si kwamba jambo hakufanya alifanya lakini kuna matundu kwenye ushahidi wa yule mtoto, sasa lazima Bunge letu katika nia ile ile ya kuwalinda watoto wetu, lazima tufanya mabadiliko kama hayo mabadiliko yataisaidia Mahakama kuweza kufika mahali ambapo wanaweza kuwa na maamuzi ya aina fulani ambayo pengine yote yanatupeleka kwenye kuhakikisha jamii yetu inakuwa inalindwa na hasa watoto wadogo wanaofanyiwa vitendo hivi vya kukatili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hilo nimelisema kwa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, lakini pia kwa sababu kuna Wizara sasa mahsusini inayoshughulika na hili naamini nitafanya utafiti huko, halafu muone namna sisi Bunge tupo tayari kabisa kushughulika na hicho kifungu kama ndicho kinachowafanya waliofanya makosa warudi mtaani.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo hapa kutoka kwa Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba siku ya kesho Jumanne tarehe 31 Mei, 2022 saa 7.30 mchana kwenye ukumbi wa Msekwa kutakuwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

na Semina kwa ajili ya Wabunge wote. Semina hii itakuwa inahusu migongano baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu.

Waheshimiwa Wabunge, tunaombwa tuhudhurie semina hii ili tukapate kutoa mawazo yetu, lakini pia kusikia hatua mbalimbali ambazo Serikali inachukua kwenye maeneo ambayo wana changamoto hii ya wanadamu na hawa Wanyama wakali wanapokuwa wamehitilafiana ama wameingiliana kwenye maeneo yao ya himaya.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne,
Tarehe 31 Mei, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*